**16 APRILI, 2026**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 16 Aprili, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: -**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI: -**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MHE. EDWARD O. KISAU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA: -**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali na swali la kwanza litaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Sasa ninamwita Mheshimiwa Morris Joseph Makoi, Mbunge wa Moshi Vijijini, aulize swali lake.

Na. 103

**Ujenzi wa Barabara ya Mbokomu - Mti Mrefu - Moshi Vijijini**

**MHE. MORRIS J. MAKOI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Mbokomu - Mti Mrefu kilometa 13.94 kwa kiwango cha lami ili kuchochea utalii?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Morris Joseph Makoi, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa Barabara ya Mbokomu – Mti Mrefu katika Wilaya ya Moshi. Katika mwaka wa fedha 2024/25 Serikali ilitenga bajeti ya shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami nzito *(asphalt concrete)* mita 200 na tayari zimekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga bajeti ya shilingi milioni 225 kwa ajili ya ujenzi ya barabara hiyo kwa urefu wa meta 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mahitaji makubwa ya matengenezo ya barabara kiwango cha lami, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa awamu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Morris Joseph Makoi.

**MHE. MORRIS J. MAKOI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri na ya kutia moyo ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile barabara ya Rau Madukani - Mamboleo - Materuni - Shimbwe yenye urefu wa kilometa 16.7 ni barabara ambayo ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyowaahidi watu wa Uru Mashariki na Shimbwe kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami kwa maana ya mwendelezo, lakini hiyo barabara ndiyo ambayo inaenda kwenye maanguko makubwa ya maji katika Wilaya ya Moshi na maanguko haya yanachochea sana pato la utalii kwa Halmashauri ya Moshi na wanaingiza karibu shilingi milioni 25 kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani pamoja na kukamilisha ahadi ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ina mpango gani kuhakikisha basi barabara hii pamoja na kujenga lami kiwango cha meta 500, 500, ina mpango gani kuhakikisha sehemu inayobaki inapitika muda wote ili kusaidia watalii kufika kwenye maanguko hayo, kuwasaidia wananchi kusafirisha mazao yao, lakini kikubwa zaidi kuchochea uchumi wa wananchi na utalii kwa ujumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Wilaya ya Moshi ina vijiji 40 ambavyo vimezunguka Mlima Kilimanjaro. Hivi vijiji 40 ndivyo ambavyo vinabaki na madhila yote ya kuzima moto na mahangaiko yote panapotokea uharibifu ndani ya Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa kutenga 20% mpaka 30% ya mapato ya *KINAPA* au utalii wa Mlima Kilimanjaro kusaidia maendeleo ya vijiji 40 vinavyozunguka mlima kama vile ujenzi wa barabara ambazo zimeharibika sana, lakini vilevile ujenzi wa vyoo katika taasisi za umma ambazo Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, anapigia upatu kwa kiwango kikubwa kuhakikisha kwamba hakuna ukosefu wa vyoo katika shule za sekondari na msingi, lakini pia kukarabati shule za sekondari na msingi katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ndiyo swali langu la pili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza, ninampongeza sana Mheshimiwa Morris Joseph Makoi, Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijijini kwa namna ambavyo kwa kweli anafanya kazi kubwa ya kuwasemea Wananchi wa Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu kwamba Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, siku zote akitoa ahadi na maelekezo yanatekelezwa. Sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tulishachukua agizo la Mheshimiwa Rais la kujenga barabara hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja na tunafahamu tutakwenda kuijenga kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari hivi sasa tumeshaiweka kwenye vipaumbele vya Wizara yetu kupitia *TARURA* kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa awamu ili kuhakikisha kwanza wananchi wanapata huduma bora za usafiri na usafirishaji, lakini pili tunaendeleza na kuboresha huduma za utalii, lakini pia na huduma nyingine kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, ninakuhakikishia barabara hiyo ipo kwenye vipaumbele vya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, ni kweli kwamba Mlima Kilimanjaro unazungukwa na vijiji hivyo takribani 40 na tunafahamu kwamba kuna mashirikiano kati ya wananchi, lakini na taasisi za Serikali na taasisi binafsi. Tunaendelea kuhakikisha kwamba kupitia *TANAPA* na Wizara ya Maliasili na Utalii, tutaendelea kuongea nao na kuwasiliana nao kuona namna nzuri ya kushirikiana katika kuboresha mazingira ya huduma za jamii, barabara, lakini na mambo mengine kwa vijiji hivi ambavyo vinazunguka Mlima Kilimanjaro.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Nilikuona Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali dogo la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza, tunaishukuru Serikali kwa kujenga barabara ya kutoka Vwawa hadi Ndolezi kwa kiwango cha lami. Ni lini sasa Serikali itaendeleza kujenga kuanzia Ndolezi – Mlangali – Shomola – Iyula? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Hasunga amekuwa mfuatiliaji wa karibu sana wa masuala ya jimbo lake la Vwawa lakini pia barabara. Ninakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kama ulivyosema tayari Serikali imeshajenga barabara hiyo, lakini tunafahamu bado tunahitaji kuendelea na ujenzi. Ninaomba nikuhakikishie kwamba safari ni hatua, tunaendelea kutenga bajeti kwa awamu na lengo la Serikali ni kuhakikisha barabara hiyo inajengwa kiwango cha lami, ili kuwezesha wananchi wa Vwawa na maeneo mengine jirani kupata huduma bora za usafiri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali dogo la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mogitu - Balang'dalalu - Lalaji yenye urefu wa kilometa 45 ni barabara yenye msingi sana kwa uchumi wa Wilaya ya Hanang. Je, ni lini Serikali itaanza ukarabati wa barabara hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni kweli kwamba barabara hii ya Mogitu - Balang'dalalu ambayo ipo katika Jimbo la Hanang ambalo lina msemaji mahiri sana Mheshimiwa Asia Halamga, mwakilishi bora kabisa wa wananchi wa jimbo hilo, ameshaleta hoja hiyo mara kadhaa Serikalini. Sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tumeshaiweka kwenye mpango kwa ajili ya ujenzi. Tunafahamu barabara hii haijajengwa muda mrefu na ni barabara muhimu sana kwa shughuli za uchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Hanang' kwamba Serikali hii sikivu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka kipaumbele kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa awamu.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Fadhili Chilombe, swali dogo la nyongeza.

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alivyofika Tunduru alitoa ahadi ya kujengwa Barabara ya Misechela - Tunduru. Barabara hii ni kati ya barabara ambazo zinatoa uzalishaji mkubwa sana wa korosho. Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza ahadi hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kusini amekuwa akifuatilia sana suala la ujenzi wa barabara hiyo na sisi tunafahamu kwamba hiyo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi ahadi za viongozi wetu wa kitaifa ni kipaumbele nambari moja.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kutenga fedha kuhakikisha barabara hiyo inajengwa na dhamira ya Serikali na Mheshimiwa Rais kuwatumikia na kuwahudumia wananchi wa Tunduru inafikiwa.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Marirta Kivunge.

**MHE. MARIRTA G. KIVUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, je, ni lini barabara ya lami ya kutoka Elerai – Kamwanga, Wilayani Longido itaanza kujengwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge na ninaomba tu nimhakikishie kwamba barabara zote za kimkakati ambazo zina umuhimu mkubwa wa shughuli za kiuchumi na kijamii katika halmashauri zetu kote nchini, ikiwemo Halmashauri ya Longido zinaendelea kutengewa fedha kwa awamu ili kuhakikisha kwamba zinajengwa aidha kiwango cha changarawe au kiwango cha lami kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Kwa hivyo, nimkuhakikishie kwamba hiyo barabara itaendelea pia kutengewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kumuelekeza meneja wa *TARURA* Mkoa wa Arusha na Wilaya ya Longido, kuifanyia tathmini barabara hiyo na kuwasilisha mpango kazi ambao wame-*internalize* ndani ya mkoa na sisi ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tuweze kuona namna ya kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa Mvita Mustafa Ali, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 104

**Kuwaendeleza Walengwa wa *TASAF* Waliohitimu Kwenye Uzalishaji**

**MHE. MVITA MUSTAFA ALI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaendeleza...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge unataja tu namba ya swali na unaomba swali lako lijibiwe.

**MHE. MVITA MUSTAFA ALI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaendeleza walengwa wa *TASAF* waliopata ruzuku ya uzalishaji na kutolewa baada ya kuhitimu mpango huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mvita Mustafa Ali, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji na ufuatiliaji wa shughuli za Mpango wa *TASAF* hufanywa na halmashauri husika chini ya uratibu wa *TASAF* ambapo wanufaika wa mpango hupatiwa mafunzo na kufuatiliwa kwa karibu baada ya kuhitimu mpango ili kuhakikisha wanafikia malengo waliojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itahakikisha kuwa walengwa wa *TASAF* waliohitimu mpango baada ya kupata ruzuku ya uzalishaji wanakuwa sehemu ya uchumi endelevu kwa kuwasaidia kujiunga na mifumo ya kifedha, kupata masoko na kuendeleza stadi za ujasiriamali ili kuwabadilisha kutoka walengwa wa ruzuku kuwa wajasiriamali wenye uwezo wa kujitegemea, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mvita Mustafa Ali, maswali ya nyongeza.

**MHE. MVITA MUSTAFA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali langu la kwanza linasema; kuna wanufaika wangapi wanawake ambao wamehitimu katika mpango huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili linasema; je, unaweza kuliambia Bunge hali zao hao wanufaika kiuchumi katika mpango huu kwa ujumla wake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kunusuru kaya maskini ni kuhakikisha kwamba walengwa wanapatiwa uwezo na mwisho wa siku wana uwezo wa kujitegemea. Kwa kufikia hivyo, Serikali imefanya tathmini ya kutosha na kubaini kaya 431,730 ambao tayari wameweza kujitegemea na sasa hawategemei tena ruzuku ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kaya hizo wapo wanawake 757,730 ambao wameweza sasa kusimama na kujitegemea kiuchumi. Hata hivyo, swali lake la pili linasema hali za kiuchumi, hali zao za kiuchumi kwa hawa walengwa ni nzuri na

wanaendelea kuimarika kwa kufuatiliwa kwa karibu na mamlaka za halmashauri za vijiji na mamlaka za halmashauri zetu za mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba walengwa waliohitimu baada ya kuwezeshwa wapo, lakini pale walipowezeshwa basi wameendelea kusimama vizuri.

Mheshimiwa Mweyekiti, ninaendelea kutoa wito na kukumbusha halmashauri zetu nchini kwamba waendelee kufuatilia kaya hizi kwa karibu ili kuhakikisha kwamba zile kaya zinaendelea kuimarika lakini waweze kuwaunganisha na fursa zinazopatikana ndani ya halmashauri ikiwemo mikopo ya 10%; 4/4/2 ili waweze kuendelea kujitegemea kiuchumi badala ya kutegemea ruzuku ya Serikali, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, nilikuona Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali dogo kwa kifupi.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nilitaka kufahamu ni sheria ipi inatumika kuwabana wale wote ambao wanaingiza walengwa *fake* kwenye hii programu ya *TASAF* na wale wananchi wenyewe ambao wanajijua wana uwezo halafu wanaingia kwenye hiyo programu wanachukuliwa hatua gani? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mfumo wa kupata walengwa ambao wanatakiwa kujiunga na *TASAF* ni shirikishi. Wananchi wamekuwa wakishirikishwa kupitia Serikali zao za vijiji na mitaa ili kuwabaini walengwa wenye sifa wa kujiunga na mfumo huo au na mpango ule wa kunusuru kaya maskini. Hata hivyo, yapo maeneo ambayo yamebainika kwamba watu wanaingia kwenye mfumo huo ambao hawana sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kufanya tathmini na kuwabaini na pale inapobainika kwamba mlengwa aliyewekwa kwenye mpango hana sifa basi mara moja anaondolewa kwenye mpango. Pia, Serikali imeendelea kuchukua hatua hasa kwa viongozi wale wa Serikali za Mitaa wakiwepo Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata ambao wamehusika katika kuingiza watu kwenye mpango ambao hawana sifa basi wameendelea kuchukuliwa hatua za kinidhamu na mamlaka zao za utumishi na pale inapotambulika au inapofahamika kwamba kuna njia zilizotumika za rushwa basi wameendelea kuchukuliwa hatua na mamlaka husika zinazoshughulikia masuala mazima ya rushwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Nilikuona Mheshimiwa Maryam Mwinyi, swali dogo la nyongeza na kwa kifupi.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa swali dogo la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzindua Awamu ya Tatu ya Mpango wa Kaya Maskini hapa nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maryam Mwinyi kuwa Serikali kwa sasa imekamilisha, tuko hatua ya mwisho kabisa ya kwenda kuanza Mpango wa Awamu ya Tatu ya Kunusuru Kaya Maskini na mpango huo uko kwenye hatua za mwisho kuhakikisha kwamba tunakwenda kutekeleza ili utekelezaji uanze kwa haraka. Mpango huu wa awamu ya tatu, ni kwenda kuboresha yale mapungufu yaliyojitokeza kwenye awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tayari imeshakamilisha, ni utekelezaji unakwenda kuanza hivi karibuni.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea, sasa namwita Mheshimiwa Dougras Didas Massaburi, Mbunge wa Kivule aweze kuuliza swali lake. Kwa niaba yake.

Subiri Mheshimiwa *microphone* iwake, washa za pembeni.

Na. 105

**Ujenzi wa Barabara ya Msongola – Mbande – Chamazi**

**MHE. DOUGRAS D. MASSABURI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Msongola – Mbande hadi Chamazi kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dougras Didas Massaburi, Mbunge wa Kivule, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Msongola – Mbande (kilometa 7.4) ni sehemu ya Barabara ya Chanika – Mbagala Rangitatu yenye jumla ya kilometa 29.2 ambapo jumla ya kilometa 25.4 zimejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, ujenzi wa kilometa 3.8 zilizobaki katika sehemu ya Msongola – Mbande unaendelea ambapo kwa sasa jumla ya kilometa 1.6 zimewekwa tabaka la lami, kilometa 1.1 zipo kwenye tabaka la kokoto *(CRR)* na kilometa 1.1 zipo kwenye hatua za matabaka ya udongo. Ujenzi wa barabara hii unatarajia ukamilike mwezi Juni, 2026.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dougras Didas Massaburi, maswali ya nyongeza.

**MHE. DOUGRAS D. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa imefanyika kama ambavyo amesema Mheshimiwa Waziri na kwa hakika nakushukuru sana kwa namna ambavyo umekuwa ukipambana na barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la nyongeza, kwa kuwa kipande hicho kinachoanzia Msongola kuelekea Mbande ni kipande ambacho tayari Serikali imekwishaanza kukifanyia kazi, isipokuwa barabara ya kutoka kipande hicho cha Msongola kurudi Kituo cha Polisi kwenda Kwanjomoke kuna vijiji unapita hapo katikati mpaka pale Daraja la Mto Mzinga kwa maana ya *Mvuti Centre*. Barabara ile ni mbovu na imeharibika, imechakaa kabisa hivi sasa imebaki kuwa ni sehemu kubwa ya vumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini mpango wa Serikali hasa ukizingatia maandalizi ya *AFCON* wananchi wengi wanatokea Jimbo la Ukonga kupitia Kata ya Chanika, lakini Jimbo la Segerea hii kwao ni kama sehemu ya *shortcut* rahisi zaidi kuweza kufika kwenye Uwanja wa Chamazi ambao ndiyo unakwenda kufanyiwa mazoezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, jana nilimsikia Mheshimiwa Waziri akiongelea vizuri kabisa kwenye hotuba ile ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mpango wa kuweka taa za barabarani kuanzia maeneo ya kule Mbande, maeneo ya Mbagala, Kisewe mpaka Uwanja wa Chamazi.

Sasa basi Serikali ina mpango gani taa hizohizo mpaka ziweze kutoka kipande hicho ambacho wanajenga Barabara cha Msongola - Kigogo kuelekea mpaka eneo la Mto Mzinga ili kuweza kuweka mazingira yanayovutia zaidi na amani na usalama wa Watanzania wanaoishi Jimbo la Kivule…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa

**MHE. DOUGRAS D. MASSABURI:** ...hususan kwenye Kata ya Msongola? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dougras Didas Massaburi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ninampongeza sana kwa kufanya kazi nzuri ya wananchi wa Kivule na mbili, barabara ya kutoka Kituo cha Polisi kuelekea uelekeo wa Chanika ambayo ameieleza kuwa imeharibika sana, nataka tu kumhakikishia kwamba hivi sasa uelekeo wa upatikanaji wa fedha za kufanya *maintenance* ya barabara ni uelekeo mzuri sana na wakandarasi wetu wa ndani tumeendelea kuwalipa na ninatoa maelekezo kwa Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Dar es Salaam kuipa kipaumbele barabara hii yenye *population* kubwa ya watu ili kuhakikisha kwamba mashimo na migogoro yote ya barabara hii iweze kutatuliwa, na nitakwenda mwenyewe kwa kuwa eneo hilo ni eneo linapita katika eneo la jimbo langu pia. Kwa hiyo, nitakapokuwa nakwenda Mkuranga, nitapita kuona maendeleo ya marekebisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ameuliza swali lililohusu Chamazi – Mbagala Rangitatu kuelekea katika Uwanja wa Azam ambao pia tunayo matumaini ya kwamba utakwenda utumike kwa ajili ya *AFCON*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama jana nilivyoeleza kwa ufupi wakati nikichangia hoja ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba barabara ya kutoka Mbagala Rangitatu – Chamazi – Mbande – Msongola – Chanika na yenyewe imekuwa ni barabara yenye ufinyu mkubwa na msongamano mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo matumaini Uwanja ule wa *Azam Complex* utakwenda kutumika kwa ajili ya mazoezi, ni mpango wa Serikali, tutakwenda kufanya jambo la upanuzi walau barabara hiyo pia iweze kutanuliwa kwa kiwango cha kuongeza hata *lane* moja ili tuweze kupunguza msongamano na tutaweka

na taa za barabarani ili wananchi waweze kupata nafuu ya kupita kwa urahisi na kuona maendeleo ya nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Neema Majule, swali dogo la nyongeza.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kwa muda gani barabara ya kutoka *Kongwa Junction* – Mpwapwa – Kibakwe itajengwa? Barabara hii tumeisubiri sana, Wabunge zaidi ya watatu wamekuwa wakiisemea barabara hii kwa miaka kumi sasa. Tunaomba Serikali itupe majibu ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya *Kongwa Junction* – Mpwapwa ni miongoni mwa zile barabara ambazo zinasubiri upatikanaji wa fedha ili tuweze kumlipa mkandarasi na aweze kufanya kazi. Kama nilivyokwishaeleza jana, msimamo wetu ni kuhakikisha barabara zile zote ambazo ni viporo, uelekeo wa Serikali ni kwenda kuzikamilisha na barabara zile ambazo zote tulishasaini mikataba na makandarasi, ndizo zitakazokwenda kuwa kipaumbele, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Nilikuona Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, swali dogo la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, barabara ya kutoka Kahama inapita Kulole – Chambo mpaka maeneo ya Nzega pale mpakani ni barabara ambayo inaunganisha mikoa miwili ya Tabora pamoja na Shinyanga imeharibika sana na ndiyo uchumi wa mikoa hiyo miwili. Ni lini itaanza kukarabatiwa kwa ajili ya kuwahudumia wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya barabara inayounganisha kati ya Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Shinyanga, ni ukweli kwamba barabara hii ni muhimu katika uchumi wa wananchi na kulingana na hali ya mvua imeharibika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumtoa hofu na nawatoa hofu Waheshimiwa Wabunge wote, Serikali inafanya tathmini ya kina ya barabara zote zilizoathiriwa kwa mvua na tutakwenda kuzifanyia marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalamu wetu wa *TANROADS* wapo kazini, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kila mmoja kwa nafasi yake anijulishe barabara anayoiona kuwa imeharibika sana, tutakwenda kuiboresha ili kutoa unafuu na urahisi kwa wananchi wetu katika shughuli zao za kujitafutia riziki za kila siku. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini aweze kuuliza swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

Na. 106

**Fidia kwa Wananchi Kupisha Mradi wa *Mtwara Corridor***

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO K.n.y. MHE. DKT DAMAS D. NDUMBARO** aliuliza: -

Je, lini Serikali italipa fidia wananchi ili kupisha ujenzi wa barabara ya *Mtwara Corridor*?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Barabara ya *Mtwara Corridor* yaani *Songea Bypass* ni sehemu ya mradi mkubwa wa ukarabati wa Barabara ya Songea – Lutukira (kilometa 100). Serikali imekamilisha uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi huu. Aidha, Serikali imelipa fidia kwa sehemu ya Songea – Lutukira (kilometa 100) na tunaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa sehemu iliyobaki ya *Mtwara Corridor (Songea Bypass)*. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, maswali ya nyongeza.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Kwa kuwa Manispaa ya Songea ina mpango wa kuwa jiji, je, ni lini Serikali italipa fidia na kuanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, barabara za Mlete, Mshangano, Ndilimalitembo na Subira? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Barabara ya Msamala – Mwengemshindo ni barabara muhimu kwa kuwa barabara hii inaelekea katika hospitali ya rufaa inayotoa huduma katika Mkoa wa Ruvuma na nchi jirani ya wenzetu wa Msumbiji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara kwa kiwango cha lami itakayojenga barabara ya Mkoa mzima wa Ruvuma katika eneo hilo linaloelekea hospitali ya wilaya? Barabara za Mwengemshindo ni muhimu sana katika eneo hilo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini yaliyoulizwa na Mheshimiwa

Mbunge wa Viti Maalum kwa niaba yake, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza lini tutalipa fidia, kama nilivyoeleza katika jawabu la msingi kwamba barabara kubwa ya Lutukira – Songea yote kilometa 100 tulishalipa fidia, imebaki sehemu ndogo kwa ajili ya kufanya *bypass*. Naomba kuwaomba Wana-Songea ya kwamba kazi iliyokwishakufanyika ni kubwa na tuko njiani tunakwenda kusaini mkataba na mkandarasi wa kujenga barabara hii muhimu sana ya *bypass* na ya Lutukira – Songea, waandae ngoma ya Lizombe, siku nitakapokwenda pale, tutakwenda kushereheka na kujibu maswali ya jambo hili linalohusu fidia ya wananchi ambayo tuna uhakika kwamba tutailipa ili tuweze kujenga barabara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, barabara inayoelekea hospitali ya wilaya, kama jana ilivyoelezwa hapa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI upande wa *TURURA*, sisi na TAMISEMI tunafanya kazi kwa karibu sana. Tutazungumza na wenzetu ili kuhakikisha kwamba barabara hizi za mitaa zinafayiwa kazi kwa pale Songea ili wananchi waweze kupata huduma za afya hospitalini kwa unafuu, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri nilikuona Mheshimiwa Josephine Kapoma, swali dogo la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ukizungumzia uchumi wa Morogoro huwezi kukwepa Barabara ya Mikumi – Kidatu, na mwezi uliopita tumeshuhudia barabara hii ilikosa mawasiliano kwa zaidi ya siku mbili. Je, sasa ni hatma gani ya Serikali kwa barabara hii ya Mikumi – Kidatu?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Morogoro, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro ni miongoni mwa mikoa ambayo kadri mvua zinavyonyesha, tunashuhudia mkwamo mkubwa sana wa kukatika kwa mawasiliano. Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya kazi kubwa sana kwenye miradi ya dharura ambapo hata mwaka huu tumeshuhudia katika maeneo mengi ya nchi ikiwemo Barabara ya Kusini iliyokuwa maarufu sana kwa kukatika kwa mvua, hatujasikia kelele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uelekeo wetu sasa ni kwenda kuongeza nguvu katika Mkoa wa Morogoro ikiwemo barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge. Tunataka tuondoshe kabisa tatizo la kukatika mawasiliano wakati wa mvua za msimu wa masika ili wananchi waweze kuendelea kufanya shughuli zao za maendeleo ya kila siku bila ya matatizo yoyote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na swali namba 107, sasa namwita Mheshimiwa Cosmas Mtesigwa Bulala, Mbunge wa Kwimba aweze kuuliza swali lake.

Waheshimiwa Wabunge, wengi tumewasha *microphone* naomba tuzime ili aweze kuuliza swali lake.

Na. 107

**Ujenzi wa Barabara kwa Kiwango cha Lami – Mwanza**

**MHE. COSMAS M. BULALA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa Barabara ya Ngudu – Hungumalwa na Ngudu – Mabuki kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cosmas Mtesigwa Bulala, Mbunge wa Kwimba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kiwango cha lami wa Barabara ya Magu – Ngudu – Hungumalwa yenye urefu wa kilometa 71 na Barabara ya Mabuki – Jojiro – Ngudu yenye urefu wa kilometa 25.42 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa awamu ya kwanza, Serikali imeanza ujenzi wa sehemu ya Isabdula – *Bukwimba Station* (kilometa 10) katika Barabara ya Magu – Ngudu – Hungumalwa na utekelezaji wake umefikia 10% na kwa Barabara ya Ngudu – Jojiro – Mabuki ujenzi umeanza kwa sehemu ya Ngudu hadi Kijiji cha Icheja yenye urefu wa kilometa tatu na umefikia 40%. Kwa sehemu zilizobaki, Serikali itaendelea na utaratibu wa kutafuta fedha kwa ajili ya kuhimiza ujenzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Maswali ya nyongeza Mheshimiwa Cosmas Bulala.

Waheshimiwa Wabunge, tuliowasha *microphone* naomba tuzime ili mwenye nafasi ya kuuliza swali lake la nyongeza apate nafasi.

**MHE. COSMAS M. BULALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali, pamoja na majibu hayo ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Wilaya ya Kwimba ndiyo Wilaya pekee katika Mkoa wa Mwanza ambayo haijaunganishwa na Makao Makuu ya Mkoa kwa barabara ya lami na kwa sababu hii, viongozi wakuu wa Serikali katika ziara zao akiwemo Makamu wa Rais alivyofika Hungumalwa mwaka 2023 aliahidi kutujengea kipande cha kilometa 10 kutoka Ngudu kwenda Jojiro mpaka Mabuki na Waziri Mkuu alipofanya ziara yake tarehe 18 Mei, 2025 na wewe Mheshimiwa Waziri ulikuja naye Ngudu, aliahidi pia kutujengea kilometa 10 kutoka Ngudu – Jojiro kwenda Mabuki.

Je, ni upi mpango wa Serikali kutimiza ahadi hizi za viongozi wakuu wa nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mkandarasi *Jossam and Company* amepewa kandarasi ya kujenga kipande cha kilometa tatu katika Mji wa Ngudu kuelekea Icheja, mpaka sasa kazi imesimama kwa sababu mkandarasi hajalipwa fedha yake. Je, upi mpango wa Serikali kumlipa mkandarasi ili aendelee na kazi hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cosmas Bulala, Mbunge wa Jimbo la Kwimba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nampongeza sana anafanya kazi nzuri kwa wananchi wa Kwimba na la pili Mheshimiwa ahadi za viongozi, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote panapo ahadi za viongozi wetu, sisi wasaidizi hatutaangusha ahadi zile, kila ahadi ni sehemu ya mpango wa utekelezaji tulioupanga katika awamu ya bajeti ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ikiwa ni pamoja na hii ahadi ya kutoka Ngudu kwenda Mabuki, uzuri ni kwamba kipande cha barabara kilishakuwa na mkandarasi kwa hiyo tutaendelea. Miongoni mwa ile miradi viporo kuiongezea fedha barabara hiyo ili kilometa za lami zipate kuongezeka sawa na ahadi za viongozi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya makandarasi ni swali la pili la *Comrade* Mheshimiwa Cosmas Bulala, Mbunge wa Kwimba, kwamba ni lini tutamlipa Mkandarasi Jossam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi Jossam ni mmoja katika makandarasi wazawa wanaofanya kazi nzuri sana na wanajitahidi. Hata jana katika malipo ambayo tumeyaidhinisha Mkandarasi Jossam, Mkandarasi Mumangi, Mkandarasi *Kings,* Mkandarasi Samota, Mkandarasi Sumry wote tumewapa malipo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaendelea kulipa malipo ya makandarasi kadri ya fedha zinazopatikana, ikiwa ni

pamoja na mkandarasi anayejenga kule Tunduma, mkandarasi anaitwa Narmo naye ni mzawa jumla ya fedha shilingi bilioni 166 mwezi Januari mpaka jana tumezilipa kwa makandarasi wazawa na ndiyo kipaumbele na msisito wa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Tinnar Chenge, swali dogo la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwa kuwa barabara ya kutoka Bariadi kwenda Lamadi imeharibika sana, je, nini mpango wa Serikali kuitengeneza barabara hii muhimu kwa uchumi wa Mkoa wa Simiyu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana ni ukweli barabara hii kubwa ya Bariadi – Lamadi ikiwa ni pamoja na ile inayotoka Lamadi inayokwenda mpaka Bunda, inayokwenda mpaka Musoma ni miongoni mwa barabara kuu zilizoharibika sana. Ninataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Simiyu, Mheshimiwa Tinnar Chenge kwamba barabara hii ni miongoni mwa barabara tunazokwenda kuzipa kipaumbele kwenye marekebisho tutakayoyafanya kupitia nfuko wetu wa barabara. Waheshimiwa Wabunge na tunao mpango mkubwa mtauona wa kwenda kufanya marekebisho hayo makubwa kwa kuipa nguvu Bodi yeti ya Mfuko wa Barabara ili tufanye matengenezo kwa barabara kuu zote zile za kiuchumi zinazobeba uchumi wa Taifa letu, ikiwemo hii ya Bariadi – Lamadi ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Motto nilikuona, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. ASHA S. MOTTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mtwara kuna mradi mkubwa sana wa barabara inayotoka Mnivata – Nanyamba –

Tandahimba – Newala mpaka Mitesa, barabara hii ina miradi midogo midogo ya ujenzi wa mabweni, stendi na maghala pamoja mizani, je, ni lini miradi hii midogo midogo itaanza kujengwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Asha Motto, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mtwara, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli mradi huu ambao tunaufanya kwa pamoja, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Afrika *(AFDB)* ni mradi mkubwa ambao unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza anataka kujua miradi ile iliyoibuliwa na halmashauri zenyewe. Halmashauri ya Masasi, Halmashauri ya Newala, Halmashauri ya Mtwara – Nanyamba na kadhalika, Tandahimba wao wameibua miradi, wapo waliopendekeza stendi za magari, wako waliopendekeza mabweni ya watoto, mabwalo na hata waliopendekeza matanki ya maji. Tumeshapata makandarasi na tayari wameshaanza hatua za mwanzo, tunakamilisha hatua na mdau wetu wa maendeleo *(AFDB)* muhimu katika *procurement* ili fedha za awali zitoke makandarasi wale wakimbize kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninayo taarifa juu ya kusuasua kwa mkandarasi anayejenga barabara hii ya Mnivata – Newala. Nataka nimwambie aongeze kasi usiku na mchana wakati wowote tutamshukia kama mwewe na tuko tayari hata kumuondosha katika kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale Wabunge wa Mtwara, wawe na hakika ya kwamba Serikali iko macho taarifa tunazo kwamba mkandarasi huyu anazembea na watalamu wangu kuanzia Meneja wa Mkoa, Msimamizi wa Mradi kwa maana ya *Engineer* Mkazi na wengine wafanye kazi yao ipasavyo, wasicheke na

yeyote katika kuhakikisha kwamba barabara hii inafanyiwa kazi kikamilifu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa ni Wizara ya Maji, namwita Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum aweze kuuliza swali lake.

Na. 108

**Kunusuru Uharibifu Wa Vyanzo Vya Maji**

**MHE. MARTHA F. MARIKI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kulinda mabonde na mazingira ili kunusuru uharibifu wa vyanzo vya maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Maji inaendelea na Programu Maalum ya Uhifadhi wa Vyanzo vya Maji inayotekelezwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2035. Lengo la mkakati huo ni kulinda mabonde ya maji na mazingira ili kunusuru uharibifu wa vyanzo vya maji. Utekelezaji wa programu hiyo unashirikisha sekta zinazohusiana na maji pamoja na taasisi zake ambapo utekelezaji wake unafanyika kupitia timu ya kisekta ya Kitaifa iliyoundwa kwa kujumuisha Sekta ya Maji, Kilimo, Mifugo, Maliasili na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia programu hiyo kazi mbalimbali zinatekelezwa ikiwemo kutambua vyanzo vya maji, kuweka mipaka na kuvitangaza vyanzo hivyo kwenye Gazeti la

Serikali, kupanda miti rafiki wa maji kwenye vyanzo vya maji na kufanya kilimo na ufugaji rafiki wa mazingira. Hadi sasa jumla ya vyanzo 3,285 vimetambuliwa ambapo kati ya hivyo vyanzo 359 vimewekewa mipaka na vyanzo 106 vimetangazwa katika Gazeti la Serikali kuwa maeneo tengefu. Aidha, jumla ya miti rafiki milioni sita imepandwa katika vyanzo vya maji pamoja na kujenga mabirika ya kunyweshea mifugo 86 ili kudhibiti uingizaji wa mifugo kwenye maeneo ya vyanzo vya maji na kudhibiti mmomonyoko na uharibifu wa mazingira kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Mariki, maswali ya nyongeza.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uwepo wa sheria, miongozo ya kulinda mabonde na vyanzo vya maji lakini tumeendelea kushuhudia uvamizi katika vyanzo vya maji kinyume na sheria. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na uharibifu huo unaoendelea katika vyanzo vya maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili; upi mkakati wa Serikali wa kuwashirikisha, kuwawezesha wananchi wanaoishi katika maeneo ambayo ni karibu na vyanzo vya maji pamoja na mabonde ili waweze kufanya biashara ambazo zitawapatia kipato ambacho kitatokana na wao kulinda vyanzo vya maji, mfano biashara ya hewa ya ukaa, kilimo cha umwagiliaji badala ya kufanya shughuli ambazo zinaharibu vyanzo vya maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali zuri na la muhimu sana katika mustakabali wa upatikanaji wa maji nchini ambapo vyanzo vya maji ndiyo msingi wa upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa na kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Mbunge anaifanya ni kwa sababu pia ndani ya Mkoa wa Katavi ambapo Mheshimiwa Mbunge anatoka tuna vyanzo takribani 71, hii inaonesha namna gani ameendelea kuona namna gani vyanzo hivi vinahitajika kulindwa ili kuhakikisha kwamba kuwe na uendelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa shughuli za kibinadamu ikiwemo kilimo na ufugaji zimekuwa changamoto sana kwa sababu wengi wamekuwa wakihitaji maji kwa ajili ya kunyweshea mifugo yao, lakini kilimo na hii inatokana na mabadiliko ya tabianchi ambapo unakuta kwamba mvua sasa zinakuwa hazitabiriki, matokeo yake kunakuwa na uvamizi katika vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tumeanzisha kutoa miradi ya kipato kwa jamii hiyo ili kupunguza utegemezi katika vyanzo vyetu vya maji, lakini la pili, tumeendelea kujenga mabirika ili yatumike kwenye kunyweshea mifugo ili wasiweze kuingiza katika vyanzo vya maji; na tatu tumeendelea kutoa elimu kwa umma ili waone vyanzo hivi ni msingi wa upatikanaji wa maji na maji ni afya na maji ni uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la pili, ni kweli kabisa utoaji wa kipato kwa jamii umeonyesha matokeo Chanya, lakini vilevile Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya miradi hiyo ya kijamii ikiwemo biashara ya ukaa lakini pamoja na kilimo cha umwagiliaji lengo ni kuhakikisha kwamba jamii nzima inatambua umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali kupitia dirisha la mabadiliko ya tabianchi tumeendelea kutafuta fedha ili kuhakikisha kwamba wananchi wengi zaidi wanaendelea kufikiwa katika miradi hiyo ya kijamii, lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba tunaepusha vyanzo vyetu vya maji na uvamizi ambao umeendelea kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Serikali tutaendelea kushirikiana na wananchi ili kuhakikisha kwamba vyanzo vyetu vinabaki kuwa salama. *Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali dogo la nyongeza. Waheshimiwa naomba maswali yawe kwa ufupi.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo.

Je, ni lini mkandarasi anayejenga Mradi wa Kihesa – Mgagao, Kata ya Ng'uruhe, Wilaya ya Kilolo atalipwa malipo yake ila wananchi wameusubiri, huu mradi umesubiriwa kwa muda mrefu sana kwa wananchi wa Ng'uruhe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kazi kubwa ya ufuatiliaji wa mradi huo unaofanywa na Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya wananchi wa Kilolo. Mradi huu umeishafikia 90% na tunatambua kwamba Serikali tunatakiwa kuwalipa wakandarasi ili waweze kumalizia, nimtoe hofu mkandarasi huyu tunaenda kumlipa fedha na mradi huu utakamilika ili uweze kutoa matokeo kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Yahya Mhata, swali dogo la nyongeza kwa ufupi.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, katika Jimbo langu la Nanyumbu, Kata ya Sengenya, Kijiji cha Mara kulikuwa na mradi mkubwa wa maji pale mkandarasi amepewa fedha, lakini haonekani katika eneo la tukio. Nini kauli ya Serikali juu ya mkandarasi huyu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji nimwelekeze Katibu Mkuu kumtafuta mkandarasi huyu haraka iwezekanavyo ili tujue changamoto iko wapi, kwa sababu tunapomlipa fedha halafu ni pesa za walipakodi na mradi unasimama hii ni dharau kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie kwamba tutachukua hatua kali kwa wakandarasi wote ambao wameonekana kuwa na tatizo kama hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, sasa namwita Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mbunge wa Mbarali, aweze kuuliza swali lake.

Waheshimiwa tuliowasha *microphones* naomba tuzime ili Mheshimiwa Bahati aweze kuuliza swali lake. *(Makofi)*

Na. 109

**Kukamilisha Mradi wa Maji wa Nyaugenge - Mbarali**

**MHE. BAHATI K. NDINGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mradi wa Nyaugenge ili wananchi wa Kata ya Mapogoro wapate maji – Mbarali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mbunge wa Jimbo la Mbarali, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utafutaji wa fedha za kuanza utekelezaji wa Mradi wa Maji Nyarugenge uliopo Kata ya Mapogoro, Wilayani Mbarali, Mkoani Mbeya. Mradi huo unatarajia kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 3.7 ambapo unalenga kuhudumia zaidi ya wananchi 40,723 waishio kwenye vijiji 11 vya Wilaya hiyo. Miongoni mwa kazi zinazotarajiwa kutekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa dakio, ukarabati wa tanki lenye ujazo wa lita 75,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 36.3 sanjari na ujenzi wa vituo vitano vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupunguza adha ya upungufu wa upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa maeneo hayo, Serikali imekamilisha uchimbaji wa kisima kirefu katika Kijiji cha Mabadaga chenye uwezo wa kuzalisha lita 3,500 kwa saa. Kwa sasa utaratibu za ujenzi wa kioski *(point source)* kwa ajili ya kutolea huduma ya maji kwa wananchi zinaendelea, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bahati Ndingo, swali la nyongeza.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, tunathamini na tunatambua mchakato ambao Serikali mmefanya ya hatua za haraka za kuchimba kisima, lakini kisima kile bado hakijatatua changamoto ya maji kwenye Kata ya Mapogoro. Kwa umuhimu wake kama unavyoona uhitaji wa vijiji 11 matumaini yao ni mradi wa Nyaugenge uanze kazi na tayari mkandarasi amekwishapatikana lakini hajasainishwa mkataba ni lini sasa Serikali kwa unyeti na umuhimu na uhitaji mkubwa wa Wananchi wa Nyaugenge mradi huu utaanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali namba mbili, sisi kwa Wilaya ya Mbarali tulikuwa na bajeti ya shilingi 2,430,000,000 ya kuwalipa wakandarasi. lakini mpaka sasa wakandarasi wamelipwa shilingi milioni 234.4 sawa na 9.7% ya matarajio tukiwa tumebakiza miezi miwili na nusu kufunga mwaka wa fedha, hiyo hali imesababisha Wakandarasi wa Mradi wa Chimala,

Itamboleo, Nyakazombe, Ipwani, Igava na maeneo mengine miradi kusimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwa muda uliobaki miradi hii inakwenda kumalizika? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mbunge wa Mbarali kama ifuavayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninatumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Bahati kwa ushirikiano anaotupatia kwa taarifa, lakini pia kwa uelewa wake wa ufuatiliaji wa miradi ndani ya jimbo lake na kwa kuwatetea wananchi wake wa Mbarali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, niende moja kwa moja kweye mradi huu wa vijiji 11. Mradi huu kwa umuhimu wake na kwa sababu mkandarasi amepatikana na hakuna taratibu zozote zilizokiukwa, na hakuna changamoto ya kisheria, kwa niaba ya Waziri wa Maji, kama mkandarasi amepatikana kwa haki bila kuwa na ukiukwaji wa taratibu zozote, ninamwelekeza kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, Katibu Mkuu - Wizara ya Maji atoe kibali cha kusaini mkataba mara moja ili wananchi wa maeneo ya vijiji 11 wapate huduma ya maji safi na salama bila kuchelewesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna sababu ya kuchukua maamuzi ya haraka ili wananchi wapate huduma hiyo, lakini katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge amesema, eneo la Ilongo, eneo la Chimala, Itamboleo, Igava, Miyombweni, Imalilosongwe, pamoja na uchimbaji wa visima ambavyo amesmea, ni kweli kabisa pesa iliyopelekwa ni shilingi milioni 234.4. Tunakiri na tunatambua umuhimu wa miradi hii kukamilika kwa wakati. Nikutoe wasiwasi, miradi hii na wakandarasi hawa ndani ya kipindi cha mwaka huu wa fedha wataendelea kupatiwa fedha kulingana na zitakavyokuwa zinapatikana. Lengo ni

kwamba miradi hiyo iweze kuendelea, isisimame na matokeo yake iwe tatizo kwa wananchi badala ya kuwa suluhusho la changamoto ya maji katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, nilikuona Edifonsi Kanoni, aulize swali dogo la nyongeza.

**MHE. EDIFONSI J. KANONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaipongeza Serikali kwa kujenga chujio katika Mji wa Matai.

Swali langu, kuna miradi ya maji inayoendelea ambayo imesimama kwa muda mrefu katika Kata ya Legezamwendo, Kata ya Mbuluma, Kata ya Kisumba na Kata ya Mnamba. Lini Serikali itakamilihsa ujenzi wa miradi hii ili wananchi wa Wilaya ya Kalambo waweze kunufaika na miradi ya maji? Shukrani, *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi mingi inayoendelea nchini kote ikiwemo miradi ya Mheshimiwa Mbunge, nimtoe hofu, tunao mkakati wa kuhakikisha kwamba miradi ambayo ipo ukingoni kukamilika ipelekewe fedha kwa haraka ili iweze kukamilika kwa wakati, ianze kutoa matokeo na baadaye mkakati wetu ni kwenda katika miradi ambayo iko katika asilimia katikati kama 50, 60, baadaye tunaeleka fedha inakamilishwa. Baada ya hapo tunaenda kwenye miradi ambayo iko katika asilimia chini ya utekelezaji kabisa, tunapeleka fedha baadaye sasa ndiyo tunaanza utekelezaji wa miradi mipya, lengo ni kwamba tuwe na miradi inayoanza na kukamilika na kutoa

matokeo badala ya kuwa na utitiri wa miradi ambayo haitoi matokeo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Japhael Lufungija, aulize swali lake dogo la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Ichemba ni bwawa pekee linalotegemewa katika Jimbo la Ulyankulu, na ni bwawa linalotegemewa kunufaisha kata tisa pamoja na vijiji 24. Lini mradi huu utatekelezwa ili kuondoa uhaba wa maji katika Jimbo la Ulyankulu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Ulyankulu kaka yangu Mheshimiwa Lufungija kwa kasi kubwa ambayo ameanza nayo ya kuwatetea wananchi wa Ulyankulu, na ninakiri kabisa kwamba leo atakuwa anaongea zaidi ya mara tano kuhusu suala hili, na bahati nzuri tunakaa kwenye *seat* jirani pale, kila siku ananiuliza kuhusu mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu, majibu ya Serikali ambayo nimeshampatia na majibu ambayo amekuwa akiyafuatilia kila siku, ninataka kusema mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba mradi huo hautosimama, utatekelezwa na utakamilika kama ambavyo amekusudia kutatua changamoto ya kumtua mama ndoo kichwani Wananchi wa Ulyankulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Happiness Ngwando.

**MHE. HAPPINESS D. NGWANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Wilaya ya Tunduru pia kuna miradi ambayo haijakamilika

takribani miaka mitatu sasa ikiwepo Misechela, Liwanga, Mchoteka, Masuguru, Tuwemacho, Nakapanya na Namwinyu, lakini Nakapanya wanadai *local fundi* shilingi milioni 52.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini miradi hii itatekelezwa na hawa *local fundi* watalipwa pesa yao kwa kuwa wananchi hawa walipokea miradi hii kwa majani mengi wakiamini watafanyiwa ile kiu yao ya maji itaisha? Ninaomba kujua, ni lini pesa hizi zitapelekwa? Wananchi wa maeneo haya ni wengi sana lakini hawana maji. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na sisi Wizara ya Maji chini ya Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, tumejipanga kuhakikisha miradi yote inaendelea kutekelezwa, kuhakikisha wakandarasi wanaodai fedha wanaendelea kulipwa, kuhakikisha wakandarasi wanapolipwa wanarudi *site* wale ambao wameondoka. Lengo ni kwamba miradi yote iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, mpaka sasa katika vijiji 12,318 tunavyo vijiji 1,575 ambavyo vimebaki bila kuwa na mifumo rasmi ya utoaji wa huduma ya majisafi na salama. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, katika mkakati huo tutahakikisha kwamba miradi ambayo inaendelea ndani ya eneo la Tunduru kama alivyosema na miradi itakayoanzishwa kuhakikisha kwamba tunakamilisha vile vijiji 1,575. Eneo la Tunduru tutalipatia kipaumbele kuhakikisha wananchi wa Tunduru wanapata huduma ya maji safi na salama kwa wakati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Mbwilo Kapunda.

**MHE. BAZILIO K. MBWILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa Serikali tayari ilishasaini mkataba wa kuchimba bwawa kwa ajili ya maji ya wananchi wa Mji wa Namanyere

kuanzia mwaka 2024, je, sasa Serikali iko tayari kumpatia pesa mkandarasi ili aanze kazi hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mkandarasi ameshapatikana na bwawa hili ni la muhimu sana kwa wananchi wa Mheshimiwa Mbunge, na kumbuka kwenye ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tuliweza kuonana na ukaongelea kuhusu suala hili hili la Namanyere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, Serikali tunayo dhamira ya kuhakikisha mradi huu unakamilika. Dhamira hiyo itaendana sambamba na kuhakikisha kwamba tunatoa fedha mradi huu unaanza ili uweze kukamilika na wananchi wako wa Namanyere waweze kupata huduma ya majisafi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini aweze kuuliza swali lake.

Mheshimiwa Koka, sogea pembeni, jaribu kuwasha *microphone* za pembeni. Mheshimiwa Koka, jaribu kuhama upande wa pili.

Waheshimiwa Wabunge, mliowasha *microphone* tafadhali tunaomba mzime wote, tumpe nafasi Mheshimiwa Koka. *(Makofi)*

Na. 110

**Mradi wa Tenki la Maji Pangani Kibaha**

**MHE. SILVESTRY F. KOKA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa Tenki la Maji Pangani, Kibaha baada ya mkandarasi kukabidhiwa eneo la kazi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Jimbo la Kibaha Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi ya Kibaha kwa ujumla wake yanapata huduma ya maji safi na salama kupitia chanzo cha mtambo wa Maji wa Ruvu Juu ambapo upatikanaji wake ni wa kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha huduma hiyo, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa maji unaohusisha ujenzi wa tanki lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni sita katika eneo la Pangani, wilayani Kibaha. Kazi nyingine zinazotekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa kituo cha kupokea na kusukuma maji chenye ujazo wa lita 540,000 sanjari na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 18.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo upo kwenye hatua za awali za utekelezaji na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2027 ambapo unalenga kuhudumia zaidi ya wananchi 6,800 waishio kwenye maeneo ya Pangani, Lulanzi, TAMCO, Mtakuja, Kilimahewa pamoja na Msufini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sylivestry Koka, maswali ya nyongeza.

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wenye thamani ya shilingi bilioni 8.9 ulipokelewa na wananchi hawa wa Mitaa ya Pangani, Lulanzi, Muheza, Shalumumba kwa furaha kubwa Disemba, 2023. Hadi leo ni asilimia nne tu ya mradi iliyotekelezwa.

Sasa swali langu la kwanza, ni lini fedha yote itakabidhiwa kwa mkandarasi ili mradi huu ambao tayari umekwishamaliza miaka mitatu bila utekelezaji kukamilika uweze kukamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Kata ya Viziwaziwa ina tatizo kubwa la maji na tayari kuna mpango wa Mradi wa Tenki la Maji wa shilingi bilioni 6.5.

Ni lini sasa Serikali itapeleka fedha ili mradi huu uweze kutekelezwa, wananchi hawa wa Viziwaziwa katika Manispaa yetu ya Kibaha waweze kupata maji, wasiwe ni watazamaji wa maji kuelekea Dar es Salaam? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na napenda kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, Mbunge mahiri kabisa, Mbunge ambaye amekuwa akiwatetea wananchi wa Kibaha Mjini kwa awamu ya nne sasa, ambapo ameonesha umahiri kwa kuwasemea na sisi Serikali tunamwahidi ushirikiano katika awamu yake hii ya nne, na tunahakikisha kwamba miradi iliyoko katika jimbo lake inaendelea kutekelezwa kwa umakini na kwa ubora unaohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, tunao mradi wa shilingi bilioni 8.9, lakini pia hatulipi fedha kwa pamoja. Tunalipa fedha inafikia hatua fulani mkandarasi analeta hati ya madai kulingana na kazi iliyofanyika, Serikali inamlipa. Baada ya hapo anaendelea na kazi, analeta tena hati ya madai tunamlipa. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, mkandarasi atakapokuwa anawasilisha hati za madai, Serikali itaendelea kumlipa ili aweze kuendelea na hatua zinazofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kuhusiana na kata ambapo kuna ujenzi wa mradi wa shilingi bilioni 6.5. Nimtoe hofu pia kwamba Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo tumekuwa na maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba miradi yote ambayo tumeshaianzisha ni lazima ikamilike,

tumtoe hofu tutaendelea kupeleka fedha kwa kadlri zitakavyopatikana ili malengo yetu yaweze kutimia, na malengo ya wananchi wa Mheshimiwa Koka yaweze kutimia kwa kupata huduma ya majisafi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Zuberi Mfaume, swali dogo la nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge nitakaowapa nafasi ninaomba maswali yawe mafupi.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni lini sasa mkandarasi atarudi *site* katika mradi mkubwa wa shilingi bilioni tano wa Kibana ulioko katika Tarafa ya Matombo, Jimbo la Morogoro Kusini? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuberi Mfaume kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi ambaye hayuko *site* tunatambua kulikuwa na changamoto ya malipo na tumeshaanza ku-*engage* naye. Nimtoe hofu, tunaamini kwamba ndani ya muda mfupi tutakuwa tumefikia mwisho wa mazungumzo na mkandarasi ataweza kuendelea na kazi. Lakini pia, tutahakikisha kwamba madai yake tunaanza kuyalipa japo angalau kwa kuanza kidogo kidogo ili aweze kurejea *site* na kufanya kazi ili mradi usisimame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Ghati Chomete, swali la nyongeza.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ya swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa Miji 28 wa Tarime – Rorya wa shilingi bilioni 134 ambao ulikuwa ukamilike mwaka 2025, mpaka sasa mradi ule uko 15% na mkandarasi haendelei na kazi kwa sababu ya malipo.

Je, ni upi mkakati mzuri wa Serikali kwa kuhakikisha fedha hizo zinakwenda ili akinamama wa Rorya, akinamama wa Tarime Vijijini na Mjini waweze kunufaika na mradi huo? Ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Ghati, Mbunge kutoka Mkoa wa Mara, Mbunge mahiri kabisa, anawapambania akinamama wa mkoa mzima wa Mara, na sisi Serikali tunafahamu dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inamtua mama ndoo kichwani na ndiyo maana Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri kabisa wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ilichukua maamuzi mazito kabisa ya kuwekeza zaidi ya shilingi bilioni 134 kwa ajili ya wakazi wa Rorya na wakazi wa Tarime, lakini vilevile mradi huo huo kwa baadaye tutakuja kuutegemea kwa ajili ya Mugumu kule Serengeti, ili uweze kusaidia katika mradi mwingine ule mdogo wa shilingi bilioni 21 unaoendelea pale Mugumu Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu, Serikali imejidhatiti, kama ambavyo nilisema hapo awali, tunao mpango wa kuanza kuhakikisha kwamba mradi mmoja baada ya mwingine tunaupelekea fedha ili iweze kukamilika. Hatuna sababu ya kuwa na miradi ambayo haiendelei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu mkandarasi huyo atarudi *site* baada ya kuwa tumeongea naye, lakini pia kikubwa tuendelee kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge na tuwe na subira. Mradi huu ni mkubwa sana ambao unahitaji mambo mengi sana yafanyike kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, Kata za Itonjanda, Ndevelwa, Ifucha na Ntalikwa, ni kata ambazo ziko pembezoni kabisa mwa Jimbo la Tabora Mjini. Serikali iliamua kujenga magati ya maji kwa ajili ya wananchi hao, lakini magati hayo hayatoshelezi kabisa wananchi waliopo kwenye kata hizo.

Nini mpango wa Serikali kutenga bajeti ili kuweza kuongeza magati ya maji kwa wananchi wa kata hizo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa, Mbunge wa Tabora Mjini na ninampongeza sana dada yangu Mheshimiwa Hawa kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya pale Tabora Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka amekuwa akisemea kuhusu hizi kata za pembezoni, lakini pia tumeshatoa maelekezo kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora Mjini kufanya tathmini ili tuweze kujua kwamba tunahitaji kuongeza magati ama tunahitaji kuongeza mtandao wa maji ili wananchi waunganishiwe moja kwa moja majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huo ndiyo utatoa picha ya nini kifanyike ili Serikali sasa iweze kutenga bajeti na kwenda kutatua tatizo la wananchi wa Mheshimiwa Hawa. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Abubakar Omari.

**MHE. ABUBAKAR A. OMARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Manonga ninapenda kuuliza, mradi wa maji wa Ziwa Victoria kutoka Nkinga – Mwisi – Chabutwa – Nsimbo umesimama ambao ulikuwa ukamilike Aprili mwaka jana na umesimama mpaka sasa

hivi ukiwa katika 10% tu ya mradi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuendelea na mradi huo ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata maji safi na salama? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji mzuri wa mradi huu. Kwanza kabisa mradi huu hauwezi kusimama, nimtoe hofu, lakini vilevile, mradi huu tunao mpango wa kuhakikisha kwamba unapelekewa fedha ili uweze kuendelea na tunafahamu kwamba mradi huu ulitakiwa kukamilika mwaka jana, lakini kulikuwa na changamoto za mtiririko wa fedha, lakini mpaka sasa tumeuweka kwenye vipaumbele vyetu vya Wizara ya Maji kuhakikisha kwamba mradi huu unapelekewa fedha na unakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Abdallah Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, Mradi wa Makonde ambao ulitakiwa kukamilika mwaka jana, kwa sababu ni miongoni mwa miradi ya miji 28 hadi sasa umetekelezwa kwa 36% tu na changamoto zinazokabiliwa na mkandarasi huyu wa Serikali nazifahamu ikiwemo kutokulipwa kwa wakati.

Je, Serikali inampango gani wa kumaliza changamoto hizo ili mkandarasi akamilishe mradi huu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Chikota, Mbunge kwa kuendelea kuusemea mradi huu wa Makonde, lakini pia natambua changamoto ambazo zimekuwepo, labda nimtoe hofu kwamba tunazo hatua nzuri sana, tumefikia katika mazungumzo na mkandarasi huyu. Nimtoe hofu tutakapomaliza

mazungumzo naamini kwamba mkandarasi huyu atarudi *site* na ataanza kuutekeleza mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mradi umefikia hatua ambayo ni nzuri kabisa kwa sababu asilimia kubwa ya mradi ule ni mabomba na *structure* zenyewe ambazo zimeshakamilika, kwa hiyo akisharudi kazi iliyobaki ni ya miezi michache inakuwa imekamilika.

Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, tunalifanyia kazi kumaliza changamoto za mkandarasi wetu, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea ninaomba kuwataarifu kuwa Mheshimiwa Dkt. Jumaa Hamidu Aweso, anakaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea, sasa ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, namwita Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, Mbunge wa Mwanakwerekwe, aweze kuuliza swali lake. *(Makofi)*

Na. 111

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi na Uhamiaji– Mwanakwerekwe**

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Polisi na Uhamiaji Mwanakwerekwe kwani vilivyopo ni chakavu na vinatoa huduma kwa majimbo matano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la

Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, Mbunge wa Mwanakwerekwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kujenga upya Kituo cha Polisi na Uhamiaji Mwanakwerekwe, hii ni kutokana na vituo hivyo kuchakaa sana na eneo vilipo kuna mpango mkubwa wa uendelezaji wa miji. Kazi ya ujenzi huo inatarajia kutekelezwa kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Zanzibar katika mwaka wa fedha 2026/2027. Aidha, wakati wa ujenzi huo wananchi wataombwa kupata huduma katika vituo vya polisi vya karibu kama vile Magogoni, Mwembe Madafu na kwa upande wa Uhamiaji katika jengo jipya la Uhamiaji lililopo Mazizini ambalo kwa sasa lipo kwenye hatua za mwisho kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, swali la nyongeza.

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa eneo la Mwanakwerekwe, limepanda hadhi baada ya kujengwa *flyover* na vituo vingi vya Serikali kuwekeza katika jimbo hilo la Mwanakwerekwe, je, hamuoni sasa kuna haja ya kufanya eneo hilo kuwa Kanda Maalum ya Kipolisi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. nimshukuru sana Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, kwa namna anavyofuatilia kwa karibu shughuli za maendeleo katika eneo lake la Jimbo la Mwanakwerekwe, lakini na ukanda mzima wa eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la haja na hoja ya Kanda Maalum ya Kipolisi au ya Kiusalama, nilieleza jana kwamba itategemea na hali halisi ya mambo makuu matatu na kati ya

hayo nilieleza moja ni la kiulinzi; la pili la kiutawala na jambo la tatu ni suala la miundombinu.

Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuangalia umuhimu wa namna gani ya kulitazama upya eneo hilo na ikiwa kutatokezea haja ya kufanya hivyo na hoja zikijitosheleza basi itakuwa tayari kuweza kutekeleza mapendekezo hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, swali dogo la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili nimekuwa nikiuliza mara kwa mara; Wilaya ya Maswa ni wilaya kongwe, ya kwanza kabisa katika Mkoa wa Simiyu, haina kituo cha polisi. Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi Wilaya ya Maswa? Naomba Serikali ije na majibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nimshukuru sana Mheshimiwa Esther, kwa suala lake hili muhimu na kama alivyoeleza, amekuwa akiliuliza mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba zipo wilaya kama nilivyoeleza wakati nikitoa majibu ya msingi jana kwamba karibu wilaya 75 ama majengo yake ni machakavu au hazina kabisa majengo yenye hadhi ya wilaya na Serikali kupitia Jeshi la Polisi tunaendelea na hatua za kuweza kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Polisi wa Daraja la "B" kwa maana ya ngazi ya wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

Waheshimiwa tunaendelea na swali letu la mwisho, linaulizwa na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 112

**Uhitaji wa Gari la Zimamoto – Mbulu Mjini**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka gari la zimamoto Mbulu Mjini?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na jitihada mbalimbali za kuliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kulipatia vitendea kazi vya kisasa kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wananchi. Aidha, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji tayari limepeleka gari jipya la zimamoto na uokoaji aina ya *IVECO 189* lenye ujazo wa maji lita 5,000 na lita 500 za *foam* litakalotoa huduma katika maeneo ya Mbulu Mjini na maeneo mengine yaliyopo ndani ya wilaya hiyo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa jitihada zake, ombi la gari hili lilidumu kwa miaka mitatu na sasa gari limepelekwa. Ninatoa shukrani za dhati kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni moja; kwa kuwa sasa gari limeshapelekwa na Wilaya ya Mbulu ni wilaya kongwe, je, Serikali inamkakati gani wa kuwajengea Ofisi ya Zimamoto katika Wilaya ya Mbulu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nimshukuru sana Mheshimiwa Zacharia, kwa hoja yake hii ya msingi ya kwamba kwa kuwa sasa tumepeleka gari, kwa hiyo kituo tuna mpango gani kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Serikali ina mkakati wa kuhakikisha kwamba kila wilaya nchini ikiwemo Wilaya ya Mbulu inajengwa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji. Katika hali ya sasa tunaendelea kutenga bajeti katika kila mwaka ili kuendelea na zoezi hilo la ujenzi wa vituo katika maeneo mbalimbali ya mikoa na wilaya. Hata hivyo kwa upande wa eneo la Wilaya ya Mbulu, kwa sasa bado Jeshi la Zimamoto halina kiwanja cha kujenga jengo hilo la ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa na Jeshi la Zimamoto ni kupitia Afisa wetu wa Zimamoto na Uokoaji wa Wilaya ya Mbulu, tayari ameshaandika barua kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo ili kuweza kupatiwa kiwanja na hatimaye kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa Kipindi chetu cha Maswali na Majibu. Sasa nichukue fursa hii kuwatambulisha wageni waliopo nasi siku ya leo Bungeni.

Kwanza ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika, ambao ni wageni wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uwekezaji na Mipango, ambao ni Mheshimiwa John Mongella, Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi Bara, karibu sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Wageni wengine ni Dkt. Fred Msemwa, Katibu Mkuu Uwekezaji; Ndugu Nehemiah Mchechu, Msajili wa Hazina; Dkt. Blandina Kilama, Kaimu Katibu Mtendaji Tume ya Taifa ya Mipango; na Balozi Dkt. Azizi Ponary Mlima, Mwenyekiti wa Bodi *(TISEZA)*. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Gilead Teri, Mkurugenzi Mtendaji Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi *(TISEZA);* yupo pia Profesa Lucian Msambichaka, mgeni maalumu wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Bernard Konga, Mkurugenzi wa Sera na Mipango; tunaye Ndugu Fadhili Chilumba, Mkurugenzi Uwekezaji Sekta Binafsi, Wizara ya Mipango; Tunaye Ndugu, Elikana Mtumweni, Mkurugenzi Uwekezaji Sekta ya Umma Wizara ya Mipango; na tunaye Ndugu Baraka Eligaesha, Mkurugenzi Kitengo cha Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara na Usajili, Wizara ya Mipango. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Lightness Mauki, Mkurugenzi Msimamizi Utendaji wa Taasisi za Biashara, Ofisi ya Msajili wa Hazina; tunaye Ndugu David Shambwe, Mkurugenzi Usimamizi wa Utendaji wa Taasisi Zisizo za Biashara, Ofisi ya Msajili wa Hazina; tunaye Ndugu Emmanuel Luvanda, Mkurugenzi wa Mipango Taifa na Maendeleo Ofisi ya Msajili wa Hazina; tunaye Ndugu Benjamini Chilumba, Mkurugenzi Utawala na Usimamizi Rasilimali Watu, Tume ya Taifa ya Mipango; na tunaye Ndugu Salome Kingdom, Mkurugenzi wa Ufuatiliaji, Tathimini na Usimamizi wa Utendaji Kazi, Tume ya Taifa ya Mipango. *(Makofi)*

Tunaye Profesa Henry Mosha ambaye ni Mwalimu wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, sasa ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambaye ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi wa Wilaya ya Ruangwa na viongozi wa wazee wa Ruangwa, mkoani Lindi, karibuni. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 11 wa Mheshimiwa Kaspar Mmuya, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu Dodoma wanaotoka Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi, wakiongozwa na Mwalimu Abduly Kitani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Athumin Omary Mapalilo, Ndugu Christopher Mpenga kutoka mkoani Mtwara. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, ambao ni Shirika la Kusimamia Watoto Wenye Changamoto za Ulemavu kutoka Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Baraka Ulimboka ambao ni wanafunzi na wafanyakazi kutoka mkoani Mbeya. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Pascal Lucas Lutandula amabo ni viongozi wa Chama cha Ufugaji Tanzania kutoka Chato, mkoani Geita. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, ambao ni viongozi sita wa Jumuiya ya Wanafunzi na Vijana wa Kiislamu nchini kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 50 wa Umoja wa Vijana wa Chama Vha Mapinduzi, tawi la Chuo Kikuu Jordan kutoka mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Tunao wanachama 100 na viongozi wawili wa Taasisi ya Timu Ushindi Tanzania kutoka jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wetu wote karibuni sana.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo mbele ya Bunge lako tukufu, ikiwa ni taarifa ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na taarifa ya Mwenyekiti wa Kamti ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kukutana tena katika Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Tatu. Ni kwa neema na rehema zake tu kwamba leo hii nimepata fursa ya kuwasilisha hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ya mwaka 2026/2027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni hotuba yangu ya kwanza ya bajeti tangu nilipoteuliwa kufuatia uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kuniteua tena kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Ninamuahidi kumrudishia imani hii kwa kuwa mtiifu kwake, kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Chama Cha Mapinduzi na kwa kuchapa kazi kwa bidii na maarifa ili kutimiza maono yake ya kuiona Tanzania ikiwa Taifa jumuishi lenye ustawi, lenye haki na Taifa linalojitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninamtakia Mheshimiwa Rais, afya njema, amani, utulivu na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa majukumu yake makubwa ya kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi njema anayoifanya katika kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu ya kuijenga Tanzania yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ninamtakia mafanikio makubwa katika kuendelea kuijenga Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kwanza kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Kumi na Mbili wa Tanzania; pili kwa kuanza kazi vizuri, hili tunaliona kwa usimamizi mzuri wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni na ziara ambazo zimezidi kuimarisha imani ya wananchi kwa Serikali yao, lakini tatu nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri ya bajeti ya ofisi yake na ambayo aliiwasilisha kwa umahiri mkubwa. Hotuba hiyo imejenga msingi wa hotuba za bajeti za Wizara ikiwemo hotuba ambayo naiwasilisha leo hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kwanza kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Mbunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pili kwa jinsi alivyoanza kazi yake vyema katika kuliongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa na tunajionea hata vifaa vya kisasa kabisa vya kuongelea, kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha ninampongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninawatakia kila la heri katika kuendelea kulifanya Bunge letu kuwa chombo imara cha kutunga sheria, kuisimamia Serikali na kuwakilisha wananchi kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri wote kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara mbalimbali wanazozisimamia. Ninawaahidi ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yetu. Kipekee, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge waliopo hapa kwa kuchaguliwa na wananchi kuwa wawakilishi wao hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapohitimisha shukrani zangu ninaomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya uongozi mahiri na makini wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo; Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle – Makamu Mwenyekiti; na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa michango, ushauri na miongozo waliyotupatia wakati maandalizi ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Aidha, ninamshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leornad kwa ushirikiano wake kupitia wasaidizi wake wanaomsaidia katika Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana kwa masikitiko makubwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kufuatia kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu na Mbunge wa Jimbo la Isimani; Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa

Jimbo la Peramiho na Mheshimiwa Halima Idd Nassor, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Tutaendelea kuwakumbuka kwa mchango wao katika kulitumikia Taifa. Tunaendelea kumuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha hoja yangu mbele ya Bunge lako Tukufu. Hoja yangu imegawanyika katika maeneo makubwa manne; kwanza, nitatoa Taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi kwa mwaka 2025/2026; pili, nitatoa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka huo na tatu, nitawasilisha Mapendekezo ya Vipaumbele na Mpango Kazi kwa mwaka 2026/2027 na nne, nitawasilisha Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango Kazi kwa mwaka 2025/2026; katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali ilikamilisha maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo na kuzinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 17 Julai, 2025 Jijini Dodoma. Aidha, Serikali ilikamilisha maandalizi ya nyenzo muhimu za utekelezaji ambazo pia Bunge lako Tukufu liliidhinisha, nyenzo hizi ni Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Taifa, Mwongozo wa Ufuatiliaji, Tathmini, Kujifunza na Uwajibikaji na nne, Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati, Tume ya Taifa ya Mipango imeandaa Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Mipango ya Maendeleo *(National Development Plans and Project Management Information System)* ambao utawezesha upangaji, uchambuzi, ufuatiliaji na tathmini pamoja na ufungaji wa utekelezaji wa miradi kufanyika kidijitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwahimiza Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mashirika na Taasisi zote za umma kuwasilisha programu na miradi ya maendeleo kupitia mfumo wa huu, kuanzia tarehe 1 Julai, 2026, Tume ya Taifa

ya Mipango haitapokea wala kuchakata taarifa zozote za miradi ya maendeleo ambazo hazijapitia katika mfumo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga utamaduni wa kufanya maamuzi kwa kuzingatia ushahidi wa kisayasi, Tume ya Taifa ya Mipango imeandaa Ajenda ya Taifa ya Utafiti *(Research Agenda)* ya mwaka 2026/2027 hadi 2030/2031 kwa lengo la kutoa mwongozo wa taasisi za umma na binafsi katika kufanya utafiti utakaowezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uwekezaji wa sekta binafsi; kwa mujibu wa taarifa ya hali ya uwekezaji ya Dunia ya *UNCTAD* ya mwaka 2025 (*World Investment Report 2025),* Tanzania imeendelea kuimarisha utendaji wake wa mtiririko wa uwekezaji, ambapo uwekezaji kutoka nje ulifikia dola za Marekani bilioni 1.72 mwaka 2024, ukilinganisha na dola bilioni 1.34 mwaka 2023, sawa na ukuaji wa 28.3% katika kipindi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa hii katika ukanda wa Afrika Mashariki, Tanzania ilishika nafasi ya tatu kwa kuvutia uwekezaji kutoka nje, ikiwa nyuma ya Ethiopia iliyovutia dola bilioni 3.98, na Uganda yenye dola bilioni 3.31 na ikafuatia Tanzania ikiwa mbele ya Kenya na Rwanda. Kwa ujumla, taarifa inaonesha kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye ukuaji wa haraka wa uwezekaji Barani Afrika ikiwa imeshika nafasi ya 11 kwa ukubwa kwa mitaji kutoka nje *(foreign direct investment)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, kiwango halisi cha mitaji ya uwekezaji kutoka nje kimeongezeka kutoka dola za Marekani milioni 944 mwaka 2020 hadi kufikia dola bilioni 1.72 mwaka 2024, ikiwa ni ongezeko la 45.1% katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia taarifa ya uwekezaji wa mwaka 2023, sekta zinazoongoza kwa uwekezaji kutoka nje ni madini, uzalishaji viwandani, fedha na bima na habari na mawasiliano ambazo kwa pamoja zilichangia 82.4% ya uwekezaji wote nchini kwa kipindi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa usajili wa miradi ya uwekezaji, hadi mwezi Machi, 2026, Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi *(TISEZA)* ilisajili jumla ya miradi mipya 611 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 6.2 ambayo inatarajiwa kuzalisha ajira mpya 102,463. Aidha, kumekuwepo na miradi ya upanuzi 45 yenye thamani ya dola za Marekani milioni 586.12 ambayo inatarajiwa kuzalisha ajira mpya 9,472. Sekta zilizoongoza kwa usajili wa miradi hiyo ni uzalishaji viwandani kwa 47.4%; usafirishaji kwa 13.1%; ujenzi wa majengo ya biashara kwa 12.0%, Utalii kwa 10.2%; kilimo kwa 7.8% na Mikoa inayoongoza kwa kuvutia uwekezaji ni Dar es Salaam 34.8%; Pwani 21.2%, Arusha 7.3%; Mwanza 4.1%; na Dodoma 4.1%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji imeendelea kuhamasisha na kuwezesha uwezekeshaji katika Kanda Maalum za Kiuchumi *(Special Economic Zones - SEZ)* na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya miradi 19 ilisajiliwa na kupewa leseni ya uendeshaji na ya uendelezaji. Miradi hii ina thamani ya dola za Marekani milioni 331.51 ambayo inategemewa kuzalisha ajira 11,762, na mauzo ya nje yanayokadiriwa kufuikia dola za Marekani milioni 885.23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza msukumo wa uwekezaji katika *Special Economic Zones (SEZ), TISEZA* imebainisha maeneo matano ya kimkakati na kuweka vivutio maalum visivyo vya kikodi. Maeneo hayo ni *Bagamoyo Eco-Maritime City* yenye hekta 152, Nala-Dodoma yenye ukubwa wa hekta 607, Kwala-Kibaha yenye hekta 40.5, Buzwagi-Kahama yenye hekta 1,333, na Upanuzi wa *Benjamin William Mkapa Special Economic Zone* – Mabibo-Dar es Salaam yenye hekta 1.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2025 *TISEZA* ilisajili miradi 915 yenye thamani ya dola za Kimarekani bilioni 10.95, ikiwa ni rekodi mpya ya kusajili miradi mingi zaidi nchini tangu kuanzishwa kwa utaratibu wa kusajili miradi ya uwekezaji mwaka 1996. Kwa ujumla wake, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita idadi ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa na *TISEZA* imeongezeka kutoka miradi 256 mwaka 2021 hadi miradi 915 mwaka 2025, ikiwa ni ongezeko la 257.4% katika kipindi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza utaratibu mpya wa kuchakata takwimu za uwekezaji unaofanywa na kampuni za Kitanzania nje ya nchi *(outward investment)*. Takwimu za awali zinaonesha kuwa zaidi ya dola za Marekani bilioni 3.1 zimewekezwa nje kupitia makampuni za Kitanzania. Uwekezaji huu umefanyika katika nchi mbalimbali zikiwepo; Kenya, Uganda, Rwanda, Sudani Kusini, DRC, Zambia, Zimbabwe, Malawi, Msumbiji, Afrika Kusini, Japan, Korea Kusini, Qatar na Oman. Hatua hii ni muhimu katika kukuza diplomasia ya kiuchumi na katika kuyawezesha makampuni ya Kitanzania kuongeza wigo wa bidhaa zake katika soko la nje, kuwa shindani zaidi na kuwezesha uhaulishaji wa teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa sekta binafsi nchini ni kielelezo kuwa mazingira ya biashara na uwekezaji yanaendelea kuimarika. Hatuna budi kuwashukuru na kuwapongeza *champions* wetu wa uwekezaji nchini ambao wamekuwa chachu kubwa ya kuvutia wawekezaji. Hawa ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado tuna fursa ya kukuza uwekezaji kwa kuendelea kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kuimarisha huduma kwa wawekezaji nchini *TISEZA* imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma katika Kituo cha Pamoja cha Uwezeshaji Uwekezaji *(One Stop Facilitation Centre)*. Pamoja na hatua nyingine Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imepandisha hadhi afisa wake katika kituo hiki kwa kumteua Kamishna Msaidizi wa Ardhi mwenye hadhi sawa na Kamshna wa Ardhi wa Mkoa ambaye pamoja na mamlaka mengine atakuwa na mamlaka kamili ya kutoa hati ya umiliki wa ardhi na hivyo kupunguza usumbufu kwa wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza wigo wa utoaji wa huduma kwa wawekezaji, Serikali imeandaa mwongozo wa

watoa huduma kwa wawekezaji *(Investor's Service Provider*). Mwongozo huu umeweka vigezo na masharti kwa mtoa huduma. Hadi sasa zaidi ya watoa huduma 100 wamesajiliwa na kupata mafunzo ya namna ya kuwezesha uwekezaji na kutangaza fursa mbambali za uwekezaji zilizopo nchini. Orodha ya watoa huduma hawa itawekwa kwenye tovuti na matangazo mbalimbali kwa ajili ya kuongeza uwazi na uwanda mpana kwa wawekezaji katika kuwachagua watoa huduma hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwawezesha vijana na wawekezaji wenye mitaji midogo *TISEZA* ilizindua Kituo cha Usaidizi wa Upatikanaji wa Vifaa/Bidhaa na Mauzo ya Nje mwezi Machi, 2026 katika Ofisi zilizopo *Benjamin Mkapa Special Economic Zone*, Mabibo – Dar es Salaam. Kituo hiki kimeanzishwa kwa ushirikiano kati ya *TISEZA* na Kampuni ya *Nexa International Centre*. Kituo hiki kinatoa huduma maalum kwa kipaumbele kwa wawekezaji wadogo na vijana, pamoja na wawekezaji wanaohitaji msaada katika kukuza shughuli zao za biashara na uwekezaji. Aidha, kituo kinalenga kuwezesha upatikanaji wa mitaji, masoko ya nje kwa bidhaa zinazozalishwa nchini, kurahisisha usafirishaji wa mizigo kuingia na kutoka nchini, pamoja na kuwezesha upatikanaji wa malighafi, mashine na vifaa muhimu kutoka kwa vyanzo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji wa umma; uwekezaji wa wa Serikali katika mashirika, taasisi, wakala za Serikali na kampuni zinazomilikiwa kwa hisa chache umeongezeka kutoka shilingi trilioni 85.38 mwaka 2023/2024 hadi kufikia shilingi trilioni 90.61 kwa mwaka 2024/2025 ikiwa ni sawa na ongezeko la 7%. Aidha, kwa upande wa uwekezaji wa Serikali nje ya nchi, hadi kufikia mwaka 2024/2025, ulifikia shilingi trilioni 1.67, kutoka shilingi bilioni 846.22 mwaka 2023/24 ikiwa ni sawa na ongezeko la 98%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sehemu ya kuendelea kuboresha utendaji wa mashirika ya umma, Serikali imeendelea kufanya tathmini ya utendaji na majukumu ya mashirika yao. Lengo la hatua hii ni kubaini mashirika ambayo majukumu yake yamepitwa na wakati, mashirika ambayo yanaingiliana kimajukumu na yale ambayo yamegeuka kuwa mzigo kwa walipa kodi au kukwaza ukuaji wa biashara nchini. Matokeo ya

tathmini hii inaiwezesha Serikali kuchukua hatua stahiki ikiwemo kufuta mashirika yanayobainika kuwa uwepo wake hauna tija na kuunganisha mashirika ambayo majukumu yake yanagongana, kuingiliana na kufanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia tathmini ya utendaji na majukumu ya wa mashirika ya umma iliyofanyika mwaka 2023 Serikali ilielekeza kuunganishwa kwa mashirika ya umma 14 na kufuta mashirika mengine matatu. Hadi sasa mashirika matatu yalishafutwa na mashirika mawili kuunganishwa ambayo ni *TIC* na *EPZA* ambayo ilikuja ikaunganishwa na kuunda *(TISEZA)*. Serikali inaendelea na kukamilisha taratibu za kisheria kuunganisha mashirika yaliyobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Msajili wa Hazina imefanya uthamini wa mali mbalimbali zilizorejeshwa Serikalini, zikiwemo kiwanda kimoja cha *Tembo Chipboards,* mashamba matatu ya maua yaliyopo Arusha ambayo ni Malalua*, Kili Flora Chekereni* na *Kili Flora Usa River*, shamba la Basuto lililopo Manyara, mashamba manne ya *NAFCO* yaliyopo *West Kilimanjaro* pamoja na shamba la *KPL* Mngeta lililopo Morogoro. Zoezi hili litaiwezesha Serikali kutafuta wawekezaji wenye tija katika mashamba na viwanda hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Msajili wa Hazina imesimamia ubinafsishaji wa viwanda sita vilivyorejeshwa Serikalini ambavyo ni *NMC Mzizima*, *NMC Isaka*, *CDA Integrated Industry Limited, Kilimanjaro Paddy, Moshi Pesticides* na *Unique Steel Rolling*. Taratibu za kisheria za ukamilishaji mchakato wa ubinafsishaji unaendelea kwa kuzingatia taratibu na sheria husika ili kuhakikisha Serikali inanufaika ipasavyo na mali hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji; Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji imeratibu utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI). Kupitia mpango huu, Serikali ililenga kuondoa vikwazo vinavyokwamisha uanzishwaji na uendeshaji wa biashara kwa kufanya mapitio ya sheria na kanuni ambazo siyo rafiki kwa biashara, kupunguza au kufuta tozo na ada zenye kero kwa wafanyabiashara, kuondoa mwingiliano wa majukumu

miongoni mwa taasisi za udhibiti, pamoja na kuanzisha na kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya utoaji huduma ili kuongeza ufanisi, uwazi na urahisi wa kufanya biashara nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Serikali ilifanya mapitio ya jumla ya sheria 28 zilizokuwa zinazorotesha mazingira ya biashara sambamba na kufuta au kupunguza jumla ya tozo na ada 245. Baadhi ya maboresho muhimu yaliyofanyika ni pamoja na kupunguza ushuru wa huduma *(service levy)* kutoka 0.3% hadi 0.25% ya pato ghafi kupitia Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, kupunguza ushuru wa hoteli kutoka 10% hadi 2%, kufuta ada za upakiaji na upakuaji katika baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, na kurejesha kanuni nafuu za usimamizi wa mazingira za mwaka 2021. Vilevile, Serikali imeimarisha udhibiti wa utozwaji wa ada na tozo kupitia marekebisho ya Sheria ya Bajeti na Sheria ya Fedha za Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2025/2026; katika mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi ya Msajili wa Hazina ilipangiwa kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi trilioni 1.696. Chanzo cha maduhuli ni gawio, michango ya 15% ya mapato ghafi ya taasisi zinazochangia, mapato yanayotokana na uendeshaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu Tanzania *(TTMS)*, rejesho la riba na mikopo, ziada na mapato mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya shilingi bilioni 779.91 zilikusanywa sawa na 85% ya lengo kwa kipindi hicho. Aidha, inatarajiwa kuwa sehemu iliyobaki ya makusanyo itapatikana katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025/2026 ambapo kampuni ambazo Serikali ina hisa hutoa gawio baada ya kukamilisha ukaguzi wa hesabu na mashirika yanayotoa mchango wa 15% ya mapato ghafi hukamilisha kuwasilisha michango hiyo na malimbikizo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 157.85 kwa mafungu yote matatu. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla

ya shilingi bilioni 107.26 zilipokelewa sawa na 67.95% ya kiasi kilichoidhinishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwasilishe mapendekezo ya vipaumbele na mpango kazi kwa mwaka 2026/2027; mapendekezo ya vipaumbele na mpango kazi wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2026/2027 yamezingatia kikamilifu malengo na matarajio yaliyoainishwa katika Dira 2050, Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2050, Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027 – 2030/2031, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 na Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Kufungua Bunge la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyotolewa na Mheshimiwa Rais, tarehe 14 Novemba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mapendekezo haya yamezingatia majukumu ya mapya ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kama yalivyoainishwa katika mgawanyo wa majukumu ya Ofisi uliotolewa kupitia Gazeti la Serikali Na. 686 la tarehe 19 Disemba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu haya yamehusisha usimamizi wa maendeleo ya sekta binafsi na kuratibu program za kuondoa umaskini nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia majukumu yake na mwongozo niliyoeleza hapo juu, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji na Taasisi inazozisimamia imepanga kutekeleza majukumu matano yafuatayo: -

(i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Dira 2050, Mpango wa Maendeleo wa Taifa Miaka Mitano na Mpango wa Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2026/2027;

(ii) Kuhamasisha, kuwezesha na kutoa huduma kwa wawekezaji wa sekta binafsi;

(iii) Kuimarisha uwekezaji wa umma;

(iv) Kuimarisha mazingira ya biashara; na

(v) Kuratibu programu za kuondoa umaskini nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Dira ya 2050 na nyenzo zake pamoja na hatua nyingine Tume ya Taifa ya Mipango itatekeleza yafuatayo.

(i) Kuandaa Mwongozo wa Taifa wa Tafiti na Ubunifu ili kuweka utaratibu utakaowezasha watafiti na wabunifu kufanya shughuli zao na kuchangia kikamilifu katika maandalizi na utekelezaji wa mipango;

(ii) Kutayarisha mfumo wa kidijitali wa tafiti yaani *natural research portal* ili kuhifadhi tafiti na kuchakata matokeo ya tafiti na kuibua mikakati ya kuzitumia kuleta mageuzi kiutendaji na kiutekelezaji;

(iii) Kuratibu maandalizi ya mipango ya maendeleo ya mikoa (*Reginal Development Plans)* na mipango ya maendeleo ya halmashauri *(Council Development Plans*). Mipango hii inalenga kuhakikisha utekelezaji mathubuti wa afua za kimkakati katika ngazi ya mkoa na halmashauri kwa kuzingatia fursa mahususi na changamoto za kipekee katika maeneo hayo ya kiutawala;

(iv) Kuratibu uandaaji wa wasifu wa kiuchumi *(Regional Economic Profiles)* kwa kila Mkoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kuzingatia rasilimali zinazopatikana katika maeneo hayo;

(v) Kuratibu, ufuatiliaji na usipimaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kitaifa kwa kuzingatia mfumo wa kitaifa wa usimamizi wa mipango ya maendeleo *(National Result Based Monitoring, Evaluation Learning and Accountability Framework)*;

(vi) Kutathmini hali ya rasilimali za nchi katika sekta mbalimbali kwa lengo la kuwezesha uwekezaji wenye tija; na

(vii) Kuendelea kufuatilia mwenendo wa hali ya uchumi kikanda na kimataifa ili kupendekeza hatua zinazopaswa kuchukuliwa katika kuimarisha usimamizi wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Tume ya Taifa ya Mipango itaandaa Mwongozo wa Mashirikiano ya Kiuchumi baina ya Tanzania na nchi nyingine *(Economic Cooperation Frame Work)*, hatua hii inalenga kubainisha vigezo vitakavyotumika katika ushirikiano wa Tanzania na nchi nyingine au taasisi za kikanda na kimataifa ili kufikia vipaumbele vya nchi kwa kuzingatia mipango ya maendeleo na dira ya taifa ya 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mwongozo huu, Serikali itaimarisha uratibu wa mikataba ya ushirikiano kupitia Tume za Pamoja za Ushirikiano *(Joint Permanent Commissions - JPC)*, ili kuhakikisha inaendena kikamilifu na mipango ya kitaifa, kuleta tija kwa uchumi na kuchangia ustawi wa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kuhamasisha, kuwezesha na kutoa huduma kwa wawekezaji wa sekta binafsi wa ndani na nje ya nchi mwaka 2026/2027 Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kupitia mamlaka ya uwekezaji na maeneo maalum ya kiuchumi imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo: -

(i) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa vivutio vilivyopo ili kuandaa mwongozo mpya wa vivutio kwa wawekezaji nchini, msisitizo utawekwa katika kuhakikisha kuwa vituo hivyo vinachochea uwekezaji mkubwa wa kimkakati na hususan uwekezaji wa ndani unaoweza kuleta mageuzi ya viwanda, kukuza viwanda vidogo na vya kati na kuongeza ajira kwa vijana. Lengo kuu ni kuiwezesha Tanzania kuwa kitovu cha uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya soko la ndani, soko la ukanda wa Afrika Mashariki na Bara la Afrika kwa ujumla. Aidha, mwongozo utapendekeza vivutio maalum kulingana

na maeneo ya kijiografia ili kila mkoa uvutie wawekezaji kulingana na jeografia ya mkoa husika na fursa zinazopatikana katika mkoa huo. Mwongozo huu pia utajumuisha vivutio maalum vya uwekezaji kwa wazawa ili kuleta hamasa na kuongeza kasi ya ukuwaji wa uwekezaji wa ndani. Hatua hii itaenda sambamba na kuandaa Kitabu cha Orodha ya Vivutio *(Investments Insenve Compendium Book)*.

(ii) Kuongeza ardhi iliyoandaliwa kwa ajili ya uwekezaji *(LandBank for Investment)* kwa kufanya utambuzi wa maeneo yenye sifa stahiki kwa uwekezaji, ulipaji wa fidia, uendelezaji wa miundombinu wezeshi kama barabara, umeme, maji, gesi na mawasiliano. Aidha, *TISEZA* itahamasisha sekta ya umma na binafsi kuwasilisha ardhi zao kwa ajili ya kutafutiwa wawekezaji. Taarifa kuhusu maeneo haya zitakusanywa na kuhifadhiwa katika mifumo ya mawasiliano na ofisi na *TISEZA* ili kuwezesha wawekazaji kuzipata wakiwa mahala popote duniani.

(iii) Kuandaa mkakati wa kuvutia wawekezaji wa kimkakati katika sekta ya uunganishaji na utengenezaji wa magari. Hatua hii inafutia tathmini ya awali iliyofanywa na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa kushirikiana na Taasisi ya *Africa Association Automotive Manufacturer* ya Afrika Kusini ambayo ilibaini fursa kubwa ya kuvutia wawekezaji katika sekta hii. Mkakati utaainisha aina ya wawekezaji wanaolegwa, aina ya uzalishaji unaokusudiwa pamoja na vivutio vitakavyowekwa ili kuhakikisha ushindani wa sekta hii katika ngazi ya Bara la Afrika. Shabaha yetu ni kuwa ifikapo mwaka 2030 Tanzania iwe miongoni mwa vinara wa uzalishaji na uunganishaji wa magari katika Bara la Afrika.

(iv) Kuhamasisha, kuwezesha na kutoa huduma kwa wawekezaji waliopo na wanaotarajia kuwekeza ndani ya maeneo maalum ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje *(Export Processing Zones)*. Katika kuvutia

wawekezaji kuwekeza na kuzalisha bidhaa katika maeneo haya, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji itaweka mikakati mbalimbali ikiwemo kurahisisha usajili ndani ya maeneo haya, kuboresha miundombinu wezeshi, kuhamasisha ubora wa bidhaa ili kukidhi viwango vya kimataifa na kuhamasisha matumizi ya teknolojia mpya katika uzalishaji wa bidhaa.

(v) Kuandaa maeneo maalum ya uwekezaji kwa ajili ya vijana na *TISEZA* itatenga maeneo maalum ya uwekezaji kwa ajili ya vijana kupitia program ya *Youth Industrial Special Economic Zones* ambayo itawezesha vijana kupata ardhi kwa ajili ya kujenga viwanda. Maeneo hayo yatajengwa katika maeneo maalum ya uwekezaji yaliyopo katika mikoa ya Dodoma eneo la Nala ekari 100 zimetengwa kwa ajili ya vijana, Pwani - Kwala ekari 20 zimetegwa kwa ajili ya vijana, Mara - Bunda ekari 100 zimetengwa kwa ajili ya vijana, Ruvuma –Songea ekari 100 kwa ajili ya vijana na Pwani – Bagamoyo ekari 20 kwa ajili ya vijana. Vijana watapewa fursa ya kuwekeza kama watu binafsi ama kupitia vikundi na wataweza kushiriki katika sekta mbalimbali za uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kuimarisha uwekezaji wa umma mwaka 2026 pamoja na mambo mengine Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imepanga kukamilisha Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma, pamoja na mambo mengine Muswada utapendekeza hatua zifuatazo: -

(i) Kuzanzishwa kwa mamlaka ya usimamizi wa uwekezaji wa umma;

(ii) Kuanzishwa kwa mfuko wa uwekezaji wa umma;

(iii) Kuanzasha mfumo wa ushindani katika upatikanaji wa Watendaji Wakuu na Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma; na

(iv) Kuongeza uhuru wa kujiendesha kwa mashirika yanayofanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2017 Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina itaendelea na zoezi la tathmini ya utendaji na taasisi za umma na kuchukuwa hatua stahiki ikiwemo kuunganisha taasisi na mashirika ya umma ambayo majukumu yake yanashabihiana na kufuta taasisi na mashirika ya umma ambayo malengo ya kuanzishwa kwake yamepitwa na wakati au majukumu yake yanaweza yakafanywa na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji pamoja na hatua nyingine Serikali imepanga kukamilisha na kuanza kutekeleza mkakati wa kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji. Mkakati huu utahusisha maeneo makubwa 11 yafuatayo: -

(i) Ujuzi wa kazi, maendeleo ya rasilimali watu, mafunzo na utafiti;

(ii) Miundombinu na huduma za msingi za umma;

(iii) Muundo wa taasisi, mipango na uratibu wa taasisi;

(iv) Mabadiliko ya mtazamo wa kibiashara na uwajibikaji;

(v) Uwekezaji na matumizi ya mifumo ya kidijitali *(digitalization);*

(vi) Uanzishwaji wa biashara na mazingira ya biashara;

(vii) Eneo na majengo ya kufanyia biashara;

(viii) Fedha na uwekezaji;

(ix) Utatuzi wa migogoro ya kibiashara na ufilisi wa kampuni;

(x) Ulinzi wa haki za ubunifu na miliki bunifu; na

(xi) Upatikanaji wa masoko ya ndani na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchochea uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Serikali itaanzisha programu maalum ya upimaji kwa kila mwaka kwa mamlaka ya Serikali za mitaa kuhusu mazingira ya biashara na uwekezaji katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia programu hii mikoa itapimwa na kushindanishwa kwa kuzingatia vigezo vya kuhamasisha, kuwezesha, kulinda na kuhudumia wawekezaji na kuimarisha mazingira ya biashara katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa kukamilisha mazingira ya biashara na uwekezaji Serikali imepanga kuandaa mapendekezo ya Sheria ya Uwezeshaji wa Biashara *(Business and Investment Facilitation Act)* itakayosaidia kurahisisha majukumu ya udhibiti, kudhibiti adhabu na ukaguzi usio lazima na kusaidia urasimishaji wa biashara na kuongeza wigo wa kodi. Sheria hii itatumika kama chachu ya kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuongeza ushindani wanchi kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha programu ya kuondoa umaskini nchini, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji itafanya uchambuzi wa kina wa programu zinazotekeleza afua zinazolenga kuondoa umaskini nchini ambazo zitatekelezwa katika kupitia sekta husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa kushirikiana na Ofisi na Taifa ya Takwimu pamoja na taasisi nyingine za utafiti, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji itaandaa taarifa ya hali ya umaskini nchini kwa lengo la kutambua ni kwa kiasi gani programu zilizotekelezwa zimechangia katika kuondoa umaskini nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ili kuwa na uratibu thabiti wa programu za kuondoa umaskini nchini, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji itaandaa mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji wa umaskini *(National Poverty Monitory and Framework)*. Mfumo huu pamoja

na mambo mengine utajumuisha viashiria vya kupima umaskini, mifumo ya ukusanyaji takwimu, uratibu wa taasisi, uchambuzi na utoaji wa taarifa pamoja na matumizi ya matokeo katika kupanga na kutekeleza sera na bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viashirio hivyo vitasaidia kuhakikisha kuwa taarifa sahihi zinapatikana na kutumika katika kufanya maamuzi kwa maendeleo yan chi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza kazi ambazo tunapanga kuzifanya kupitia mpango kazi huo. ninaomba sasa niwasilishe Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2026/2027 Ofisi ya Msajili wa Hazina - Fungu 007 imepangiwa kukusanya na kuchangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya shilingi trilioni 1.79 kutoka kwenye vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi kupitia gawio, michango ya 15% ya mapato ghafi, mapato yatokanayo na Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu Tanzania *(TTMS)*; rejesho la riba na mikopo ya ziada na mapato mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu ambayo nimeainisha katika hotuba yangu hii, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji inaliomba Bunge lako tukufu lipokee, lijadili na kuidhinisha jumla ya shilingi 144,850,349,000 kwa mchanganuo ufuatao: -

Mosi, Fungu Namba 11, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, tunaomba kuidhinishiwa Matumizi ya Kawaida shilingi 26,244,864,000 na Miradi ya Maendeleo shilingi 9,141,447,000, ikiwa ni jumla kwa fungu hili shilingi 35,386,311,000.

Pili, Fungu Namba 66 Tume ya Taifa ya Mipango tunaomba kuidhinishiwa Matumizi ya Kawaida shilingi 39,322,083,000 na Miradi ya Maendeleo shilingi 9,319,512,000 kwa Fungu hili jumla shilingi 48,641,595,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu Namba 007, Ofisi ya Msajili wa Hazina tunaomba kuidhinishiwa shilingi

60,451,752,000 ikiwa ni Matumizi ya Kawaida na shilingi 370,691,000 ikiwa ni Matumizi ya Miradi ya Maendeleo, jumla katika Fungu hili ni shilingi 60,822,443,000. Tumeainisha maombi haya katika ukurasa wa 49, jedwali namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kabla ya hitimisho ninaomba urudie zile *figure* za Tume ya Mipango Fungu 66, ile kwa ajili ya *record ya Hansard*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Namba 66 – Tume ya Mipango tunaomba kuidhinishiwa Fungu Namba 66 tunaomba kuidhinishiwa Matumizi ya Kawaida 39,322,083,000 na Miradi ya Maendeleo shilingi 9,319,512,000 jumla katika fungu hili shilingi 48,641,595,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, kama nilivyotangulia kusema awali Mkutano huu wa Bunge la Bajeti ni wa kwanza katika kuanza kutekeleza Dira 2050 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Muda Mrefu pamoja na Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2026/2027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, huu ni mkutano wa kwanza katika kuanzisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2029. Hivyo, sisi kama Wabunge tunalo jukumu kubwa katika kuweka misingi imara ya kufikiwa kwa malengo na matarajio ya Dira 2050 pamoja na ahadi tulizozitoa kupitia ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, ninapohitimisha hotuba yangu, ninaomba kusisitiza mambo sita yafuatayo: -

(i) Ni kweli nchi yetu imejaliwa rasilimali nyingi za asili, ikiwemo ardhi, madini, maji, misitu na wanyama. Hata hivyo, ili rasilimali hizi zilete tija na kuchochea maendeleo ya uchumi ni lazima na kutumika kuboresha maisha ya watu wetu ni lazima zikutane na

mitaji na teknolojia. Hivyo, basi tusiogope wala kuona aibu kuvutia na kutumia mitaji na teknolojia kutoka popote, ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuendeleza rasilimali zetu katika kufanikisha malengo yetu ya kiuchumi na kijamii. Rasilimali peke yake bila mitaji na teknolojia haziwezi kutusaidia;

(ii) Watekelezaji wakuu wa mipango yetu ya maendeleo ni sekta ya umma na sekta binafsi. Sekta ya umma na sekta binafsi ni timu moja inayosaka ushindi. Ushindi wenyewe ni kukuza uchumi na kuboresha maisha ya watu. Ushindi wa timu moja hutegemea ushirikiano wa wachezaji. Hivyo basi, ni muhimu kuendelea kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kutekeleza malengo yetu ya kiuchumi. Tuwe na lengo na juhudi za pamoja; tukiwa na sauti moja tutakuwa na wimbo mzuri wenye mvumo, sekta ya umma na sekta binafsi;

(iii) Ni muhimu tujenge uthubutu wa kujaribu mapya na kujenga utamaduni wa kutenda. Hivyo, tuwalinde na kuwathamini watu wanaothubutu kufanya mambo mapya;

(iv) Dhima ya uongozi wowote ukiwemo uongozi wetu hatimaye ni maendeleo ya uchumi na maisha ya watu wetu. Hivyo basi, kila hatua tunayochukua na kila nadharia tunayoifikiria lazima ilenge katika kukuza uchumi na kuboresha maisha ya watu wetu. Hivyo, katika kupima mafanikio kwa mipango ambayo tunayo katika kupima mafanikio ya juhudi zetu tutazingatia vigezo vya kukuza uchumi, kuboresha maisha ya watu na hii tunazingatia kupitia kupanuka na kuimarika kwa ubora wa huduma za jamii, kupungua kwa umaskini na kuongezeka kwa ajira hususan miongoni mwa vijana;

(v) Sisi ni Taifa linalomwamini Mungu na tunamwomba sana Mungu kila siku na hili ni jambo jema sana kama nchi, ni mtaji mkubwa. Hata hivyo, lazima tutambue kuwa maendeleo hayateremshwi kutoka mbinguni.

Viongozi na wananchi lazima kujenga imani kwamba hatimaye maendeleo ya kweli ni matokeo ya bidii na maarifa katika kazi. Lazima tujenge utamaduni na nidhamu ya kuchapa kazi kama njia pekee na ya uhakika ya kupata maendeleo yetu kama wanadamu, kama jamii na kama Taifa.

(vi) Mwisho, tuendelee kusisitiza na kutekeleza kwa vitendo nidhamu ya kubana matumizi na kutumia vizuri rasilimali watu, kutumia vizuri rasilimali zetu ikiwemo rasilimali muda, muda nao ni rasilimali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe kwa kuwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na taasisi zilizo chini yake kwa kufanikisha maandalizi ya hotuba yangu ya bajeti niliyoiwasilisha hapa, hawa ni pamoja na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni ambaye ni Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kijana mchapakazi sana huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Dkt. Tausi Mbaga Kida, Katibu Mkuu Mipango na Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango, anayesimamia vizuri sana Tume yetu ya Taifa ya Mipango, Ndugu yetu Dkt. Fred Matola Msemwa, Katibu Mkuu anayesimamia vizuri sana sekta yetu ya uwekezaji, Ndugu Nehemiah Kyando Mchechu, Msajili wa Hazina anayetusaidia sana katika kusimamia na kuratibu mashirika yetu ya umma, na kijana wetu Ndugu Gilead John Teri, Mkurugenzi Mkuu wa *TISEZA* ambaye anamsaidia sana Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba wawekezaji wanakuja na wanabaki katika nchi hii. Pamoja na menejimenti na watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na taasisi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafsi hii hii pia, kama alivyotambulishwa, kutambua uwepo wa moja wa walimu wangu na walezi wangu muhimu sana ambao wametoa mchango mkubwa kunijenga hivi nilivyo. Huyu ni Profesa Henry Joseph Mosha, Profesa wa miaka mingi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, aliyenifundisha katika ngazi mbalimbali, lakini muhimu sana

kanilea kitaaluma na ndiye aliyenitia moyo kuendelea kuwa kiongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka niliteuliwa kuwa Mkuu wa Idara, nimetoka tu *Ph.D* nikakataa, nikasema mimi nataka kufanya machapisho. Profesa huyu ndiye aliyeniita, akaniasa, usikatae nafasi ya uongozi katika utumishi wa umma, ndiyo nikaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya walimu wengine walionifundisha, Profesa, Mungu akubariki sana na nimefurahi kwamba umefika hapa Bungeni leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru wadau mbalimbali wa maendeleo kwa mchango wanaotoa katika maendeleo ya nchi yetu. Ninaomba kuwataja angalau wachache ambao tulishirikiana nao kwa karibu, Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto *(UNICEF), TradeMark Africa, Gas Africa,* Sekta Binafsi ya Tanzania *(Tanzania Private Sector Foundation),* Chemba ya Biashara ya Taifa *(TNCC)* na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania *(CTI)* na wengine wote ambao tumefanayanao kazi kwa ukaribu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu na wa kipekee kabisa, niwashukuru makampuni mbalimbali ya ndani na nje ya nchi, yaliyowekeza na yanayoendelea kuwekeza nchini mwetu na wengi wamekuja hapa leo, tunashukuru sana kwa kutuunga mkono. Uwekezaji wao ndiyo roho ya uchumi wa nchi yetu, tunawatambua, tunawathamini na tutaendelea kuwapa kila aina ya msaada wanaouhitaji ili waendelee kufanikiwa. Kwa sababu, mafanikio ya wawekezaji ndiyo mafanikio yetu kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia, kwamba hotuba yangu hii inapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji pamoja na taasisi zake www.popi.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kurudia kuliomba Bunge lako kupitisha Makadirio ya Mapato ya shilingi trilioni 1.792 na Matumizi ya jumla ya shilingi

144,850,349,000 kwa ajili ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2026. Kati ya kiasi hicho, shilingi 126,018,699,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 18,831,650,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na tumeionesha jedwali namba moja, ukurasa wa 49 wa kitabu cha hotuba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hutuba yangu hii, pamoja na kitabu cha hotuba tulichowasilisha na gharama zake zote ziingie katika Kumbukumbu za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI KWA MWAKA 2026/27 ILIYOWASILISHWA NA MHESHIMIWA PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1. UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo mbele ya Bunge lako Tukufu, ikiwa ni taarifa ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ninaomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka 2026/27 yanayojumuisha Fungu 11 - Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; Fungu 66 - Tume ya Taifa ya Mipango; na Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina.

**1.1 Shukrani na Pongezi**

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kukutana tena katika Mkutano wa tatu wa Bunge la Kumi na Tatu, na iliyonipa mimi fursa hii ya kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ya mwaka 2026/27.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa kuwa hii ni hotuba yangu ya kwanza ya bajeti tangu nilipoteuliwa kufuatia uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** kwa kuniamini na kuniteua tena kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Ninamuahidi kumrushia imani hii kwa utii kwake, kwa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Chama Cha Mapinduzi, na kwa kuchapa kazi kwa bidii na maarifa ili kutimiza maono yake ya kuiona Tanzania ikiwa Taifa jumuishi, lenye ustawi zaidi, lenye haki na linalojitegemea.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** Naomba pia niungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninamtakia Mheshimiwa Rais afya njema, amani, utulivu na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa majukumu yake makubwa ya kitaifa.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** Ninapenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Balozi, Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi anayoifanya katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu ya kuijenga Tanzania yetu.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ninamtakia mafanikio makubwa katika kuendelea kuijenga Zanzibar.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** Ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mambo matatu. Kwanza, ninampongeza kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa 12 wa Tanzania (wa kumi kama Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania). Pili, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuanza kazi vizuri kunakothibitishwa na vigezo angalau vitatu. Mosi, ni utulivu bungeni tangu Bunge hili la 13 lianze. Pili, usimamizi mzuri wa shughuli za serikali unaonesha matokeo ya wazi kupitia vikao

mbalimbali vya mawaziri na watendaji wengine wa serikali. Tatu, ziara ambazo amekuwa akizifanya kwa wananchi ambazo zinaambatana na uzinduzi wa miradi ya maendeleo na usikilizwaji na utatuzi wa kero za wananchi.

Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ya bajeti ya ofisi yake na ambayo aliiwasilisha kwa umahiri mkubwa. Hotuba hiyo imejenga msingi wa hotuba za bajeti za wizara ikiwemo hotuba yangu ninayoiwasilisha hapa leo.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ninakupongeza wewe binafsi, **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb),** kwanza kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na pili kwa jinsi ulivyoanza kazi vyema katika kuliongoza bunge hili kwa umahiri mkubwa. Aidha, ninampongeza **Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb),** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uongozi wenu thabiti umelifanya Bunge kuendelea kuwa chombo imara cha kutunga Sheria, kusimamia Serikali na kuwakilisha wananchi kwa ufanisi.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuwapongeza **Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri wote** kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza wizara mbalimbali wanazozisimamia. Ninawaahidi ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yetu. Kipekee kabisa, nimpongeze **Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya (Mb),** kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ninapohitimisha shukrani zangu ninaomba kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya uongozi wa **Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb) –** Mwenyekiti; **Mheshimiwa Edwin Enos Swalle (Mb)** – Makamu Mwenyekiti; na Wajumbe wa Kamati kwa michango, ushauri na miongozo waliyotupatia katika maandalizi ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Ninaishukuru Kamati kwa ushirikiano ambao tumekuwa nao tangu tulipoanza shughuli za kamati. Aidha, ninamshukuru Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wake kupitia wasaidizi wake wanaosimamia Kamati hii.

## 1.2 Salamu za Pole

**11. *Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa, ninaungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa pole kwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kufuatia kuondokewa na wapendwa wetu **Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi (Mb), aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) na Mbunge wa Jimbo la Isimani, Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama,** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho na **Mheshimiwa Halima Idd Nassor,** aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Tutaendelea kuwakumbuka kwa mchango wao katika kulitumikia Taifa. ***Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.***

## 1.3 Mpangilio wa Hoja

**12. *Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo ya utangulizi, naomba kuwasilisha hoja iliyo mbele yetu kwa mjadala na idhini ya Bunge lako Tukufu. Hoja yangu imegawanyika katika maeneo makuu manne (4): Taarifa ya utekelezaji wa Mpango kwa Mwaka 2025/26; Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2025/26; Mapendekezo ya Vipaumbele vya Mpango wa Mwaka 2026/27; na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2026/27.

# 2. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO KWA MWAKA 2025/26

## 2.1 Utangulizi

**13. *Mheshimiwa Spika,*** Kwa mujibu wa mgawanyo wa majukumu ya Wizara yaliyoainishwa katika Gazeti la Serikali kupitia Tangazo la Serikali (GN) Namba 407A la tarehe 22 Juni, 2023, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ilikuwa na majukumu 12 kama ifuatavyo- *Sera za Uwekezaji na Utekelezaji wake; Uhamasishaji wa Uwekezaji wa Ndani na wa Kigeni; Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara; Masuala ya Tume ya Taifa ya Mipango; Masuala ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi; Masuala ya Uwekezaji wa Umma; Uratibu na Maendeleo ya Kongani za Viwanda, Maeneo ya makazi na Mgawanyo wa Viwanda; Uchakataji wa Bidhaa kwa ajili ya Mauzo ya Nje; Uhamasishaji wa Mauzo ya Nje; Mashirika ya*

*Kimataifa yanayohusika na Uwekezaji; Uboreshaji wa Utendaji na Maendeleo ya Rasilimali Watu katika Ofisi hii; na Usimamizi wa Taasisi zilizo Chini ya Ofisi, Mashirika ya Umma, Wakala, Mipango na Miradi inayosimamiwa na Ofisi.* Hivyo, taarifa ya utekelezaji inawasilishwa kwa kuzingatia maeneo yanayoakisi majukumu hayo, pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 na Mwongozo wa Bajeti ya Serikali wa Mwaka 2025/26. Majukumu yametekelezwa kupitia Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na taasisi zilizo chini yake, ambazo ni Tume ya Taifa ya Mipango, Ofisi ya Msajili wa Hazina, na Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania *(Tanzania Investment and Special Economic Zones Authority - TISEZA)*.

**2.2 Maandalizi ya Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa**

**14. *Mheshimiwa Spika,*** Kama tunavyokumbuka, kufuatia kukamilika kwa maandalizi yake na kuidhinishwa kwake, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua rasmi Dira 2050 tarehe 17 Julai, 2025 jijini Dodoma. Kufuatia hatua hii, na kama sehemu ya maandalizi ya utekelezaji wa Dira 2050, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Mipango imeandaa nyenzo muhimu za utekelezaji ambazo ni Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu *(Long Term Perspective Plan – LTPP 2026/27 - 2050/51)*, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano *(Five Year Development Plan – FYDP IV 2026/27 - 2030/31)*, Mwongozo wa Ufuatiliaji, Tathmini, Uwajibikaji na Kujifunza *(Result Based Monitoring, Evaluation, Accountability and Learning - RBMEA&L 2026/27 - 2030/31)* na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka Mmoja *(Annual Development Plan – ADP 2026/27)*.

**15. *Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Taifa ya Mipango imeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Mipango ambao unaelekeza taasisi zote za umma hatua za kufuata katika uandaaji wa mipango yao, uwekezaji na biashara. Mwongozo huu unalenga kuhakikisha matumizi yenye tija ya rasilimali za umma; kufungamanisha malengo ya maendeleo na jitihada za taasisi za umma; na kuweka utaratibu unaowezesha upangaji wa pamoja kuanzia ngazi ya Taifa hadi Halmashauri.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mwongozo huu ulianza kutumika Disemba 2025 kwa lengo la kuhakikisha maandalizi ya mipango na bajeti za Wizara, Taasisi za Umma, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2026/27 yanazingatia maudhui ya Dira 2050 pamoja na vipaumbele mahsusi vya FYDP IV. Katika kuhakikisha mwongozo huo unazingatiwa, Tume ya Taifa ya Mipango imeendelea kutoa msaada wa kitaalamu kwa Wizara, Taasisi za Umma, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika maandalizi ya Mipango ya Mageuzi ya Kisekta (Sectoral Transformation Plans) kwa sekta tisa (9) za mageuzi zilizoainishwa katika Dira 2050, Mipango ya Maendeleo ya Mikoa (Regional Development Plans) na Mipango ya Maendeleo ya Halmashauri (Councils Development Plans). Hatua hii itasaidia kuhakikisha ufungamanishaji stahiki wa Dira 2050 na FYDP IV katika mipango ya kisekta, Mikoa na Halmashauri na kuongeza umadhubuti wa utekelezaji.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Taifa ya Mipango imeendelea na uandaaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 ambao unaanzisha rasmi safari ya utekelezaji wa Dira 2050 katika kipindi cha muda mfupi kupitia Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31(FYDP IV) wenye dhima ya **"Mageuzi kwa ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji Ajira".** Mpango huu unalenga upangaji wa kimkakati na mageuzi ya mifumo na utawala bora; mageuzi ya kiuchumi; mageuzi ya mashirika ya umma ili kuongeza mchango wake katika uwekezaji; na mageuzi ya maandalizi ya miradi ili kuvutia uwekezaji katika sekta za mageuzi zitakazoleta ukuaji endelevu wa uchumi. Mpango huo umeainisha maeneo matano (5) ya kipaumbele ambayo ni: utawala, amani, usalama na utulivu; kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani kupitia sekta za kimageuzi; kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya jamii; uhifadhi wa mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi; na kutumia kikamilifu vichocheo vya maendeleo. Aidha, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 yalikamilika na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Februari 2026.

### 2.2.1 Utoaji wa Elimu kwa Umma kuhusu Dira 2050

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Taifa ya Mipango imeendelea kuelimisha umma kuhusu Dira 2050 kupitia mikutano na makongamano 18 yaliyohusisha wadau mbalimbali wakiwemo makundi ya vijana, sekta binafsi, wadau katika sekta ya miundombinu na Kamati za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kutoa elimu kwa umma kuhusu Dira 2050. Aidha, Ofisi imeanzisha kipindi maalum cha Dira 2050 kupitia televisheni ya TBC1 na ITV ambapo hadi kufikia Machi 2026, jumla ya vipindi 36 vimeandaliwa na kurushwa

### 2.2.2 Usimamizi wa Mipango na Miradi ya Maendeleo

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kufikia malengo ya mipango; ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa ni nyenzo muhimu za usimamizi na uwajibikaji. Hivyo, Tume ya Taifa ya Mipango imeimarisha ufuatiliaji na tathmini ya mipango na miradi ya maendeleo kwa kuandaa Mwongozo wa Ufuatiliaji, Tathmini, Uwajibikaji na Kujifunza Unaozingatia Matokeo ya Dira 2050. Mwongozo huu unaainisha mfumo uliojengwa katika misingi ya usimamizi unaozingatia matokeo na unaolenga kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mipango unafuatiliwa kwa kuzingatia mnyororo wa matokeo, hususan katika ngazi ya matokeo ya muda mfupi (outputs) na matokeo ya muda wa kati (outcomes). Lengo la mwongozo huu ni:-

i) Kufuatilia utekelezaji wa shughuli na matumizi ya rasilimali dhidi ya malengo ya mwaka;

ii) Kupima maendeleo ya utekelezaji wa viashiria vya muda mfupi, wa kati, na muda mrefu;

iii) Kubaini changamoto na kupendekeza hatua za kuzitatua kwa wakati;

iv) Kuandaa na kuwasilisha taarifa sahihi za utekelezaji ambazo zitakuwa msingi wa kufanya maamuzi ya kisera na kiutendaji; na

v) Kuwa kigezo kikuu cha motisha na uwajibikaji kwa Wakuu wa Taasisi za Umma.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** mfumo huu umeainisha ngazi tatu (3) za ufuatiliaji ambazo ni: **Mosi:** Ufuatiliaji katika ngazi ya shughuli ambapo watekelezaji wa miradi na afua zote za mpango wanapaswa kufuatilia moja kwa moja utekelezaji na kutoa taarifa, **Pili:** Ngazi ya matokeo ya muda mfupi ambapo utekelezaji wa shughuli utazalisha matokeo ya muda mfupi ambayo yatafanyiwa ufuatiliaji na watekelezaji, waratibu wa mipango katika ngazi ya wizara, pamoja na ngazi ya kitaifa ikiwemo Tume ya Taifa ya Mipango, kwa msingi wa robo mwaka, nusu mwaka na mwaka; na **Tatu:** Ngazi ya matokeo ya muda wa kati ambapo ufuatiliaji utafanyika ili kupima mabadiliko katika upatikanaji, ubora na matumizi ya huduma kwa walengwa yanayotokana na matokeo ya moja kwa moja. Ufuatiliaji huu utafanywa na wizara, taasisi na mamlaka husika kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango, kwa kutumia tafiti, takwimu za kiutawala na mapitio ya utekelezaji ya mara kwa mara. Taarifa zitakazoandaliwa zitatumika kupima mafanikio ya mpango na kufanya maboresho ya kisera na kiutendaji.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** ufuatiliaji huu utafanyika kupitia ziara za ukaguzi wa miradi, taarifa za utekelezaji za robo mwaka wa miradi na viashiria vya mpango; Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Mipango ya Maendeleo na vikao vya mapitio ya utekelezaji vya kila robo mwaka. Aidha, tathmini zitafanyika ili kupima ufanisi, tija, uendelevu na matokeo ya mpango. Tathmini hizo zitajumuisha: Tathmini ya utekelezaji wa mpango kwa robo mwaka, nusu mwaka, na mwisho wa mwaka kupitia viashiria vya matokeo ya moja kwa moja na matokeo ya muda wa kati; na Tathmini maalum kulingana na mahitaji.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile Tume ya Taifa ya Mipango imeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Miradi ya Maendeleo ambao unaimarisha utaratibu wa kuibua, kuandaa, kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo ili kuongeza tija katika matumizi ya fedha. Mwongozo huu umeweka bayana taratibu, vigezo vya uchambuzi na tathmini za miradi na hivyo kuwa rafiki kwa watumiaji katika ngazi zote. Aidha, Mwongozo huu umejumuisha

mabadiliko ya kisheria na kimuundo katika usimamizi wa miradi na programu za maendeleo, ajenda mtambuka ikiwemo mabadiliko ya tabianchi, ushiriki wa sekta binafsi na uhamasishaji wa vyanzo mbadala vya ugharamiaji wa miradi ya maendeleo.

**23. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuwezesha ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati (real -time monitoring), Tume ya Taifa ya Mipango imeandaa Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Mipango ya Maendeleo (National Development Plans and Project Management Information System – NPMIS) ambao utawezesha upangaji, uchambuzi, ufuatiliaji na tathmini pamoja na ufungaji wa utekelezaji wa miradi kufanyika kidijitali. Mfumo huu umeanisha malengo mahsusi manne (4) ya Dira 2050, shabaha 19 na viashiria ambapo miradi itatakiwa kuonesha namna itakavyowezesha utekelezaji ya Dira 2050 kupitia mipango ya muda wa kati na muda mfupi. Hii itasaidia ukusanyaji wa taarifa sahihi na kwa wakati za programu na miradi ya maendeleo na hivyo kurahisisha ufuatiliaji na tathmini za utekelezaji wa mipango kwa kuzingatia malengo, shabaha, maeneo ya vipaumbele na afua mbalimbali kupitia viashiria vya matokeo. Hatua hii itawezesha kuongeza uwazi, uwajibikaji na upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi kwa ajili ya kufanya maamuzi ya haraka na yenye ushahidi. Lengo ni kuongeza wigo wa ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi zote za utekelezaji na hivyo kupata utekelezaji wa jumla wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka na kujenga msingi wa kujitathmini katika kufikia malengo ya Dira 2050.

**24. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile Mfumo wa Kitaifa wa Mipango ya Maendeleo utahakikisha unakusanya taarifa zote za msingi zinazohusika na hali ya umaskini nchini, upatikanaji wa huduma za kijamii, ujumuishwaji katika huduma za fedha (financial inclusion) na hali ya kipato kwa ngazi ya kaya. Hivyo, Tume ya Taifa ya Mipango kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu itafungamanisha mfumo wa miradi na mifumo mingine ili kuwezesha kufuatilia hali ya umaskini nchini na kupendekeza hatua stahiki.

**25. *Mheshimiwa Spika,*** Ofisi yangu na Tume ya Taifa ya Mipango imeendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha katika usimamizi wa

uchumi na miradi ya maendeleo ili kuongeza tija katika matumizi ya fedha na hatimaye kufikia malengo ya kiuchumi na kijamii na utoaji wa huduma kwa wananchi. Ushirikiano huo umewezesha kufanyika kwa uchambuzi wa miradi 450 inayoendelea na utekelezaji na kuainisha miradi ya kipaumbele **416** iliyojumuishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/27; na kufanya uchambuzi na uainishaji wa **miradi** 26 ya kipaumbele kati ya 38 iliyowasilishwa na Wizara ya Fedha kwa ajili ya ufadhili wa fedha za nje kwa mwaka 2026/27.

**26. *Mheshimiwa Spika,*** nichukue nafasi hii kuwahimiza Wizara, idara za serikali zinazojitegemea na mashirika na taasisi za umma kuwasilisha programu na miradi ya maendeleo kupitia Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Mipango ya Maendeleo ili kuchambuliwa na kupitishwa kabla ya kuwasilishwa Wizara ya Fedha. Kuanzia tarehe 1 Julai, 2026, Tume ya Taifa ya Mipango haitapokea wala kufanyia kazi taarifa zozote za miradi ya maendeleo nje ya mfumo huo.

### 2.2.3 Kuongeza Matumizi ya Tafiti ili Kukuza Ubunifu Katika Upangaji na Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo

**27. *Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha upangaji unazingatia matokeo ya tafiti kwa kuakisi mahitaji halisi ya Taifa, Tume ya Taifa ya Mipango imeendelea kuhakikisha kuwa upangaji wa mipango ya maendeleo unaongozwa na tafiti na utekelezaji unatumia mbinu bunifu ili kuongeza tija katika matokeo tarajiwa. Hivyo, katika kipindi cha mwaka 2025/26 Tume ya Taifa ya Mipango imeandaa Ajenda ya Taifa ya Utafiti 2026/27 – 2030/31 kwa lengo la kutoa mwongozo kwa taasisi za umma na binafsi katika kufanya utafiti utakaowezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya muda mfupi na muda wa kati. Ajenda hiyo imeainisha maeneo makuu matano (5) ambayo ni:

i) Utawala bora, ufanisi wa taasisi, na mifumo ya utoaji huduma. Eneo hili ni muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV) na Dira 2050 kwa ujumla;

ii) Mageuzi ya kiuchumi, Uwekezaji na Tija (Economic Transformation, Investment and Productivity). Kwa kuzingatia Dira 2050 na Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/27 – 2050/51, mwelekeo huu unasisitiza mabadiliko ya kimuundo yanayotokana na ukuaji endelevu wa uzalishaji, kupanua uwezo wa viwanda, uundaji wa mtaji wenye nguvu, na ushirikiano wa kina katika masoko ya kikanda na kimataifa. Kufikia malengo haya kunahitajika kuwepo kwa shughuli za kiuchumi za thamani ya juu zinazoungwa mkono na mifumo bora ya uzalishaji, uvumbuzi, na mazingira ya biashara ambayo huvutia na kudumisha uwekezaji wa ndani na nje. Kipaumbele kinawekwa katika kutoa ushahidi wa kitafiti unaotekelezeka ili kuimarisha ushindani thabiti, kuimarisha mwitikio wa uwekezaji, kuimarisha uwezo wa viwanda, kukuza biashara, na kuboresha ushindani wa mauzo ya nje;

iii) Ustawi wa pamoja, jumuishi na unaojenga uwezo wa wananchi (Human Capability, Inclusion and Social Cohesion). Eneo hii linaakisi nguzo ya pili ya Dira 2050 na linalenga kutoa majibu kwa masuala muhimu yanayohusu maendeleo ya watu;

iv) Utunzaji wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi (Environmental Integrity and Climate Resilience). Eneo hili linalenga kutatua changamoto za kimazingira, mabadiliko ya tabianchi, na masuala yanayohusu uchumi wa buluu kulingana na nguzo ya tatu ya Dira 2050; na

v) Masuala yanayohusu Mienendo ya Idadi ya Watu na Maendeleo Endelevu (Population Dynamics and Sustainable Development). Eneo hili la utafiti limeibuliwa kwa kuzingatia ongezeko la idadi ya watu, hususani mijini. Ili kuwezesha mipango ya Taifa kuzingatia idadi ya watu, ipo haja kubwa ya kupata uelewa mpana unaotokana na matokeo ya tafiti za kisayansi ili kuiwezesha Serikali kupanga mipango kwa matumizi endelevu ya rasilimali tulizonazo.

**28. *Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa kutumia matokeo ya tafiti kwa ajili ya kupata ushahidi wa kisayansi katika

uandaaji wa mipango na usimamizi wa utekelezaji wake, Tume ya Taifa ya Mipango iliandaa mkutano wa mashauriano wa watafiti uliofanyika tarehe 23-24 Machi 2026 Dodoma kwa lengo la kuwakutanisha Watafiti kutoka Taasisi mbalimbali na Wakurugenzi Wasaidizi wa Sera, Utafiti na Ubunifu wa Wizara na Taasisi za Serikali kwa lengo la kujadili namna watakavyoweza kutumia Ajenda za Utafiti kufanya tafiti za kibunifu zitakazosaidia maandalizi ya mipango na utekelezaji wake ili kufikia shabaha za FYDP IV. Mkutano huo ulibeba maudhui ya kuonesha umuhimu wa kufungamanisha tafiti katika mchakato wa upangaji (Aligning research with National Planning Process). Hatua hii inaonesha nia ya Serikali kuondoa migongano katika utekelezaji wa afua za maendeleo na hivyo kufikia malengo na shabaha za Dira 2050 kama inavyotarajiwa.

**29. *Mheshimiwa Spika,*** nitoe rai kwa Wizara, Taasisi za Umma, Sekretariati za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa tunapoanza utekelezaji wa Dira 2050 Julai Mosi, 2026 shughuli zote za tafiti zitatakiwa kufungamanishwa na Ajenda ya Taifa ya Utafiti 2026/27-2030/31. Hatua hii itawezesha kutoa ushahidi wa kisayansi uliofanyiwa utafiti kuhusu changamoto halisi za kiuchumi na kijamii nchini. Vilevile, itawezesha upangaji wa mipango ya muda mfupi yenye tija na matokeo makubwa kwa taifa.

### 2.2.4 Kuwezesha Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Upangaji na Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo:

**30. *Mheshimiwa Spika,*** Katika kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo, Tume ya Taifa ya Mipango ilifanya majadiliano na wadau wa sekta binafsi kutoka mikoa mbalimbali kwa lengo la kujadili changamoto na fursa zilizopo ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Hii ilikuwa ni sehemu hatua muhimu katika kuandaa fahirisi ambayo ni nyenzo ya kitaifa ya kupata mtazamo halisi wa kina wa sekta binafsi (private sector firm-level insights) katika maeneo ya: Mazingira ya Kikanuni na Kisera; Utawala Bora na Ubora wa Taasisi; Miundombinu na Utoaji wa Huduma; Upatikanaji wa Mitaji na Huduma za Kifedha; Soko la Ajira na Ujuzi wa Rasilimali Watu; na Hali ya Uchumi Jumla.

**31. *Mheshimiwa Spika,*** Fahirisi inayoandaliwa ni nyenzo muhimu katika ufuatiliaji wa utendaji wa sekta binafsi na kutoa msingi thabiti wa kufanya maamuzi ya kisera na kimkakati kwa wakati muafaka. Aidha, matokeo ya fahirisi hii yatajenga msingi wa kufanya midahalo na majadiliano na sekta binafsi ili kupata maoni yatakayowezesha kutafsiri sera mbalimbali ambazo zitachochea maendeleo nchini. Hivyo, nitoe rai kwa sekta zote nchini kuhakikisha inatoa kipaumbele na kumtambua sekta binafsi kuwa mshiriki muhimu katika kuchochea mageuzi ya kiuchumi na kukuza ajira.

### 2.3 Hali ya Uwekezaji wa Sekta Binafsi

**32. *Mheshimiwa Spika,*** Kwa mujibu wa taarifa ya hali ya uwekezaji ya Dunia ya UNCTAD ya mwaka 2025 **(World Investment Report 2025),** Tanzania imeendelea kuimarisha utendaji wake wa mtiririko wa uwekezaji, ambapo uwekezaji kutoka nje ulifikia dola za Marekani **bilioni 1.72** mwaka 2024, ukilinganisha na **dola bilioni 1.34** mwaka 2023, sawa na ukuaji wa **asilimia 28.3.**

Kwa mujibu wa taarifa hii, katika ukanda wa Afrika Mashariki, Tanzania ilishika **nafasi ya tatu** kwa kuvutia uwekezaji kutoka nje, nyuma ya Ethiopia iliyovutia takribani dola bilioni **3.98,** na Uganda yenye dola bilioni **3.31,** huku ikiwa mbele ya Kenya (takribani dola bilioni **1.50**) na Rwanda (takribani dola milioni **819).** Licha ya kuwa nafasi ya tatu kwa kiwango cha uwekezaji, Tanzania ilikuwa ya kwanza kwa kasi ya ukuaji wa uwekezaji kutoka nje katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, ikizidi wastani wa ukanda (asilimia 12).

**33. *Mheshimiwa Spika,*** Taarifa hiyo pia imebainisha kuwa, kwa upande wa ukanda wa SADC, Tanzania imeendelea kuwa miongoni mwa nchi za **nafasi ya kati hadi juu (takribani nafasi ya 5–6),** ikilinganishwa na nchi zinazoongoza kama Afrika ya Kusini, Msumbiji na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo ambazo huvutia uwekezaji mkubwa zaidi unaochangiwa na miradi mikubwa ya mafuta, gesi na madini. Kwa ujumla, takwimu hizi zinaonesha kuwa Tanzania ni **miongoni mwa nchi zenye ukuaji wa haraka wa uwekezaji barani Afrika (nafasi ya 11 kwa ukubwa wa FDI ).**

**34. *Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, kiwango cha mitaji ya uwekezaji kutoka nje (FDIs) kimeongezeka kutoka dola za Marekani milioni 944 mwaka 2020 hadi kufikia dola bilioni 1.72 mwaka 2024, ikiwa ni ongezeko la asilimia 45.1 katika kipindi hicho.

**35. *Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia taarifa ya uwekezaji wa mwaka 2023, sekta zinazoongoza kwa uwekezaji kutoka nje ni madini, uzalishaji viwandani, fedha na bima, na habari na mawasiliano, ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 82.4 ya uwekezaji wote nchini kwa kipindi hicho.

**36. *Mheshimiwa Spika,*** nchi kumi zilizoongoza kwa uwekezaji kwa kuzingatia takwimu za uwekezaji za mwaka 2023 ni Visiwa vya Clayman, Mauritius, Uingereza, Uholanzi, China, Canada, Afrika Kusini, Barbados, Kenya, na Nigeria.

**37. *Mheshimiwa Spika,*** upande wa usajili wa miradi ya uwekezaji, katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti hii, hadi mwezi Machi 2026, TISEZA imesajili jumla ya miradi mipya 611 yenye thamani ya dola za Marekani milioni 6,233.97 ambayo inatarajiwa kuzalisha ajira mpya 102,463. Aidha kumekuwepo na miradi ya upanuzi 45 yenye thamani ya dola za Marekani milioni 586.12 ambayo inatarajiwa kuzalisha ajira mpya 9,472. Sekta zilizoongoza kwa usajili wa miradi hiyo ni uzalishaji viwandani (47.41%), usafirishaji (13.11%), ujenzi wa majengo ya biashara (12.04%), Utalii (10.21%), kilimo (7.77%), Sekta zingine za huduma, rasilimali watu, miundombinu ya kiuchumi, nishati, ujenzi, madini na mafuta, pamoja na mawasiliano ya simu (9.46%). Mikoa inayoongoza kwa kuvutia uwekezaji ni Dar es Salaam (34.76%), Pwani (21.19%), Arusha (7.32%), Mwanza (4.12%) na Dodoma (4.12%), kama ilivyobainishwa katika kiambatisho namba 1 na 2. Kwa ujumla miradi hii inaenda kuchangua kwenye ukuaji wa Uchumi kwa kuongeza ajira, fedha za kigeni, na mapato yatokanayo na kodi kama ilivyoainishwa katika kiambatisho na tatu.

**38. *Mheshimiwa Spika,*** Aidha, kupitia programu ya uwekezaji katika maeneo maalumu ya kiuchumi (SEZ), jumla ya Miradi 19 yenye thamani ya dola za Marekani Milioni 331.51 ilisajiliwa ikitegemewa kuzalisha ajira 11,762, na mauzo ya nje

yanayokadiriwa kuwa dola za Marekani Milioni 885.23. Miradi hiyo imesajiliwa katika sekta ya kilimo , uzalishaji viwandani na madini katika mikoa ya Iringa, Lindi, Njombe, Ruvuma, Kilimanjaro, Pwani, Mtwara, Arusha Dodoma, Tanga na Dar es Salaam. Wawekezaji katika maeneo hayo wanatoka, Tanzania, Hispania, India, Marekani, China, Ubeligiji, Afrika Kusini, Uturuki, Eritrea, Singapore, Ethiopia, Dubai, na Na Nevis.

**39.** ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 2025 TISEZA ilisajili miradi 915 yenye thamani ya dola bilioni 10.95, ikiwa ni rekodi mpya ya kusajili miradi mingi zaidi nchini tangu kuanzishwa kwa utaratibu wa kusajili miradi ya uwekezaji mwaka 1996. Kwa ujumla wake, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita idadi ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa na TISEZA imeongezeka kutoka miradi 256 mwaka 2021 hadi miradi 915 mwaka 2025, ikiwa ni ongezeko la asilimia 257.4 katika kipindi hicho.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji imeanza kuchakata takwimu za uwekezaji unaofanywa na kampuni za watanzania nje ya nchi (outward investment). Takwimu za awali zinaonesha kuwa zaidi ya dola za Marekani Bilioni 3.1 zimewekezwa nje kupitia Kampuni za Kitanzania. Uwekezaji huu umefanyika katika nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Sudani Kusini, DRC, Zambia, Zimbabwe, Malawi, Msumbiji, Afrika Kusini, Japan, Korea Kusini, Qatar na Oman-Sohar. Uwekezaji huu ni muhimu katika kuziwezesha kampuni za kitanzania kuongeza wigo wa bidhaa zake katika soko la nje, kuwa shindani zaidi, na kuwezesha uhaulishaji wa teknolojia. Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa uwekezaji huu umefanyika katika sekta ya uzalishaji viwandani (chakula, vinywaji, saruji , usindikaji wa mazao ya kilimo, sukari); nishati na mafuta/gesi (uingizaji, uhifadhi na usambazaji wa petroli) na usafirishaji na ugavi (logistics), fedha (benki na huduma za kifedha ) na vyombo vya habari.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ukuaji wa uwekezaji nchini ni kielelezo kuwa mazingira ya biashara na uwekezaji yanaendelea kuimarika. Hatuna budi kuwashukuru na kuwapongeza champions wetu wa uwekezaji nchini ambao wamekuwa chachu kubwa ya kuvutia wawekezaji. Hawa ni Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado tuna fursa ya kukuza uwekezaji kwa kuendelea kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

### 2.4 Mapitio ya Sera ya Taifa ya Kuhamasisha Uwekezaji ya Mwaka 1996 na Kuandaa Mkakati wa utekelezaji

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Kuhamasisha Uwekezaji ya Mwaka 1996 na kuandaa Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya Mwaka 2026 ambayo iko hatua za kuidhinishwa. Sera hiyo imezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (Dira 2050), Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu (LTPP 2050) na Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP IV), na mazingira ya sasa ya uwekezaji na biashara nchini, Kikanda na Kimataifa. Aidha, Sera inalenga kuweka mazingira bora ya uwekezaji wa umma na binafsi nchini kwa kubainisha masuala muhimu yakiwemo; uratibu na ufanisi wa vivutio vya kikodi na visivyo vya kodi, upatikanaji wa ardhi iliyotayari kwa ajili ya uwekezaji, ushiriki mpana wa nchi katika minyororo ya thamani ya kikanda na kimataifa, ubunifu na uhamishaji wa teknolojia, vyanzo mbalimbali vya mitaji ikiwemo ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), Masoko ya mitaji na Hati fungani za watanzania waishio nje ya nchi (diaspora bonds).

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, Ofisi imekamilisha uandaaji wa Mkakati wa Taifa wa Uwekezaji 2026-2031 ambao upo katika hatua za kuidhinishwa serikalini. Mkakati huu unatoa mwongozo wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwekezaji 2026 ili kufanikisha malengo ya Dira 2050. Aidha, mkakati huu unatafsiri malengo ya maendeleo ya Taifa kuwa hatua zinazotekelezeka, zilizopangwa kwa mpangilio, na zenye mwelekeo wa matokeo, huku ukiweka mfumo thabiti unaoratibu nyenzo za mipango ya kitaifa, vipaumbele vya kisekta, na majukumu ya taasisi ili kuhamasisha uwekezaji endelevu na wenye matokeo makubwa. Utekelezaji wa Mkakati huu ni muhimu katika kuweka mazingira wezeshi kwa uwekezaji wa ndani na nje katika Sekta ya Umma na Binafsi ili kuweka msingi wa ukuaji endelevu wa uchumi kwa kuelekeza

uwekezaji kwenye sekta za kipaumbele zilizoainishwa katika Dira 2050.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** Usimamizi wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uwekezaji utafanywa kupitia mifumo ya utoaji taarifa iliyoainishwa wazi inayounganisha Wizara, Idara na Wakala za Serikali, taasisi kuu za uratibu, pamoja na vyombo vya kisheria vya usimamizi. Aidha, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mkakati huu utaunganishwa katika mifumo iliyopo ya ufuatiliaji na tathmini ya Wizara, Idara na Wakala husika, kwa kutumia mbinu zinazozingatia matokeo yanayolingana na Dira 2050.

### 2.5 Kuratibu na kusimamia Majadiliano ya Mikataba ya Uwili ya Kimataifa ya Uwekezaji (Bilateral Investment Treaties – BITs)

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi inaendelea na jukumu la kusimamia majadiliano na kuratibu utekelezaji wa mikataba ya uwili ya kukuza na kulinda uwekezaji. Hadi kufikia mwezi Machi 2026, Tanzania imesaini mikataba ishirini (20) kati ya hiyo, mikataba kumi (10) ipo katika hatua za utekelezaji, mikataba 8 haijaanza utekelezaji na mikataba miwili (2) imesitishwa. Aidha, Ofisi imepokea rasimu za mikataba mipya kutoka katika nchi nane (8) ikiomba kufanya majadiliano na kusaini mikataba nao. Nchi hizo ni Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Canada, Hungary, Indonesia, Qatar, Japan, Vietnam, na Urusi. Majadiliano hayo yako katika hatua mbalimbali.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** majadiliano ya Mikataba ya Uwili ya Kulinda na Kuhamasisha uwekezaji baina ya nchi mbili yaliyofanyika yamewezesha nchi kukuza mazingira bora ya uwekezaji duniani ambapo kupitia mikataba hiyo, nchi zilizohusika katika kushirikiana zimeweka misingi ya kisheria inayolinda haki za wawekezaji wa pande zote, kuongeza uaminifu, na kupunguza hatari za kisiasa na kiuchumi. Katika kuhakikisha nchi inanufaika na majadiliano hayo, Ofisi inakamilisha maandalizi ya Mkataba kifani (BITs-Model) ambao unatoa mwongozo katika majadiliano na kuweka masharti ya mkataba ambayo ni rafiki kwa mazingira ya Tanzania kwa kuzingatia sheria za nchi na miongozo ya kikanda na kimataifa.

## 2.6 Kuratibu na Kusimamia Uwekezaji Katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZ)

**47. *Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kusimamia uwekezaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi (SEZ) kupitia Mwongozo wa Uendelezaji na Usimamizi wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi wa Mwaka 2024. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya Miradi 19 imesajiliwa na kupewa leseni ya uendeshaji na ya uendelezaji. Miradi hii ina thamani ya dola za Marekani Milioni 331.51, ambayo inategemea kuzalisha ajira 11,762, na mauzo ya nje yanayokadiriwa kuwa dola za Marekani Milioni 885.23. Miradi hii ipo katika mikoa ya Iringa (1), Lindi (1), Njombe (3), Ruvuma (1), Dar es Salaam (1), Kilimanjaro (1), Pwani (3), Mtwara (5), Arusha (1), Dodoma (1) na Tanga (1). Wawekezaji wakubwa ni kutoka Tanzania, Uhispania, Marekani, China, Ubelgiji, Afrika ya Kusini, Uturuki, India, Dubai, Nevis (Bahari ya Karibiani), Eritrea, Singapore na Ethiopia. Aidha, ili kuongeza msukumo wa uwekezaji katika SEZ, Ofisi imebainisha SEZ tano (5) za kimkakati na kuweka vivutio maalum visivyo vya kikodi. SEZ hizo ni Bagamoyo Eco-Maritime City and Intermodal Transport Bagamoyo- Phase I hekta 152, Nala-Dodoma yenye ukubwa wa hekta 607, Kwala-Kibaha (hekta 40.5), Buzwagi-Kahama (hekta 1,333), na Upanuzi wa Benjamin William Mkapa –Mabibo-Dar es Salaam (hekta 1.3).

**48. *Mheshimiwa Spika,*** utaratibu huo wa kuwa na SEZ za kimkakati umeanza kuleta mafanikio ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2026 TISEZA imesaini mikataba ya ardhi na kampuni 27 kwa ajili ya kuwekeza katika maeneo hayo. Kampuni hizo zitawekeza katika viwanda vya: kutengeneza vifungashio vya chakula, uchakataji wa mazao ya kilimo (korosho, kahawa, viungo, na mafuta ya kula), uzalishaji wa bidhaa za chuma na chuma zilizochanganywa na madini mengine (ferro alloys), uzalishaji wa madawa pamoja na uunganishaji wa magari ya aina mbalimbali kwa kutumia teknolojia za kisasa. Miradi hii inategemea kuwekeza zaidi Shilingi Bilioni 797 na kuzalisha ajira zaidi ya 20,460 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.

## 2.7 Kuratibu Uhamasishaji na Uwezeshaji wa Uwekezaji wa Sekta Binafsi

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuhakikisha elimu na fursa za uwekezaji inatolewa na kutangazwa ipasavyo kwa wawekezaji wa ndani na nje, Ofisi kupitia TISEZA imefanya kampeni za Kitaifa ya kuhamasisha uwekezaji. Kampeni hizo ziliwezesha kuunganisha wazalishaji katika mnyororo wa thamani, kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji, kuelimisha wawekezaji kuhusu Kituo Kimoja cha Uwezeshaji Uwekezaji (One Stop Facilitation Centre - OSFC) kilichopo TISEZA, na kutoa elimu kuhusu vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi vinavyotolewa kwa wawekezaji wa ndani na nje baada ya kupata cheti cha uwekezaji kinachotolewa na TISEZA.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio yaliyopatikana kutokana na kampeni hizo ni: kuongezeka kwa usajili wa miradi mipya, kuongezeka kwa miradi ya upanuzi, pamoja na kuongezeka kwa usajili wa miradi katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi. Kwa mujibu wa Mwongozo wa Ufanyaji Biashara na Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2026 (Tanzania Business & Investment Guide, 2026), Ofisi kupitia TISEZA imesajili jumla ya miradi 915 yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 10.95. Miradi hiyo ipo katika sekta mbalimbali zikiwemo viwanda (manufacturing), ujenzi wa majengo ya biashara, usafirishaji, utalii na kilimo. Taarifa hiyo imebainisha pia kuwa nchi zilizoongoza katika uwekezaji kutoka nje (FDI) ni Falme za Kiarabu, China, India, Singapore na Ufaransa. Aidha, kwa mujibu wa taarifa zilizorekodiwa na TISEZA, miradi hiyo, inatarajiwa kuzalisha ajira zaidi ya 162,895.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, jumla ya miradi 60 ilisajiliwa kupitia Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZ) ambapo uwekezaji mkubwa upo katika sekta ya viwanda na unatarajiwa kuwekeza dola za Marekani milioni 499 pamoja na kuzalisha ajira 8,434. Katika miradi ya upanuzi, jumla ya miradi 45 ilisajiliwa katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 ikilinganishwa na miradi 36 katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Aidha, katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi, miradi minne (4) ilisajiliwa yenye thamani ya dola za Marekani milioni 145.34, ikitarajiwa kuwekeza katika sekta mbalimbali hususan kuongeza thamani ya mazao ya kilimo kama

parachichi na korosho, pamoja na kuzalisha ajira 4,411 na mauzo ya nje yanayokadiriwa kufikia dola za Marekani milioni 128.85.

**52. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha uwekezaji wa nje, Ofisi imeratibu na kuhudhuria makongamano/mikutano na majukwaa ya nje ya kuhamasisha uwekezaji katika nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), China, India, Marekani, Madagascar, Canada, Uingereza, Japan, Poland, Ethiopia, Uganda, Kenya, Nigeria, Qatar, Rwanda, Algeria, Uturuki, Msumbiji, Singapore, Angola na Misri. Kupitia makongamano na mikutano hii, Ofisi ilitangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini. Kupitia uhamasishaji huo, jumla ya miradi 12, yenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 182.07, ambayo inategemea kuzalisha ajira 6,619, na mauzo ya nje yanayokadiriwa kuwa Dola za Marekani Milioni 750.46 imesajiliwa. Baadhi ya nchi zilizotoa wawekezaji ni China, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), India, Ethiopia, Uturuki, Marekani, na Singapore. Aidha, katika uwekezaji wa jumla (General Investments). Miradi 386 iliweza kusajiliwa kutoka nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu, China, India, Marekani, Canada, Uingereza, Japan, Poland, Ethiopia, Uganda, Kenya, Nigeria, Qatar, Rwanda, Uturuki, Singapore, na Misri.

**53. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuwawezesha wawekezaji, Ofisi imeboresha upatikanaji wa huduma katika Kituo cha Pamoja cha Uwezeshaji Uwekezaji (One Stop Facilitation Centre - OSFC). Maboresho yaliyofanyika ni pamoja na ukarabati wa jengo la Ofisi na kuongeza idadi ya Wizara/Taasisi zinazotoa huduma kutoka 12 hadi 14 ikiwemo Wizara ya Kilimo na Tume ya Madini. Sambamba na kuongezeka kwa Wizara na Taasisi zinazotoa huduma, Ofisi inafanya jitihada kuhakikisha kwamba maafisa waliopo katika Kituo hicho wanaweza kufanya maamuzi. Jitihada hizo zimeanza kuleta mafanikio ambapo kwa sasa kuna Kamishna Msaidizi wa Ardhi mwenye hadhi sawa na Kamshna wa ardhi wa mkoa ambae anaweza kutoa hati ya umiliki wa ardhi. Aidha, Ofisi iliwatembelea wawekezaji zaidi ya 721 kwa lengo la kuangalia utekelezaji na maendeleo ya uwekezaji wa miradi yao (Aftercare Services).

**54. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza wigo wa utoaji wa huduma kwa wawekezaji, Ofisi kupitia TISEZA imeandaa

Mwongozo wa watoa huduma kwa wawekezaji (Investor's Service Provider - ISPs). Mwongozo huu umeweka vigezo na masharti kwa mtoa huduma. Hadi sasa, zaidi ya watoa huduma 100 wamesajiliwa, na kupata mafunzo ya namna ya kuwezesha uwekezaji na kutangaza fursa mbambali za uwekezaji zilizopo nchini.

Orodha ya watoa huduma hawa itawekwa kwenye tovuti na matangazo mbalimbali kwa ajili ya kuongeza uwazi na uwanda mpana kwa wawekezaji katika kuwachagua watoa huduma.

### 2.8 Maboresho ya Mifumo ya TEHAMA

**55. *Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kanzidata ya Taifa ya Uwekezaji (National Investment Data System). Mfumo huu unalenga kutatua changamoto ya upatikanaji wa takwimu sahihi za uwekezaji kutoka ndani na nje unaofanyika hapa nchini kupitia taasisi na sekta mbalimbali. Kwa ajili ya kupata takwimu sahihi na halisia za uwekezaji nchini, mfumo una moduli maalumu itakayowawezesha maafisa wa vitengo vya Biashara, Viwanda na Uwekezaji waliopo katika ngazi za mikoa na wilaya kuingiza taarifa za maendeleo ya miradi ya uwekezaji katika maeneo yao ikiwemo; hali ya mradi kwa wakati huo, kiasi cha mtaji uliowekezwa na idadi ya ajira. Mfumo umewezesha kuhifadhi taarifa za miradi ya uwekezaji iliyokusanywa na kuhakikiwa kutoka mikoa ya Mwanza (683), Mara (148), Shinyanga (163) na Simiyu (44). Ofisi itaendelea na zoezi la kukusanya na kuhakiki taarifa za miradi ya uwekezaji kutoka mikoa mingine.

### 2.9 Programu ya Vijana ya Huduma Jumuishi za Usaidizi wa upatikanaji wa vifaa/bidhaa na mauzo ya nje

**56. *Mheshimiwa Spika,*** Ofisi kupita TISEZA ilizindua Kituo cha Usaidizi wa Upatikanaji wa Vifaa/Bidhaa na Mauzo ya Nje mwezi Machi, 2026 katika Ofisi zilizopo Benjamin Mkapa SEZ, Mabibo – Dar es Salaam. Kituo hiki kimeanzishwa kwa ushirikiano kati ya TISEZA na kampuni ya Nexa International Centre. Kituo hiki kinatoa huduma kwa kipaumbele kwa wawekezaji wadogo na vijana, pamoja na wawekezaji wanaohitaji msaada katika kukuza

shughuli zao za biashara na uwekezaji. Aidha, Kituo kinalenga kuwezesha upatikanaji wa mitaji, masoko ya nje kwa bidhaa zinazozalishwa nchini, kurahisisha usafirishaji wa mizigo kuingia na kutoka nchini, pamoja na kuwezesha upatikanaji wa malighafi, mashine na vifaa muhimu kutoka kwa vyanzo sahihi.

### 2.10 Kuimarisha Uwekezaji wa Umma

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Ofisi kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina iliendelea kuimarisha usimamizi wa uwekezaji wa umma kupitia Mashirika na taasisi za Umma na hivyo kuchangia Mapato Yasiyo ya Kodi (Non-Tax Revenue – NTR) kwenye Mfuko wa Serikali. Katika mwaka wa fedha 2025/26 Ofisi kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ilipanga kukusanya mapato kiasi cha **Shilingi trilioni 1.69.** Hadi Machi, 2026 imefanikiwa kukusanya mapato yasiyo ya kikodi kiasi cha **Shilingi billioni 773.37** ikilinganishwa na mapato ya **Shilingi bilioni 664.53** kwa kipindi kama hiki kwa mwaka 2024/25. Mapato yaliyokusanywa hadi Machi, 2026 ni sawa na **asilimia 85** ya lengo la kipindi husika. Sehemu ya makusanyo iliyobaki inatarajiwa kupatikana katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025/26 ambapo kampuni ambazo Serikali ina hisa hutoa gawio baada ya kukamilisha ukaguzi wa hesabu na mashirika yanayotoa mchango wa asilimia 15 ya mapato ghafi hukamilisha kuwasilisha michango hiyo na malimbikizo yake.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2025 yamefanyika mabadiliko ya Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370 kwa kuondoa kifungu cha 8(1)(f) na kuongeza kifungu cha 9(1) ambacho kinaelekeza kuweka viwango tofauti kwa Wakala wa Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma ya kuchangia hadi asilimia 40 ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali kila mwezi badala ya utaratibu uliopo sasa wa kiwango kimoja cha asilimia 15 ya mapato ghafi kila robo mwaka. Mabadiliko ya Sheria yamefanyika ili kuhakikisha Uwekezaji wa Umma unaofanyika unakuwa na tija kwa Serikali.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi inaendelea na mkakati wa kufanya mageuzi katika utendaji wa Taasisi na Mashirika ya umma yenye lengo la kuboresha utendaji na kuongeza mchango wa mashirika

hayo katika Pato la Taifa. Ni matarajio yetu kuwa mchango wa Mashirika ya umma utaendelea kuongezeka kila mwaka kupitia mchango wa mapato yasiyo ya kodi katika Mfuko Mkuu wa Serikali, ajira na uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma na kufikia azma ya Mashirika ya Umma kuchangia asimilia nane (8) ifikapo 2050 katika uchumi wa nchi kama ilivyoainishwa katika Dira 2050.

**60. *Mheshimiwa Spika,*** Kwa ujumla wake, uwekezaji wa ndani wa Serikali kwenye mashirika, taasisi, wakala za Serikali na kampuni zinazomilikiwa kwa hisa chache umeongezeka kutoka shilingi trilioni 85.38 mwaka 2023/24 hadi kufikia shilingi trilioni 90.61 kwa mwaka 2024/2025 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia saba (7). Aidha, kwa upande wa uwekezaji wa Serikali nje ya nchi, hadi kufikia mwaka 2024/25, ulifikia shilingi trilioni 1.67, kutoka shilingi bilioni 846.22 zilizorekodiwa kwa mwaka 2023/24 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 98. Ongezeko hilo limetokana na mageuzi yanayofanyika katika utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma na jitihada kubwa zinazoendelea katika usimamizi wa uwekezaji wa Serikali katika Mashirika hayo na kampuni ambazo Serikali ina umiliki wa hisa chache. Kuongekeza kwa uwekezaji huo kuna faida mbalimbali ikiwemo: ongezeko la mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, kuimarika kwa huduma za kijamii kwa wananchi (afya, maji, elimu, na usafirishaji), miundombinu, biashara na ajira kwa Watanzania.

**61. *Mheshimiwa Spika,*** Katika kuendelea kuimarisha usimamizi wa uwekezaji katika mashirika ya umma, Serikali inakusudia kuwasilisha bungeni Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma. Pamoja na mambo mengine, muswada huu unalenga kuanzisha mamlaka ya usimamizi wa uwekezaji wa umma, kuanzisha mfuko wa taifa wa uwekezaji, kuzipa mamlaka na uhuru zaidi taasisi za umma zinazofanya biashara, na kuimarisha mazingira ya ushirikiano katika uwekezaji kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

**62. *Mheshimiwa Spika*,** Aidha, Serikali imeendelea kufanya tathmini ya utendaji na majukumu ya mashirika ya umma. Lengo la hatua hii ni kubaini mashirika ambayo majukumu yake yamepitwa na wakati, mashirika ambayo yanaingiliana

kimajukumu, na yale ambayo yamegeuka kuwa mzigo kwa walipa. Kufuatia tathmini ya utendaji na majukumu ya mashirika ya umma hatua stahiki huchukuliwa ikiwemo kufuta mashirika yanayobainika kuwa uwepo wake hauna tija na kuunganisha mashirika ambayo majukumu yake yanagongana, kuingiliana au kufanana.

**63. *Mheshimiwa Spika,*** Kufuatia tathmini ya utendaji na majukumu ya wa mashirika ya umma iliyofanyika mwaka 2023 Serikali ilielekeza kuunganishwa kwa mashirika ya umma 14 na kufuta mashirika mengine matatu. Hadi sasa mashirika matatu yalishafutwa na mashirika mawili kuunganishwa (TIC na EPZA ziliunganishwa na kuunda TISEZA). Serikali inaendelea na kukamilisha taratibu za kisheria kuunganisha mashirika yaliyobaki.

**64. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilifanya tathmini ya mali na miradi ya kimkakati katika sekta ya umma kumi na mbili (12). Miradi iliyofanyiwa ufuatiliaji na tathmini ni pamoja na Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi; Shamba la Kibiashara la Kilimo lililo chini ya usimamizi wa Chuo cha Kilimo cha Sokoine - SUA; Shirika la Masoko Kariakoo; Kituo cha Uwekezaji cha APC – kilichopo chini ya Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi; Chuo cha Taifa cha Usafirishaji; Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DSM); na Kampuni ya Ubungo Plaza (Serikali ni mwanahisa), Kiwanda cha Nguo cha Musoma (Musoma Textile Industries), Kiwanda cha Maziwa cha Musoma (Musoma Diarly), Hoteli ya Musoma (Musoma Hotel), Kiwanda cha Nyama cha Tanganyika Packers, na Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka (BRT).

**65. *Mheshimiwa Spika,*** tathmini hiyo ilibainisha mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji ikiwemo ajira kwa wananchi na kuongezeka kwa uzalishaji. Aidha, changamoto mbalimbali zilibainika ikiwemo kutokuendelezwa kwa baadhi ya viwanda na miradi kwa muda mrefu, utendaji usioridhisha kwa baadhi ya miradi na changamoto za sheria za manunuzi katika utekelezaji wa baadhi ya miradi. Kufuatia tathmini hiyo, Ofisi ilitoa mapendekezo kwa Wizara za Kisekta na Taasisi zinazohusika na miradi kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji wa miradi hiyo

inakamilika. Vilevile, Serikali imeanza kuchukua hatua za haraka ili kuimarisha usimamizi wa miradi hiyo kwa kuzingatia kuwa Serikali imewekeza fedha nyingi kwa lengo la kupata tija.

**66. *Mheshimiwa Spika,*** Ofisi kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imefanya uthamini wa mali mbalimbali zilizorejeshwa Serikalini, zikiwemo kiwanda kimoja cha Tembo Chipboards, mashamba matatu ya maua yaliyopo Arusha ambayo ni Malalua, Kili Flora Chekereni na Kili Flora USA River, shamba la Basuto lililopo Manyara, mashamba manne ya NAFCO yaliyopo West Kilimanjaro pamoja na shamba la KPL Mngeta lililopo Morogoro. Zoezi hili litaiwezesha Serikali kutafuta wawekezaji wenye tija katika mashamba na viwanda hivyo.

**67. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika, Ofisi kupitia Msajili wa Hazina imetekeleza ubinafsishaji wa viwanda sita (6) vilivyorejeshwa Serikalini ambavyo ni NMC Mzizima, NMC Isaka, CDA Intergrated Industry Limited, Kilimanjaro Paddy, Moshi Pesticides na Unique Steel Rolling. Taratibu za kisheria za ukamilishaji Mchakato wa ubinafsishaji unaendelea kwa kuzingatia taratibu na sheria husika ili kuhakikisha Serikali inanufaika ipasavyo na mali hizo. Aidha, Ofisi itahakikisha inaimarisha ufuatiliaji wa mashamba au viwanda ambavyo wawekezaji waliuziwa lakini hawajaendeleza ili kuchukua hatua stahiki za kuendeleza mashamba na viwanda hivyo.

**68. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 ilipanga kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Uratibu wa Uwekezaji wa Umma Nchni (National Guidelines for Coordination of Public Investment). Lengo la mwongozo huo ni kutoa mwelekeo wa Kisera kuhusu uratibu wa Uwekezaji wa Umma. Hadi Machi, 2026 rasimu ya mwongozo imekamilika na tayari umewasilishwa kwa wadau zikiwemo Wizara, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Taasisi za Umma, Sekta Binafsi na Wadau wa Maendeleo kwa ajili ya kutoa maoni yatakayosaidia uboreshaji wa mwongozo husika. Mwongozo huu utawezesha kuwa na uratibu mzuri wa Uwekezaji wa Umma hususan katika Mashirika na taasisi za Umma.

**69. *Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu Mkutano Mkuu wa Tatu wa mwaka wa Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi na

Mashirika ya Umma (CEO Forum 2025) kwa lengo la kuwakumbusha wajibu na msingi wa dhamana waliyopewa na Serikali katika kusimamia utendaji wa Taasisi za Umma. Mkutano huo ulifanyika tarehe 23 – 26 Agosti, 2025 jijini Arusha ambapo mgeni rasmi alikuwa ni **Mhe. Dkt. Philip Isdori Mpango,** Makamu wa Rais mstaafu akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkutano huo ulihudhuriwa na washiriki 650 ambapo mada mbalimbali ziliwasilishwa zikilenga kuwajengea uwezo na kuwapa uzoefu Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma. Mkutano huo ulikuwa na Kauli Mbiu isemayo ***"Ushirikiano endelevu katika mazingira ya ushindani wa kimataifa – nafasi ya Mashirika ya Umma"*** ambapo kwa mwaka 2024 kauli mbiu ilikuwa ***"Mikakati ya Taasisi na Mashirika ya Umma Kuwekeza Nje ya Tanzania''***

**70. *Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2025/26 Ofisi kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ilifanya mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi na Maafisa Watendaji Wakuu zaidi 200 ambazo Serikali ina umiliki wa hisa chache. Lengo la Mkutano huo lilikuwa ni kuwakumbusha umuhimu wao kwenye Bodi kwani Serikali ina mategemeo makubwa ya Makampuni hayo kuchangia utekelezaji wa DIRA 2050 kufikia GDP ya Dola za marekani Trilioni moja ifikapo 2050 kupitia gawio. Mafunzo hayo yalifanyika tarehe 16 – 18 Machi, 2026 jijini Arusha.

**71. *Mheshimiwa Spika,*** jitihada hizi za kufanya vikao vya mara kwa mara na wenyekiti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma pamoja na mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi kwa kampuni ambazo Serikali inaumiliki wa hisa chache ni afua muhimu ya kuwezesha kufikia shabaha ya Dira 2050 ya mchango wa mashirika ya umma wa asilimia 10 na asilimia 0.5 hadi 1 katika Pato la Taifa ifikapo ,mwaka 2030 kwa Mashirika ya Umma na Taasisi ambazo Serikali ina umiliki wa hisa chache mtawalia. 2.11 Kuimarisha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji

**72. *Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeratibu utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI). Kupitia Mpango huu, Serikali imelenga kuondoa vikwazo vinavyokwamisha uanzishwaji na uendeshaji wa biashara kwa kufanya mapitio ya sheria na kanuni ambazo sio rafiki kwa

biashara, kupunguza au kufuta tozo na ada zenye kero kwa wafanyabiashara, kuondoa mwingiliano wa majukumu miongoni mwa taasisi za udhibiti, pamoja na kuanzisha na kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya utoaji huduma ili kuongeza ufanisi, uwazi na urahisi wa kufanya biashara nchini. Hatua hizi zimekusudiwa kujenga mazingira rafiki, yanayotabirika na yenye ushindani zaidi kwa wawekezaji wa ndani na nje.

**73. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Ofisi imefanikiwa kufanya mapitio ya jumla ya sheria 28 zilizokuwa zinazorotesha mazingira ya biashara sambamba na kufuta au kupunguza jumla ya tozo na ada 245. Baadhi ya maboresho muhimu yaliyofanyika ni pamoja na kupunguza ushuru wa huduma (service levy) kutoka asilimia 0.3 hadi 0.25 ya pato ghafi kupitia Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, kupunguza ushuru wa hoteli kutoka asilimia 10 hadi 2, kufuta ada za upakiaji na upakuaji katika baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa, na kurejesha kanuni nafuu za usimamizi wa mazingira za mwaka 2021. Vilevile, Serikali imeimarisha udhibiti wa utozwaji wa ada na tozo kupitia marekebisho ya Sheria ya Bajeti na Sheria ya Fedha za Umma. Juhudi hizi zimesaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa biashara na kuongeza motisha kwa uwekezaji nchini.

**74. *Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imezijengea Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji zilizopo katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kuzipatia viti (693) na meza (693). Aidha, ununuzi wa kompyuta (desktop) 609 na vifaa vya kutunzia umeme (U.P.S) 609 umekamilika na vinatarajiwa kusambazwa ifikapo Juni, 2026. Upatikanaji wa vifaa hivi utaongeza ufanisi wa Idara hizo katika kuwahudumia wafanyabiashara na wawekezaji kwenye maeneo yao.

**75. *Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeandaa rasimu ya Mkakati wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji. Mkakati huo umejikita katika kufanya maboresho kwenye maeneo muhimu 11 ambayo ni: Ujuzi wa kazi, Maendeleo ya Rasilimali Watu, Mafunzo, Utafiti na Maendeleo; Upatikanaji wa Miundombinu na Huduma za Msingi za Umma; Muundo wa Taasisi, Uratibu na Mipango; Mabadiliko ya Mtazamo wa Kibiashara na Uwajibikaji; Uwekaji na

Matumizi ya Mifumo ya Kidijitali; Uanzishaji wa Biashara na Mazingira ya Uwekezaji; Maeneo na Majengo ya kufanyia Biashara na Uwekezaji; Upatikanaji wa Mitaji; Utatuzi wa Migogoro ya Biashara na Ufilisi wa Kampuni; Upatikanaji wa Masoko ya Ndani na Nje; na Ulinzi wa haki za ubunifu na miliki bunifu. Maboresho katika maeneo hayo yataiwezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa katika kuweka mazingira bora na wezesheji ya biashara na uwekezaji na hivyo kuvutia zaidi uwekezaji wa ndani na nje ya nchi.

## 3. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2025/26

### 3.1 Mwenendo wa Mapato na Matumizi hadi Machi, 2026 (Fungu 11, Fungu 07 Na Fungu 66)

#### 3.1.1 Makusanyo ya Maduhuli

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kupitia Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina iliidhinishiwa kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi trilioni 1.696.** Chanzo cha maduhuli ni gawio, michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi ya Taasisi zinazochangia, mapato yanayotokana na uendeshaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTMS), rejesho la riba na mikopo, ziada na mapato mengineyo.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2026, jumla ya **Shilingi bilioni 779.91** zilikusanywa sawa na **asilimia 85** ya lengo kwa kipindi hicho. Aidha, inatarajiwa kuwa sehemu iliyobaki ya makusanyo itapatikana katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025/26 ambapo kampuni ambazo Serikali ina hisa hutoa gawio baada ya kukamilisha ukaguzi wa hesabu na mashirika yanayotoa mchango wa asilimia 15 ya mapato ghafi hukamilisha kuwasilisha michango hiyo na malimbikizo yake.

#### 3.1.2 Bajeti iliyoidhinishwa

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 157.85** kwa Mafungu yote matatu (3). Fedha zilizoidhinishwa zinajumuisha

Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 134.34** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 23.51** ni kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi bilioni 111.82** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi bilioni 22.53 Matumizi ya Mishahara. Aidha, Fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha **Shilingi bilioni 14.55** fedha za ndani na Shilingi bilioni 8.95 fedha za nje.

### 3.1.3 Matumizi

**79. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mafungu yote matatu (3) imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 107.26** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 67.95** ya kiasi kilichoidhinishwa. Kati ya kiasi kilichopokelewa, **Shilingi bilioni 13.92** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi bilioni 87.10** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi bilioni 6.24** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, kati ya fedha zilizopokelewa kiasi cha **Shilingi bilioni 100** sawa na **asilimia 93.23** zilitumika.

## 4. MAPENDEKEZO YA VIPAUMBELE VYA MPANGO KWA MWAKA 2026/27

### 4.1 Utangulizi

**80. *Mheshimiwa Spika,*** Mapendekezo ya Vipaumbele na Mpango wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka 2026/27 yamezingatia malengo na matarajio yaliyoainishwa katika Dira 2050, Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2050, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Kufungua Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyotolewa tarehe 14 Novemba, 2025. Aidha, Mapendekezo haya yamezingatia majukumu ya mapya ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kama yalivyoainishwa katika mgawanyo wa majukumu ya Ofisi ulitolewa kupitia Gazeti la Serikali Na. 686 la tarehe 19 Disemba, 2025.

Majukumu haya yamehusisha maeneo ya maendeleo ya sekta binafsi, na kuratibu program za kuondoa umaskini nchini.

### 4.2 Kuratibu na kusimamia Utekelezaji wa Dira 2050

#### 4.2.1 Kuimarisha Matumizi ya Tafiti, Takwimu na Suluhu za Kiubunifu katika Upangaji na Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo

81. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi kupitia Tume ya Taifa ya Mipango inalenga kuhakikisha uandaaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo unazingatia matokeo ya tafiti. Msingi wa kipaumbele hiki unatokana na Tume kutekeleza kazi za: kuandaa Mwongozo wa Taifa wa Tafiti na Ubunifu ili kuweka utaratibu utakaowawezesha watafiti na wabunifu kufanya shughuli zao na kuchangia kikamilifu katika maandalizi na utekelezaji wa mipango; Kutayarisha Mfumo wa Kidijitali wa Tafiti (National Research Portal) ili kuhifadhi tafiti na kuchakata matokeo ya tafiti na kuibua mikakati ya kuzitumia kuleta mageuzi kiutendaji na kiutekelezaji na kufikia malengo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

82. ***Mheshimiwa Spika***, hatua hizo zitafuatiwa na kufanya Kongamano la Watafiti kila mwaka ili kujadili na kubadilishana uzoefu kuhusu kazi mbalimbali za tafiti zilizofanyika, mafanikio yaliyopatikana, changamoto zinazokabili watafiti pamoja na kuimarisha mahusiano na ushirikiano baina ya taasisi za utafiti ndani na nje ya nchi. Hivyo, matokeo ya tafiti na utambuzi wa vipaumbele *(prioritization)* yatawezesha uandaaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28; uandaaji wa moduli ya uchumi jumla *(macroeconomic policy framework);* uratibu wa maandalizi ya Mipango ya Mageuzi ya Sekta *(Sector Transformation Plans)* na Mipango ya Maendeleo ya Mikoa *(Regional Development Plans)*. Hatua hii inalenga kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa FYDP IV kwa kuweza kuwafikia wananchi kwa ngazi za mikoa na halmashauri.

83. ***Mheshimiwa Spika*****,** Ili kuimarisha ufungamanishaji wa Dira 2050 na Mipango mingine ya maendekeo (Mpango Elekezi 2025/26-2050/51 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

2026/27-2030/32) katika ngazi za Mikoa na Halmashauri na kuongeza ufanisi katika utekelezaji, Tume ya Taifa ya Mipango kupitia Mwongozo wa Uandaaji wa Mipango ya Taifa (National Planning Guidelines) umeelekeza Mikoa na Halmashauri hatua za kufuata katika uandaaji wa mipango ya uwekezaji na biashara. Hii inahusisha kuandaliwa Mipango ya Maendeleo ya Mikoa (Regional Development Plans - RDP) pamoja na Mipango ya Maendeleo ya Halmashauri (Council Development Plans – CDPs). Mipango hii inalenga kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa afua za kimkakati katika ngazi ya Mikoa na Halmashauri kwa kuzingatia fursa mahsusi na changamoto za kipekee katika maeneo hayo ya kiutawala. Hatua hii inalenga kuhakikisha matumizi yenye tija ya rasilimali zilizopo katika kila mkoa na Halmashauri, kufungamanisha malengo ya maendeleo na kuweka utaratibu unaowezesha upangaji wa pamoja kuanzia ngazi ya Taifa hadi Halmashauri. Kwa kutumia mwongozo huu, Mikoa na Halmashauri itaweza kuaanda wasifu wa kiuchumi (regional economic profile) katika maeneo yao ya utawala na kufungamanisha na mipango ya kitaifa ili kufikia malengo ya Dira 2050.

#### 4.2.2 Kufuatilia Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa

**84.** ***Mheshimiwa Spika*****,** baada ya kukamilika kwa uandaaji wa nyenzo za utekelezaji wa Dira 2050, Ofisi kupitia Tume ya Taifa ya Mipango itajielekeza katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa nyenzo hizo. Hatua hii itahusisha kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/27, programu za kielelezo saba (7) na miradi fungamanishi 38 iliyoainishwa katika mwaka 2026/27 kupitia Wizara za kisekta ili kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini unafungamanishwa na programu hizo. Ufuatiliaji huo utafanyika kupitia Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Mipango ya Maendeleo kwa lengo la kupata taarifa za miradi na programu za maendeleo kwa wakati na hivyo kuandaa taarifa za ufuatiliaji.

### 4.2.3 Kufuatilia Utekelezaji wa Maeneo Muhimu ya Vipaumbele vya Taifa

**85. *Mheshimiwa Spika,*** usimamizi wa utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo na za kipaumbele utaongozwa na matokeo ya maabara *(labs)* mbili (2) zitakazofanyika mwaka 2026/27. Maabara hizo ni Programu ya Mji wa Uwekezaji wa Bahari - Bagamoyo na Usafiri Fungamanishi (Bagamoyo Eco Maritime City and Intermodal Transport) pamoja na maabara ya kipaumbele cha kwanza cha FYDP IV kuhusu mageuzi ya utawala na mifumo ya sheria. Lengo la kufanyika kwa maabara hizo ni kubaini changamoto na utatuzi wake, kuandaa mpango wa kina wa utekelezaji kwa kila mradi, kuainisha muda wa utekelezaji na kuandaa viashiria vya utendaji kwa kila miradi.

### 4.2.4 Kutathmini Rasilimali za nchi

**86. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Ofisi kupitia Tume ya Taifa ya Mipango kwa kushirikiana na sekta husika itatathmini hali ya rasilimali za nchi katika sekta za maji, ardhi na madini ili kuwezesha uwekezaji wenye tija.

### 4.2.5 Kuimarisha Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa

**87. *Mheshimiwa Spika,*** Ofisi kupitia Tume ya Taifa ya Mipango itaendelea kuhakikisha matokeo ya farihisi ya mitazamo ya sekta binafsi katika maeneo saba inafanyiwa kazi kupitia ufuatiliaji katika sekta. Aidha, mpango kazi wa utekelezaji wa maeneo yatakayoibuliwa na sekta binafsi kupitia farihisi hii utaandaliwa. Sekta binafsi itapewa taarifa ya utekelezaji wa changamoto husika kupitia majadiliano na midahalo.

**88. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile Ofisi itaendelea kufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa hali ya uchumi kikanda na kimataifa ili kubainisha na kupendekeza hatua zitakazochukuliwa na Serikali katika usimamizi wa uchumi. Aidha, kutokana na uchambuzi huo, Tume ya Taifa ya Mipango itaandaa Mwongozo wa Mashirikiano ya Kiuchumi baina ya Tanzania na

nchi nyingine *(Economic Cooperation Framework)*. Hatua hii inalenga kubainisha vigezo vitakavyotumika katika ushirikiano wa Tanzania na nchi nyingine au taasisi za kikanda na kimataifa ili kufikia vipaumbele vya nchi kwa kuzingatia mipango ya maendeleo na Dira 2050. Kupitia mwongozo huo, Serikali itaimarisha uratibu wa mikataba ya ushirikiano kupitia Tume za Pamoja za Ushirikiano (Joint Permanent Commissions – JPC) ili kuhakikisha inaendana kikamilifu na mipango ya kitaifa, kuleta tija kwa uchumi, na kuchangia ustawi wa jamii. Hatua hii itaimarisha mshikamano wa sera, kuongeza ufanisi wa ushirikiano wa kimataifa, na hatimaye kufikia dhamira na malengo ya Dira 2050.

### 4.2.6 Kuendelea Kujenga Uelewa kwa Umma Kuhusu Dira 2050 na Majukumu ya Tume ya Taifa ya Mipango

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Taifa ya Mipango itaendelea kuelimisha umma, taasisi za Serikali na sekta binafsi kuhusu nafasi zao katika utekelezaji wa mipango ili kufikia shabaha za Dira 2050. Elimu kwa umma itajikita katika kubainisha majukumu na namna utekelezaji unafungamanishwa na majukumu ya taasisi nyingine za umma na sekta binafsi. Kipaumbele hiki kitatekelezwa kupitia utoaji wa elimu kuhusu Dira 2050 na nyenzo zake, utoaji wa taarifa za wazi *(publications)* kuhusu utendaji na ambavyo utekelezaji wa majukumu ya Tume umechangia katika maendeleo ya nchi na mabadiliko ya ustawi wa Taifa na wananchi kwa ujumla.

### 4.2.7 Kuendelea Kuimarisha Utendaji Kazi Kupitia Mifumo ya TEHAMA na Kuwajengea Uwezo Watumishi Katika Kusimamia Uchumi, Upangaji na Utekelezaji wa Mipango

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Taifa ya Mipango itaendelea kuimarisha utendaji kazi wake wa usimamizi wa uchumi, uandaaji wa mipango na usimamizi kupitia mifumo ya TEHAMA. Aidha, Tume itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwawezesha kupata mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika maeneo mbalimbali ya kitaalamu kama vile uchambuzi na usimamizi wa miradi, upangaji, utafiti

na ubunifu. Hatua hii inalenga kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu na kufikia malengo yanayotarajiwa.

### 4.3 Kuhamasisha, Kuwezesha na Kutoa Huduma kwa Wawekezaji wa Sekta Binafsi

#### 4.3.1 Mapitio ya Mwongozo wa Usimamizi na Uendelezaji wa Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (SEZ)

91. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Ofisi imejipanga kuhakikisha kuwa utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano (Five Year Development Plan-FYDP IV) ambao unatekeleza Dira 2050 unaleta mageuzi ya msingi ya kiuchumi, ikiwa ni pamoja na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda yenye ushindani kimataifa. Katika kufikia azma hiyo, Ofisi itafanya mapitio ya kina ya Mwongozo wa Usimamizi na Uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZ).

92. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mapitio hayo, Ofisi itafanya tathmini ya utekelezaji wa vivutio vilivyopo ili kubaini ufanisi wake na maeneo yanayohitaji maboresho. Msisitizo utawekwa katika kuhakikisha kuwa vivutio hivyo vinachochea uwekezaji mkubwa wa kimkakati unaoweza kuleta mageuzi ya viwanda, kukuza viwanda vidogo na vya kati, na kuongeza ajira kwa vijana. Lengo kuu ni kuiwezesha Tanzania kuwa kitovu cha uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya soko la ndani, ukanda wa Afrika Mashariki, na bara la Afrika kwa ujumla. Aidha, Mwongozo utapendekeza vivutio maalumu kulingana na maeneo ili kila mkoa uvutie wawekezaji kulingana na jiografia ya mkoa husika na fursa zinazopatikana. Vilevile, Mwongozo utajumuisha vivutio vya uwekezaji kwa wazawa ili kuleta hamasa na kuongeza kasi ya ukuaji wa uwekezaji wa ndani.

#### 4.3.2 Kuongeza kiasi cha Ardhi iliyoandaliwa kwa ajili ya Uwekezaji (Landbank)

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Ofisi itahakikisha uwepo wa ardhi ya kutosha iliyoandaliwa kwa ajili ya uwekezaji kwa kufanya utambuzi wa maeneo yenye sifa stahiki kwa uwekezaji, ulipaji wa fidia, uendelezaji wa miundombinu

wezeshi kama barabara, umeme, maji, gesi na mawasiliano. Aidha, Ofisi itahamasisha Sekta ya Umma na Binafsi kuwasilisha ardhi zao kwa ajili ya kutafutiwa wawekezaji. Taarifa kuhusu maeneo haya zitakusanywa na kuhifadhiwa kidigitali katika mifumo ya mawasiliano ya Ofisi na TISEZA ili kuwezesha wawekezaji kuzipata wakiwa mahali popote duniani.

### 4.3.3 Kuandaa Mkakati wa Kuvutia Uwekezaji wa Kimkakati katika Sekta ya Uunganishaji na Utengenezaji wa Magari

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi kwa kushirikiana na wadau itaandaa Mkakati wa kuvutia uwekezaji wa kimkakati katika sekta ya uunganishaji na utengenezaji wa magari. Hitaji hili limetokana na tathmini ya awali iliyofanywa na Ofisi kwa kushirikiana na Taasisi ya Africa Association Automotive Manufacturer (AAAM) ya Afrika ya Kusini ambayo ilionesha fursa kubwa ya kuvutia wawekezaji katika sekta hii. Mkakati utaainisha aina ya wawekezaji wanaolengwa, aina ya uzalishaji unaokusudiwa, pamoja na vivutio vitakavyowekwa ili kuhakikisha ushindani wa sekta hii katika ngazi ya bara la Afrika. Dhamira ni kuwa, ifikapo mwaka 2030 Tanzania iwe miongoni mwa vinara wa uzalishaji wa magari katika bara la Afrika.

### 4.3.4 Kuhamasisha mauzo ya nje

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi itaendelea kuhamasisha, kuwezesha na kutoa huduma kwa wawekezaji waliopo na wanaotarajia kuwekeza ndani ya Maeneo maalum ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje (EPZ). Katika kuvutia wawekezaji kuwekeza na kuzalisha bidhaa zinazokubalika katika masoko ya nje, Ofisi itaweka mikakati mbalimbali ikiwemo; kurahisisha usajili ndani ya EPZ, kuboresha miundombinu wezeshi, kuhamasisha ubora wa bidhaa ili kukidhi viwango vya kimataifa na kuhamasisha matumizi ya teknolojia mpya katika uzalishaji wa bidhaa.

### 4.3.5 Kuandaa Maeneo Maalum ya Uwekezaji kwa ajili ya Vijana

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi itatenga maeneo Maalumu ya Uwekezaji kwa ajili ya Vijana kupitia program ya *Youth Industrial Special Economic Zones* ambayo itawawezesha

vijana kupata ardhi kwa ajili ya kujenga viwanda (Industrial shades). Maeneo hayo yatatengwa katika Maeneo Maalum ya Uwekezaji yaliyopo katika mikoa ya: Dodoma (Nala, Ekari 100), Singida (Musisiri- Iramba, Ekari 100), Pwani (Kwala, Ekari 20), Mara (Bunda, Ekari 100), Ruvuma (Songea, Ekari 100) na Bagamoyo (Pwani, Ekari 20). Vijana wataweza kuwekeza kama watu binafsi au kwa vikundi, na wataweza kushiriki katika sekta mbalimbali.

**4.3.6 Kuandaa Kitabu cha Orodha ya Vivutio (Tax & Non Tax incentives compendium Book)**

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa wawekezaji, katika mwaka 2026/27, Ofisi itaandaa kitabu kimoja chenye orodha ya vivutio vinavyotolewa katika sekta mbalimbali ili kuwarahisishia wawekezaji kuvipata mahali pamoja. Taarifa katika Kitabu hiki zitahuishwa kila mwaka ili kujuisha mabadiliko mbalimbali ya vivutio yatakayokuwa yanajitokeza katika sekta.

**4.3.7 Uratibu wa Mikutano ya Kitaifa ya Uwezeshaji Wawekezaji (National Investment Facilitation Forums)**

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi itaratibu mikutano ya kitaifa ya uwezeshaji uwekezaji inayolenga kujadili na kutatua changamoto zinazoathiri uwekezaji nchini. Miongoni mwa maeneo yatakayojadiliwa yatahusu: sera na kanuni, masuala ya kodi, upatikanaji wa ardhi, vibali vya mazingira, miundombinu, na uratibu wa taasisi za Serikali.

**4.4 Kuimarisha Uwekezaji wa Umma**

**4.4.1 Kuendelea kufanya mageuzi na maboresho ya utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma**

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwa na Taasisi na Mashirika ya Umma yanayoweza kujiendesha kwa tija na kuchangia mapato katika Mfuko Mkuu wa Serikali na kutimiza malengo ya DIRA 2050, kwa kuboresha mazingira ya biashara nchini na kutoa

huduma bora kwa watanzania, Ofisi katika mwaka 2026/27 imepanga kutekeleza yafuatayo:

**4.4.1.1 Kukamilisha Sheria ya Uwekezaji wa Umma**

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa Fedha 2026/27 Ofisi itahakikisha Sheria ya Uwekezaji wa Umma inakamilika. Kutungwa kwa Sheria hiyo pamoja na mambo mengine kutawezesha Taasisi na Mashirika ya Umma kujiendesha kwa tija zaidi na hivyo kuchangia katika ukuaji wa Uchumi kulingana na malengo yaliyoainishwa katika Dira 2050.

**4.4.1.2 Upatikanaji wa Mitaji kwa ajili ya uwekezaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma**

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha upatikanaji wa mitaji kwa Taasisi na Mashirika ya Umma, Ofisi pamoja na mambo mengine imepanga kukamilisha taratibu za kuanzishwa kwa Mfuko wa Uwekezaji utakaokuwa na jukumu la kutafuta fedha kwa ajili ya mitaji ya uwekezaji kupitia mashirika ya umma. Vyanzo vya mfuko huu vitazingatia kigezo kikuu cha kutoathiri vyanzo vya msingi vya fedha kwa ajili Mfuko Mkuu wa Serikali.

**4.4.1.3 Kuimarisha Utaratibu wa Upatikanaji wa Watendaji Wakuu na Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma kwa njia ya Ushindani**

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupanua wigo wa kupata watendaji mahiri katika uendeshaji wa mashirika ya umma ili kuyapa mashirika haya uwezo wa kushindana kimataifa, katika mwaka 2026/27 Ofisi imepanga kuanzisha utaratibu wa upatikanaji wa watendaji wakuu au wajumbe wa vyombo vya usimamizi katika mashirika ya umma kwa ushindani bila kuathiri mamlaka ya mamlaka za uteuzi.

**4.4.1.4 Uhuru wa Kujiendesha kwa Mashirika Yanayofanya Biashara**

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwa na taasisi na mashirika ya Umma shindani Nchini katika mwaka 2026/27 Ofisi imepanga kuyapa

mashirika yanayofanya biashara uhuru wa kujitegemea ili kuweza kuongeza ufanisi na pia kuyawezesha kushindana katika soko la biashara katika sekta zao ndani na nje ya nchi. Hatua hii itayafanya mashirika ya kibiashara kuwa na sura kamili ya kampuni za kibiashara (corporate identity) ili yajiendeshe kwa tija na faida inayokusudiwa. Hata hivyo, uhuru huo utaambatana na uwekezaji wa vigezo vya utendaji kazi ambavyo vitasaidia upimaji wa utendaji wa mashirika hayo.

### 4.4.1.5 Kuendelea kufanya Tathmini ya Kina kuhusu Utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi katika mwaka wa fedha 2026/27 itaendelea na zoezi la tathmini ya utendaji wa Mashirika na taasisi za Umma na kuchukua hatua stahiki ikiwemo kuunganisha Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo majukumu yake yanashabihiana au kufuta Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo malengo ya kuanzishwa kwake yamepitwa na wakati au majukumu yake yanaweza kutekelezwa na Taasisi nyingine. Aidha, Ofisi itachukua hatua ya kuyarekebisha au kuyafuta mashirika ambayo yanakwamisha mazingira bora ya biashara nchini.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi la tathmini litaambatana na kuyapanga mashirika na taasisi hizo kulingana na majukumu yao ili kurahisisha usimamizi wenye tija wa Taasisi na Mashirika ya Umma. Tathmini itabainisha mashirika ya kibiashara, udhibiti na ya kutoa huduma na kupendekeza mfumo mzuri wa usimamizi na vigezo vya kupima tija na ufanisi wa kila taasisi kwa kuzingatia muktadha wa majukumu yake. Ni matarajio ya Ofisi kuwa na Mashirika ya Umma machache yatakayoendeshwa kwa tija ikiwa ni pamoja na: kuongeza ajira, kuongeza mapato katika Mfuko Mkuu wa Serikali na kuchangia ukuaji wa uchumi kwa ujumla.

***106.* Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2026/27 Ofisi itaendelea na majukumu ya kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utendaji kwa kuhuisha miongozo ya usimamizi wa utendaji kwa Mashirika na Taasisi za Umma ili kuongeza tija na kupunguza utegemezi katika bajeti ya Serikali; kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika taasisi na mashirika ya umma, kufanya Tafiti na Uchambuzi wa Kiuchumi na Uwekezaji wa Taasisi za Umma kwa lengo la kubaini

fursa za uwekezaji pamoja na fursa za ufadhili wa uwekezaji na kuboresha mseto wa uwekezaji (investment portfolio mix) wa Serikali kupitia marekebisho ya kimuundo (restructuring) na upanuzi wa uwekezaji wenye tija.

### 4.5 Kuimarisha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji

#### 4.5.1 Kuanzisha Mpango wa Kupima Utendaji wa Sekretariati za Mikoa kwa Kuzingatia Kigezo cha Kuhamasisha, Kuwezesha na Kuhudumia Uwekezaji na Kukuza Biashara

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuchochea uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji, Serikali itaanzisha programu ya kuvutia uwekezaji katika kila mkoa. Kupitia programu hiyo, Mikoa itapimwa kwa kuzingatia vigezo vya kuhamasisha, kuwezesha, kulinda na kuhudumia wawekezaji. Lengo ni kupima maendeleo ya maboresho ya mazingira ya biashara na uwekezaji kwa ngazi ya mikoa na kulinganisha utendaji kati ya sekta mbalimbali kwa kuzingatia maeneo ya kijiografia. Motisha itatolewa kwa Mikoa itakayofanya vizuri ili kuwa na muendelezo wa uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

#### 4.5.2 Kuandaa Mapendekezo ya Sheria ya Uwezeshaji Biashara

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imepanga kuandaa Mapendekezo ya Sheria ya Uwezeshaji Biashara (Business Facilitation Act) itakayosaidia kurahisisha majukumu ya udhibiti; kudhibiti adhabu na ukaguzi usio wa lazima; na kusaidia urasimishaji wa biashara na kuongeza wigo wa kodi. Sheria hii itatumika kama chachu ya kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuongeza ushindani wa nchi kimataifa.

#### 4.5.3 Kukamilisha na kuanza kutekeleza Mkakatai wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Ofisi itakamilisha na kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji, kwa lengo la kuondoa vikwazo vinavyokwamisha uanzishwaji na uendeshaji wa biashara na uwekezaji.

## 4.6 Kuimarisha Sekta Binafsi Katika kuchukua nafasi yake kama injini ya maendeleo ya uchumi

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mageuzi ya uchumi wa Tanzania hayatachochewa tu na sera tunazoziandaa, bali pia na uimara, ushindani, na imani ya sekta yetu binafsi. Ni wakati sasa wa kuelekeza nguvu zetu katika utekelezaji madhubuti, uratibu thabiti, na matokeo yanayopimika. Ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi unabaki nguzo kuu ya maendeleo ya taifa, na utekelezaji wa vipaumbele hivi kwa mwaka wa fedha 2026/27 unalenga kuhakikisha Tanzania inachukua nafasi thabiti kikanda na kimataifa, ikichochea ukuaji wa uchumi, ajira, na uwekezaji endelevu.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza fikra hizi za kimageuzi, Ofisi itahakikisha inaimarisha ushirikishwaji jumuishi wa Wajasiriamali Wadogo sana, wadogo na wakati ( Micro, Small, Medium Entreprises - MSMEs), vijana, wanawake, na wadau wa ngazi zote kutoka ngazi ya Taifa hadi Wilayani. Aidha, Ofisi inaiona Sekta Binafsi kama mbia muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo nchini. Hivyo, Ofisi itafanya tathmini na kuandaa Taarifa ya Hali ya Sekta Binafsi Tanzania (The State of Private Sector in Tanzania Report) ili kutoa takwimu na uchambuzi unaotegemea ushahidi, kufuatilia utendaji na matokeo ya mageuzi, na kusaidia maamuzi ya kitaifa ya mipango na sera.

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** wakati umefika sasa wa kufanya mageuzi ya msingi katika mfumo wa majadiliano kati ya Serikali na sekta binafsi; hatuwezi kuendelea na mfumo usio jumuishi unaowaacha pembeni wahusika wakuu wa uchumi wetu ambao ni biashara ndogo na za kati, sekta isiyo rasmi, vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa sababu bila kuwapa nafasi ya moja kwa moja katika maamuzi, tunazuia kwa mikono yetu wenyewe kasi ya ukuaji wa uchumi na kupunguza tija ya sera tunazozitunga.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi za Sekta Binafsi zinapaswa kuwa chombo madhubuti chenye uwakilishi wa kitaifa kuanzia ngazi ya Mikoa na Serikali za Mitaa, kinachokusanya na kuwasilisha sauti halisi ya wafanyabiashara na wawekezaji wa Tanzania, na kinachotumia ushahidi na takwimu katika kufanya maamuzi

yenye matokeo ya haraka na yanayopimika. Ofisi itaboresha mifumo ya majadiliano kati ya Serikali na Sekta Binafsi kwa kuhakikisha uwakilishi jumuishi na ufuataliaji madhubuti wa utekelezaji wa makubaliano ya maboresho.

### 4.7 Kuratibu Programu za Kuondoa Umasikini

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu ina programu mbalimbali za kuondoa umasikini ambazo zimekuwa zikiratibiwa na kutekelezwa na sekta mbalimbali. Katika kutekeleza jukumu lake jipya ililokasimiwa, Ofisi itafanya uchambuzi wa kina wa programu zinazotekeleza afua zinazolenga kuondoa umasikini nchini ambazo zinatekelezwa kupitia sekta husika. Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na Taasisi za utafiti, itaandaa Taarifa ya Hali ya Umasikini nchini kwa lengo la kutambua ni kwa kiasi gani programu zinazotekelezwa zimechangia katika kuondoa umasikini.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kuwa na uratibu thabiti wa programu za kuondoa umasikini nchini, Ofisi itaandaa Mfumo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Umaskini (National Poverty Monitoring Framework). Mfumo huo, pamoja na mambo mengine, utajumuisha: viashiria vya kupima umaskini, mifumo ya ukusanyaji wa takwimu, uratibu wa taasisi, uchambuzi na utoaji wa taarifa, pamoja na matumizi ya matokeo katika kupanga na kutekeleza sera na bajeti. Viashiria hivyo vitasaidia kuhakikisha kuwa taarifa sahihi zinapatikana na kutumika katika kufanya maamuzi kwa maendeleo ya nchi yetu.

## 5. MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/27

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuweza kutekeleza vipaumbele vya Mpango wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2026/27, sasa ninaomba kuwasilisha rasmi Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Ofisi kwa mwaka 2026/27 kwa muhtasari ufuatao:

## 5.1 Mapato

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27 Ofisi kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina - Fungu 007 imepangiwa kukusanya na kuchangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya **Shilingi trilioni 1.79** kutoka kwenye vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi kupitia gawio, michango ya **asilimia 15** ya mapato ghafi, gawio, mapato yatokanayo na Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTMS); rejesho la riba na mikopo, ziada na mapato mengineyo.

## 5.2 Matumizi

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji na Taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako tukufu lipokee, lijadili na kuidhinisha jumla ya **Shilingi 144,850,349,000** ikiwa **Shilingi 126,018,699,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 18,831,650,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2026/27. Uchambuzi wa kina wa matumizi kwa kila Fungu umeainishwa katika **Jedwali Na. 1.**

**Jedwali Na. 1:** Matumizi kwa Fungu 11; 07; na 66

| Na. | Fungu 011: Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji | |
|---|---|---|
| i) | Matumizi ya Kawaida | 26,244,864,000 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | 9,141,447,000 |
| | **Jumla Ndogo A** | **35,386,311,000** |
| ii) | **Fungu 066: Tume ya Taifa Mipango** | |
| | Matumizi ya Kawaida | 39,322,083,000 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | 9,319,512,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **48,641,595,000** |
| iii) | **Fungu 07: Ofisi ya Msajili wa Hazina** | |
| | Matumizi ya Kawaida | 60,451,752,000 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | 370,691,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **60,822,443,000** |
| Jumla Kuu - Matumizi ya Kawaida | | 126,018,699,000 |
| Jumla Kuu - Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | | 18,831,650,000 |
| **Jumla Kuu kwa Mafungu Yote** | | **144,850,349,000** |

## 6. HITIMISHO

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyotangulia kusema awali, Mkutano huu wa Bunge la Bajeti ni wa kwanza katika kuanza utekelezaji wa Dira 2050 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Muda Mrefu (LTTP 2050), Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo (FYDP IV) na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2026/27. Pia, ni mkutano wa kwanza katika kuanza utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2025 kupitia bajeti mbalimbali za kisekta. Tunalo jukumu kubwa katika kuweka misingi imara ya kufikiwa kwa malengo na matarajio ya Dira 2050.

**120. *Mheshimiwa Spika,* Ninapohitimisha hotuba yangu, ninaomba kusisitiza mambo Matano.**

- Mosi, ni kweli nchi yetu imejaliwa raslimali nyingi za asili, ikiwemo ardhi, madini, maji, misitu, na Wanyama. Hata hivyo, ili raslimali hizi zilete tija na kuchochea maendeleo ya uchumi ni lazima zikutane na mitaji na teknolojia. Hivyo, basi tusiogope wala kuona aibu kutumia mitaji na teknolojia kutoka nje kwa lengo la kuendeleza raslimali zetu katika kufanikisha malengo yetu ya kiuchumi na kijamii. Kufanikisha tunahitaji kuendelea kuelimisha miongoni mwa watendaji wa serikali na jamii kwa ujumla katika kuendelea kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili wawekezaji walete mitaji na teknolojia nchini.

- Pili, ni muhimu kuendelea kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kutekeleza malengo yetu ya kiuchumi. Ni muhimu kwa sekta ya umma na sekta ya umma tukajiona kuwa timu moja inayohitaji. Ushindi wa timu moja hutegemea ushirikiano wa wachezaji. Tuwe na lengo na juhudi za pamoja; tukiwa na sauti moja tutakuwa na wimbo mzuri wenye mvumo.

- Tatu, ni muhimu tujenge uthubutu wa kujaribu mapya na kujenga utamaduni wa kutenda

- Nne, Dhima ya uongozi wowote hatimaye ni maendeleo ya uchumi na maisha ya watu. Hivyo, kila hatua tunayochukua na kila nadharia tunayoifikiria ilenge katika kukuza uchumi na kuboresha maisha ya watu. Hili ni somo ambalo hata Mwalimu Nyerere alijifunza baada ya kutoka katika madaraka. Kwa maneno yake alipata kusema: *if I were to become president again, I am sure we could do a lot of things". "I have learnt one important lesson. Wherever I have gone, I have been reminded that you can't have a good philosophy, idea or theory to restructure a society if that philosophy, idea or theory is not translated into the tummy, bread and butter".*

- Tano, sisi ni Taifa linalomuamini Mungu na tunamuomba sana Mungu kila siku. Hili ni jambo jema sana. Hata hivyo, lazima tutambue kuwa maendeleo hayateremshwi na Mungu. Viongozi na wananchi lazima kujenga imani kwamba maendeleo ni matokeo ya bidii ya kazi. Tujenge utamaduni na nidhamu ya kuchapa kazi kama njia pekee ya kupata maendeleo yetu kama wanadamu, kama jamii na kama Taifa.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** Nihitimishe kwa kuwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Taasisi zake kwa kufanikisha maandalizi ya Hotuba ya Bajeti ninayoiwasilisha. Kwa umuhimu wao ninaomba niwataje kama ifuatavyo: **Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya (Mb),** Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; **Dkt. Tausi Mbaga Kida,** Katibu Mkuu - Mipango na Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango; **Dkt. Fred Matola Msemwa,** Katibu Mkuu - Uwekezaji; N**dugu Nehemiah Kyando Mchechu**, Msajili wa Hazina; **Ndugu Gilead John Teri,** Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania; **Menejimenti na Watumishi wote** wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. **Asanteni sana kwa ushirikiano wenu!**

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ninawashukuru wadau wa ndani na nje ya nchi kwa michango yao iliyosaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, pamoja na taasisi zilizo chini yake wakiwemo: Benki ya Dunia; Umoja wa Ulaya; Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto

(UNICEF); TradeMark Afrika; Gatsby Africa; Sekta Binafsi ya Tanzania (TPSF); Chemba ya Biashara ya Taifa (TNCC); na Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania (CTI).

Aidha, Ofisi inazishukuru Wizara zote za Kisekta, Idara Zinazojitegemea, Taasisi, Mashirika ya Umma na Wakala za Serikali (MDAs); Sekretarieti za Mikoa (RSs); na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) ambazo zimekuwa zikiwezesha Ofisi kutekeleza majukumu yake yanayohusu mipango na uwekezaji kwa nyakati tofauti. Ushirikiano wenu umechangia katika kuimarisha mipango ya kitaifa na sekta ya uwekezaji kupitia utekelezaji wa afua mbalimbali za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa umuhimu wa kipekee kabisa, ninayashukuru makampuni mbalimbali, ya ndani na kutoka nje ya nchi, yaliyowekeza na yanayoendelea kuwekeza nchini mwetu. Uwekezaji wao ndio roho ya uchumi wa nchi yetu. Tunawatambua, tunawathamini na tutaendelea kuwapa kila aina ya huduma wanayohitaji ili waendelee kufanikiwa katika uwekezaji wao kwani kufanikiwa kwao ndio kufanikiwa kwetu kama nchi.

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Ofisi ambayo ni www.popi.go.tz

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baada ya maelezo hayo, sasa ninaomba Bunge likubali kujadili na kupitisha makadirio ya mapato ya **Shilingi 1,792,228,000,000** na matumizi ya jumla ya **Shilingi 144,850,349,000** kwa ajili ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2026/27. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 126,018,699,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 18,831,650,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kwa niaba yake nimwite Mheshimiwa Zena Maulidi Katambo.

**MHE. ZENA M. KATAMBO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, ili kwa niaba ya Mwenyekiti na Wajumbe wote niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, naomba taarifa hii ya Kamati, iwekwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard* kama ilivyowasilishwa mezani kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa taarifa hii umegawanyika katika sehemu kuu tano, kama zilivyoainishwa katika ukurasa wa nne wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa Kamati kufanya uchambuzi kuhusu utekelezaji wa bajeti hii kwa mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2026/2027 unatokana na masharti ya Kanuni ya 121(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2025. Kanuni hiyo, inaeleza utekelezaji wa makadirio hayo, kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawanda ya uchambuzi; katika uchambuzi huo, Kamati ilipokea kujadili na kuchambua jumla ya mafungu matatu ambayo ni Fungu Namba 07, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu Namba 11, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Fungu Namba 66, Tume ya Taifa ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026; uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezajii wa bajeti ya mwaka 2025/2026 ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji umeangazia maeneo makuu manne ambayo ni makusanyo ya maduhuli kuanzia Januari, 2025 hadi Februari, 2026; upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ya maendeleo kuanzia Julai, 2025 hadi Februari, 2026; ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026; na uzingatiaji wa maazimio ya Bunge yaliyotolewa kupitia Taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli; Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji katika mwaka wa fedha 2025/2026 ilipangiwa kukusanya mapato ya kodi kiasi cha shilingi trilioni 1.6 kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina kutokana na vyanzo mbalimbali ikiwemo michango ya 15% ya mapato ghafi ya mashirika ya umma, yenye sifa ya kutoa gawio na rejesho la riba na mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Februari, 2026 Ofisi imekusanya kiasi cha shilingi bilioni 716.06 sawa na 42.21% badala ya kiwango kinachotakiwa kufikiwa cha 66.7% ifikapo mwezi Februari. Ofisi ya Msajili wa Hazina, inategemewa na Serikali katika kuhakikisha maduhuli ya fedha za Serikali yanakusanywa kikamilifu. Kushindwa kukusanya maduhuli kwa kiwango kinachojitosheleza, kunaathiri uwezo wa Serikali wa kutoa huduma za kijamii kwa wananchi. Ili kutoathiri uwezo wa Serikali katika kuwafikishia huduma wananchi, Kamati inashauri kwamba Ofisi ya Msajili wa Hazina, iongeze kasi na kubuni mikakati itakayowezesha ukusanyaji wa maduhuli kufikia lengo la mwaka wa fedha 2025/2026. Maelezo zaidi kuhusu makusanyo ya maduhuli, yanapatikana Katika ukurasa wa saba na wa nane wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo hadi kufikia mwezi Februari, 2026; mwenendo wa upatikanaji wa fedha za bajeti kwa mafungu matatu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ni kama ifuatavyo:-

Fungu Namba 07, Ofisi ya Msajili wa Hazina; awali Ofisi ya Msajili wa Hazina iliidhinishiwa bajeti ya shilingi bilioni 62.3 fedha hizo zinajumuisha matumizi ya kawaida ya shilingi bilioni 60.6 na miradi ya maendeleo shilingi bilioni 1.67. Hata hivyo, mwezi Februari, 2026 bajeti ya Ofisi hii iliongezewa fedha za *OC* kwa ajili ya matumizi maalum kiasi cha shilingi bilioni 12.22 na hivyo kuongeza bajeti ya ofisi kwa mwaka 2025/2026 kufikia shilingi bilioni 72.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa ongezeko hili la bajeti, lilitokana na mahitaji maalumu yaliyojitokeza ikiwemo kugharamia gharama za *UDART* kuingiza nchini mabasi mapya ya mwendokasi. Katika utekelezaji wa bajeti hiyo, hadi kufikia mwezi Februari, 2026 Ofisi ya Msajili wa Hazina ilipokea fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida jumla ya shilingi bilioni 54.23 sawa na 74% ya kiasi kilichoidhinishiwa. Kiasi hicho kinajumlisha fedha za mishahara shilingi bilioni 4.48 fedha kwa ajili ya *OC* ya kuendeshea ofisi, shilingi bilioni 30.228 na fedha kwa ajili ya *OC* ya matumizi maalum shililngi bilioni 18.904. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo hadi kufikia mwezi Februari, 2026 ofisi hii ilipokea jumla ya shililngi bilioni 1.67 kiasi ambacho ni 100% ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa fedha katika Fungu Namba 07, Ofisi ya Msajili wa Hazina, ilikuwa ya kuridhisha. Ni matumaini ya Kamati kuwa kutokana na kupokea kiasi kinachotosheleza bajeti iliyotengwa, ofisi hiyo itatekeleza majukumu yaliyoainishwa kwa ufanisi. Maelezo zaidi kuhusu mapokezi ya fedha katika ofisi hii yanapatikana Katika ukurasa wa nane hadi wa tisa wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Namba 11, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 34.87 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 22.39 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, zikijumuisha

mishahara shilingi bilioni 8.7 na *OC* shilingi bilioni 13.7. Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya mendeleo ni shilingi bilioni 12.475 zikijumuisha fedha za ndani shilingi bilioni 6.183 na fedha za nje shilingi bilioni 6.29.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya matumizi ya kawaida inayojumuisha mishahara na *OC* hadi kufikia mwezi Februari, 2026 ofisi hiyo ilipokea jumla ya shilingi bilioni 12.35 sawa na 55.17% ya kiasi kilichoidhinishwa. Kwa upande wa fedha za maendeleo, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ilipokea jumla ya shilingi bilioni 2.6 sawa na 20.88% ya fedha iliyoidhinishwa ambapo kiasi hicho kinajumuisha fedha za ndani shilingi bilioni 1.51 na fedha za nje shilingi bilioni 1.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini inaonesha kuwa kiasi cha fedha za maendeleo kilichopokelewa si cha kuridhisha. Endapo hali hiyo itaendelea hadi ifikapo mwezi Juni, 2026 wakati wa kuhitimishwa kwa bajeti ya mwaka wa fedha 205/2026 ni dhahiri kuwa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka huu haitakamilika. Maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa Fungu Namba 11 yanapatikana katika ukurasa wa 10 hadi wa 13 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Namba 66, Tume ya Taifa ya Mipango; kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Tume ya Taifa ya Mipango iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 48.51 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 39.14 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 5.145 ni mishahara na shilingi bilioni 34 ni kwa ajili ya *OC*. Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo zilitengwa shilingi bilioni 9.36.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2026 fedha za matumizi ya kawaida zilipokelewa jumla ya shilingi bilioni 22.56 sawa na 57.64% ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo hadi Februari, 2026 Tume ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 1.96 sawa na 20.9% ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha za bajeti katika Tume ya Taifa ya Mipango kwa ajili ya miradi ya maendeleo hauridhishi. Uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa

kiasi kikubwa cha fedha za maendeleo zilizoainishwa, zililenga kutekeleza mradi wa kufanya tafiti zitakazoarifu maandalizi ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kuwezesha utendaji wa majukumu kupitia mifumo ya TEHAMA na uchambuzi wa maandiko wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupokelewa kwa fedha za miradi hiyo kwa 20.9% tu kuna athari kwa Tume ya Mipango ya kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Ni muhimu fedha hizo zikatolewa kikamilifu ili kuiwezesha Tume ya Taifa ya Mipango kufanya kazi ya kuandaa mipango ya nchi kwa ukamilifu pamoja na kusimamia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzii wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026; Kamati ilitembelea mradi mmoja unaohusu Kongani Maalum ya Uwekezaji wa Buzwagi, unaotekelezwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo unajulikana kama *Buzwagi Special Economic Zone* na ulitangazwa rasmi kuwa Ukanda Maalum wa Uwekezaji kupitia Tangazo la Serikali Namba 142 la tarehe 3 Machi, 2024. Eneo hilo lilikabidhiwa kwa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama baada ya shughuli za uchimbaji wa madini kufungwa mwaka 2021. Aidha, Taasisi ya *TISEZA* imepewa kazi ya kutoa ushauri wa kitalaam ili kuwezesha uwekezaji kufanyika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipotembelea na kukagua mradi huo ilibaini uwepo wa miundombinu iliyoachwa na kampuni iliyokuwa ikichimba madini katika eneo hilo. Baadhi ya miundombinu hiyo ni pamoja na majengo, barabara, kiwanja cha ndege, mitambo ya umeme yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa megawati 48, mifumo ya ulinzi na maji. Uwepo wa miundombinu hiyo ni kichocheo cha kuvutia uwekezaji katika eneo hilo. Mbali na miundombinu hiyo ukaguzi wa Kamati ulishuhudia utekelezaji wa miradi mingine ikiwemo mradi wa kuzalisha maji kiasi cha lita milioni 10 kwa siku kwa lengo la kuchochea mazingira bora ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa eneo hilo limepangwa kutumika kwa ajili ya shughuli sita za uwekezaji na huduma. Shughuli hizo ni vyuo vya ufundi, viwanda, uchenjuaji wa madini, uzalishaji wa nishati jadidifu, shughuli za ujenzi na makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na lengo hilo jema, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa bado kuna masuala mbalimbali yanayopaswa kutazamwa na kupatiwa ufumbuzi ili kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji katika eneo hilo. Maelezo zaidi kuhusu masuala haya yanapatikana katika ukurasa wa 16 hadi 20 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati; wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2025/206; Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa bajeti ya ofisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati. Licha ya utekelezaji huo mzuri, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa, maagizo yenye mwendelezo wa utekelezaji yaendelee kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027; uchambuzi wa mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ulijikita katika maeneo makuu mawili ambayo ni makadirio ya makusanyo ya maduhuli na makadirio ya matumizi ikijumuisha matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Uchambuzi kuhusu maeneo hayo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makadirio ya makusanyo ya maduhuli; katika mwaka wa fedha 2026/2027, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji kupitia Fungu Na. 07; Ofisi ya Msajili wa Hazina inaomba kuidhinishiwa kukusanya mapato yasiyo ya kodi jumla ya shilingi trilioni 1.79 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Kiasi hicho ni ongezeko la shilingi bilioni 95.9, sawa na 5.66% ikilinganishwa na makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ambapo iliidhinishwa shilingi trilioni 1.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuongeza kiwango cha maduhuli kwa mwaka ujao kwani ikiwa ukusanyaji wake utafikia leo utasaidia kupatikana kwa fedha ambazo zitatumika kufikisha huduma za kijamii kwa wananchi wa hivyo kuboresha ustawi wao. Maelezo zaidi kuhusu makadirio ya maduhuli yanapatikana katika ukurasa wa 21 hadi 23 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027; katika mwaka wa fedha 2026/2027, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji katika mafungu yake matatu inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 144.85. Kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 126.02 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha shilingi bilioni 22.42 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 103.6 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 18.83 kinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti inayoombwa kwa mwaka 2026/2027 imepungua kwa kiasi cha shilingi bilioni 13 sawa na punguzo la 8.2% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/2026. Uchambuzi umebaini kuwa punguzo hilo linatokana na fedha za matumizi ya kawaida kupungua katika mwaka 2026/2027 ambapo kiasi kinachoombwa ni shilingi bilioni 126.02 wakati katika mwaka wa fedha unaoisha wa 2025/2026 ziliombwa shilingi bilioni 134.34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi zaidi wa Kamati unaonesha kuwa fedha za mwaka 2025/2026 kwa matumizi ya kawaida ziliongezeka zaidi kupitia Fungu Namba 07 Ofisi ya Msajili wa Hazina kutokana na nyongeza ya bajeti iliyotokea mwezi Februari, 2026 ambapo ziliongezwa shilingi bilioni 12.22 katika fedha za *OC* za matumizi maalum kwa ajili ya kugharamia mabasi mapya ya mwendokasi. Maelezo zaidi kuhusu makadirio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 yanapatikana katika ukurasa wa 23 hadi 26 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati; ili kusaidia Serikali katika utekelezaji mzuri wa bajeti hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri na maoni ya jumla; kwa kuwa utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo unasuasua, na kwa kuwa kusuasua huko kunaathiri Wizara na taasisi zake kushindwa kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopangwa, hivyo basi, Serikali ihakikishe fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mwaka 2025/2026 zinatolewa kikamilifu katika muda uliobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri na maoni mahsusi; Fungu Namba 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina; kwa kuwa ukusanyaji wa maduhululi ya Serikali unatokana na mchango wa 15% ya mapato ghafi ya mashirika umepungua katika mwaka wa fedha 2026/2027, na kwa kuwa makadirio ya mwaka 2026/2027 katika vyanzo vingine yapo juu ikilinganishwa na mwaka unaoisha, hivyo basi, ili kutokuathiri kiwango cha makusanyo katika mwaka 2026/2027, Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe inaongeza usimamizi wa mashirika ya umma na kuhakikisha kuwa mashirika hayo yanachangia ipasavyo mapato yasiyo ya kikodi na hivyo kuiwezesha Ofisi hiyo kufikia lengo la makusanyo lililoidhinishwa katika mwaka 2026/2027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina imekuwa ikilazimika kubeba gharama za matukio ambayo hayatabiriki *(contingent liability)* yanayotokea katika mashirika mbalimbali ya umma kama ilivyokuwa kwa Shirika la *UDART* kwa kulipia gharama za uingizaji wa mabasi mapya ya mwendokasi, na kwa kuwa mashirika ya umma nayo pia yana vifungu kama hivyo katika bajeti zao, na kwa kuwa uwepo wa fedha hizo unasaidia kutatua changamoto zisizotabirikia endapo zitajitokeza, hivyo basi, Ofisi ya Msajili wa Hazina na mashirikia ya umma inayoyasimamia zitenge fedha katika kifungu cha *contingent liability*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Namba 011 - Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; kwa kuwa Serikali ilishaeleza Bungeni kuwa itaanza mchakato wa kuajiri Wakurugenzi Wakuu na Wajumbe wa Bodi wa baadhi ya taasisi za umma kwa njia ya ushindani, na kwa kuwa Serikali ilishaelezwa kuwa upatikanaji wa Watendaji hao na Wajumbe wa Bodi kwa njia ya ushindani una manufaa kwa umma, hivyo basi, ili kutekeleza azma hiyo, Serikali

ianze utaratibu wa kuwapata Wakurugenzi Wakuu na Wajumbe wa Bodi kwa njia ya ushindani mapema iwezekanavyo, ikiwemo kuweka wazi orodha ya mashirika ya umma ambayo yatapaswa kutumia mchako wa huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuwa eneo yalipokuwa machimbo ya dhahabu Buzwagi sasa limegeuzwa na kuwa Eneo Maalum la Uwekezaji la Buzwagi, na kwa kuwa, bado kuna baadhi ya wananchi wanaozunguka eneo hilo wanaamini kwamba eneo hilo lina madini ya dhahabu, na kwa kuwa imani hiyo inaweza kuathiri usalama wa wawekezaji wanaopenda kuwekeza katika eneo hilo, hivyo basi, ili kutokuathiri uwekezaji katika eneo hilo, Serikali ihakikishe inaendelea kuimarisha ulinzi wa eneo hilo pamoja na kutoa elimu itayaowawezesha wananchi hao kubadili mtazamo wao juu ya matumizi ya eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali inakusudia kuingia mikataba maalum ya uwekezaji na baadhi ya wawekezaji katika Eneo Maalum la Uwekezaji Buzwagi, na kwa kuwa Serikali inauzoefu wa kutosha kuwa baadhi ya wawekezaji wanaweza kupewa maeneo hayo lakini wakayatumia kinyume na makubaliano, hivyo basi, ili kudhibiti kutokea kwa changamoto hiyo, Serikali ihakikishe wawekezaji wote waliopewa maeneo ya uwekezaji katika eneo la Buzwagi na maeneo mengine kama hayo, wanaanza uwekezaji mapema kama ilivyokusudiwa na kukubalika katika mikataba ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bado kuna sheria na kanuni nyingi zinazosababisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kuwa magumu, na kwa kuwa Ofisi ya Mipango na Uwekezaji ina wajibu wa kuhakikisha sheria na kanuni hizo zinaboreshwa ikiwemo kuunganisha taasisi zenye majukumu yanayofanana hususan taasisi za udhibiti, hivyo basi, ili kuweka mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kuwa rafiki, Serikali ihakikishe, kwa kushirikiana na taasisi nyingine zenye jukumu la kurekebisha sheria, inazipitia sheria na kanuni zote na kuunganisha au kupunguza taasisi za udhibiti zenye majukumu yanayofanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Namba 66 – Tume ya Taifa ya Mipango; Serikali ihakikishe inaandaa na kuanza kutumia nyenzo bora za Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 ili kuweza kuleta tija kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe inafanya tathmini kuhusu miradi ya kimkakati inayotekelezwa na inayotarajiwa kutekelezwa na Serikali kupitia Wizara na taasisi mbalimbali ili kuhakikisha kwamba hakuna muingiliano katika kutekeleza miradi na ikiwezekana kuwepo kwa ushirikiano kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo miongoni mwa Wizara na taasisi mbalimbali ili kuhakikisha kuwa miradi hiyo inakuwa na thamani ya fedha iliyokusudiwa na inaleta tija kwa wananchi na Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; ninapenda kukushukuru wewe binafsi; Naibu Spika; na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. *(Makofi)*

Aidha, kwa dhati kabisa, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Mipango. *(Makofi)*

Vilevile, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Mbunge – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji; pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya kwa ushirikiano wao mkubwa ambao wameendelela kuipatia Kamati yetu wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa ofisi hiyo pamoja na taasisi zake kwa

ushirikiano walioipatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Tausi Mbaga Kida ambaye pia ni Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango na Ndugu Fred Matola Msemwa – Katibu Mkuu anayesimamia Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini sio kwa umuhimu, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati Dkt. Damas Ndumbaro, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1. Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 121 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, natumia fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja

na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

### 1.2. Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya **Kanuni ya 145** ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 kwa kugawanyika katika Sehemu Tano kama ifuatavyo: -

(a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, msingi na muundo wa taarifa hii;

(b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa fedha 2025/2026 katika maeneo yanayohusu makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;

(c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

(d) Sehemu ya Nne inahusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati; na

(e) Sehemu ya Tano ni hitimisho ikijumuisha shukrani.

### 1.3. Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi na Maoni ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais-Mipango na Uwekezaji ya mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa fedha 2026/2027 unatokana na masharti ya **Kanuni ya 121(4)** ikisomwa kwa pamoja na **vifungu 6(2)(b) na 7 (1)(a)** vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025. Kanuni na vifungu hivyo vimeweka masharti yanayoelekeza Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya

kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

### 1.4. Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua jumla ya mafungu matatu (3) ambayo ni: -

a) **Fungu 7** – Ofisi ya Msajili wa Hazina;
b) **Fungu 11** - Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji; na
c) **Fungu 66** – Tume ya Taifa ya Mipango.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

### 2.1. Vipengele vya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** katika vikao vya Kamati vilivyoketi tarehe 10 na 26 ya mwezi Machi, 2026, Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua Taarifa za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji zilizohusu, pamoja na mambo mengine, Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa hizo ziliwasilishwa na **Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb),** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji**.** Uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa hizo umeangazia maeneo makuu manne ambayo ni: -

(a) Makusanyo ya maduhuli kuanzia Julai, 2025 hadi Februari, 2026;

(b) Upatikanaji wa fedha za Bajeti za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026;

(c) Ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026; na

(d) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa kupitia Taarifa ya Kamati wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## 2.2. Uchambuzi Kuhusu Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji katika mwaka wa fedha 2025/2026, ilikadiria kukusanya mapato yasiyo ya kodi kiasi cha **Shilingi 1,696,260,540,000.00** kupitia Fungu Na. 07- Ofisi ya Msajili wa Hazina. Fedha hizo zilipangwa kukusanywa kutoka kwenye vyanzo sita (6) ambavyo ni Michango ya asilimia 15 ya Mapato Ghafi ya mashirika ya umma yenye sifa, Gawio, Marejesho ya Mfumo wa Usimamizi wa Nyendo za Mawasiliano ya Simu (**TTMS)**, Rejesho la Riba na Mikopo, ziada na malipo mengineyo na Ukusanyaji kutoka kwenye mapato ya ubinafsishaji.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli hayo unaonesha kuwa Ofisi hii kupitia Fungu Na. 07 hadi kufikia mwezi Februari, 2026, imekusanya kiasi cha **Shilingi 716,064,740,000.00** sawa na **asilimia 42.21** ya lengo la mwaka. Kiwango hicho si cha kuridhisha, kwani hadi Februari, 2026 kiwango cha makusanyo kilipaswa kufikia **asilimia 66.7.**

Ofisi ya Msajili wa Hazina inategemewa na Serikali katika kuhakikisha maduhuli ya fedha za Serikali kupitia mashirika mbalimbali ya umma yanakusanywa na kuwasilishwa mfuko mkuu kikamilifu. Kushindwa kukusanya maduhuli kwa kiwango kinachotosheleza cha asilimia, kuna punguza uwezo wa Serikali ktoa huduma za kijamii. **Ili kuondokana na athari hizo, ni rai ya Kamati kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina iongeze kasi na kubuni mikakati itakayowezesha ukusanyaji wa maduhuli kupitia mashirika mbalimbali kufikia lengo lililokusudiwa katika mwaka wa fedha 2025/2026**.

## 2.3. Upatikanaji wa Fedha za Bajeti kwa Kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026

**Mheshimiwa Spika,** katika kushughulikia bajeti ya Ofisi hii, Kamati imeangazia mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida ambayo

yanajumuisha mishahara (PE) na matumizi mengineyo (OC) pamoja na fedha kwa ajili ya maendeleo. Tathmini ya utekelezaji wa bajeti hadi februari, 2026 kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo: -

### 2.3.1 Fungu Na. 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina

**Mheshimiwa Spika**, katika bajeti iliyosomwa bungeni mwezi Aprili, 2025, Ofisi ya Msajili wa Hazina iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 62,255,822,000.00.** Katika kiasi hicho, fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni **shilingi 60,585,131,000.00**, kiasi hiki kikujumuisha fedha za mishahara (PE) **shilingi 8,662,948,000.00** na fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) **shilingi 51,922,183,000.00**. Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ilikuwa **shilingi 1,670,691,000.00**

**Mheshimiwa Spika,** ilipofika mwezi Februari, 2026, kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, bajeti ya ofisi hii iliongezwa kwenye kipengele cha fedha za dharura (**contingent liability**) kwa kuongezewa fedha za matumizi mengineyo (OC) **shilingi 12,221,256,915.52,** na hivyo kutanua bajeti ya ofisi kufikia **shilingi 72,806,387,915.52.** Ongezeko hilo lilitokana na mahitaji maalum mbalimbali yaliyojitokeza ikiwemo kugharamia gharama za kuingiza nchini mabasi mapya ya mwendokasi kwa kulipia kodi ya *VAT*, wakala wa meli, gharama za *wharfage*, uondoshaji wa mizigo, usajili wa mabasi na gharama nyingine za bandari (port charges). Mchanganuo wa mapokezi ya fedha hizo unafafanuliwa hapa chini kama ifuatavyo: -

(a) Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, hadi kufikia Februari, 2026 Fungu hili lilipokea **shilingi 54,233,820,005.03** kati ya kiasi kilichoidhinishwa cha shilingi **72,806,387,915.52**, sawa **na asilimia 74**. Katika kiasi kilichopokelewa, **shilingi 4,481,892,921.04** ni kwa ajili ya mishahara, **shilingi 49,192,835,487.77** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, ambapo katika matumizi hayo mengineyo (OC), **shilingi 30,288,636,027.20** ni kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi na **Shilingi 18,904,199,460.57** ni kwa ajili ya matumizi maalum.

(b) kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia mwezi Februari, 2026 ofisi hii ilipokea jumla ya **shilingi 1,670,691,000.00** kati ya kiasi cha **shilingi 1,670,691,000.00** kilichoidhinishwa, sawa na **asilimia 100** ya lengo. Kwa ujumla, hali ya mapokezi ya fedha hadi Februari, 2026 inaoneshwa katika **Jedwali Na. 1** kama ifuatavyo: -

**Jedwali 1: Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 kwa Fungu 7**

| Eneo | Kiasi Kilichoidhinishwa | Kiasi kilichopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara (PE) | 8,662,948,000 | 4,481,892,921.04 | 51.74 |
| OC-Uendeshaji wa Ofisi | 33,033,044,000 | 30,288,636,027.20 | 91.69 |
| OC-Matumizi Maalum | 31,110,395,915.52 | 18,904,199,460.57 | 60.77 |
| Jumla Ndogo | 72,806,387,915.52 | 53,674,728,408.81 | 73.72 |
| Maendeleo | 1,670,691,000 | 1,670,691,000 | 100 |
| **Jumla Kuu** | **74,477,078,915.52** | **55,345,419,408.81** | **74.31** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji 2025/2026 na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla hali ya upatikanaji wa fedha kwa kila sehemu katika Fungu Na. 7-Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikuwa ya kuridhisha kwa kuvuka kiwango cha wastani wa **asilimia 66.7** inayolengwa kufikiwa ifikapo mwezi februari. **Ni matumaini ya Kamati kuwa, Ofisi itatekeleza majukumu yaliyoainishwa kwa ufanisi kwa ustawi wa wananchi.**

**2.3.2 Fungu Na. 11- Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 34,867,493,000.00**, kati ya fedha hizo **Shilingi 22,392,185,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 8,716,784,000.00** ni Mishahara (PE) na **Shilingi 13,675,401,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC). Aidha, **Shilingi 12,475,308,000.00** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **shilingi 6,182,746,000.00** ni fedha za ndani na **shilingi 6,292,562,000.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2026, tathmini ya mapokezi ya fedha hizo inaonesha kama ifuatavyo: -

(a) Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida (OC na mishahara), zilipokelewa jumla ya **Shilingi 12,353,988,338.84** ya kiasi kilichoidhinishwa, sawa na utekelezaji wa **asilimia 55.17** ya lengo. Katika kiasi hicho, mishahara ilipokelewa shilingi **4,990,137,077.00** sawa na **asilimia 57.25** ya mishahara iliyoidhinishwa, na matumizi mengineyo (OC) **shilingi 7,363,851,261.84** sawa na **asilimia 53.85** ya fedha zilizoidhinishwa.

(b) Kwa upande wa fedha za maendeleo, fungu 11 lilipokea **shilingi 2,605,205,731.66** sawa na **asilimia 20.88** ya lengo la **Shilingi 12,475,308,000.00** iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi **1,505,207,731.66** ni fedha za ndani, sawa na **asilimia 24.34** ya fedha za ndani zilizoidhinishwa, na shilingi **1,099,998,000.00** ni fedha za nje, sawa na **asilimia 17.48** ya fedha za nje zilizoidhinishwa. Mchanganuo kuhusu upatikanaji huo unaoneshwa katika **Jedwali Na. 2** la Taarifa.

**Jedwali 2: Upatikanaji wa Fedha hadi February, 2026 kwa Fungu 011**

| Eneo | Kiasi Kilichoidhinishwa | Kiasi kilichopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara (PE) | 8,716,784,000 | 4,990,137,077.00 | 57.25 |
| Matumizi Mengineyo (OC) | 13,675,401,000 | 7,363,851,261.84 | 53.85 |
| Jumla Ndogo | 22,392,185,000 | 12,353,988,338.84 | 55.17 |
| Maendeleo Ndani | 6,182,746,000 | 1,505,207,731.66 | 24.34 |
| Maendeleo Nje | 6,292,562,000 | 1,099,998,000 | 17.48 |
| Jumla Ndogo | 12,475,308,000 | 2,605,205,731.66 | 20.88 |
| **Jumla Kuu** | **34,867,493,000** | **14,959,194,070.5** | **42.90** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka 2026/2027 na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya mapokezi ya fedha kwa Fungu 011- Wizara ya Mipango na Uwekezaji inaonekana kuwa si ya kuridhisha kwa upande wa fedha za maendeleo. Endapo hali hiyo itaendelea kuwa si ya kuridhisha hadi itakapofika mwezi Juni, 2026 wakati wa kuhitimisha mwaka wa fedha wa 2025/2026, ni dhahiri kuwa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka huu haitakamilika.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, baadhi ya miradi iliyolengwa kutekelezwa mwaka 2025/2026 ambayo haikuwa imepokea fedha ililenga kukuza uwekezaji nchini. Baadhi ya miradi hiyo ni mradi unaohusu Uendelezaji wa Maeneo Maalum kwa Uzalishaji wa Bidhaa kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi, Uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi (*Tanzania Min Tiger Plan 2020*), na Programu ya Kuboresha Mazingira ya Biashara nchini.

Kutokupokelewa kwa fedha zilizotengwa, kunaendelea kusababisha miradi iliyokusudiwa kutekelezwa ili kurahisisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kutokutekelezwa kwa kiwango kilichokusudiwa. Kwa mfano, katika mradi wa programu ya kuboresha mazingira ya biashara, moja ya kazi iliyopangwa kutekelezwa ni kufanya mapitio ya sheria, na kuunganisha majukumu yanayofanana ya taasisi.

Katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050, inaonekana kuwa mojawapo ya vikwazo vya kukua kwa biashara nchini ni migongano ya sera, sheria na kanuni na kuwepo kwa muingiliano wa majukumu ya taasisi za udhibiti[1]. Kwa kuwa fedha za mradi huu hazikupokelewa, ni vigumu jukumu hili kufanyika kwa ufanisi uliokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa ikiwemo lengo la Dira ya Maendeleo ya Taifa, 2050 kama lilivyofafanuliwa katika Ukurasa wa 49 wa Kitabu cha Dira, **Kamati inashauri kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo hususan miradi inayohusu uwekezaji na uboreshaji wa mazingira ya biashara nchini, zitolewe ipasavyo ili wananchi waweze kunufaika na uboreshaji huo**.

[1] Ukurasa wa 48 hadi 49 wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025-2050

### 2.3.3 Fungu Na. 66 – Tume ya Taifa ya Mipango

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 48,506,646,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 39,145,369,000.00,** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 5,145,369,000.00** ni Mishahara (PE) na **Shilingi 34,000,000,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC). Aidha, **Shilingi 9,361,277,000.00** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya mapokezi ya fedha hizo inaonesha kuwa hadi kufikia Februari, 2026 mapokezi ya fedha zilizotengwa yalikuwa kama ifuatavyo: -

**(a)** Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida (OC na Mishahara), Tume imepokea jumla ya **shilingi 22,562,402,361.31** sawa na **asilimia 57.64** ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Kati ya kiasi hicho, **shilingi 2,775,931,330.00** ni kwa ajili ya mishahara, sawa na **asilimia 53.95** ya lengo, na **shilingi 19,786,471,031.31** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), sawa na **asilimia 58.20** ya lengo.

**(b)** Kwa upande wa fedha za maendeleo, Tume imepokea jumla ya **shilingi 1,960,588,361.92** sawa na **asilimia 20.9** ya fedha iliyoidhinishwa.

Mchanganuo wa upatikanaji wa fedha kwa **fungu 066** ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 3**.

**Jedwali 3: Upatikaji wa Fedha hadi Februari, 2026 kwa Fungu 66**

| Eneo | Kiasi Kilichoidhinishwa | Kiasi kilichopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara (PE) | 5,145,369,000 | 2,775,931,330.00 | 53.95 |
| Matumizi Mengineyo (OC) | 34,000,000,000 | 19,786,471,031.31 | 58.20 |
| Jumla Ndogo | 39,145,369,000 | 22,562,402,361.31 | 57.64 |
| Maendeleo | 9,361,277,000 | 1,960,588,361.92 | 20.9 |
| **Jumla Kuu** | **48,506,646,000** | **24,522,990,723.23** | **50.56** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka 2026/2027 na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** tathmini inaonesha kuwa, hadi februari, 2026, upatikanaji wa fedha za bajeti katika Tume ya Taifa ya Mipango kwa ajili ya miradi ya maendeleo hauridhishi. Uchambuzi zaidi wa Kamati unaonesha kuwa, kiasi kikubwa cha fedha za maendeleo (**shilingi Bilioni 8** kati ya **Bilioni 9.36** zilizoidhinishwa) zililenga kutekeleza mradi wa kufanya tafiti zitakazotaarifu maandalizi na utekelezaji wa mipango ya maendeleo na kuwezesha utendaji wa majukumu kupitia mifumo ya TEHAMA ikijumuisha moduli za uchumi jumla na uchambuzi wa maandiko ya miradi.

Kutokupokelewa kwa fedha za miradi iliyotengwa kikamilifu, kuna athari kwa Tume ya Mipango ya kushindwa kutekeleza majukumu yake, na hivyo kuathiri usimamizi wa mipango iliyokusudiwa kutekelezwa ikiwemo miradi ambayo utekelezaji wake unategemea uchambuzi na maoni ya Tume ya Mipango. **Ni maoni ya Kamati kuwa, fedha za maendeleo hususan fedha zilizotengwa kutekeleza miradi inayokusudia kuboresha mipango ya nchi, zitolewe kikamilifu na kwa wakati. Kutolewa huko kutaiwezesha Tume ya Taifa ya Mipango kufanya kazi ya kuandaa mipango ya nchi kwa ukamilifu pamoja na kusimamia utekelezaji wake.**

### 2.4 Ukaguzi wa Miradi ya maendeleo Iliyotengewa Fedha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Katika Wizara ya Mipango na Uwekezaji na mafungu yake matatu, Kamati ilitembelea mradi mmoja unaohusu Kongani Maalum ya Uwekezaji ya Buzwagi, unaotekelezwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga. Mradi huo unajulikana kama *Buzwagi Special Economic Zone* (BSEZ) na ulitangazwa rasmi kuwa Ukanda Maalum wa Uwekezaji kupitia **Tangazo la Serikali Na. 142 la tarehe 8, Machi, 2024**. Eneo hilo lina ukubwa wa **Mita za Mraba 13,335,456.69**, na kwa sasa linalimikiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kahama. Aidha, TISEZA imepewa kazi ya kutoa ushauri wa kitalaam ili kuwezesha uwekezaji kufanyika katika eneo hilo na imetoa leseni Na. 18 ya uendelezaji wa eneo hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa, awali eneo hili lilikuwa mahsusi kwa ajili ya shughuli za uchimbaji wa madini ya dhahabu

chini ya Kampuni ya *Barrick Gold Mine*. Aidha, baada ya shughuli za uchimbaji wa dhahabu kufungwa mwaka 2021, ndipo kulifanyika upembuzi ambao ulionesha kuwa eneo hilo linafaa kuanzishwa kongani maalum ya uwekezaji.

Lengo kuu la kuanzishwa kwa *Buzwagi Special Economic Zone* (BSEZ) ni kuendeleza shughuli za kiuchumi katika manispaa na wilaya ya Kahama. Kupitia mradi huo, inategemewa kukazibwa pengo la manufaa ya kiuchumi na kimapato lililosababishwa na kufungwa kwa shughuli za uchimbaji wa madini katika eneo hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipotembelea na kukagua mradi huu, ilibaini uwepo wa miundombinu iliyoachwa na Kampuni iliyokuwa ikichimba madini katika eneo hilo, ambayo inaweza kutumika kama kichocheo cha uwekezaji katika eneo hilo. Mojawapo ya miundombinu iliyopo katika eneo hilo ni majengo, barabara, kiwanja cha ndege chenye uwezo wa kuhudumia **watu 250**, mitambo ya umeme yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa **Megawati 48**, mifumo ya ulinzi na maji. Mbali ya miundombinu hiyo, ukaguzi wa Kamati ulishuhudia utekelezaji wa miradi mingine katika eneo hilo. Miradi hiyo inalenga kuongeza na kuboresha miundombinu yae neo hilo na kwa lengo la kuvutia wawekezaji.

Mojawapo ya shughuli zilizokuwa zikitekelezwa ni ujenzi wa mtambo wa kuzalisha maji kiasi cha lita **Milioni Kumi** kwa siku kutokana na uwepo wa maporomoko ya maji ya mvua yaliyopo katika eneo hilo. Gharama za mradi huo ni shilingi **4,600,000,000.00** ambapo Serikali ya Tanzania inagharamia **asilimia 38** na Kampuni ya Barrick **asilimia 62**. Ujenzi ulianza mwezi Juni, 2025 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2026.
Kamati ilipotembelea mradi huu, ujenzi wake ulikuwa umefikia **asilimia 78**.

**Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa mradi wa maji katika eneo hilo, mbali na maji hayo kutumiwa katika shughuli za uwekezaji, lakini pia mradi unakusudiwa kuwa chanzo cha maji katika mji mdogo wa Kahama. Chanzo hicho kitaipunguzia Manispaa ya Kahama gharama za kulipia huduma ya maji yanayosambazwa kwa wananchi, na hivyo kupunguza bei ya maji kwa wakazi wa mji wa Kahama na maeneo jirani.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu uwekezaji katika eneo hilo, Kamati ilielezwa kuwa, eneo hilo limepangwa kutumika kwa ajili ya shughuli sita za uwekezaji na huduma. Shughuli hizo ni **Vyuo vya Ufundi, Viwanda, uchenjuaji wa madini, uzalishaji wa nishati jadidifu, shughuli za ujenzi na makazi (smart city**). Hadi wakati Kamati ilipofanya ukaguzi wake mwezi Machi, 2026, ilielezwa kuwa jumla ya wawekezaji thelathini na tano **(35)** wameonesha nia ya kuwekeza katika eneo husika. Kati yao, mwekezaji mmoja ambayo ni Kampuni ya ***East Africa Conveyers Service*** ilikuwa imesha anza uzalishaji, Kampuni nne zilikuwa katika hatua mbalimbali za usajili na leseni na zilizobakia zilikwa hazijaanza mchakato licha ya kuonesha nia ya kuwekeza.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu uwezo na mkakati wa Manispaa ya Kahama kusimamia uwekezaji katika eneo hilo, Kamati ilifahamishwa kuwa Manispaa hiyo ipo katika mchakato wa kuingia kwenye makubaliano (MoU) na TISEZA, ili taasisi hiyo iweze kuwa mwendeshaji (operator) wa eneo hilo. **Kamati inakubaliana na mpango wa Manispaa kuingia makubaliano hayo na TISEZA, jambo ambalo litawezesha uwekezaji kufanyika katika mazingira wezeshi na yenye utulivu.**

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na lengo hilo jema, bado kuna masuala mbalimbali ambayo Serikali inatakiwa kuyatatua ili kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji katika eneo hilo. Kwa mfano, Kamati wakati wa ukaguzi wake ilijionea kuwa eneo hilo linalindwa na askari polisi kwa usimamizi wa karibu wa Kampuni ya Madini ya Barrick. Uwepo wa ulinzi mkali katika eneo hilo ni mojawapo ya mambo yanayowafanya wananchi wanaozunguka eneo hilo kuwa na Imani kubwa kuwa bado kuna madini ikiwemo madini ya dhahabu katika eneo hilo. Kutokana na mtazamo huo, Kamati inaona bado kuna wasiwasi wa eneo hilo kuvamia na wananchi wenye Imani hiyo ili kufanya shughuli za uchimbaji mdogo mdogo wa madini.

**Mheshimiwa Spika,** hali hiyo inaweza kusababisha kukosekana kwa usalama wa eneo hilo ikiwemo kwa wawezekaji wanaokusudia kuwekeza katika eneo hilo. Hali hiyo inaweza kujitokeza pale ambapo Kampuni ya Barrick itaondoka moja kwa moja katika eneo hilo. Hali hiyo inaweza kuharibu mahusiano ya

kimikataba ya uwekezaji kati ya Serikali na wawekezaji watakaokuwemo katika eneo husika. **Ni mtazamo wa Kamati kuwa, kabla ya uwekezaji kuanza kwa kiasi kikubwa na kabla ya Kampuni ya Barrick kuondoa huduma ya ulinzi katika eneo hilo, Serikali itoe elimu ya kutosha na kuwawezesha wanachi wanaozunguka eneo hilo kuelewa na kufahamu kuwa eneo hilo ni muhimu kwa ajili ya shughuli za uwekezaji unaokusudiwa kwa manufaa ya nchi kwa ujumla.**

### 2.5 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati. Licha ya utekelezaji huo mzuri, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa maagizo yenye muendelezo wa utekelezaji yaendelee kutekelezwa.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, mnamo tarehe 26 Machi, 2026; Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulijikita katika maeneo makuu mawili ambayo ni Makadirio ya makusanyo ya maduhuli na makadirio ya matumizi. Tathmini ya uchambuzi kuhusu maeneo hayo ni kama ifuatavyo: -

### 3.1 Maduhuli kwa Mwaka 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji kupitia **Fungu Na. 7**-Ofisi ya Msajili wa Hazina inaomba kuidhinishiwa kukusanya mapato yasiyo ya kodi jumla ya **shilingi 1,792,228,000,000.00**. Kiasi hicho ni ongezeko la

**shilingi 95,967,460,000.00**, sawa na **asilimia 5.66** ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaoisha wa fedha 2025/2026, ambapo iliidhinishwa **shilingi 1,696,260,540,000.00**. Vyanzo vya fedha kwa mwaka 2026/2027 vinafanana na vyanzo vya mwaka wa fedha 2025/2026, isipokuwa kwa chanzo kimoja kinachohusu ubinafsishaji kilichokuwepo katika mwaka wa fedha unaoisha, ambacho hakitakuwepo katika mwaka wa fedha unaofuata. Uchambuzi zaidi umeainishwa katika **Jedwali Na. 4** la Taarifa ya Kamati.

**Jedwali 4: Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2026**

| FUNGU Na. 07 | MAKADIRIO YA MADUHULI MWAKA 2025/2026 | MAKADIRIO YA MADUHULI MWAKA 2026/2027 | PUNGUFU | % |
|---|---|---|---|---|
| Michango 15% Mapato Ghafi | 784,516,580,000 | 723,008,750,636.97 | (61,507,829,363.0) | -7.84 |
| Gawio | 743,878,340,000 | 835,821,063,433.54 | 91,942,723,433.54 | 80 |
| Marejesho ya TTMS | 5,000,000,000 | 9,797,007,201.00 | 4,797,007,201 | 95.94 |
| Rejesho Riba na Mikopo | 37,000,000,000 | 62,221,135,357.80 | 25,221,135,357.80 | 68.17 |
| Ziada na mengineyo | 122,365,630,000 | 161,380,043,370.69 | 39,014,413,370.69 | 31.88 |
| Mapato ya Ubinafsishaji | 3,500,000,000 | - | -3,500,000,000 | -100 |
| **JUMLA KUU** | **1,696,260,540,000** | **1,792,228,000,000.00** | **95,967,460,000** | **5.66** |

*Chanzo: Randama za Ofisi ya Rais-Mipango na Uwekezaji na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** tathmini inaonesha kuwa, Mapato makubwa yanakusudiwa kuongezeka kwenye maeneo ya Gawio, Riba na

Mikopo, marejesho ya *TTMS* pamoja na ziada ya malipo mengineyo. Aidha, upungufu wa mapato unategemea kutoka kwenye eneo la michango ya **asilimia 15** ya mapato ghafi ambapo mapato katika chanzo hicho yanakadiwriwa kupungua kwa **asilimia 7.84** ya chanzo. Vilevile, chanzo cha ubinafsishaji kilichokuwepo katika mwaka wa fedha unaoisha, hakitakuwepo katika mwaka wa fedha unaofuata. Licha ya kupungua kwa chanzo mojawapo cha mapato, lakini mapato yameongezeka kutokana na makadirio kuongezeka kwenye vyanzo vingine. **Kamati inashauri Ofisi ya Msajili wa Hazina kuongeza kasi na kuweka mikakati thabiti ya kuyasimamia mashirika ya umma ili yaweze kuchangia kwa kiasi kikubwa katika makusanyo ya mapato yasiyokuwa ya kikodi.**

### 3.2 Makadirio ya matumizi kwa mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji katika mafungu yake matatu inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 144,850,349,000.00**. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 126,018,699,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha **shilingi 22,421,115,000.00** kwa ajili ya mishahara na **shilingi 103,597,584,000.00** kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Aidha, kiasi cha **shilingi 18,831,650,000.00** kinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** bajeti ya mwaka 2026/2027 imepungua kwa kiasi cha **shilingi 13,000,868,915.52** sawa na punguzo la **asilimia 8.236** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/2026 ambapo makadirio yalikuwa **shilingi 157,851,217,915.52.** Uchambuzi umebaini kuwa, punguzo hilo linatokana na fedha za matumizi ya kawaida kupungua katika mwaka 2026/2027, ambapo kiasi kinachoombwa ni **shilingi 126,018,699,000.00,** wakati katika mwaka wa fedha unaoisha wa 2025/2026 ziliombwa **shilingi 134,343,941,915.52.** Kiasi cha mwaka 2025/2026 katika matumizi ya kawaida ni zaidi kwa shilingi **8,325,242,915.52** ikilinganiwa na mwaka 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi wa Kamati unaonesha kuwa, fedha za mwaka 2025/2026 za matumizi ya kawaida ziliongezeka zaidi kupitia **Fungu Na. 7** Ofisi ya Msajili wa Hazina kutokana na

nyongeza ya bajeti iliyotokea mwezi Februari, 2026 ambapo ziliongezwa **shilingi 12,221,256,915.52** katika kipengele cha fedha za dharula. Endapo kusingekuwa na nyongeza hiyo, bajeti ya mwaka 2026/2027 ingekuwa pungufu kwa kiasi cha **shilingi 779,612,000.00** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/2026, kiasi ambacho hakina utofauti mkubwa, na hivyo kuashiria kuwa bajeti ya miaka yote ya fedha 2025/2026 na 2026/2027 inaelekea kulingana kiwango.

**Mheshimiwa Spika,** ulinganisho wa bajeti kwa Mwaka 2025/2026 na makadirio ya matumizi ya mwaka unaofuata wa 2026/2027 kwa kila fungu ni kama inavyooneshwa katika **majedwali Na. 5 hadi 6** katika taarifa hii.

Kwa upande wa **Fungu Na. 07**-Ofisi ya Msajili wa Hazina-**Jedwali Na. 5** linaonesha hali ya ulinganisho wa kibajeti kama ifuatavyo: -

**Jedwali 5: Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi kwa Mwaka 2025/2026 na Mwaka 2026/2027 - Fungu Na. 7**

| OFISI YA MSAJILI WA HAZINA- FUNGU 07 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **FEDHA** | **CHANZO** | **2025/2026** | **2026/2027** | **ONGEZEKO/UPUNGUFU** | **ASILIMIA** |
| **MAENDELEO** | NDANI | 370,691,000 | 370,691,000 | 0.00 | **0** |
| | NJE | 1,300,000,000 | 0.00 | (1,300,000,000) | **100** |
| | **Jumla ndogo** | **1,670,691,000** | **370,691,000** | **(1,300,000,000)** | **77.81** |
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | OC | 64,143,439,915.52 | 51,922,183,000 | (12,221,256,915.52) | **19.05** |
| | MISHAHARA | 8,662,948,000 | 8,529,569,000 | (133,379,000) | **1.54** |
| | Jumla ndogo | **72,806,387,915.52** | **60,451,752,000** | (12,354,635,915.52) | **16.97** |
| **JUMLA KUU** | | **74,477,078,915.52** | **60,822,443,000** | **(13,654,635,915.52)** | **18.33** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais-Mipango na Uwekezaji na Usanifu wa Kamati*

Kwa upande wa **Fungu Na. 011**-Ofisi ya Rais-Mipango na Uwekezaji -**Jedwali Na. 6** linaonesha hali ya ulinganisho wa kibajeti kama ifuatavyo: -

**Jedwali 6: Ulinganisho wa bajeti ya Matumizi kwa Mwaka 2025/2026 na Mwaka 2026/2027 - Fungu Na. 011**

| OR-MIPANGO NA UWEKEZAJI- FUNGU 011 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **FEDHA** | **CHANZO** | **2025/2026** | **2026/2027** | **ONGEZEKO/UPUNGUFU** | **ASILIMIA** |
| **MAENDELEO** | NDANI | 6,182,746,000 | 6,182,746,000 | 0.00 | **0** |
| | NJE | 6,292,562,000 | 2,958,701,000 | (3,333,861,000) | **52.98** |
| | **Jumla ndogo** | **12,475,308,000** | **9,141,447,000** | (3,333,861,000) | **26.72** |
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | OC | 13,675,401,000 | 17,675,401,000 | 4,000,000,000 | **29.249** |
| | MISHAHARA | 8,716,784,000 | 8,569,463,000 | (147,321,000) | **1.69** |
| | Jumla ndogo | **22,392,185,000** | **26,244,864,000** | 3,852,679,000 | **17.2** |
| **JUMLA KUU** | | **34,867,493,000** | **35,386,311,000** | **518,818,000** | **1.488** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais-Mipango na Uwekezaji na Usanifu wa Kamati.*

Aidha, kuhusu **Fungu Na. 066**-Tume ya Taifa ya Mipango, **Jedwali Na. 7** linaonesha hali ya ulinganisho wa kibajeti kama ifuatavyo: -

**Jedwali 7: Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi kwa Mwaka 2025/2026 Mwaka 2026/2027 - Fungu Na. 066**

| TUME YA TAIFA YA MIPANGO- FUNGU 066 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **FEDHA** | **CHANZO** | **2025/2026** | **2026/2027** | **ONGEZEKO/UPUNGUFU** | **ASILIMIA** |
| **MAENDELEO** | NDANI | 8,000,000,000 | 8,000,000,000 | 0.00 | **0** |
| | NJE | 1,361,277,000 | 1,319,512,000 | (41,765,000.00) | **3.07** |
| | **Jumla ndogo** | **9,361,277,0000** | **9,319,512,000** | (41,765,000.00) | **0.45** |
| **MATUMIZI** | OC | 34,000,000,000 | 34,000,000,000 | 0.00 | **0.0** |
| **YA KAWAIDA** | MISHAHARA | 5,145,369,000 | 5,322,083,000 | 176,714,000 | **3.43** |
| | **Jumla ndogo** | **39,145,369,000** | **39,319,512,000** | 174,143,000 | **0.45** |
| **JUMLA KUU** | | **48,506,646,000** | **48,641,595,000** | **134,949,000** | **0.28** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais-Mipango na Uwekezaji na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** tathmini inayotokana na ulinganifu wa fungu kwa fungu kama ulivyochambuliwa kupitia majedwali, athari za kibajeti zinaonekana zaidi katika fungu Na. 7 Ofisi ya Msajili wa Hazina. Katika ofisi hiyo, kumekuwa na ongezeko la bajeti ambalo linatokana na nyongeza ya mwezi Februari, 2026 ambapo ziliongezwa **shilingi 12,221,256,915.52** katika kipengele cha fedha za dharula, kama ilivyokwisha elezwa awali.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia majadiliano ya kina yaliyofanywa na Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, ili kusaidia katika utekelezaji mzuri wa bajeti hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi hiyo kama ifuatavyo:

(i) **Kwa kuwa** utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo unasuasua, **na kwa kuwa** kusuasua huko kuna athiri Wizara na taasisi zake kushindwa kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopangwa, **hivyo basi,** Serikali ihakikishe fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mwaka 2025/2026 zinatolewa kikamilifu katika muda uliobaki.

### 4.2 Ushauri Mahsusi Fungu kwa Fungu

#### 4.2.1 Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina

(i) **Kwa kuwa** ukusanyaji wa maduhululi ya Serikali unaotokana na mchango wa asilimia 15 ya mapato ghafi ya mashirika umepungua katika mwaka wa fedha 2026/2027, **na kwa kuwa** makadirio ya mwaka 2026/2027 katika vyanzo vingine yapo juu ikilinganishwa na mwaka

unaoisha, **hivyo basi,** ili kutokuathiri kiwango cha makusanyo katika mwaka 2026/2027, Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe inaongeza usimamizi wa mashirika ya umma na kuhakikisha kuwa mashirika hayo yanachangia ipasavyo mapato yasiyo ya kikodi na hivyo kuiwezesha Ofisi hiyo kufikia lengo la makusanyo lililoidhinishwa katika mwaka 2026/2027.

(ii) **Kwa kuwa** Ofisi ya Msajili wa Hazina imekuwa ikilazimika kubeba gharama za matukio ambayo hayatabiriki (*contingent liability*) yanayotokea katika mashirika mbalimbali ya umma, kama ilivyokuwa kwa shirika la ***UDART*** kwa kulipia gharama za uingizaji wa mabasi mapya ya mwendokasi, **na kwa kuwa** mashirika ya umma nayo pia yana vifungu kama hivyo katika bajeti zao, **na kwa kuwa** uwepo wa fedha hizo unasaidia kutatua changamoto zisizotabirikia endapo zitajitokeza, **hivyo basi**, Ofisi ya Msajili wa Hazina na mashirikia ya umma inayoyasimamia zitenge fedha katika kifungu cha *contingent liability*.

**4.2.2 Fungu 011 - Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji**

(i) **Kwa kuwa** Serikali ilishaeleza Bungeni kuwa itaanza mchakato wa kuajiri Wakurugenzi Wakuu na Wajumbe wa Bodi wa baadhi ya taasisi za umma kwa njia ya ushindani, **na kwa kuwa** Serikali ilishaelezwa kuwa upatikanaji wa Watendaji hao na Wajumbe wa Bodi kwa njia ya ushindani una manufaa kwa umma, **hivyo basi,** ili kutekeleza azma hiyo, Serikali ianze utaratibu wa kuwapata Wakurugenzi Wakuu na Wajumbe wa Bodi kwa njia ya ushindani mapema iwezekanavyo, ikiwemo kuweka wazi orodha ya mashirika ya umma ambayo yatapaswa kutumia mchako wa huo.

(ii) **Kwa kuwa** eneo yalipokuwa machimbo ya dhahabu Buzwagi sasa limegeuzwa na kuwa eneo maalum la uwekezaji la Buzwagi (BSEZ), **na kwa kuwa**, bado kuna baadhi ya wananchi wanaozunguka eneo hilo wana amini kwamba eneo hilo lina madini ya dhahabu, **na**

**kwa kuwa** imani hiyo inaweza kuathiri usalama wa wawekezaji wanaopenda kuwekeza katika eneo hilo, **hivyo basi,** ili kutokuathiri uwekezaji katika eneo hilo, Serikali ihakikishe inaendelea kuimarisha ulinzi wa eneo hilo pamoja na kutoa elimu itayaowawezesha wananchi hao kubadili mtazamo wao juu ya matumizi ya eneo hilo.

(iii) **Kwa kuwa** Serikali inakusudia kuingia mikataba maalum ya uwekezaji na baadhi ya wawekezaji katika eneo maalum la uwekezaji Buzwagi, **na kwa kuwa** Serikali inauzoefu wa kutosha kuwa baadhi ya wawekezaji wanaweza kupewa maeneo hayo lakini wakayatumia kinyume na makubaliano, **hivyo basi,** ili kudhibiti kutokea kwa changamoto hiyo, Serikali ihakikishe wawekezaji wote waliopewa maeneo ya uwekezaji katika eneo la Buzwagi na maeneo mengine kama hayo, wanaanza uwekezaji mapema kama ilivyokusudiwa na kukubalika.

(iv) **Kwa kuwa** bado kuna sheria na kanuni nyingi zinazo sababisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kuwa magumu, **na kwa kuwa** ofisi ya Mipango na Uwekezaji ina wajibu wa kuhakikisha sheria na kanuni hizo zinaboreshwa ikiwemo kuunganisha taasisi zenye majukumu yanayofanana hususan taasisi za udhibiti, **hivyo basi,** ili kuweka mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kuwa rafiki, Serikali ihakikishe, kwa kushirikiana na taasisi nyingine zenye jukumu la kurekebisha sheria, inazipitia sheria na kanuni zote na kuunganisha au kupunguza taasisi za udhibiti zenye majukumu yanayofanana.

### 4.2.3 Fungu 66 – Tume ya Taifa ya Mipango

(i) Serikali ihakikishe inaandaa na kuanza kutumia nyenzo bora za Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 ili kuweza kuleta tija kwa wananchi.

(ii) Serikali ihakikishe inafanya tathmini kuhusu miradi ya Kimkakati inayotekelezwa na inayotarajiwa kutekelezwa na Serikali kupitia Wizara na taasisi mbalimbali ili kuhakikisha kwamba hakuna muingiliano katika kutekeleza miradi na ikiwezekana kuwepo kwa ushirikiano kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo miongoni mwa Wizara na taasisi mbalimbali ili kuhakikisha kuwa miradi hiyo inakuwa na thamani ya fedha iliyokusudiwa na inaleta tija kwa wananchi na Taifa.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, kwa dhati kabisa, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb –**Mwenyekiti**
2. Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb.
5. Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb.
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
7. Mhe. Asha Hussein Saleh, Mb.
8. Mhe. Esther Edwin Malleko, Mb.
9. Mhe. Maryam Ussi Yahya, Mb.
10. Mhe. Nassoro Rashid Nassoro, Mb.
11. Mhe. Dkt. Neema Peter Majule, Mb.
12. Mhe. Nyamizi Simon Mhoja, Mb
13. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb.
14. Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mb.
15. Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb
16. Mhe. Timida Mpoki Fyandomo, Mb.
17. Mhe. Dkt. Yahaya Esmail Nawanda, Mb.
18. Mhe. Yohana Stephen Msita, Mb.

19. Mhe. Zena Maulid Katambo, Mb.
20. Mhe. Hussein Nassoro Amar, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru, **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ambae pia ni Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Mipango, Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo, (Mb) –Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji na Mhe. Dkt. Pius S. Chaya (Mb)-Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa ushirikiano wao mkubwa ambao wameendelela kuipatia Kamati yetu wakati wote.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi hiyo pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioipatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Tausi Mbaga Kida ambaye pia ni Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango, Ndg. Fred Matola Msemwa – Katibu Mkuu anayesimamia Uwekezaji na Ndg. Nehemiah Kyando Mchechu - Msajili wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leornard kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, ninamshukuru pia kwa kutupatia Sekretarieti ambayo inamsaidia kazi za kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

16 Aprili, 2026

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zena Katambo, tunakushukuru sana kwa uwasilishaji huo kwa niaba ya Kamati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nitambue tena uwepo wa wageni asubuhi hii ambao ni wageni wa Mheshimiwa Profesa Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; kwanza ni Menejimenti ya Tume ya Taifa ya Mipango na Watumishi wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wawekezaji na wadau wa maendeleo. *(Makofi)*

Wapo pia Wajumbe wa Timu ya Maandalizi, karibuni. *(Makofi)*

Pia wapo Wajumbe wa Timu ya Maandalizi ya Dira 2050, karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni Wajumbe wa Timu ya Maandalizi ya Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, karibuni. *(Makofi)*

Wapo pia Wakuu wa Taasisi za Utafiti, Viongozi wa Sekta Binafsi, karibuni. *(Makofi)*

Pia wapo Umoja wa Vyama vya Wafanyabiashara. *(Makofi)*

Wageni wengine ni viongozi kutoka Bunge la Wanafunzi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Morris Joseph Makoi, wakiongozwa na Ndugu Leopard Olomi Mkulima kutoka Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma, Mbunge, ambao ni wafanyakazi wa *Clam Sisters* kutoka Mbeya, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wote karibuni katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea na uchangiaji wa hii Wizara. Waheshimiwa Wabunge ninaomba tu kuwakumbusha Wizara hii tunapaswa kuhitimisha leo na ninaomba sana wachangiaji wote tuzingatie muda kama ambavyo kengele itakuwa inatuongoza hapa.

Tunaanza na Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, ajiandae Mheshimiwa Edward Kisau, Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja, pia ajiandae Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle pamoja na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na orodha itaendelea.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia muda. Nianze kwa kusema kwamba Waheshimiwa Wabunge hii ni Wizara ambayo ndiyo roho ya nchi, kwa hiyo, tunalazimika kuipitisha hii bajeti japokuwa mimi ninaiona ni ndogo, lakini mwakani tutaboresha kwa nini iongezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili hitimisho la Mheshimiwa Waziri zile *point* sita ulizozitoa ni za muhimu sana. Sasa mimi utaona jinsi ambavyo ninaweka nyama kwenye hizo *point* zako sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa niaba ya wananchi wa Musoma Vijijini ni lazima tuunge mkono hii bajeti kwa sababu; kwanza, Wizara inafanya vizuri, isitoshe miradi yetu miwili mikubwa ya kimkakati ipo kwenye orodha ya Tume ya Mipango ambalo ni Bwawa la Bugwema, mkandarasi amepatikana kutoka China, tena mkandarasi mkubwa mradi wa shilingi bilioni 800 watakabidhiwa hivi karibuni; na mradi wa pili, ni barabara yetu ya kilometa 92. Tumejengewa kilomita tano bado *TANROADS* wanapambana na mkandarasi wao, nina imani kwamba watakamilisha na miradi yetu yote miwili Mheshimiwa Waziri ibaki kwenye vitabu vyenu mpaka ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongee mambo ya kitaifa zaidi. Hii miradi miwili ya Musoma Vijijini ninamshukuru Mheshimiwa Rais alivyokuja Musoma Vijijini nilimuomba na kweli yote

inatekelezwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri fikisha salamu zetu za Musoma Vijijini tunamshukuru kwa miradi yetu miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kama ulivyosema Mheshimiwa Waziri tunaanza kutekeleza Dira ya 2050. Malengo makuu umeyasema, uchumi mzuri, uchumi imara na maisha bora kwa Watanzania. Tumejipima tumejipa kwamba itakapofika mwaka 2050 Pato letu la Taifa *(GDP)* liwe dola trilioni moja na pato la mtu mmoja mmoja *GDP per capita* iwe dola 7,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninatoa ushauri wa mipango ambayo inaweza ikatufikisha huko. Kwa sababu dira inashughulikia watu walioko kwenye Tume ya Mipango watakuwa wanaweka maanani wakati tunatengeneza hiyo dira yetu mwaka jana tulikuwa Watanzania milioni 70.5, baada ya miaka mitano mwaka 2030 tutakuwa milioni 77.5 na mwaka 2050 tutakuwa Watanzania sio chini ya milioni 140.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo pendekezo langu la kwanza kwa Tume ya Mipango ni suala la ardhi, makazi na mipangilio mizuri ya kiuchumi. Kwa sasa 38.5% yaani Watanzania milioni 27 wanaishi mijini, itakapofika mwaka 2050 Watanzania asilimia 65 yaani watu milioni 90 watakuwa wanaishi mijini. Kwa hiyo, ongezeko la watu kwenda mijini ni kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni Jiji la Dar es Salaam, kwa sasa lina watu takribani milioni 8.6, mwaka 2030 Dar es Salaam itakuwa katika majiji makubwa duniani itafikisha watu milioni 10. Tunapokwenda 2050 watakuwa watu milioni 15. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na timu yako kuna suala la mipango miji na vijiji hapa. Wananchi wanaongezeka, ardhi haiongezeki, kwa hiyo hili nalo ni la kuweka maanani wataalam wetu wa mipango, yaani *population density. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii watu 80 wanakalia *square kilometre* moja, 2030 watakuwa watu 92 *square kilometre* moja na mwaka 2050 watakuwa watu 145 wanakalia *square kilometre* moja. Kwa hiyo, Tume ya Mipango inamaanisha ardhi, lazima tupange vizuri mambo ya makazi, ya kilimo, ya ufugaji na shughuli

za kiuchumi kama viwanda na hata shule zetu tunazojenga ardhi inapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu nia ya Dira ya 2050 ni maisha bora ya Watanzania, lazima tuwe na vipimo na hivi vipimo huwezi ukajipima mwenyewe. Vipimo vyote lazima ujilinganishe na kujilinganisha nimechukua nchi ambazo tulikuwa tunazizidi au tunafanana wakati tunapata Uhuru mwaka 1961, na lazima tuwe tunarejea haya. Kwa hiyo, mwaka 1961, wakati Tanganyika inapata uhuru pato letu la mtu mmoja mmoja *GDP per capita* ya Tanganyika, ya wakati huo ilikuwa dola 285. Msikilize vizuri, hii inaenda na takwimu, kwa hiyo, makofi yasiwe mengi, takwimu zinakuja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yaani wakati tunapata uhuru pato letu la mtu mmoja mmoja Tanganyika ilikuwa dola 285. Leo mwaka 2025 pato letu ni dola 1,315. Kujilinganisha, Kenya mwaka 1961 pato la mtu mmoja mmoja lilikuwa dola 99, tulikuwa tunawazidi, lakini leo Kenya mgao wao ni dola 2,500, wametuzidi. Muhimu hapa ndiyo nitawachukua mpaka mwisho, na Mwenyekiti ukinisikia naongea kuhusu nishati ujue nakaribia kumalizia, kwa hiyo vumulia kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, India mwaka 1961, *GDP per capita* ya India ilikuwa dola 88, kwa hiyo, tulikuwa tunawazidi mbali sana. Leo hii mwaka jana *GDP per capita* ya India ni dola 2,818. Tuliwazidi wametuzidi, ndivyo hivyo nasema vipimo vya sisi kujipima. China mwaka 1961 *GDP per capita* ilikuwa dola 76. Leo hii China ni dola 14,730. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, mahali pa kujipima kama tunafanya vizuri lazima tuichukuwe India na China kila mara, maana yake tuliwazidi mwaka 1961.

Kwa hiyo, kipimo cha kwanza cha mafanikio ya Dira ya mwaka 2050 ni uchumi na Mheshimiwa Waziri wameongea kwa ufasaha kabisa, lakini kwa sasa mwaka 2050 tunataka kufikisha pato letu dola trilioni moja, lakini kwa sasa ni bilioni 87. Tunataka kufikisha *GDP per capita* dola 7,000, kwa sasa ni dola 1,315. Kwa

hiyo, safari yetu siyo nyepesi. Kipimo cha pili cha mafanikio ya dira ya mwaka 2050. Kipimo cha pili ni *HDI (Human Development Index)*. Hiki kipimo ni kizuri zaidi kuliko cha hizo *GDP per capita*, kwa sababu hiki kinaweka maanani hali ya afya ya wananchi wako, maisha, miaka wanayoiishi hapa duniani *(life expectancy),* inachukua mambo ya elimu, inachukua mambo ya kipato na inachukua hali ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukichukua hicho kipimo kwa sasa hatujui 2050 tutakuwaje. Kwa sasa hicho kipimo Tanzania ni 0.555. Kwa hiyo karibu tuko 50%, lakini wenzetu wa China tuliokuwa tumewazidi wao ni 0.79 wametuzidi kidogo. Wahindi tuliokuwa tunawazidi mwaka 1961 kwenye hiki kipimo cha *HDI* sasa hivi ni 0.685.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipimo cha tatu kama dira itafanya vizuri *QLI* yaani *Quality of Life Index* na hii ni nzuri zaidi kuzidi vingine viwili kwa sababu, sasa hii inachukua hata uwezo wa mtu kununua vitu yaani *purchasing power* ya mtu, inachukua mambo ya usalama, elimu, afya, mazingira, *national factors*, *social factors* kama raia wako wanaraha, wanafurahi, wanakaa wana huzuni huzuni, wanasikitika, yote haya yanachukuliwa. Hicho kipimo ni kipya duniani na sasa hivi anayeongoza kwenye hicho kipimo ni Uholanzi ana *point* 213. China yetu tunayoichukua ipo kwenye nafasi ya 53 na India iko kwenye nafasi ya 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, *point* sita alizosema Mheshimiwa Waziri ni za muhimu sana hasa ile ya kwanza kutumia teknolojia. Sasa sisi wanasayansi, siwezi kujitoa, na mimi nilikuwa kwenye hicho kikao, tulikaa chini tukaona sayansi itahudumia watu vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukaja na *formula*, sasa wale watu wa mipango naomba na nyinyi muiandike hii *formula*. Wewe ulisema unachukua *point*, andika hii. Yaani hii *formula*, wote tuichukue halafu tutajipima mbele ya safari, yaani namaanisha *prosperity* ya Taifa, ustawi wa Taifa kwenye karne ya 21, siyo karne ya 20. Ustawi unahitaji namba moja, *science*, namba mbili, *technology*, namba tatu, *innovation*, namba nne ameiongea vizuri Mheshimiwa Waziri, *human capital*, namba

tano, *financial capital*, namba sita, *markets*, namba saba, hii ni *plus minus*, *earth resources* au *raw materials,* lakini kuna nchi kama Japan, Korea haina *raw materials*, ndiyo maana tuliweka *plus minus*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii tulivyofanya miaka ya huko tukiwa na wenzangu tulikuwa tunatengeneza mchoro, tunaiona kama nchi imefanikiwa. Sasa Mheshimiwa Waziri umeongea vizuri kwenye hii *formula* ya mafanikio, nachukua moja, *human capital*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *WHO* inasema kwamba, kama tunataka kupata afya nzuri duniani, *nurse* mmoja ahudumie wagonjwa nane. Kwa hiyo, tunategemea Mheshimiwa Profesa, tukionana mwakani au wakati wa bajeti, tunataka tufikie hilo lengo la *WHO*, *nurse* mmoja wagonjwa nane, ndiyo vipimo hivyo, daktari mmoja wagonjwa elfu moja, lakini kwa sasa Tanzania daktari mmoja anahudumia wagonjwa 20,000. Kwa hiyo, dira yetu ya maendeleo itutoe daktari mmoja wagonjwa 20,000 mpaka daktari mmoja wagonjwa 1,000 kama ilivyo pendekezwa na *WHO,* tupate hiyo mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja ma-*engineer* viwanda, ukitaka kiwanda kifanye vizuri mambo ya *engineering* na *construction*, unahitaji *professional engineer* mmoja, awe na ma-*technician* watano au sita. *One to five or one to six*. Tutajipima na Tume ya Mipango mtupatie mkakati wa kufika hapo na ndiyo maana, sisi hela za kutoka nje ni chache, Wahindi ni wengi kwa sababu, India kwenye kila watu 1,000, vijana nane wana-*gradute* na shahada ya *engineer*. Nakuja namalizia, namalizia na wewe umesema jioni huongei, si ndiyo! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Profesa malizia tulishakuongezea pia na muda kidogo.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni suala la elimu, hili naliacha tutaongea kwenye bajeti kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwa kumalizia, mapinduzi na hili la mwisho nivumilie dakika moja. Mapinduzi yote ya uchumi toka

*first industrial revolution* mwaka 1960 mpaka 1860, miaka 100 ya kwanza ya mapinduzi ya viwanda duniani yalihitaji vitu viwili. Ilikuwa nishati, ilikuwa ni *coal* na chuma. Mapinduzi ya pili yalihitaji umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namalizia kwa kusema kwamba *development vision* yetu ya mwaka 2050 itahitaji umeme kiasi gani ili tuweze kufanikiwa hivyo, kwa sababu sasa hivi mapinduzi yetu ya umeme ya mtu mmoja mmoja ni *unit* 245 kwa mwaka. China wanazo zaidi 7,000 na mwisho uchumi wa China, hili ndio *statement* ya mwisho, uchumi wa China yaani *GDP* ya China trilioni 20.8 umeme, uwezo wa kuzalisha umeme ndani ya China ni *gigawatt* 3950, yaani *megawatt* 3,950,000.

**MWENYEKITI:** Ahsante Profesa

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa India wenye *GDP* ya trilioni 4.2, uwezo wake wa umeme ni *gigawatt* 520.5 yaani *megawatt* 520,500. Je, sisi *Vision 2050 GDP* ya trilioni moja tuna umeme kiasi gani? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante Profesa kwa mchango wako mzuri, na tulimuongezea muda kidogo. Sasa tunaendelea Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kitu kimoja tu, kuongea baada ya Profesa Muhongo ni mambo mawili, *it either a high bar or the beginning of very funny joke,* lakini nitajaribu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza Profesa Kitila Mkumbo na Naibu Waziri pamoja na timu nzima kwa kazi nzuri wanayofanya. Profesa umeongea vizuri sana, *my only wish* ni kwamba namna sasa ya kuchukua haya tunayozungumza halafu tukayaweka kwenye matendo, tukifanya hivyo Taifa letu litakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujua matatizo yetu haimaanishi kwamba ndio tumeshatengeneza... na sisi huwa tunashindwa

sana kwenye matendo, lakini kuandika *document* nzuri nitarudia na tukishindwa tutaandika nyingine nzuri kwa nini tumeshindwa, sio njia nzuri sana. Kwa hiyo, ni vizuri tukaanza kutekeleza zaidi. *Document* zetu kama hii *vision* itachukua safari ndefu sana, Marais karibu watatu huko mbele mpaka tumalize miaka 25, na sisi tulidhani kwa sababu sisi tumepata heshima Bunge hili na Profesa Kitila kwamba sisi ndio tumeandika Dira nyingine mpya ambayo ina *plans* ambazo ni *very ambitious,* lakini wataalam wanatuambia kama alivyosema Profesa Muhongo kwamba inawezekana na niwapongeze safari hii na Ofisi ya *Attorney General* katika kutengeneza sheria hii ya Tume ya Mipango, kitu ambacho ni kipya haikuwahi kuwa kwenye sheria zote za Tume hii ya Mipango, ni kifungu cha 6(4) ya sheria hii. *It was an attempt* na inasema hivi; "Mpango wowote wa muda mfupi na muda mrefu ulioandaliwa kwa mujibu wa sheria hii na sheria nyingine iliyotungwa na Bunge na kuidhinishwa na Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, haitabadilishwa ama kuachwa kutekelezwa katika muda uliopangwa kutekelezwa bila idhini ya Bunge hili."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *innovation* nzuri sana, kwa sababu ukisoma ripoti za huko nyuma utekelezaji umekuwa hafifu sana na ni kwa sababu tu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameandika ilani hii katika kipindi hiki cha Awamu ya Sita, lakini baada ya miaka mitano atamaliza kipindi chake cha madaraka, hatujui anayekuja ni nani, lakini atakuja na mwingine tena, akija na *vision* tofauti ama akija na vipaumbele tofauti maana yake dira ya miaka 25 inaweza isitekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii *attempt* yake ilikuwa ni kujaribu kuweka mkakati wa kufanya Bunge lishiriki kwamba watu wasije wakabadilisha, lakini Bunge litaweza kufanya hiyo kazi peke yake kama itabadilisha hata na Kanuni za Bunge ili tutafute namna maalum, tuwe tunasikia ripoti hii ya utekelezaji wa dira hapa Bungeni, kama anavyofanya *CAG,* kama tunavyopata ripoti za TAKUKURU, bila kufanya hivyo haitoshi kuandikwa kwenye sheria. Sheria *and itself,* sio *self executing*, hapana, *not in the page*...unaweza ukawa na sheria nzuri sana, lakini tusipoweka nidhamu ya utekelezaji hatutaweza ku....

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nilikuwa naangalia Profesa Kitila hapo, mnasema *private sector* na tunawashukuru sana *private sector* leo hii hapa, ni 70% yaani hii dira ili tuweze kutekeleza mchango wa *private sector* ni 70%, halafu taasisi za umma ni 30% na Profesa ameongea vizuri hapa kwamba tuwashirikishe.

Sasa mimi nikawa najiuliza, hivi mtu wa 30% ndio anamshirikisha wa 70% ama wa 70% ndio anatakiwa amshirikishe wa 30%? *It a way round actually*. Kwa hiyo, kwa kweli tuwasikilize *private sector, it should be a big job* kufikiri tumetengeneza dira ya maendeleo inayosema *private sector* ni 70% halafu tunasema tutawashirikisha, *I think it should be the other way round*. Wao ndio watushirikishe kwenye barabara hii ya kutekeleza dira kwa sababu ni ukweli usiopingika kwamba nchi zote *private sector rate growth* na kama alivyosema Profesa Muhongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia *document* moja hapa, mabingwa wale ambao sasa hivi wao wanaitwa *the trillion dollar club* nchi 20 na kama alivyosema Profesa Muhongo, China ipo, *South Korea* ipo, India ipo na wataalam wanatuambia pamoja na kwamba dira yetu ni *ambitious*, lakini ni *achievable* kwa sababu wanawaangalia hawa ambao walitoka nyuma yetu wakati fulani na sasa wapo mbele. Tatizo ni moja tu, sisi tunazo *barriers*, zinaitwa *structural problems*, ukiangalia leo makusanyo ya *TRA* kwa miaka kadhaa mfululizo mwaka 2023, 2024, 2025 tume-*exceed targets*, ni zaidi ya 103%, 103% *but that is not the point*, kwa sababu bado sisi *consistently* bajeti yetu *deficit* ni 3.4, kwa sababu *is not about* makusanyo, hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuanze kuangalia kitu kinachoitwa *tax to GDP ratio* ambayo ni *12.9% to 13%*, wakati kwa nchi za *SADC* kwa *average* ni 16%. Kwa hiyo, tusiangalie habari ya makusanyo, inawezekana hata tuna *exceed target* kwa sababu labda tunajiweka malengo ya chini kidogo, kwa hiyo, twende sasa kwenye zile *structural core reforms*, haya lakini Profesa ulikuwa unatuambia, ungetamani leo tusiwe tunajadili vyoo hapa, ni kweli *I agree with you*, lakini haitoshi halmashauri zetu hali zake ni mbaya sana, wataalam wanatuambia ili waweze kutekeleza na kufikia malengo yao, lazima wawe wana *contribute 8% of the*

*GDP*. Sasa leo wako chini, *it is not enough* kuwaambia tu hatutaki kusikia habari ya vyoo hapa, ni lazima tuwasaidie.

Kwa hiyo, Tume hii ya Mipango ni muhimu, muhimu sana na nimefurahi sana wakati unahitimisha ulisema hivi na Gilead Teri afanya kazi vizuri sana kutufanyia wawekezaji waje, lakini kilichonifurahisha zaidi siyo kuwaleta tu, wanabaki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu unajua hata hatuhitaji sana kutangaza nchi yetu, nchi yetu inajitangaza yenyewe kwa sababu ya *resources* alizotupa Mwenyezi Mungu na wale wakubwa wale, wanasoma tu, *they will come*. *So,* kuwatangaza tu, *it's not an issue,* je, wanabaki na kubaki kwao ni jinsi tunavyo-*behave*. Sheria zetu zikoje, ni *predictable* ama zinabadilika badilika kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia sheria hapa, nzuri sana ambayo ilitengenezwa na Bunge lililopita, ni nzuri sana kwa sababu wataalam wanatuambia, lazima *raw materials* zetu zibaki hapa nchini, lazima zibaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiendelee ku... na nchi zimefanya vizuri ambazo zimezuia *resources* na tulikuwa na sheria hapa nzuri sana ambayo inaitwa *The Natural Wealth and Resources something*. Sasa sheria ile ni nzuri sana, lakini shida yake ni moja tu mnataka mwekezaji akiwa ana tatizo, mnamlazimisha aende kwenye mahakama zetu, hakuna *investor* atakubali kitu kama hicho, *no way*. Ni afadhali tu-*train* watu wetu waweze ku-*litigate* kwenye Mahakama za Kimataifa, lakini mtu analeta naweka *resources* zote hapa, halafu sasa ana-*attempt* labda kufungua kesi unamwambia, fungua na hapa hapa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa *Attorney General* muangalie kifungu hicho cha 11. Kama tunataka kuondoa *barriers* za watu kuwekeza, *I think it is fair* ku-*create* mazingira mazuri ili wale ama tufanye mahakama zetu ziwe nzuri zaidi, ama tuvutie zile *international arbitration*. Leo Mauritius inafanya vizuri sana kwa sababu ni *centre of arbitration,* kwa hiyo, tukifanya hivyo, hivyo ndiyo kuweka mazingira vizuri. Mheshimiwa Profesa, programu yenu ya Mkumbi, *Mkumbi II* sasa. *Mkumbi I* yenyewe ukiichukua

leo hatujatekeleza sana, sasa sisi tunaogeza tu majina. *Mkumbi I, Mkumbi II, Mkumbi III* halafu unabadilisha badilisha tu maneno, lakini mambo yale yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa angalia hapa, tusije tukaanza kukuita Mheshimiwa Profesa Mkumbi huko mbele kama tusipoweza kutekeleza haya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuna *sector* inaitwa *informal sector* watalaam wanatuambia, ipo nje ya *tax system* kwa sababu ya *complications* zilizopo kwenye kodi zetu na sheria zetu. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais ametengeneza Tume ile ya Kodi, sasa tunaamini Mheshimiwa *Attorney General*, wewe sasa kazi yako ni kuchukua ile na kuleta sheria zote ambazo zimekuwa *proposed.* Tumalize, tuondoe *barriers* hizi katika uchumi wetu, tukifanya hivyo, nadhani tutatengeneza mazingira mazuri katika mwisho wa siku, haya yote tunafanya *for whose benefit?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amesema tuache tabasamu, tuache utu, uwajibikaji na nidhamu. Mheshimiwa Profesa hatutaki tutangaze nchi kama vile tunauza hivi kwa maana ya ardhi, *no. Uniqueness* ya nchi kama Tanzania ni kwamba maskini wana ardhi zao, kwa hiyo, ile programu yenu ile ya kuchukua wale Watanzania wenye ardhi zao na kuwa-*connect* na *investor is the best ever* kwa sababu tunataka Watanzania wapate mitaji, lakini utajiri wa ardhi yao iendelee kubaki. Kwa hiyo, Profesa, *recommendations* zote za Kamati ya kwetu myachukue yote, tusingetegemea leo Tume ya Mipango na yenyewe walie kwamba hawajepata pesa za bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna eneo la kuli-*ringfence*, ninyi ndiyo mpatiwe hela zote kila wakati kwa sababu ninyi ndiyo kama nilivyosema Mheshimiwa Profesa Muhongo, ninyi ndiyo roho yetu kwa miaka 25 ijayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante muda wako umeisha.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante.

Naomba nitambue wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, Naibu Waziri ambao ni Dkt. Vincent Mashinji, Mkuu wa Wilaya ya Manyoni; Ndugu Maimuna Likunguni, Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya Manyoni; Ndugu Tano Makambala, Mwenyekiti wa Halmshauri Manyoni; Bi. Anastazia Tutuba, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni; na Ndugu Paulina Nicodemus, Katibu wa Mheshimiwa Mbunge, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa, tunaendelea nilimwita Mheshimiwa Twaha Mwakioja.

**MHE. TWAHA S. MWAKIOJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali yate nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na baraka hii ya uhai.

Pili, nikushukuru wewe kwa nafasi hii na tatu nitumie nafasi hii kwa kinywa kipana, kwa kujiamini nimpongeza sana Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua uzito wa namna gani wa kuiendea michakato hadi kufikia kuandaa Dira ya 2025. Ni kazi nzito, inahitaji muda, inahitaji akili kwa kweli Mheshimiwa Profesa na timu yako tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi ziende zaidi kwa ndugu zangu wa Tume ya Taifa Mipango chini ya Katibu Mkuu, dada yangu Ndugu Tausi Kida na watendaji wote na watumishi wote watume kwa namna ambayo walivyojipanga na kuratibu hadi kufikia leo hii tuna dira ambayo ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa na mipango mikubwa ya Kitaifa kama dira, kama mpango wa miaka mitano wa nne, kama mpango wa mwaka mmoja, anayelengwa hapa ni mtu, hatulengi kitu kingine. Tunavyomlenga mtu tunakusudia matokeo ya mwisho kabisa *(end result)* ni ustawi wa mwanadamu, ni ustawi wa Mtanzania. Tukiangalia mipango ambayo tunayo, mpaka

sasa hali yetu ya kupungua umaskini imekuwa inapungua kwa taratibu sana. Changamoto juu ya hili ni nyingi na siku nikipata nafasi katika hali ya uchumi na Bajeti ya Serikali, nitawaweza kueleza kidogo kwa mapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba bajeti nyingi tunazozitengeneza zimekuwa ni bajeti za kiasi tunachokiweka na kitu tunachokiona, hatuiangalii bajeti kama programu ambayo inakwenda kutatua jambo mahususi kwenye jamii husika. Kwa mfano, nimepitia dira ya yetu ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho, nimeupitia mpango wa nne wa miaka mitano, sijaona upimaji mzuri wa hali ya maendeleo ya mtu, sijaona kipimo kinachoelezea umaskini katika mawanda yake yote ambayo ni *multi-dimensional poverty index. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunatumia kipimo kilekile cha kizamani cha kuangalia *income* ya mtu, ukizungumzia tu *income* mwananchi au mtu ana changamoto nyingi mbali na *income,* anaweza kuwa na kipato lakini bado akawa na umaskini wa elimu, akawa na umaskini wa afya, akawa na umaskini wa makazi, akawa na umaskini wa mawasiliano na kadha wa kadha. Lazima turudi nyuma nimesikia Mheshimiwa Profesa akisema kwamba wana mpango wa kutengeneza mpango mpana wa ufuatiliaji wa umaskini. Kama mpango huu utatengenezwa wajumuishe kipimo hiki na kiandaliwe *study* yake ili kiweze kutoa *data* sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipimo hiki uzuri wake kwanza kinakueleza maskini ni kina nani, kitakuambia wapo wapi, na pia kitakueleza ni wa jinsia gani, itakueleza kiasi cha umaskini wao na kitakuambia wana umaskini kwenye eneo gani, zaidi kitakwambia *intervention* gani ufanye kuwakwamua kwenye eneo hili, ni kipimo kizuri ambacho kinaweza kutumika kwenye mipango yetu ya kibajeti na kutusaidia kuondokana na bajeti ambayo inafanywa zaidi pengine wakati mwingine kwa misukumo ya kisiasa, kwa mahusiano, kwamba mimi nahitaja kituo cha afya, basi kituo cha afya kinakwenda kumbe watu wa eneo husika wana umaskini katika eneo la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kuchangia, maskini wetu wengi zaidi ya 80% ndiyo wanaoshiriki kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi. Na eneo hili ndilo ambalo linaajiri Watanzania zaidi ya 70%, hao 70% asilimia yao 80% ndiyo hawa maskini. Kwa kipimo kile cha *income poverty* ni zaidi ya watu 25% wako kwenye umaskini, *basic needs poverty* hali hii ni ya kutisha sana. Tunawekeza kwenye kilimo, tunawekeza kwenye ufugaji, tunawekeza kwenye mifugo, lakini bado Watanzania ni maskini. Watanzania ni maskini ni mengi yanatakiwa kufanyika kwenye eneo hili, lakini kwa uchache nizungumzie kwamba tuwekeze viwanda vinavyokwenda kugusa *processing* kwenye maeneo haya ya matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiwapelekea watu viwanda ambacho hakiendi kuwagusa moja kwa moja, tunachana na ile dhana ya mpango wa miaka minne wa maendeleo unaosema kwamba ni *inclusive economic growth*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *inclusive economic growth* ni uchumi shirikishi ambao unakwenda kwashirikisha Watanzania ambao ni maskini, ambao wanashiriki kwenye ufugaji, wanashiriki kwenye kilimo, wanashiriki kwenye mifugo tupeleke viwanda vya kuchakata mazao. Leo watu wanalima nyanya, leo watu wanalima mihogo, mfano Mkinga, kunalimwa na nazi, kunalimwa korosho, lakini maeneo yote haya hakuna viwanda vinavyowagusa Watanzania hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunafikiria viwanda vikubwa sana kama vile ni nchi tayari ambayo ni ya uchumi wa kwanza au uchumi wa pili wa juu, bado sisi tupo ni *developing country* tuwekeze viwanda vinavyoenda kutatua tatizo la umaskini la watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni eneo la namna la uwiano katika uwekezaji mijini na vijijini. Kwa mfano, eneo la Mkinga kuna mpaka mkubwa sana pale kati yetu na Mombasa, lile ni soko ambalo lipo huru kabisa, lakini eneo lile halina uwekezaji wa namna yoyote limekuwa ni kama barabara unayopita pale Ubungo hakuna kiwanda, hakuna soko la kimkatati la mazao ya samaki, hakuna kumbi, hakuna viwanda,

hakuna chochote na pale pakiwekezwa ipasavyo ni soko huru litaongeza ajira, litaongeza kipato na mambo mbalimbali. Nimwombe kiongozi wa *TISEZA* aiangalie Mkinga na ndugu yangu Kafulila aingalie Mkinga na namna gani tunaweza kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize eneo la mwisho mahususi. dira inazungumzia kwamba ina *pillars* tatu, ina *goals* nne, lakini katika eneo moja la uchumi tunasema ni mazingira bora ya biashara. Katika mazingira haya bora ya biashara, *strategic objectives number* nne inasema; *"accelerate transformation of productive sectors to generate quality jobs, value addition and export competitiveness."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nina dukuduku, tuna bidhaa inavyozalishwa ndani ya nchi, tuna viwanda vitano. Viwanda hivi vitano Tanga pekee yake tuna viwanda vitatu, lakini kwa bahati mbaya bidhaa hii ya *coated calcium carbonate* bado inaingizwa kutoka nje, bidhaa hii inatumia *HS Code* ya 2836.5.0 imewekewa *import duty* ya 0%. Hii tunaua viwanda vyetu vya ndani ambavyo dira yetu yenyewe inatusuta, ina tukaanga tunasema tunataka tukuze ushindani katika *export,* lakini tunaruhusu watu wanaingiza bidhaa hizi kutoka nje ilhali tuna *capacity* kiwanda hiki kimojawapo kimewekezwa zaidi ya shilingi bilioni 15 kinaweza ku-*meet market* na ziada na kupeleka nje, lakini hili halifanyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Mipango atakapokuja hapa, atueleze faida zote hizi za viwanda hivi ambavyo vitaongeza ajira, vitaongeza mapato, vitavutia uwekezaji tutapunguza *forex* tunayoitoa nje, viwanda hivi vitaweza kutumia malighafi yetu na kusambaza ajira kwa watu wetu wengi. Yote haya tunayaacha, atueleze tunataka kukuza viwanda vyetu au tunatangaza tu kwenye maandishi ilhali kwenye utendaji atujapanga namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri katika hili wakae wenzetu wa Wizara hii na Wizara ya Fedha na timu yao wafanye *in-depth analysis*. Wakiona inafaa na naamini inafaa baada ya kupitia kwa kirefu waweke *import duty* kwenye bidhaa hizi ya 25%,

haimaanishi tutaua huo uingizaji bali tutaleta *fair competition* kwa wazalishaji wa ndani na hao wanaongiza kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kukushukuru na niongeze kwa kupongeza sana watendaji wetu hawa kwa jambo hili kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, ajiandae Mheshimiwa Joseph Musukuma na Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo kwa umahiri wake wa kuwasilisha vizuri hotuba ya bajeti ya asubuhi ndani ya Bunge, lakini pia nimpongeze sana aliyesoma taarifa ya Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria Mheshimiwa Zena Katambo kwa kutoa hotuba nzuri na maoni ya Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye taarifa hii ama hotuba ya Mheshimiwa Waziri na jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri ameeleza kwa umahiri na kufafanua mipango na dira ya Wizara hii, utabaini kwamba tofauti na ambavyo pengine Wabunge wengi tunashauri, Wizara hii ama nchi hii hakuna uhaba wa mipango, mipango ipo vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wanafalsafa wanasema kujua tatizo ni sehemu ya kutatua tatizo lenyewe. Ukimsikiliza Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na Wizara yake yote kwa ujumla kwa muda wote ambao amekuwa Waziri kwenye hii Wizara utabaini kwamba wanajua matatizo, wanajua mipango muhimu ya kutupeleka kutekeleza Dira 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la muhimu hapa tunalopaswa kuisaidia Wizara hii ni kushauri na kushauri Serikali iongeze rasilimali fedha kwenye Wizara ili itekeleze mipango ya Dira 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawakumbusha sana Waheshimiwa Wabunge hii Wizara ya Mipango na Uwekezaji kama ni nyumbani ndio wanaokaa jikoni kupika chakula, tunayojadili yote ndani ya Bunge hili, tunajadili changamoto za barabara, tunajadili maji, mipango ya elimu, wanaopika ni Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na wenzake. Tafsiri yake ni nini, kama kuna jambo tunahitaji kulipa kipaumbele cha kwanza kwenye kutoa fedha 100% ni Wizara ya Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakipata fedha 100% hii Wizara watatusaidia kupanga mipango ya nchi ili Wabunge sasa tunapokuja kujadili changamoto za wananchi wetu mipango iwe imekaa sawasawa na niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri ameongea mara nyingi ndani ya Bunge hili, eneo la kwanza tunalopaswa kuangalia ili kutekeleza Dira 2050 ni kuanza kubadili mtazamo yaani *mindset*. Tunalo tatizo kwenye Wizara, tatizo kwa watendaji wanafanya mambo *business as usual* na Waziri ametuambia lazima tuhame huko tuende kwenye *business unusual*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kama kuna jambo kubwa la kihistoria, *legacy* ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ilikuwa ni uamuzi wa kukubali ushauri wa Bunge kuunda Tume ya Mipango ya nchi hii. Hili ni jambo muhimu sana kwa Taifa na ndiyo jambo pekee litakalokwenda kututoa hapa tulipo kwenda kwenye hatua nyingine. Yale yote ambayo amesema Mheshimiwa Profesa Muhongo na Wabunge wengine, msingi wake ilikuwa ni hii kuwa na Tume ya Mipango ambayo Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan alikubali kuunda Tume ya Mipango tunampongeza sana kwa jambo hili na Mwenyekiti wa tume hii ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa, mwezi wa tatu, nilikusikia ukizungumza na wadau wa biashara nchini ili kuthibitisha kwamba wewe ni mwanamapinduzi unayeamini katika watu kubadilika fikra na kwamba unajua tatizo tulilonalo na tunakopaswa kwenda, nataka ninukuu ambacho ulisema Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa anasema hivi sehemu ya hotuba yake; "Kama sehemu ya *mindset* na mtazamo ambapo tunapaswa kwenda kama Taifa ili kuongeza uchumi kwa nchi." Anasema; "tatizo Tanzania tunataka vitaasisi vidogo vidogo vingi, vinaleta usumbufu mkubwa kwenye biashara, hiyo kitu tumefanya *study, World Bank* wameonesha *study* Tanzania ni miongoni mwa nchi Barani Afrika wenye *too many regulatory authorities with conflicting functions*." Anaendelea Profesa, anasema; "Kwa hiyo, wataalamu wetu *open up your minds,* na mu-*argue* sio kama sekta, mu-*argue as a government*." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa anaendela anasema; "Chukulia picha pana zaidi, hatuwezi kwenda popote bila *economic freedom. Economic freedom* haiwezi kupatikana, inakuja *with freedom to business.* Nchi yoyote ambayo imebana uhuru wa biashara, imetengeneza geti la uhakika la kwenda kwenye umaskini." Mwisho anasema Profesa; "Kuondoka kwenye umaskini hatua ya kwanza ni uhuru wa kufanya biashara. Tusipolielewa hili tutaandika dira 500 tutabaki hapa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kuona Profesa *knows the problem* na ukisoma kwenye hotuba hii Mheshimiwa Wizara ya Mipango ilipanga kufanya tafiti mbalimbali ya miradi na maandiko mbalimbali ili kutekeleza Dira ya mwaka 2050, lakini pia kwenye hotuba hii utabaini Wizara hii ilikuwa na mipango ya kufanya utafiti na kuongeza maeneo ya uwekezaji ya kiuchumi *(special economic zones),* lakini jambo kubwa kama ambavyo Kamati yetu imebainisha utoaji wa fedha ulikuwa sio wa kuridhisha na ndio msingi wa ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali iweke mkazo wa kutoa fedha 100% kwa Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji ili kusudi haya maono, hii ndoto na matamanio yaweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, wote tunafahamu uko msemo unasema *if you want to succeed, plan; If you fail to plan, you plan to fail* na kwa hiyo, ni lazima watu wa mipango wanaopanga mipango ya nchi tuwape kipaumbele na mimi niwasihi sana Waheshimiwa Wabunge pamoja na kwamba bajeti hii ni kidogo tupitishe bajeti hii kwa 100% siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka niseme kuhusu hali ya uwekezaji nchini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha Mheshimiwa. Tunakushukuru.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Joseph Msukuma, ajiandae Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Profesa Mkumbo pamoja na wataalam wote. Kwa kweli naomba niseme kama Profesa Mkumbo tutafeli kwenye hii Wizara unayoiongoza sijui huko mbele itakuwaje. Kwa sababu mimi nakuamini sana kichwa chako Mheshimiwa Profesa na hili nalisema wazi na Profesa mwalimu wako akiwa ananisikiliza hapa na nimpongeze sana kwa kuja kumsikiliza mwanafunzi wake na mimi natamani nikizeeka siku moja mnikaribishe na nimependa *swagga* ya leo ya Profesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme wazi ni kweli tuna mipango mizuri sana hili nalisema kila siku. Mipango sio matumizi kama huisimamii. Unapopanga kitu halafu hukisimamii huwezi kufanikiwa. Na mtu yeyote mwenye mafanikio anaishi kwenye mipango yake. Najaribu kuangalia ninyi huku juu mko sawasawa kabisa. Wizara na Profesa, lakini

wanaotekeleza mipango yetu ni halmashauri huko chini. Mmewahi kufanya *research* ya maisha ya watu huko chini? na hizo halmashauri kwenye mipango yenu ama mnaletewa tu maandiko halafu *mna-copy* na *ku-paste?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe maisha ya watu ya wafanyabiashara ni maisha magumu sana hasa kule chini, mfanyabiashara yeyote aliyeko chini kwenye halmashauri na ndio kwenye chanzo hana msaada wowote kwenye halmashauri hana. Yaani kila mtu kwenye halmashauri msimamizi ambaye anatakiwa kumfanya mtu akue mkubwa kila siku anaamka kuwaza kwenda kuchukua hela tu kwa mfanyabiashara, sasa niwaombe sana tunaweza kuwa tunazungumza vizuri tunapanga vizuri lakini utekelezaji wake ni mgumu kwa sababu kule chini kwenye halmashauri ambao ndio watekelezaji hawaendani kabisa na mipango tunayoipanga kwako Mheshimiwa Profesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili Profesa huwa najaribu kujiuliza kwa elimu yangu ya kawaida na nimpongeze Rais nilimuona juzi anasema yeye mwenyewe anakata misafara na wataalam wake wengine watapanda basi. Na alipokuwa anahutubia kwenye hotuba yake hapa alitoa maelekezo na akasema malengo yake, lakini sijui ugumu uko wapi? Rais amerudia mara nyingi anasema mashirika ambayo hayana msaada nitayafuta ama nitayaunganisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nataka nijiulize kwa mfano *TBS* na *WMA* wote ni wale wale, lakini kila upande kuna *DG* kwa nini tusiondoe hilo shirika moja tukaliache *TBS* ili kikawa ni kitengo ndani ya *TBS*? Kwa sababu kazi ni ile ile wanayoifanya na wewe nayo unatuahidi tunayaunganisha sijui wanakupiga *beat* unapotelea wapi tena? Nashindwa kuelewa nenda *EWURA* kuna *EWURA* halafu kuna *PURA* kazi ni ile ile. Kwani haweza kuwa kitengo ndani ya *EWURA* mpaka kila mahala tukawe na *DG* tuwe na Mkurugenzi sijui tuwe na *V8* kama nane. Hatuoni kama tunaongeza matumizi ambayo hayana maana yoyote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye *CAMARTEC*, *TIRDO*, *TEMDO*, *SIDO* ukiangalia kazi zinazofanyika zote ni za *SIDO,* lakini kila mahala kuna *DG*. Ugumu uko wapi? Kila mwaka na Rais

ameshawaeleza mnashindwaje kuyaunganisha haya mashirika? Nenda *UDART* halafu na *DART* wote ni Wakurugenzi na wana..., jamani maprofesa na bahati nzuri profesa nimeanza vizuri wewe Profesa, Katibu wako Msemwa Profesa kina Mchechu wote wasomi wazuri. *(Makofi)*

Sasa naona Mheshimiwa Rais aje anipe kitengo humo dokta mwenye akili nikafanye kazi yangu na *Ph.D* yangu niwarekebishe huko ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuwaje na wakurugenzi ambao wote wanafanya kazi moja? Na mimi na kumbukumbu nzuri sana Profesa umeunganisha *TIC* na *EPZA* mnaonaje tunavyoenda kwa sasa? mmetengeneza *TISEZA* ile. Kwa nini mmeweza halafu hawa makorokoro tunazidi kubaki nayo tu tunapiga maneno kila siku. Wewe ukiwa Katibu wa Wizara ya Maji kulikuwa na *DAWASCO* na *DAWASA* wote kazi zile zile, lakini zote zina wakurugenzi ukaunganisha ikawa *DAWASA* unaonaje haya mafanikio?

Kwa hiyo, niombe sana Profesa mipango lazima tuwe tunaisimamia sio mnatuahidi halafu kwenye utekelezaji inakuwa haiwezekani, lazima tufike mahala kama nchi tukubaliane suala tunalolizungumza na kulipitisha kwenye mipango wetu ni lazima likatekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni upande wa kilimo. Mheshimiwa naomba niulize mimi toka kuzaliwa sijawahi kuona yaani Wizara moja ina bodi zinafika 50. Bodi ya Tumbaku, Bodi ya Korosho, Bodi ya Pareto, Bodi ya Kahawa, kila zao. Sasa na mimi kwangu tunalima mananasi, mniundie na Bodi ya Mananasi. Hizi kazi zote zinaweza kufanywa na Mwenyekiti mmoja tu mwenye akili. Bodi ya mazao, bodi ya magunia, bodi ya mbolea, bodi kila mahala tumeweka bodi. Uliona wapi? Wizara moja ina bodi karibu 50 ni kutengeneza mifereji ya watu kula na kuongeza mzigo kwa Serikali wakati matatizo bado tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nakuomba sana kama Mheshimiwa Rais amekupa kuyarekebisha kuzirekebisha Wizara na Mashirika, naomba sana fanya kazi bila kuogopa mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisoma Gazeti la Nipashe, Profesa, mimi natokea kijijini, la Machi 25 likawa linaeleza limechora picha nyingi sana za mboga za majani kwamba hizi mboga zina sumu na ilijadiliwa sana mitandaoni. Sasa kwa sisi tunaotoka kijijini chakula chetu cha kila siku ni huo mchicha, kabichi hayo mamboga mboga ya majani ambayo sasa hata mkipita mnaenda Dar es Salaam mnaona barabarani kila mahala ni bustani. Siku ya kwanza, siku ya tatu, siku saba mchicha uko sokoni na tumeshaambiwa ni sumu mpango wako ni nini tunahitaji mpango wa haraka kutunusuru kwa sisi tunaotoka kijijini siku umepata hela ndio tunakula dagaa, maisha yetu yote ni hizo hizo mboga za siku saba hafu zote zinasumu na tunakaa humu nawasikiliza wataalam wanahoji kwamba sasa hivi wagonjwa wa figo wameongezeka, tunauana wenyewe tunaonana hivi hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwa sababu hili ni kama janga baadae tutakuja kuua watu wengi zaidi ya hata ya mauaji ya kimbali. Mboga yetu sisi ni mchicha ukiwasikiliza wataalam wakuambia ukila mchana mboga saba tia mchicha, mchicha wa siku saba huo wenye sumu kila mahala. Mpango wa haraka ni nini kwako Profesa Mkumbo utusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine Profesa nimekusikiliza kwenye mpango wa, nimeona page ya *PPP* ya ndugu yangu Kafulila. Nataka kujiuliza labda *PPP* huwa ni nini, lakini mimi kila siku nikijiuliza *PPP* si ni muunganiko wa *private sector* na Serikali hebu ni wapi mnionyeshe mliungana na nani ni wapi? Sioni na leo hii unasema mnaenda kwenye 75% *private sector* na ninyi Serikali 25...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha. Ahsante.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** wapi ambapo mmefanya mkafanikiwa? Kwa hiyo, niombe sana tusimamie mipango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, tutamalizia na Mheshimiwa Arif Suleiman Premji.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi na mimi niungane na Waheshimiwa wenzangu waliotangulia kuongea hapa kuipongeza sana Wizara ya Uwekezaji chini ya Profesa Kitila Mkumbo, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa hotuba nzuri inayoleta matumaini, lakini pia niipongeze Tume ya Uwekezaji imefanya kazi kubwa na kazi nzuri sana. Na kazi hii inatuonesha kabisa namna ambavyo Dira ya Taifa inakwenda kutekelezeka kwenye Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazamo wa sera ya uchumi Tanzania unahimiza sekta binafsi kuendelea kuwa *engine* ya ukuaji wa uchumi na ajira kwenye Taifa letu, lakini pia sekta binafsi inachangia 70% ya uwekezaji na 30% inachangiwa na Serikali. Tunaipongeza *TISEZA* imeweza kusajili miradi mipya 611 lakini pia miradi 915 imeweza kusajiliwa yenye thamani ya dola bilioni 10.95. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kazi kubwa na nzuri iliyofanyika chini ya Wizara hii, tunawapongeza sana. Lakini kwa upande wa *TISEZA* tumeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri na tunafahamu kwamba kazi kubwa na msingi ambayo imejiwekea ni kumaliza umaskini kwa wananchi wa Taifa hili, sambamba na hilo kuandaa maeneo ya uwekezaji. Sasa nilikuwa naomba viwanda ambavyo tayari vimeshaanza kuwekeza kwenye Taifa letu vilindwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto, unakuta kiwanda kinazalisha bidhaa ndani ya Taifa hili na kinauza, lakini bado kuna bidhaa za aina hiyo hiyo zinaingizwa kwa msamaha wa kodi, hii sio sawa kwenye ushindani. Viwanda hivi vitakwenda kufa na viwanda hivi vikifa kuna hasara nyingi hususani wananchi wanakwenda kupoteza ajira. Tuna wimbi kubwa sana la ukosefu wa ajira kwenye Taifa letu. Kwa mfano kiwanda kimoja kiko Tanga kinashughulika na *coated calcium carbonate*. Kiwanda hiki kinazalisha takribani *metric 2500* mpaka 3000 wakati mahitaji ya Taifa ni *metric* 2,000 mpaka 2500. Maana yake kinazalisha uwezo

zaidi ya mahitaji, lakini bado kuna bidhaa hii hii inaingia kwa msamaha wa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Wizara iangalie ili tuvilinde viwanda ambavyo tayari vinafanya kazi kwenye Taifa hili. Viwanda hivi tukienda kuvipoteza hasara kubwa inapatikana kwenye Taifa hili, lakini faida ya kuvilinda viwanda hivi tunakwenda kulinda ajira za Watanzania, tunakwenda kuongeza mapato na kodi ya Serikali, lakini pia tunapunguza uuzaji wa bidhaa nje ya nchi na tunaongeza mauzo ya nje, lakini tutaongeza fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena leo kumuomba Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa mara ya pili sisi Wanadar es Salaam, wanawake na vijana wajasiriamali wa Dar es Salaam wanaomba kliniki ya ardhi ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam. Tunakwenda kwenye utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa. Dira ile kipimo chake ni wananchi huku chini. Na nimeshukuru sana kuona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna sehemu inasema kutakuwa na mafunzo ya utekelezaji wa dira, kwa sababu mpaka sasa bado 90% huku mtaani bado hawajui dira ni nini, wanakwenda kutekeleza vipi lakini wao ndio watekelezaji. Serikali imeweka mipango, wananchi huku chini ndio watekelezaji tunataka tuone uchumi mwananchi mmoja mmoja umeongezeka, lakini viwanda vimeanzishwa. Viwanda hivi vitaanzishwa hawa wanaoenda kutekeleza hii dira lazima wawe na ufahamu na uelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dar es Salaam una makundi manne ya vikundi vya akina mama. Kuna vikundi vyenye mitaji ya milioni 700 mpaka bilioni tatu vipo kwa 15%, lakini vikundi vyenye mitaji ya milioni 100 mpaka 600 vipo 20% na vikundi vyenye mitaji ya milioni 10 mpaka 50 vipo 25% bado kuna ombwe kubwa la vikundi ambavyo havina mitaji kabisa vinajitafuta hivyo ni 40%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri kupitia Tume ya Mipango tuangalie hawa wenye mitaji, wasaidiwe walelewe ili waende kutekeleza vizuri dira akinamama hawa wakiweza kufungua kampuni, Tume na hawa *TISEZA*

watusaidie basi akinamama hawa wa kampuni wapate kazi kwenye viwanda vikubwa. Kuna kazi nyingi kazi za usafi, kazi za ku-*supply* vyakula, kazi za ku-*supply material* kwenye makampuni. Badala ya mtu mmoja kupewa hiyo *tender,* mtu ana kampuni yake binafsi, vipewe vikundi na tukifanya hivyo tutainua uchumi wa wanawake. Wanawake leo wataanza na vikundi, wataanza na kampuni, watapata hizo kazi, tutawatafutia hizo kazi, lakini mwisho wa siku watatoka kwenye hizi kampuni watakwenda kwenye viwanda. Viwanda vile waajiriwa watakuwa watoto wetu ambao wengi wao wako mtaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimuombe Mheshimiwa Profesa anafahamu kabisa na yeye ni mwana-Dar es Salaam kwamba Dar es Salaam shughuli kubwa na ya msingi ni ujasiriamali. Wananchi wa Dar es Salaam wanahitaji fedha ili wafanye uwekezaji na wapo tayari hususani wanawake wa Dar es Salaam wapo tayari kuwa wawekezaji ndani ya mkoa wetu lakini ndani ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe Wizara iangalie namna sasa ya wao kuwa kiungo, kuwa wadhamini kati ya wakina mama, vijana na taasisi za kifedha. Mfano mdogo sana pale Dar es Salaam maafisa usafirishaji wa bodaboda na bajaji wanaitwa kila siku kwenye semina na taasisi za kifedha. Semina zile wanafundishwa namna ya kukopa vyombo vya moto kukopa bodaboda na kukopa bajaji lakini kuna fedha wanatakiwa waweke kama dhamana wanashindwa. Sasa hivi wamekuwa wakiitwa hawaendi sababu haiwasaidii tena walishaelewa kinachotakiwa ni hiki na hiki lakini hawana uwezo. Sasa kwa nini basi Serikali isiangalie wao kuwa mdhamini waka-*deposit* wao fedha kwenye hizo taasisi za kifedha vijana hawa wakapewa hizo bajaji, wakapewa bodaboda wakaanza kurejesha marejesho? Sababu vijana hawa hawa wanachukua bodaboda za watu, wanachukua bajaji za watu, wanafanya kwa mkataba ndani ya mwaka mmoja wanamaliza tena mikataba ambayo ni inaumiza. Kama Serikali itakuwa mdhamini na wakaenda kuweka ile fedha pale benki, vijana wakapewa hivi vyombo wataweza kurejesha zile fedha. Benki itapata hela yake, lakini na hela iliyowekwa itarudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia ajira, ni rahisi sana kumshauri kijana nenda kajiajiri, lakini kwenye uhalisia sio hivyo Waheshimiwa Wabunge. Tuwasaidie vijana wetu kundi kubwa la vijana wamejiajiri hizi shughuli ndogo ndogo.

Kwa hiyo Serikali sasa ifike mahali muwe wadhamini, akinamama wenye vikundi vikubwa wenye mitaji mikubwa muwadhamini wapate mikopo hii mikubwa twende kwenye uchumi wa viwanda. Lakini pia tuwe na *database* kwenye mikoa yetu yaani vikundi vingapi vina uwezo gani? Vikundi vingapi vina uwezo gani? Mnapotuletea fursa kama hizi tuhakikishe ni lazima wakina mama hao wasaidiwe. Kwa mfano pale Mkoa wa Dar es Salaam ndio mkoa wenye viwanda vingi na uwekezaji wingi kuliko mikoa yote. Tukipata hiyo kliniki ya ardhi, ikawa inapita kwenye kila kata au hata kiwilaya sababu tutakuwa tuna *database,* vikundi vikaitwa wakaelezwa fursa hawa wakawekeza huku hawa wakawekeza huku tutamaliza tatizo la ajira, lakini pia hiyo utekelezaji wa dira ndio utakwenda kuonekana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** umeisha? ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Arif Suleiman Premji mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nishukuru kwanza nitakuwa mchangiaji wa mwisho leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais ana mpango mzuri sana kwa ajili ya Mkoa wa Mtwara na ana dhamira njema sana kwa ajili ya mkoa wetu wa Mtwara na kwenye mkakati na hata kwenye Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi ya 2025/2030 kuna viwanda vya kimkikati, cha mbolea, cha sukari na hii ni utashi wake pia. Kwa hiyo, kwa hilo tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ilipitia misukosuko pia kwenye mambo ya *foreign policy* miaka ya nyuma. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia moja ya kazi aliyofanya ni kuzunguka kwenye nchi mbalimbali kurudisha imani, kuwaaminisha wawekezaji kwamba Tanzania ni sehemu salama na yenye amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo na ninaongea *from an investor point of view* (kama mwekezaji). Uwekezaji wowote una misingi yake na utaratibu wake, huwezi kwenda kwenye sehemu yoyote ukawekeza tu lazima utaangalia baadhi ya vitu. Moja utaangalia nishati, utaangalia eneo kwamba lina malighafi, utaangalia miundombinu, utaangalia kodi na na sera, utaangalia soko, utaangalia ardhi, lakini pia utaangalia deni la Serikali pia kwa ajili ya uchumi. Na hapo ndio unaweza ukafanya maamuzi kwamba je, niende nikawekeze nisiwekeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango tuliyokuwanayo ni mizuri, lakini bado kwenye sekta hizi ambazo tunazo, nilizozitaja kama nishati kwenye uwekezaji *coordination* ndio hakuna anaweza akaja mwekezaji akaenda *TISEZA* pale akapokelewa vizuri, anahitaji maji ataenda Wizara ya Maji, akihitaji nishati inabidi aende kwenye Wizara ya Nishati. *There is no proper coordination* na wakati mwingine inapelekea mwekezaji anakata tamaa na kuondoka anasema hapana changamoto ni nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti mimi nitakupa mfano halisi kwa ndugu zangu wa Mtwara pia. Mwekezaji anataka gesi ajenge kiwanda cha mbolea. Gesi inatoka Mtwara inapita kwenye baraza letu, lakini hatupati fursa huyo mwekezaji aweze kupewa gesi, hiyo changamoto. Lakini sio hilo tu, kuna mwekezaji mwingine wa Kiwanda cha Sukari pale pale Mtwara tayari kuna mgogoro wa ardhi, kuna wananchi wanadai fidia. Kwa hiyo, hakuna *coordination* ambayo ni nzuri kumfanya mwekezaji awe *safe*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiangalia kwenye upande wa kodi zetu, leo hii *safety* ya mwekezaji anaangalia je, mamlaka ya kodi yamekaaje? Na mfano mdogo tu wa uhalisia ukienda kwenye tovuti ya Mamlaka ya Mapato kuna mashauri mengi sana

ya kikodi, yaani ukichungulia pale kwenye *TRAB na TRAT* utaziona *all over trillions of money* hazipati usuluhishi, mwekezaji atakuwa na imani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye deni la Serikali 2025/2026; nilikuwa nasoma *annual borrowing plan* ya Serikali yetu *14.95 trillion* kwa mwaka wa fedha uliopita ambao ndio unakaribia kuisha, trilioni 14.95 ndio ilikuwa kwenye mkakati wa mwaka wa fedha kwamba tutakopa. Asilimia 75 ya fedha hizo ni fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ambayo inayoelekea ya uchumi ya nchi tunatarajia kwamba patakuwa na mfumuko wa bei na ukiangalia hata takwimu ya Machi ya *National Consumer Price Inde*x ambayo ni 3.2 inaonesha dhahiri kabisa leo hii ukisoma ile taarifa utaiona viazi vimeongezeka kwa 8.2%, utaangalia mchele umeongezeka kwa 2.6% lakini kiangalizo sasa kwa hali ambayo tunayoenda sarafu ya Tanzania itashuka thamani maana yake *rate* ya dola itapanda na italeta *effect* gani? Kwamba deni ambalo tulilolikopa litatugharimu kwenye kurudisha mathalani umechukua bilioni moja au tuseme dola milioni moja ambayo ni bilioni 2.6, sarafu ikicheza thamani ya shilingi imeshuka tuseme dola moja ikawa shilingi 3,000 maana yake tayari una *deficit* ya milioni 400 sasa milioni 400 unatoa wapi? Ndio utaanza kuchukua fedha zile zote ambazo umeziweka kwenye mipango kwenda kulipa deni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida ya muda naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa ratiba yetu iliyoanza asubuhi na tunahitimisha mchana huu na watakaoanza kuchangia jioni ataanza Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga na orodha itaendelea.

Baada ya kusema haya Waheshimiwa naomba kusitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.03 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, sasa ninamwita Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Edwin Malleko na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ajiandae.

**MHE. SULEIMAN MOHAMED RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi na mimi kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Awali ya yote ninaanza kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na mwenye kurehemu. Pili, ninamshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi kwa imani aliyoionesha juu yangu kuweza kupendekeza jina langu kwa ajili ya kupeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi kwenye nafasi ya Ubunge katika Jimbo la Mwera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ninawashukuru viongozi wa Chama Cha Mapinduzi katika ngazi ya Mkoa wa Magharibi,

Wilaya ya Mfenesini, lakini pia uongozi wa Jimbo la Mwera. Mwisho kabisa, siyo kwa umuhimu wake, ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mwera kwa namna ambavyo wamenipa imani ya kuweza kunichagua kuwa Mbunge wao katika kipindi hiki cha mwaka 2025 hadi 2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hii ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kwa namna ambavyo ameweza kuwasilisha hotuba yake iliyojaa umahiri mkubwa sana ambao umezingatia Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi, Mpango wa Miaka Mitano ambao pia una shabaha kwenye Dira yetu ya Maendeleo ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo ninakiri kwamba Mheshimiwa Waziri ni miongoni mwa Watanzania ambao wamepata bahati kubwa sana kuaminiwa na Mheshimiwa Rais. Kwanza, ameaminiwa na Mheshimiwa Rais katika utayarishaji wa Dira ya 2050, lakini kama hiyo haitoshi, Mheshimiwa Rais akiwa Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi ameweza kumwamini katika utayarishaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ambayo nayo iliweza kunadiwa katika mikoa yote na ambayo imemwezesha Mheshimiwa Rais kuweza kupata ushindi wa 97%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu utakwenda kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina na pia Tume ya Mipango na hapa ninakiri kwamba zipo jitihada tofauti ambazo zinafanywa katika Ofisi hii ya Msajili wa Hazina. Nikiangalia takwimu katika mwaka wa fedha 2019/2020, gawio pamoja na michango ambayo ilienda Serikali Kuu ilikuwa ni shilingi bilioni 753.96 lakini katika mwaka wa fedha 2024/2025 gawio pamoja na michango ambayo iliwasilishwa Serikalini ilikuwa ni shilingi trilioni 1.28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri kwamba zipo jitihada tofauti ambazo zimeweza kufanywa na Ofisi hii ya Msajili wa Hazina ambazo zimewezesha kuongezeka kwa michango pamoja na gawio kufikia 36%. Moja kati ya jitihada hizo ni kuweza kuongeza usimamizi kupitia mikataba ya wanahisa *(shareholder agreement)*, lakini pia kuweza kufanya mageuzi ya uongozi na

katika hili ninakiri kwamba baadhi ya taasisi ambazo zilikuwa zinaongozwa na wazawa kwa sababu ya hisa zetu, ziliweza kugeuzwa na sasa zinaongozwa na watanzania ikiwemo benki ya NMB, benki ya NBC pamoja na kampuni ya PUMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo ambazo zimefanywa ninakiri kwamba bado tuna changamoto kubwa sana kwenye usimamizi wa mashirika yetu haya. Kati ya mashirika 308 ambayo yaliwasilisha gawio, takwimu zinaonyesha ni mashirika 20 tu ambayo yanabeba 91% ya gawio na michango yote ambayo inawasilishwa ndani ya Serikali. Katika hili ina maana kwamba mashirika yaliyobakia 288 yote yanaingia kwenye kundi la kwamba wanawasilisha michango yenye asilimia tisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninakiri kwa kusema kwamba zipo jitihada mahususi ambazo zinapaswa kuweza kuchukuliwa ili kuweza kuona mashirika yetu tunaweza kupata faida, tunaweza kupata gawio, lakini tuweze kupata michango mikubwa ambayo itaweza kusaidia katika bajeti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano wa shirika moja kutoka Ethiopia ambalo ni *Ethiopia Telecom*. Kwa mwaka wanachangia zaidi ya bilioni 580 zenye thamani ya fedha ya Tanzania. Hapa unaweza ukaona kwamba kama tutaweza kuimarisha mashirika yetu, tutaweza kupata fedha za kutosha ambazo zitatuwezesha kuondoka hapa tulipo kwenye *deficit budget* kuelekea kwenye *balance budget* na hatimaye kuelekea kwenye *surplus budget*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wakati wanachangia kwenye hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu walilalamika juu ya mambo mengi ambayo hayaendi kwa sababu ya fedha. Ninakiri kwamba fedha tunazo tunahitaji mikakati ya kutosha ili iwe muarobaini wa kuweza kuona tunatimiza bajeti yetu na malengo ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mshauri wangu kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina, suala la msingi ambalo tunapaswa kulifanya kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina kwenye suala la uwajibikaji na utawala bora ni kuangalia namna gani tunaweza tukapata bodi

ya wakurugenzi ambao wenye dhamana ni chombo pekee ambacho ndiyo wasimamizi wa taasisi zetu hizi, lakini pia kuangalia utaratibu sahihi wa kuona namna gani tunaweza tukapata watendaji wakuu wa taasisi hizi. Watu wa aina hii mbili ndiyo wenye dhamana mahusus ambao wataweza kutuwezesha kuweza kufanya vizuri kwa taasisi zetu na mashirika yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na vipaumbele ambavyo Mheshimiwa Waziri ametuonyesha kwamba katika mwaka wa fedha 2026/2027 hivi ni miongoni mwa vitu vya msingi ambavyo wataenda kufanyia kazi. Mimi sina shaka juu ya imani ambayo Mheshimiwa Rais amempa na matumaini kwamba pamoja na michango ambayo tumewasilisha ataweza kwenda kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninafikiri ni la msingi sana kwenda kufanya ni kuona kwamba Serikali inakwenda kuwekeza katika maeneo ya kimkakati. Hapa nitolee mfano, leo Serikali tunapata gawio kutoka *Twiga Mineral* yenye *share* ya 16% tu zaidi ya shilingi bilioni 200. Unaweza ukaona kama Serikali itakwenda kuwekeza katika maeneo mahususi kama haya ya migodi tutaweza kupata fedha zenye mfano wa gawio ambazo zitaweza kutusaidia bajeti yetu hii na kuweza kuondokana na uhaba wa fedha ambao unatufanya tushindwe kutimiza malengo ambayo tumeweza kujipangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye suala la kufanya mapitio ya taasisi. Ninafahamu kwamba zipo baadhi ya taasisi ni za kimkakati, lakini zipo taasisi nyingine siyo za kimkakati. Tuone kwamba baada ya kufanya tathmini hiyo, zile taasisi ambazo ni za kimkakati tuweze kuziunganisha pamoja ili malengo ya taasisi hizo yaendelee kuweza kufanywa, lakini kwa zile taasisi ambazo zimeshindwa kufikia malengo na siyo za kimkakati ambazo mpaka sasa zinaendelea kupokea ruzuku kutoka Serikalini lakini bado nyingine hazina mchango wala gawio lolote ambalo wanalileta ndani ya Serikali, tuweze kuziondoa taasisi hizo ili tuweze kuondoa mzigo kwa Serikali yetu ambayo inaongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua muda unaenda mbio ninaomba niendelee kwenye mchango wangu wa pili kwenye eneo la Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri, mimi ni mdau wa *monitoring and evaluation* na ni mwenye Shahada ya Umahiri ya *Monitoring and Evaluation*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SULEIMAN MOHAMED RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba dakika moja kama utaridhia. Ni vigumu na ipo kanuni ambayo inatuongoza sisi watu wa *monitoring and evaluation* kwamba huwezi kuwa wewe mwenyewe unajipangia na wewe mwenyewe uweze kujifanya tathmini. Ipo haja ya kuona kwamba tunaanzisha taasisi mahususi ambayo itaripoti moja kwa moja kwa Mheshimiwa Rais yenye malengo na kazi ya kuweza kufanya ufuatiliaji na tathmini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Waziri wetu na tunamshuhudia Waziri Mkuu wetu amekuwa akienda kila sehemu kwa kazi ya kwenda kufanya ufuatiliaji na tathmini na zipo taarifa pamoja na *research* tofauti ambazo zimefanywa kwamba katika miradi ya Tanzania siyo tu kwa sababu ya fedha ambayo inakwamisha miradi hiyo, lakini baadhi ya miradi imekwama ni kwa sababu tu inakosa ufuatiliaji na tathmini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda ninaendelea kushukuru sana kwa kunipa nafasi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mwera naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Ninamwita sasa Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ajiandae, halafu atafuatia Mheshimiwa Beng'i Mazana Issa.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia kwenye Wizara hii nyeti kabisa kwa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa kumpongeza sana Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ya kuongoza Taifa hili. Sisi wanawake wa Tanzania tunamwambia tuko pamoja naye bega kwa bega afanye kazi, tunamwamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa anayoeendelea kuifanya kwenye mipango na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninampongeza sana Mwenyekiti wetu wa UWT Taifa, Mama yetu Mary Chatanda. Mama tunakupenda kazi yako ni njema umeunganisha wanawake, Mungu aendelee kukubariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda sasa moja kwa moja kwenye hoja ambazo ninachangia siku ya leo. Nianze kwa kuipongeza Wizara, imekuja na vivutio kwa ajili ya wawekezaji. Vivutio hivi vimeenda kusaidia wawekezaji wa ndani kuongezeka. Wamekuwa na vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi. Visivyo vya kikodi wameweka *one-stop centre* ambayo inawasaidia wawekezaji waweze kupata huduma zao sehemu moja bila kuhangaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vivutio vya kikodi wameweza kupunguza au kuondoa kabisa ile *import duty* katika vichwa vya malori kwenye eneo la usafirishaji, kwenye eneo la utalii, kwenye mahoteli wameondoa 100% kwenye zile tuseme *furniture* au *finishing*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye eneo la kilimo, kwenye zile mashine za kilimo kama matrekta na mitambo pia wameondoa 100% ya *import duty* ambayo inaenda kuwasaidia wakulima wetu kuweza kupata mitambo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021 nchi yetu ilikuwa ina wawekezaji wa ndani 10% tu lakini mpaka mwaka 2025 tulikuwa na wawekezaji wa ndani kwa 50% na wawekezaji wa nje kwa 50%. Kwa kipindi cha Januari mpaka Machi tumeweza kuwa na

wawekezaji wa ndani kwa 57%, ni maendeleo makubwa sana tunapongeza sana Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanyika, tulikuwa tunaiomba Serikali ione ni namna gani inaweza kuipatia Wizara hii fedha za kutosha ili ziweze kufanya kazi na miradi ya maendeleo iliyopangiwa iweze kutekelezwa kwa wakati. Katika Wizara hii, hadi kufikia Februari, 2026 Fungu Namba 11 lilipokea 20.88% tu ya zile fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamepanga miradi ya kutekeleza kutumia fedha hizo, lakini fedha hizo haziendi kwa mtiririko wa kutosha. Tunaona wamepokea 20.88% tu na hapa ndiyo sisi tunategemea suala la uwekezaji liweze kupewa kipaumbele. Walikuwa wamejiwekea miradi ambayo wataenda kutekeleza kwa kipindi hicho, kama ya uendelezaji wa maeneo kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa na mauzo nje ya nchi, lakini uendelezaji wa maeneo maalum ya kiuchumi, pamoja na programu ya kuboresha mazingira ya biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye dira tumejipambanua kwamba tunataka nchi yetu iwe namba tatu katika nchi za Afrika zinazoongoza kwa kuvutia uwekezaji na urahisi wa kufanya biashara. Kama fedha hazitolewi, tena hazitolewi kwa wakati, ni vigumu sana kuweza kuyafikia haya malengo yetu. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ione umuhimu wa kuipatia Wizara hii fedha kwa mtiririko unaofaa ili iweze kutekeleza miradi ili tuweze kukuza uwekezaji katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi waliokuwa wamejipangia, fedha haziendi kwa wakati, wale wawekezaji ambao walikuwa wametengewa yale maeneo maalum, hayo maeneo bado hayana miundombinu. Wawekezaji wanaondoka wanaenda kutafuta maeneo kwa wananchi, wanaenda kununua na mwisho wa siku maeneo yaliyopangwa hayawezi kutumika na baadaye yatavamiwa na bado tutaanza kuhangaika na wananchi waliovamia maeneo hayo. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali ione namna gani ya kupata fedha ya kuipatia Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo la kuboresha mazingira ya biashara. Sisi wote ni mashahidi, Disemba 2023, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, aliita waandishi wa habari kwa ajili ya kuwaeleza uamuzi wa Serikali wa kuyaunganisha mashirika 16 na kufuta mashirika manne kwa lengo la kuongeza tija kwa maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni 2026, miaka mitatu baada ya Mheshimiwa Waziri kwenda kutoa tamko hili mbele ya waandishi wa Habari lakini mpaka leo miaka mitatu, tunaona utekelezaji unasuasua. Kwenye hotuba yake ametusomea kwamba mpaka sasa mashirika ambayo yameunganishwa ni *TIC* pamoja na *EPZA* na ikazaliwa *TISEZA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema mashirika mengine matatu yameondolewa. Ni nini mkakati wa Serikali sasa kuhakikisha wanayafunga au kuyaunganisha hayo mashirika mengine ili sasa wafanyabiashara wasiendelee kupata mzigo mkubwa katika uwekezaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninaomba Wabunge wote muunge mkono hoja yetu na mimi pia ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Japhet Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Beng'i Mazana Issa na Mheshimiwa Amina Ali Mzee ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia nafasi, kwanza kabisa ninaanza kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, na ninaiunga mkono sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuja na dira nzuri na maono mazuri ya mwaka 2025/2050. Dira kwa kweli ni nzuri sana. Kama

tutaisimamia na kuitekeleza, tutafikia yale malengo ambayo tunayataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote walioko chini yake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika kukamilisha dira na kuja na hotuba nzuri ya bajeti ambayo imewasilishwa hapa leo. Mheshimiwa Waziri ninakupongeza sana kwa umahiri wa uwasilishaji wa hotuba nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kuipongeza Kamati yetu, Kamati ya Bunge kwa namna ilivyochambua hotuba hii, ilivyochambua bajeti hii na kuishauri Bunge kupitisha na kuiunga mkono hoja hii na ndio maana na mimi nimeanza kuiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu makubwa ya Wizara hii yameainishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri na mimi nitajikita kwenye maeneo manne. Amesema majukumu makubwa; kwanza, ni kuhakikisha anaisimamia sekta binafsi ili iweze kuchangia katika uchumi wetu; pili, kufuatilia programu mbalimbali za kupunguza umaskini nchini; tatu, kutunga kusimamia na kuratibu utekelezaji wa sera za mipango, uwekezaji na kuboresha mazingira ya biashara na ya nne ni usimamizi wa kongani ya viwanda, makazi na mgawano wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimechukua hayo maeneo, ni maeneo muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo najiuliza ni kwa nini Watanzania tuendelee kuwa maskini. Nchi ya Tanzania ni nchi ambayo tuna kila kitu, nchi ambayo tuna ardhi, tuna madini, tuna milima, tuna bahari, tuna maziwa, tuna kila kitu, kwa nini tuendelee kuwa maskini. Ni nchi ambayo tumebahatika, watu wengi nchi mbalimbali zinaitamani, zinatamani nchi yetu, zinatamani ardhi yetu, zinatamani mali zetu, kwa nini tuendelee sisi kuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Serikali zimechukua hatua kadhaa toka tumepata uhuru, nakumbuka miaka ya nyuma

wakati tumepata uhuru, watu waliamini kwamba tunatokomeza umaskini baada ya Baba wa Taifa kutuambia. Lakini tulikuja na *slogan* moja tukasema "Uhuru na Kazi." Tukapambana, tukaja tena hapa katikati tukasema, tukaja na MKUKUTA Namba 1 na Namba 2, mkakati wa kupunguza umaskini nchini, lakini sasa Serikali ya Awamu ya Sita imekuja na "Kazi na Utu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe kama haya yote tunayaona, nchi yetu tunaweza tusiwe maskini. Kwa nini tunaweza tusiwe maskini, kama nchi ya China tulikuwa tunaizidi kiuchumi *per capita income* kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Muhongo. Nchi ya India ilikuwa nyuma yetu, nchi ya Singapore ilikuwa nyuma yetu na nchi mbalimbali zilikuwa nyuma yetu sisi tulikuwa mbele. Lazima tukae chini tujiulize nini kimetokea wenzetu wamefika mbali sisi bado tunasuasua. Nilisema juzi kwamba 25% ya Watanzania bado wanaishi katika umaskini uliokithiri. Hili siyo suala la kujivunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunategemea Mheshimiwa Profesa na Wizara yako, kama *think tank* ya Taifa letu hili, lazima tutokomeze umaskini na mimi naamini inawezekana, umaskini unawezekana ukaisha. Kama Watanzania wako kwenye kilimo, wako kwenye ufugaji, wako kwenye uvuvi, wako kwenye madini, wako kwenye utalii na maeneo mengine, tunaweza tukatokomeza umaskini na tunatokomeza umaskini kwa kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna wimbi kubwa la watu, kuna wimbi kubwa la vijana hawafanyi kazi, sasa hii ni hatari hatujengi Taifa, hatuwezi kufikia haya maono ya Dira ya mwaka 2050. Kwa hiyo, hili ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo nataka kusema, uwekezaji wetu wa ndani na uwekezaji wetu katika mikoa yetu lazima uende sawasawa. Sasa hivi ukiangalia hata hapa Bungeni, bajeti yetu kwa asilimia kubwa, sisi hapa tunatumia muda mwingi kuchambua, kuchambua matumizi, matumizi, matumizi na bajeti zetu kwa asilimia kubwa zinaenda kwenye matumizi ya kawaida, lakini matumizi ya maendeleo bajeti yake ni

ndogo na sisi tunataka kufikia Dira ya mwaka 2050, hatuwezi kufikia kwa uwekezaji huu mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie halmashauri zinakusanya mapato kiasi gani, nichukulie ya Mheshimiwa Spika ile Ilala inakusanya shilingi ngapi na zile fedha wanaziwekeza kwenye nini ili ziweze kuhakikisha kwamba tunaondokana na umaskini. Halmashauri zetu hizi zinakusanya mapato mengi, taasisi nyingi zinakusanya mapato mengi, zinaondokanaje na umaskini, zinawekeza wapi, lazima tuangalie maeneo ya kuwekeza na vipaumbele ambavyo vitachochea na kuchechemua uchumi wetu ili uweze kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara zetu, sasa hivi sijui tunasema uzalishaji una viwanda, una biashara na huduma za jamii na lazima tujikite hapa. Tunayo mashirika ya umma yako mengi sana na Mheshimiwa Waziri haya mashirika kama walivyosema wenzangu asubuhi, hebu yapunguzeni yote tuache kazi zifanywe na sekta binafsi. Mashirika ya umma yako mengi, uwekezaji wa Serikali kwenye mashirika ya umma ni zaidi ya shilingi trilioni 90. Hebu angalia *return on investment, return of investment is less than 2%,* nime-*calculate*, shilingi trilioni 1.5 maana yake *is less than 2%. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii haina maana, biashara gani unawekeza unapata gawio chini ya asilimia moja, hiyo kwa kweli haijakaa sawa. Kwa hiyo, mashirika yale ambayo hayawezi kujiendesha yaondoe, yabadilishe, uza hisa, yabadilishwe yawe binafsi yakafanye kazi yakazalishe huko, lakini siyo kuyabeba na kuchukua kuweka mzigo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dakika moja, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Kwanza alituambia: "Ili nchi iendelee, tunahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora." Sasa kwa muda wa leo tunaongezea la tano, tunahitaji sayansi, teknolojia na nishati na la sita tunahitaji uzalishaji wa bidhaa na huduma ili zikashindane kwenye soko la dunia na tunahitaji amani, utulivu, umoja na mshikamano ili nchi yetu iweze kupiga hatua na tuondokane na umaskini na mambo yaendelee. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Namwita sasa Mheshimiwa Beng'i Mazana Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo ajiandae.

**MHE. BENG'I M. ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, hii ni mara yangu ya kwanza kuwepo bungeni na kuongea kwa mara ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili namshukuru Mheshimiwa Rais wangu kipenzi Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia mimi kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Chama changu Cha Mapinduzi, Jumuiya ya Wanawake Tanzania chini ya Mwenyekiti wetu mahiri Mama Mary Pius Chatanda ambaye kwa kweli anatulea, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kipekee kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri ambayo anafanya kukuza uchumi wa nchi yetu. Mheshimiwa Rais wetu ni Rais mwenye maono, mbunifu, mzoefu mkubwa kwenye masuala ya maendeleo na vilevile ni mchapakazi, lakini pia napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Profesa Mkumbo na wizara yake nzima ambao wamewasilisha hotuba nzuri sana kuhusu mipango ambayo wanaipanga kwenye wizara yao na kwa kweli wana majukumu makubwa sana katika kusogeza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kuchangia houba ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka wa

fedha 2026/2027. Kwanza kabisa napenda kuanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa nchi yetu Tanzania umekuwa ni uchumi thabiti kwa zaidi ya miaka 10, uchumi umekuwa ukikua kwa takribani miaka 15 vizuri tu. Pamoja na changamoto nyingi za duniani, lakini uchumi wetu bado umekuwa thabiti na uchumi wetu kutokana na tafiti mbalimbali ambazo zimefanyika na Benki ya Dunia miaka ya 2020, ni uchumi jumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba ni uchumi ambao unahusisha wananchi wengi hasa wajasiriamali. Tuna Sera nzuri sana ya wajasiriamali hapa nchini ambapo wananchi wengi wanaweza kuanzisha biashara zao wakati wowote na hawawezi kupingwa na mtu yeyote, lakini vilevile tuna Sera nzuri sana ya Fedha Jumuishi na Uchumi wa Kidigitali ambapo wananchi wengi wameweza kufanya miamala yao ya kifedha kupitia simu za mkononi na hivyo kuwaunganisha kwenye uchumi rasmi wa fedha bila kuwa kwenye sekta rasmi ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna utaratibu mzuri sana wa uwezeshaji wa wanawake kiuchumi pamoja na vijana kitu ambacho kinafanya uchumi wetu uwe ni jumuishi kwa kiasi kikubwa, lakini uchumi wetu kwa kiasi kikubwa pia siyo rasmi. Tuna sekta ambayo siyo rasmi ambayo ni kubwa kwa zaidi ya 60% japokuwa mchango wake kwenye *GDP* ni mkubwa pia, zaidi ya 40%. Pamoja na kwamba siyo sekta rasmi, lakini bado inachangia kwenye *GDP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema uchumi siyo rasmi tuna maana gani, ni pale ambapo tunakuwa na biashara nyingi ambazo hazijasajiliwa na vilevile ukosefu wa mikataba rasmi ya ajira kwa wale ambao wameajiriwa kwenye hizi biashara ndogo ndogo. Kutoripoti kwa mapato ni tatizo kubwa ambalo pia linapunguza kodi ambayo inachangiwa kwenye Serikali, uzalishaji mdogo katika shuguli zetu za uzalishaji na teknolojia duni katika uchumi wetu ambayo inasababisha shughuli za kichumi ziwe na kipato kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kwamba uchumi wetu, shughuli za kiuchumi zinakosa ulinzi wa kijamii kwamba watu wanaweza kufanya kazi lakini hawalipwi pensheni, hawana bima ya afya na wala hawana fidia za kazi kama pale wanapata ajali kazini. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo yanafanya uchumi wetu uwe na changamoto na ni vizuri Wizara hii ikaliangalia suala hili wakati tunafikiria kuboresha sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikienda kwenye sekta binafsi, sekta binafsi ukiangalia katika hii *informal sector* yote niliyoiongelea, ukikutana nao hawa watu, ni asilimia nne tu wana *Tin Number*. Tunapozungumzia kwamba tunataka wachangie uchumi wa nchi, lazima mtu kwa kuanza awe na *Tin Number,* lakini *Tin Number* watu hawafahamu na wala hawana hizo *Tin Number*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo jambo la muhimu katika Wizara hii katika utekelezaji wake wa mwaka ujao wa fedha, nashauri wajikite katika urasimishaji wa shughuli za kiuchumi na biashara za hawa wafanyabiashara wadogo wadogo. Tukiweza kurasimisha hizi biashara itasaidia sana kuwa tunatengeneza sekta binafsi ambayo ni kubwa kwa sababu sasa hivi kwa kweli sekta binafsi ni changa na ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye sekta binafsi ni kwamba Serikali imetengeneza fursa nyingi sana, kuna fursa za mikopo, kuna fursa za manunuzi ya umma, kuna fursa nyingi tu ambazo Serikali inazitoa kwa wajasiriamali na makundi maalum madogo madogo, lakini hawajui wananachi hawa wanazipataje hizi fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa taarifa limekuwa ni tatizo kubwa kwa wao kuweza kuzipata hizi fursa. Kwa hiyo, haya ni maeneo ambayo yanahitajika kuangaliwa kwa karibu ili wananchi wetu waweze kushiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni uchumi wa kidijiti. Tanzania sasa hivi hasa Serikali yetu tumepiga hatua sana kwenye mifumo. Tukizungumzia kupata leseni lazima uingie kwenye *TAUSI*, manunuzi ya umma lazima uingie *NeST,* ukitaka kusajili biashara

lazima uingie *BRELA*, ukitaka taarifa za masoko kuna Mfumo wa *TanTrade*, ukitaka kupata ithibati ya biashara lazima uende kwenye Mfumo wa *TBS*, ukitaka mikopo ya halmashauri lazima uingie kwenye *Wezesha Portal* na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwa wananchi wa kawaida sasa, hawaijui hii mifumo na wala hawajui *internet*, hawajui kabisa. Kwa hiyo kuna haja ya kuangalia, kwa mfano ukikutana na wananchi wa kawaida kabisa hata ukiingia hivi sokoni ukauliza watu wangapi ambao wana simu ambazo zinaweza zikaingiza *internet* yaani simu kubwa, hawana, watu wengi wana simu za viswaswadu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni muhimu sana kama tunataka kupiga hatua tuwajengee uwezo na vilevile tutengeneze uwezeshaji wa wao kuweza kupata simu za mkononi ambazo zitawawezesha kupitia kwenye hii mifumo ili waweze kupata fursa za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni utekelezaji wa Dira ya 2050 ambayo mimi napendekeza utekelezaji huu uangaliwe kwa kupitia hasa Serikali za Mitaa. Serikali za Mitaa ndipo ambapo sisi wote tunaishi, hakuna mtu ambaye hakai kwenye Serikali ya Mtaa. Kwa hiyo, tukipelekea maendeleo yetu kwenye Serikali za Mitaa, tutawafikia wananchi kwa wingi. Tanzania tuliamua kugatua madaraka mwaka 1983 tukasema madaraka ya Serikali Kuu yatakwenda Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo ni muhimu tuwape nafasi, tuwajengee uwezo, tuwape mamlaka na wapewe uwezo wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali ili tulete maendeleo ya kweli kwa wananchi, lakini tukisema kwamba Serikali Kuu bado inaendelea kufanya shughuli zake na kwenda kufanya kazi kwa wananchi moja kwa moja, hatutafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni uwekezaji; kwenye suala la uwekezaji, Wizara hii imetengeneza vituo jumuishi vya uwekezaji ambapo mwekezaji anakwenda pale, anaweza akapatiwa huduma mbalimbali na akaweza kumaliza mchakato

mzima ndani ya dakika chache, lakini tatizo tuliloliona ni kwamba katika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha, *wind up*…

**MHE. BENG'I M. ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani…

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili.

**MHE. BENG'I M. ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unga mkono hoja, *wind up* kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. BENG'I M. ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwita sasa Mheshimiwa Amina Ali Mzee, atafuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mheshimiwa Maryam Ussi Yahya ajiandae.

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nami kwa kunipa nafasi hii jioni hii ya leo. Namshukuru Mwenyezi Mungu nami kupata nafasi hii kuchangia Wizara ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kuhakikisha amefungua uchumi wa nchi yetu katika mipango hii ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji mbalimbali wa Wizara hii. Pia sina budi kushukuru Chama changu Cha Mapinduzi kikiongozwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini jumuiya yangu pendwa ya Umoja wa Vijana na mama yetu mlezi Mama Mary Chatanda, mlezi wa

wana. Tunakishukuru sana chama chetu, Jumuiya ya Umoja wa Vijana pamoja na UWT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza mchango wangu, ninajikita katika uwezeshaji wa vijana kiuchumi na upatikanaji wa ajira. Tunaamini mipango yetu imekwenda kujikita juu ya uwezeshaji wa vijana kiuchumi na ajira. Tunaamini, ndani ya bajeti hii imeeleza kuna maeneo ambayo Wizara imetenga juu ya kuwapa vijana waweze kujenga viwanda. Leo hii maeneo hayo ambayo yangekuwa tayari wameshapewa wawekezaji na vijana wamepata, tungeweza kupata fursa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii pamba inazalishwa hapa nchini, inatolewa nchini inapelekwa nje ya nchi haichakatwi ndani ya nchi. Ingependeza zaidi mazao haya ya pamba yangechakatwa ndani ya nchi, vijana wetu wengi nchini wangeweza kupata ajira na mipango mizuri ya kuweza kuwakwamua vijana wetu na kuweza kuondokana na ajira na kupata ajira zaidi ingeweza kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mipango iweze kuonesha jinsi gani vijana wanaweza kuwezeshwa katika mitaji. Serikali ina mipango mizuri, lakini mitaji ya kuwawezesha vijana bado. Mipango ya Serikali iendelee kuwawezesha vijana kimitaji, lakini pia ubunifu wa vijana. Teknolojia tunaiona inaendelea, lakini mitaji kwa vijana bado. Wizara ya Mipango iende ikaoneshe jinsi gani vijana wa Tanzania wanakwenda kuwezeshwa kimitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia uratibu madhubuti wa Serikali; tunafahamu wawekezaji wengi wanakuja nchini lakini namna gani wanaweza kuwekeza nchini. Wanatumia nchi yetu kuwekeza, lakini namna gani wanaweza ku-*control* kuajiri vijana wengi nchini? Tunaona wanakadiria wanasema wataajiri vijana 3,000 lakini wakati wa *process* zao za kuendelea kuajiri, pengine wanaajiri vijana 1,000; 2,000 hawafikii malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji, itumie nafasi hii kuhakikisha wana mipango mizuri ili vijana wetu waweze kuajiriwa zaidi kupitia Sera ya Uwekezaji na wawekezaji ambao wamekuja nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naendelea kushajihisha, tunahitaji mabilionea wengi vijana na mabilionea hawa hawatokani na kwingine zaidi ya hapa nchini. Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo tuhakikishie vijana mnakwenda kutuwezesha kimitaji, maeneo ya fursa ili vijana wengi wa kitanzania waweze kujiajiri na waweze kuwa mabilionea zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi, naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwita sasa Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, atafuatiwa na Mheshimiwa Maryam Ussi Yahya, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia Mheshimiwa Waziri wa Mipango amepata kukutana na wafanyabiashara kuongea na kupokea kero mbalimbali zinazowasibu wafanyabiashara. Mimi napendekeza, Mheshimiwa Waziri aunde idara ndani ya Wizara yake ambayo itakuwa inalea biashara za ndani. Idara hiyo inakuwa kama *incubation* kwa ajili ya biashara za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo lake ni kwamba tunaona ombwe kwamba ni nani anaweza akawatetea, siyo kule *fair competition*, siyo kule Viwanda na Biashara, lakini tunahitaji idara ambayo itakuwa inapokea *the feelings* na kilio cha wafanyabiashara wa ndani na kuweka ustawi mzuri wa biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yangu ya Bahi kupitia Kata ya Zanka katika eneo la Mayamaya, tumekuwa tunazalisha chuma ambacho kinalisha *cement* zote hapa nchini. Bahati mbaya Serikali imetoa kibali cha kuingiza *copper slag* hapa nchini ambayo hiyo nayo inatumika kutenegeneza *cement*. Ni kiwanda kimoja tu ambacho hakijaanza kuagiza, viwanda vitatu vikubwa vinaagiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili liliwahi kutokeza mwaka 2022 tukaongea Serikali ikazuia sasa tena imeanza kuruhusu *copper slag*. Mheshimiwa Waziri jambo hili ni baya naomba Serikali mlizuie kwa sababu unapoagiza *copper slag* unaua kwanza viwanda vya ndani, lakini hata sisi kwetu unatuathiri kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sambamba na jambo hilo mimi niko Kamati ya Viwanda na Biashara, tumetembelea kiwanda kile kinachozalisha *calcium carbonate* kule Tanga. Jambo hili *calcium carbonate* inayotoka nje ina *zero percent import,* mlilifanya kwa nia njema kwa sababu *calcium carbonate* ilikuwa haipatikani hapa nchini ya kutosha. Sasa tuna viwanda vitano Mheshimiwa Waziri sioni sababu ya kuendelea kuingiza *calcium carbonate* kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye mchango wangu madhubuti kuhusu hii bajeti ya Wizara ya Mipango, lakini na Dira ya 2050, dira hii itaisha mwaka 2050 nchi yetu itakuwa na miaka 89 na dira hii inakuja kutokana na mpango ambao tuliufufua ule wa mwaka 1964 – 1967, lakini pamoja na mambo yote nchi yetu ilikaa muda wa miaka mitano kabla haijaachana na sera ya falsafa ya kibepari ya ukoloni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuliamua kuchukua falsafa ya ujamaa, kwa maana ya kwamba ujamaa ni *socialism*, lakini sisi ujamaa is *made in Tanzania* na tuliiga kwa Wachina na Ulaya ya Mashariki. Tulikoiga sasa ni taifa ambalo linaongoza kwa uchumi karibia duniani na wengine wamesema hapa *GDP* ya China 1965 ilikuwa ndogo kuliko ya kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niseme kwa dhati kutoka moyoni mwangu ni kwamba *either* kwa kutokujua au kwa makusudi tunajaribu kusahaulisha falsafa ya ujamaa na kujitegemea na kwa kufanya hivyo tunatengeneza Taifa ambalo linazalisha bila kujua fikra gani tunayoitumia? Falsafa gani tunayoitumia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na bahati mbaya Serikali kupitia viongozi wake na watu wengine imekuwa haiwezi kutamka

ujamaa na sera yake ile ya kujitegemea, lakini ukienda katika Ibara ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 9 inasema; lengo la Katiba hii ni kuwezesha ujenzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vyombo vyake na udugu na amani kutokana na kufuata siasa ya ujamaa na kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeweza kuyaongelea mambo mengi ambayo tunatakiwa kuyapata kupitia ujamaa, habari ya utu, habari ya usawa wa jamii, habari ya mapambano ya rushwa na mambo mengine mengi yamewezwa kuwekwa humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa watalamu wengi wamechambua nini kilichotufelisha *The Vision 2025,* Profesa Wangwe kupitia kitabu cha Shivji cha Insha ya Mapambano ya Wanyonge wameongea kwamba kilichotokea ni kwamba tunajaribu kuendesha nchi hii bila kuwa na falsafa hasa inayoweza kutufikisha hapa na bahati mbaya kupitia Mheshimiwa Mkumbo kwenye hotuba yako na kwenye dira umeikimbia sana ujamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo mimi naamini ni zao la Chama Cha Mapinduzi na *TANU,* lakini na ni mjamaa, katika hotuba zake nyingi amenukuu habari ya utu, utu, utu katika maeneo mengine na ndiyo ilikuwa tunu kubwa ya ujamaa na mimi naamini tuendelee hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake hapa Bungeni alisema kwamba; „namuomba Mwenyezi Mungu kwa mwisho wa utumishi wa Awamu ya Sita usipimwe tu kwa vitu vitakavyoachwa bali pia kwa tabasamu la utu." Hayo ni maono makubwa katika kujenga ujamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tu ujumbe wa Mheshimiwa Rais wakati anazindua Ilani alisema vilevile kwamba; „Watanzania kwa kuzingatia kauli mbiu yetu, ninaamini kwa pamoja tutaimarisha mafanikio tutakayoyapata kwa kufanya mambo mengi mapya katika kufikia malengo ya kuboresha maisha ya

Watanzania kwa kuzingatia kauli yetu ya Kazi na Utu," bado tunaendelea na habari ya ujamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maneno ya Mheshimiwa Rais wakati wa dibaji hii ya Dira 2050 anaongelea habari kwamba mwisho kwa pamoja tusonge mbele ili kujenga Tanzania kuwa Taifa jumuishi lenye kujali misingi ya utu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka niseme kwa dhati kabisa Serikali kupitia viongozi wetu na Wizara ya Uratibu wa Sekta ibebe habari ya ujamaa kama tunu ambayo tunaweza tukaisemea, tukifanya hivi hapa tulipofika baadhi ya watu wengine wanaweza wasielewe wanaweza wakaona sisi tumeishafuata falsafa ya kibepari au tupo katikati, lakini Katiba yetu imesema hapa ni lazima sote tufuate ujamaa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nollo, kengele ilishagonga muda naomba…

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante sana na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimwite sasa Mheshimiwa Maryam Ussi Yahya, Subira Khamis Mgalu atafuatia, Timida Mpoki Fyandomo ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MARYAM USSI YAHYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. nami nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuongea, lakini pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na rehema kuwepo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangi hii bajeti ya Wizara ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji lakini kwanza kabisa kabla sijachangia nilikuwa naomba nimpongeze Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sera zake thabiti za kuwezesha uwekezaji katika nchi kwa maslahi mapana ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Wizara kwa ujumla kwa bajeti hii iliyosheheni matumaini ya maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla, naomba nimpe pongezi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niipongeze sasa Wizara *especially* katika *TISEZA* kwa sababu kwa muda tangu Julai, 2025 mpaka Machi, 2026 tayari wameshajili miradi 611, haya ni mafanikio makubwa sana na wanafanyakazi nzuri sana hasa ukizingatia upungufu wa fedha. Vilevile nchi yetu sasa hivi iko nafasi ya tatu katika kikanda katika uwekezaji, hilo ni jambo la kujivunia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nawaomba Wabunge wenzangu wote waunge mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo niliyoyasema bado kuna changamoto zinawakabili wafanyabiashara, wengi wetu hapa wamesema kuna Wabunge ambao pia ni wafanyabiashara walieleza pale asubuhi kwa kina mambo ambayo bado wafanyabiashara wanakabilianayo. Changamoto hizi pia zilisemwa katika hii dira yetu nzuri kabisa, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 katika ukurasa wa 48. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya Waziri katika ukurasa wa 30 ilielezea malengo ya Serikali kuondoa vikwazo vinavyokwamisha biashara, lakini Tume ya Mipango ambayo ndiyo ina miradi ya kuwezesha sera, kanuni na sheria za kuwawezesha wafanyabiashara kufanya biashara zao bila vikwazo na bila changamoto iliomba fedha mwaka jana mwaka wa 2024 mwaka wa bajeti wa mwaka 2024/2025 ila walipewa 20% tu ya fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba moyo wa Wizara hii ni Tume ya Mipango na kama ingepatiwa fedha hizo kwa muda muafaka, basi tungekuwa hatuongelei changamoto zote hizi ambazo tunaziongelea hivi sasa. Kwa hiyo, pamoja na kwamba naunga mkono hoja ningeiomba Seriali sasa fedha za

miradi ya maendeleo hasa zile miradi inayolenga kutekeleza kwa mipango ya nchi zitolewe kikamilifu ili tuweze kufikia malengo ya 2050 tuliyokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la uwekezaji nitaongelea kwa kifupi tu eneo la *Special Economic Zone* la Buzwagi ambalo lipo chini ya Halmashauri ya Kahama na linasimamiwa na Halmashauri ya Kahama pamoja na *TISEZA*. Eneo hili mwekezaji mkubwa tayari ameondoka, lakini kuna wawekezaji mbalimbali wa ndani na nje ya nchi ambao sasa wamejitokeza kuwekeza katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeiomba Serikali sasa ihakikishe eneo lile la Buzwagi, wale walioomba kuwekeza wanawekeza katika yale waliosema wanawekeza, tusije kukatokea matumizi mengine ukiondoa ambayo waliyaomba, kwa nini nasema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu bado kuna dhana katika wananchi wa pale kwamba eneo lile bado lina madini na wawekezaji wameomba kuwekeza katika shughuli nyingine mbalimbali *apart* ya madini, ukiondoa shughuli za madini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri, Serikali ihakikishe wawekezaji wale wanafuata sheria na wanafanya shughuli za uwekezaji walizoziomba na kama kuna mabadiliko yoyote basi sheria na kanuni zifuatwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Timida Fyandomo atafuatia, Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo na mimi kuchangia bajeti ya Ofisi hii ya Rais, Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kusimama ndani ya Bunge hili, lakini ikiwa pia mchango wangu wa leo utakuwa ni mchango wa kwanza kwa bajeti hii tangu nimekuwa Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kwa kuniwezesha, nikishukuru chama changu chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniweza kuniteua kuwa mgombea na hatimaye wananchi wa Bagamoyo waliniamini, wakamwamini na yeye na Madiwani wa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia na mimi niungane na Wanawake mbalimbali waliochangia ndani ya Bunge hili kumshukuru Mwenyekiti wetu wa UWT Taifa, Mama Mary Chatanda kwa namna ambavyo alitupa moyo, alitupa uzoefu wa namna ya kuwa mgombea wa Jimbo, lakini namna pia ya kuanza kazi ndani ya Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposimama leo ndani ya Bunge hili nianze kukupongeza sana Waziri, Mheshimiwa Profesa Kitila, Naibu Waziri Dkt. Chaya, lakini pia na Makatibu Wakuu wako ambao ni Dkt. Tausi, Dkt. Msemwa na Wakurugenzi, Mkurugenzi Ndugu Teri pamoja na Msajili wa Hazina Ndugu Mchechu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposimama naomba nijielekeze kwenye sehemu ya hotuba yako ukurasa wa 36 na 37. Ambapo ulielezea namna ufuatiliaji wa maeneo muhimu ya vipaumbele vya Taifa na katika hotuba hiyo umeeleza kwamba katika kufanya utekelezaji wa usimamizi wa miradi hiyo utaongozwa na matokeo ya maabara na moja ya maabara ambayo umeitaja ni Maabara ya Programu ya Mji wa Uwekezaji wa Bahari ya Bagamoyo na Usafiri Fungamanishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasimama hapa nikishukuru Serikali ya Chama Cha Mapinduzi Awamu ya Sita chini ya Jemedari Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha kurejesha Mji wa Bagamoyo, mji wa asili uliokuwa Makao Makuu ya Serikali ya

Kikoloni iliyohusisha nchi ya Tanganyika, Burundi na Rwanda miaka 140 lakini mji ambao karne ya 13 Washiraz walijenga misikiti na kuendeleza Mji wa Kaole. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji ambao misheni ya kwanza ya Afrika Mashariki miaka 158, lakini mji ambao ulikuwa na shughuli mbalimbali za kibiashara za dunia. Leo baada ya miaka zaidi ya 158 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anaurejesha kuwa mji wa ekolojia ya bahari, mji ambao utakuwa na wafungamanishi na usafirishaji, jambo hili kubwa ambalo umelitaja katika hotuba yako hii ambayo inabeba mpango wa maendeleo hupo wa miaka mitano pamoja na Dira ya 2050 ukiwa mradi ambao utatumia takribani shilingi trilioni 24 na sisi tuliusubiri kwa hamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayawi hayawi yamekuwa mradi umeanza, bandari imeanza na wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri ulitutembelea tarehe 30 Desemba ukaja kukabidhi hati za ardhi kwa wawekezaji wa viwanda zaidi ya saba na tumeona wawekezaji wengi wakivutiwa na eneo hilo na hivi karibuni nilimuona Mkurugenzi wa *TISEZA* akimkabidhi hati ya ardhi mwekezaji kutoka China anayekuja kuwekeza zaidi ya shilingi trilioni saba katika eneo letu la viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sisi Wana-Bagamoyo tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunampongeza, tunamuona ni mama shujaa, ni mama aliyethubu wa kuwezesha kuufanya Mji ule kuwakilisha Taifa hili katika uwekezaji mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua itajengwa bandari, utakuwa mji wa viwanda, kutakuwa na kongani ya TEHAMA pale, kutakuwa na mji wa kitalii, lakini nataka nirejee pia Hotuba yako sehemu ukurasa wa 51 kwenye yale mambo matano ulisema; "jambo la nne, dhima ya uongozi wowote hatimaye ni maendeleo ya uchumi na maisha ya watu hivyo kila hatua tunayochukua na kila nadharia tunayofikiria ilenge katika kukuza uchumi na kuboresha maisha ya watu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko hapa kuiomba Serikali kwamba licha ya kazi nzuri iliyoanza na baadhi ya watu mmeishalipa fidia, lakini naomba ili mambo yaende vizuri na kwa kuwa Mheshimiwa Rais alituahidi pia anatamani aache tabasamu, alishalianzisha kwetu Bagamayo na kwa ya Taifa zima, lakini naomba muwakumbuke wananchi wanaoendelea kudai fidia wa maeneo ya Kondo, Mlingotini, Zinga, Kilomo, Pande na Mbegani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hao wamevumilia miaka 16 lakini leo wanatabasamu, ukifika Bagamoyo nambari moja huwezi ukasema maneno matano kabla hujamtaja Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini ni wanaendelea kuwa na subira na kwa sababu Mbunge wao naye anaitwa Subira wameendelea kuwa na subira. Nakuomba Mheshimiwa Waziri ulituahidi kupitia bajeti hii nimeona tutakupitishia shilingi bilioni 18 na mimi naunga mkono moja kwa moja inawezekana sehemu ya fedha hizi ni kuanza kulipa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba tusisubiri fidia ziwe nyingi, sisi tupo tayari kupokea kidogo kidogo ili wananchi hawa waendelee kuulinda mradi, kutoa ushirikiano, kuuombea mradi kama unavyojua sisi Bagamoyo hususan eneo la Mlingotini, eneo la Mbegani kazi yetu mnaijua, lakini tumeendelea kuulinda na kuuombea na ndiyo maana mradi ule umeanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapomalizia mchango wangu najua mpango huu wa miaka mitano unahitaji miaka shilingi trilioni 477; 30% ni kutokana na Taasisi za Kiserikali zaidi ya shilingi trilioni 143. Nashauri ikiwa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji najua unapambania na sekta zingine Serikali ijielekeze kwenye sekta hii ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua mpango uliopo wa ununuzi wa ndege kwa ajili ya kufanya utafiti, kuongeza eneo la utafiti wa madini na hii sekta ya madini inachangaia 10% kwenye pato la Taifa, lakini pia Serikali ijielekeze kwenye sekta ya utalii. Niseme mnapoendelea kutekeleza huu mradi Bagamoyo tuna malikale na hapa nasimama kwa mara ya kwanza kumshukuru

Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuletea shilingi milioni 500 kukarabati Ikulu ya kwanza ya Mjerumani na haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna vivutio pale ambavyo mkiweza kuvihimarisha na kuvitia wawekezaji zaidi ndiyo tutaendelea kupata vyanzo mbalimbali vitakavyo, kujumuisha kwenye 30% ya kuhakikisha mpango huu unafanikiwa. Kwenye masuala ya 70% kwenye sekta binafsi naipongeza Serikali na Wizara yako kwa kuhakikisha sekta binafsi hii inatoa mchango mkubwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan nikikumbuka tarehe 26 Oktoba, 2018 alifanya ziara Bagamoyo na kupewa mpango mkakati wa ujenzi wa bandari hii na leo ametimiza, ahsante sana na Mungu awabariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule ajiandae.

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi nami kuweza kuchangia katika hoja hii muhimu ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Wizara ambayo ndiyo ubongo wa uchumi wa Taifa letu, lakini pili, ndiyo mhimili wa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza ninaomba niipongeze Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi chini ya uongozi mahiri wa jemedari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa inayofanyika ya kusimamia uchumi wa Taifa letu. Tumeshuhudia ukuaji wa 6.4%; mafanikio haya yanatupa matumaini kama Taifa, na mafanikio haya yatakuwa na maana zaidi endapo yatagusa maisha ya vijana moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuzungumzia mipango ya maendeleo ya Taifa bila kuzungumzia mipango ya maendeleo ya vijana. Hatuwezi kuzungumzia mipango ya maendeleo ya Taifa ambayo hayana muunganiko na mipango ya maendeleo ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mipango na Uwekezaji ndiyo inayotoa mwelekeo wa uchumi wa Taifa letu, lakini Wizara ya Maendeleo ya Vijana ndiyo inayosimamia nguvu kazi ya uchumi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kupendekeza kuwe na muunganiko wa moja kwa moja kati ya Wizara hizi mbili, ili kufanikisha mipango ya uwekezaji ambayo itakuwa imepitishwa, basi iende sambamba na mipango mahsusi ya vijana, ajira pamoja na mipango ya uwezeshaji ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia Dira 2050 tunazungumzia uchumi wa dola za Kimarekani trilioni moja, tunazungumzia kipato cha Mtanzania kufikia dola za Kimarekani 7,000. *By 2050* idadi ya Watanzania itakuwa ni Watanzania milioni 130 hadi milioni 140, ambapo idadi ya vijana wenye umri wa miaka 18 hadi 35 itakuwa ni 34.8%. Bila juhudi za makusudi za kuwekeza kwenye vijana Dira 2050 itakuwa ni ndoto nzuri katika makaratasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee vipaumbele vya Wizara ya Mipango na Uwekezaji. Ili kufikia vipaumbele vya Wizara hii, ninaishauri Wizara ya Mipango na Uwekezaji kuwa na mkakati maalum na kuwa na nyenzo ambayo itasaidia kuwekeza kwa vijana, kwa kuwatambua vijana, lakini pia kwa kuhakikisha inawaendeleza vijana, lakini pia kwa kuhakikisha inawapa matokeo vijana hao. Kwa kufanya hivi itasaidia kuwaingiza vijana katika kundi la uzalishaji na ili kukuza biashara za vijana hawa ni muhimu maeneo kama ya kodi na tozo yaweze kuzingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninasoma *paper* moja ya Korea, Wakorea walifanikiwa kuweza kutumia kodi kutengeneza

ajira. Ninaishauri Serikali yangu kuweza kutoa *tax credits* kwa taasisi ambazo zinaajiri vijana. Kwa kufanya hivyo itasaidia idadi ya vijana kuongezeka katika soko la ajira katika ajira, lakini pia itasaidia idadi ya wawekezaji kuongezeka kwa sababu tutakuwa tumewavutia zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332, Jedwali la 2, Aya ya 1(i)*(g)* kinatoa msamaha wa kodi kwa taasisi kama *SACCOS* ambazo mapato yao ni chini ya shilingi milioni 100. Sheria ya *VETA (VETA Act)* Sura ya 82(19)(i) kinatoa msamaha wa kodi kwa taasisi za kidini, lakini pia kinatoa msamaha wa kodi kwa mashirika ya kijamii. *(Makofi)*

Ninaomba kuishauri Serikali yangu kupanua wigo wa msamaha wa kodi kwa kuongeza kundi la vijana, kwa kuwapa msamaha wa kodi wa miaka mitatu ili vijana hawa waweze kukuza biashara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na tafiti za *World Bank* na Benki ya Afira ya Maendeleo, 70% hadi 80% ya vijana wanaoanzisha biashara au ya biashara ndogondogo zinazoanzishwa, zinashindwa kukuzwa kutokana na mazingira ambayo hayawawezeshi wao kuweza kuendelea kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite kuongelea suala la kuwalinda wawekezaji ambao wako ndani ya Taifa letu. Hatuweza kuweka *Import Duty Free* kwa bidhaa ambazo zinakuwa zinaingizwa katika nchi yetu, lakini pia kuna taasisi au kuna viwanada katika nchi yetu vikitumia malighafi yetu, lakini pia vikiajiri vijana wenzetu ambao wanapita kwenye mlolongo wa kodi kama kupitia *TBS*, kupitia *OSHA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara ya Mipango na Uwekezaji kushirikiana na Wizara ya Fedha iweze kuliangalia hili kwa mapana zaidi, ili kusaidia wawekezaji hawa wasiweze kuanguka, lakini pia ili kuwasaidia vijana ambao wameajiriwa na wawekezaji hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niishauri Wizara ya Mipango na Uwekezaji, Wizara ya Mipango na Uwekezaji,

ninashauri suala la uwekezaji lisichukuliwe kama ni suala la dharura. Nchi za wenzetu kama Finland na Singapore kupitia *investment education* na *financial literacy* wanatoa elimu kuanzia kwenye *scratch*, wana-*inject* elimu ya uwekezaji kuanzia watoto wanapokuwa wadogo. Hii inasaidia watoto kukua katika dhana ya kwamba hawatategemea ajira ya kuajiriwa, lakini pia, inawasaidia vijana kuwa na mantiki ya kwamba wanaweza kuwa wawekezaji wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kuzidi kuishauri Wizara kuanzisha mfumo wa kuratibu uwekezaji ambao utasaidia kujua wawekezaji wanahitaji *skills* gani kutoka kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ninaomba niipongeze Wizara ya Mipango na Uwekezaji kwa kazi kubwa inayofanya. Amesema Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake, kumeandaliwa maeneo maalum ya uwekezaji ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Wizara hii, ninaomba maeneo haya na vijana watakaopata nafasi katika maeneo haya ya uwekezaji, basi waweze kuunganishwa na sehemu wanayoweza kupata mitaji, ili isije ikatokea kwamba vijana wana eneo la uwekezaji, lakini hawana mtaji wa kuwekeza. Itafanya maeneo yetu yabaki *idle* kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazidi kushauri Serikali yangu kuangalia namna nzuri ya kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa vijana, lakini pia kuangalia namna nzuri ya kuwasaidia vijana wanaotoka vyuoni kwenda kuingia katika soko la ajira kupitia uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya vijana wa Kitanzania tunaunga mkono hoja bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa sababu ndiyo moyo wa uchumi wa Taifa letu. Sisi tukiwa kama nguvu kazi ya uchumi wa Taifa letu, basi tunaunga mkono hoja kwa 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nimwite sasa Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule na Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi pia ninachukua nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye bajeti yetu hii ya Wizara ya Mipango na Uwekezaji iliyoko chini ya Ofisi ya Rais, lakini kipekee ninachukua nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya hasa chini ya Wizara hii ambayo iko kwenye ofisi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka Bunge lililopita Wabunge tuliongea sana kwa habari ya uboreshaji wa mazingira ya mashirika ya umma, hasa ajira za watendaji na wenyeviti wa bodi, tukiomba kwamba ziwe za ushindani ili tuweze kupata *value* ya vijana wengi ambao wako mitaani wanaoweza kujitoa na kujituma, hatimaye na wao wakaweza kushiriki kwenye ujenzi wa Taifa hili kupitia kwenye taasisi au mashirika yetu haya ya umma. Hatimaye kama tulivyopata taarifa Mheshimiwa Rais aliridhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kipekee ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri pia kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa hapa Bungeni, yeye na msaidizi wake na wote ambao wanahusika katika Wizara yao, lakini zaidi Msajili wetu wa Hazina ambaye amefanya kazi kubwa sana kwenye mashirika haya ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi labda nilikuwa na maoni tu kidogo kwenye kuboresha upande wa viongozi hawa watakaopatikana kwa njia ya ushindani. Ninatamani sana kuwe na *freedom* ya wao kufanya kazi. Ninatarajia baada ya nafasi hizi kutangazwa vijana wengi hawa walioko kwenye mashirika binafsi watajitokeza. Tuna *brains* nyingi sana ziko nje ya nchi na nyingine ziko humu ndani. Watu watakuja kwenye ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba uwekwe utaratibu mzuri wa kuwa-*accommodate* vijana hawa hasa

watakapokuja kwenye mashirika yetu haya wasije wakakatishwa tamaa. Mpango uwepo mzuri pia wa kuweza kutengeneza mazingira mazuri, maana tunajua kuna Ofisi ya Msajili wa Hazina lakini bado kuna Wizara za Kisekta. Sasa viongozi hawa watakapoingia tuwe tumejipanga jinsi ya kuhakikisha kunakuwa na mipaka, Wizara ya Kisekta inashika wapi, ooh Msajili wa Hazina anashika wapi, ili hawa watu wasijekuwa *frustrated*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana nyote ni mashahidi, ninakumbuka kipindi cha nyuma *brain* kubwa kama Msajili wetu wa Hazina leo Bwana Mchechu *last time* hapa alipatapata matatizo kidogo akiwa *NHC*. Ni *brain* kubwa, ikataka kutupwa huko lakini baadaye Mheshimiwa Dkt. Samia akamrudisha, ninaelewa anafanya jambo kubwa mpaka ameweza kuboresha haya mashirika yamefika katika hatua hii. Kwa hiyo, kuna kipindi *shot* zinakuwepo, lakini tuangalie jinsi ya kuziepusha ili *brains* ambazo zipo zinafanya kazi zifanye kazi kwa Taifa hili kwa ajili ya maendeleo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ninaomba nirudi kwenye mchango. Nikirejea kwenye mpango, tunatarajia katika mpango huu wetu wa 2050 sekta binafsi itachangia *almost* 70% ya kile ambacho tunakitarajia. Sasa nilikuwa ninaangalia mchango mkubwa wa sekta hii binafsi nikawa ninajiuliza, tumeiandaa? Sekta binafsi wanajua kwamba wao wanatakiwa wachangie hicho kitu? Kama wanajua tumewapa nafasi gani kwenye kuweza kukua uchumi wa nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ninastaka tulione, tujiandae, tuwa-*engage* na wajue. Kwa sababu *sometimes* Serikali tunapanga mipango yetu lakini sisi siyo wawekezaji. Wale wanaotakiwa kuwekeza wanawaza kwenda Kenya, wanawaza kwenda maeneo mengine halafu *by the time* unakuja kushtuka mtu alishawekeza sehemu nyingine. Kwa sababu mwekezaji yeye anaangalia anapoenda kupata faida. Kwa hiyo, tuone na kuwatengenezea mazingira mazuri ya kuweza kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninayasema haya? Kumekuwepo na tabia nyingine kodi zinakuwa nyingi sana, lakini licha ya kodi *sometimes* hata *incentives* za watu wanao-*import*

kutoka nje zinakuwa nyingi sana. Bahati nzuri umekuwa Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Viwanda na Biashara kipindi kilichopita. Tumeenda maeneo mengi ulikuwa unakuta wawekezaji hata wa ndani wanalalamika. Unakuta kodi mtu amewekeza hapa, lakini anaye-*import sometimes* anakuwa na *duty free*, aliyeko hapa ulingano wa kikodi haulingani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote mnajua nchi nyingine zinafanya hata *export incentive* kwa watu wanaoweza kufanya *export* kwenda nje, kutoka kwenye nchi zao kwenda sehemu nyingine. Kwa hiyo, inakuwa ngumu mtu anayezalisha hapa kwa gharama za hapa kuweza kuwa mshindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kama Taifa tujikite kwenye vitu viwili vikubwa; *issue* ya umeme ameongea sana Profesa hapa asubuhi. Hatuwezi kuwa nchi inayotaka kwenda kwenye ushindani wa viwanda na mapinduzi makubwa kama hatuna uhakika wa umeme. Hizi megawati 4,000 tulizonazo ni ndogo. Ukitaka kuzalisha chuma tu, *process* ya kuzalisha *copper*, waya zile kwa ajili ya kuzalisha umeme, mashine moja ya *smelting* unakuta inaenda mpaka megawati 50. Moja! Sasa ukiwa na viwanda vinne vitano hapo unaweza ukajiuliza ni megawati kiasi gani zitahitajika. Kwa hiyo, lazima tulione hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwenye kuliona hili si kila kitu lazima ifanye Serikali. Kwa sababu umeme ni biashara, watu wazalishe waiuzie *TANESCO* turuhusu biashara huria mtu azalishe, ni sawa na tunavyozalisha Mwalimu Nyerere kule. Anajulikana anaingiza *unit* ngapi waweze kuuza umeme. Wamiliki wao na waweze kuuza wawe wanalipwa kwa sababu umeme ni biashara itatusaidia. Nenda kwenye barabara, si kila wakati lazima Serikali iwekeze huko. Tutafute watu wajenge barabara nzuri, watu wapite kwa kulipia ili uchumi wa nchi hii uweze kwenda. Kwa sababu Serikali hii hii ilipe mishahara, Serikali hii inunue madawa. Tutalaumiana bure hapa na vitu havitawezekana. Kwa sababu lazima ukusanye ili uweze kurudisha kule kwa wananchi. Kwa hiyo, ninaliomba hilo tuweze kuliona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na mambo mazuri yote ambayo tunayatarajia kutoka kwa wawekezaji hawa

wakubwa, kumekuwa na shida kubwa sana, sana, sana kwa wawekezaji wa ndani, hasa wakandarasi. Nyote mnaelewa, wakandarasi nchi hii wanaibeba kwa sehemu kubwa sana, lakini malipo yao yamekuwa yanachelewa kwa kiasi kikubwa. Ucheleweshaji wa malipo haya yanaathiri hata watu wengine wanaotaka kuja kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mtu anapotaka kuja kuwekeza anamuuliza mwenzake kwanza. Pamoja na kwamba Serikali imeenda kupitia Wizara zetu, kupitia Balozi imesema, lakini anayekuja kuwekeza *sometimes* wana-*communicate* wao kwa wao, amuelezee mazingira yakoje. Hata riba katika benki malipo ya wakandarasi yanachelewa, wanafilisiwa. Wakishafilisiwa ajira zinapungua, hata kulipa kodi kwenyewe kunapungua. Kwa hiyo, kila kitu lazima kiende pamoja ili tuweze kwenda sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata riba wakandarasi wa ndani wanakopeshwa kwa riba kubwa mno. Kwa hiyo, ninaomba Wizara ya Mipango na Uwekezaji wakae na *BOT* na wakae na benki wajaribu kuona. *These people are working tirelessly* kwa ajili ya kuijenga nchi hii. Malipo yao yanachelewa, lakini hakuna anayeenda kuomba riba hakuna anayeenda Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusiangalie benki za ndani zinazofadhili wakandarasi zikajaribu kuwasaidia hata kwa kushusha riba. *BOT* ihusike kwa sababu huyu mtu anapotoa pesa benki ikakwama isirudishwe maana yake benki inaathirika, yeye mwenyewe anaathirika, Serikali inaathirika kwa sababu haitakusanya kodi na mapato mengine ambayo yanatoka kwa hao watu. Kwa hiyo, tuone, ili kuweza kukuza mzunguko riba ishuke na Serikali ijitahidi. Hata pale kunapokuwa na madeni ya wakandarasi wa ndani iende ikope, kwa sababu ikishawalipa ile pesa inarudi kwenye mzunguko. Ikirudi kwenye mzunguko wanalipa kodi inakusanya tena, kuliko kuweza kuwakwamisha hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nililiona hilo nikasema niliseme ili tuone jinsi ya kusaidia kwa sehemu kubwa mambo

haya ambayo kidogo yamekuwa yanakwamisha wenzetu wasisonge mbele, yaweze kwenda mbele vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kumalizia, Mheshimiwa Rais alipoingia tulipitisha hapa sheria ya kwamba sasa hivi wakandarasi wa ndani hasa wanaofanya ujenzi waruhusiwe kupewa miradi inayoanzia shilingi bilioni 50 kushuka chini. Tunaomba hili jambo lisimamiwe. *Sometimes* unakuta mradi mmoja wa shilingi bilioni 200, kwa nini usifanye loti nne wakandarasi wa Kitanzania wakapata kazi hata loti nne kila mmoja akashika moja moja ili iweze kusaida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kuona kampuni zinatoka Uganda zinajenga barabara DRC, zinajenga barabara nchi nyingine, sisi wakandarasi wa Kitanzania hata kwao tu barabara ya shilingi bilioni 50 hawawezi kujenga. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niliona hilo. Ninakushukuru sana kwa nafasi, ahsante sana; ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa. Nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule akifuatiwa na Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma, Mheshimiwa Naibu Waziri ajiandae.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi ya kuchangia tena kwenye Bunge lako Tukufu. Nianze na mimi kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa nafasi hii, lakini pia moja kwa moja na mimi ninamshukuru sana Mheshimwia Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa nchi yetu, kwa kazi kubwa sana anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasimama kwa ujasiri kuweza kuongea mambo ya maendeleo, kwa maana tayari kuna maendeleo makubwa sana yamekwishafanyika. Ni miaka michache tu nyuma tusingeweza kusema mambo haya. Tuna ujasiri kwa sababu tayari tumeendelea sana kiuchumi. Hivyo,

ninampongeza sana Rais wangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia pongezi za pili ziende kwenye Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji kwa kazi kubwa waliyoifanya kutuletea mpango huu ambao kweli utatubeba kwa mwaka huu, lakini ni sehemu tu ya dira yetu ya miaka 25, kuanzia mwaka 2025 hadi 2050. Hiki ni kipande tu ambacho tunaenda kukifanya lakini kweli tunaona kabisa matumaini makubwa, kwamba tunaianza vizuri dira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Profesa Kitila, ninampongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Chaya, ninawapongewa pia wataalamu wote ambao wamekaa na kuweza kutoka na mpango huu. Mpango huu una matumaini makubwa. Moja kwa moja ninaunga mkono hoja kabla sijaanza kutoa mawazo yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninasema kwamba mpango ni mzuri, lakini kuna mambo ambayo inabidi tusisitize au mambo ambayo inabidi tuyaangalie kwa tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kabisa ni mambo ya kilimo. Hata kama tutataka kufanya maendeleo makubwa sana, tujikite zaidi kwenye mipango ya kutekeleza ya kilimo kwa maana ndiyo inayoajiri Watanzania wengi zaidi, 85% ya Watanzania wameajiriwa na kilimo. Hivyo, tukipeleka *resources* nyingi kwenye kilimo tunaenda kufanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni viwanda; viwanda hivi ni vile vidogovidogo na vya kati ambavyo pia vinachukua sehemu kubwa ya Watanzania. Pia itatoa ajira nyingi zaidi kwa vijana na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kupunguza tozo ambazo siyo rasmi kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo wakiwepo wajasiriamali, ambao ndiyo pia imebeba kundi hili kubwa la wanawake na vijana. Tukifanya marekebisho hayo au tukisisitiza marekebisho hayo ninafikiri tunaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine la nne ni mafunzo ya amali, vijana wetu waweze kujifunza mafunzo haya ili wabadilishe *mindset* ya kutegemea ajira ili waweze kujiajiri wenyewe. Vijana wakianza kujiajiri wenyewe wataweza kufanya vizuri kuchangia pato letu la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine la nne ni mafunzo ya amali, vijana wetu waweze kujifunza mafunzo haya ili wabadilishe *mindset* ya kutegemea ajira ili waweze kujiajiri wenyewe. Vijana wakiweza kujiajiri wenyewe wataweza kufanya vizuri kuchangia pato letu la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mambo ya mikopo hiyo ambayo tumekuwa tukiisema mara nyingi hapa Bungeni, sasa tutoke na mfuko wa dhamana ambao utakaa kwenye mabenki yetu ili vijana, wanawake na makundi maalum waweze kupata mikopo. Tukifanya mambo haya kwa pamoja hapo ndipo sasa tunaenda kupambana na umaskini, lakini mimi niseme tu ya kwamba naunga mkono sana jitihada za nchi yangu kuwatunza wawekezaji wa nje na wawekezaji wa ndani kwa kuwatia moyo wawekezaji wa ndani sasa hivi wameanza kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nasema kwamba hatuna umaskini mkubwa kiasi hicho Tanzania, nikizunguka nchi za Kiafrika nakuta nchi ambazo ni maskini hata mlo ni shida, sisi tuna vyakula vya kutosha sisi ni maskini kwa vipi? Lakini pia tuna madini sisi ni maskini kwa vipi, tuna ardhi ya kutosha sisi ni maskini kwa nini? Lakini tuna misitu, tuna maziwa ikiwepo Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, tuna bahari sisi ni maskini kwa vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kazi kubwa iliyopo ni kubadilisha *mindset* ya Watanzania, sisi sio maskini, tufanye kazi kwa bidi, tunaenda kukuza uchumi wetu, tunaenda kutoka. Rais wetu amefanya kazi kubwa kuleta maendeleo makubwa kwa miradi ya kijamii, sasa ni kazi ya Mtanzania mmoja mmoja mwenyewe kufanya kazi kwa bidi, kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho tu niseme ya kwamba Wizara ya Mipango na Maendeleo hatuwezi kwenda na mambo

ya uchumi tukimweka mwanamke nyuma. Mwanamke awe sehemu ya hii mipango na maendeleo, sauti ya mwanamke katika uchumi, mchango wake katika maendeleo tukiisikiliza tunaenda, kwanza ndio waliojikita zaidi kwenye Uchumi. Ajira ya wanawake kwenye mambo ya kilimo ni 85% lakini tukiwachukua wanawake tukawashirikisha vizuri kuanzia kwenye kupanga, kutekeleza na kutathimini nchi yetu inaenda kuvuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini imefikia hatua hatutaongea umaskini tukija kwenye Bunge lako tukufu, tutaongea jinsi ya kutengeneza mamilionea na mabilionea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Nimwite sasa Josephine Joseph Kapoma, atafuatiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Johari na atafuatiwa na Naibu Waziri Dkt. Pius Chaya, Mtoa Hoja ajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nashukuru kwa kupata nafasi hii tena kusimama katika hili Bunge Tukufu kuchangia katika Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji ambayo kwa sasa ndio *talk of the town* na kwa nini ni *talk of the town*, kwa sababu mageuzi na mapinduzi ya kiuchumi ndio atakayoenda kutatua kero ya maji, yatakayoenda kutatua kero za barabara, kero za madawati, kero za shule na kero zote kadhalika wakadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa naomba kujikita kwenye Dira ya 2050. Natamani sana Dira ya 2050 isibaki kwenye makaratasi na natamani sana kaka yangu Profesa Kitila Mkumbo asibaki kuitwa mzee wa MKUMBI I, MKUMBI II, MKUMBI III kwa sababu tunaenda kuitekeleza hii Dira ya 2050 kwa mapana sana. Naona sasa ni wakati ambao Serikali inatakiwa impe nguvu ya ziada *TISEZA*, wachangiaji ambao wamepita wameonesha kabisa ni kiasi gani *TISEZA* imekuja na mapinduzi ya kiuchumi. Mwezi uliopita Dkt. Profesa Kitila, alikuwa na ziara mkoani Morogoro na alifanikiwa kutembelea viwanda vya sukari na mashamba ya

miwa. Tumeona uwekezaji mkubwa ambao unaendelea Morogoro na mafanikio haya kwa ukubwa wake yamefanywa na *TISEZA,* lakini sasa katika hilo hilo, uwekezaji huu ambao umefanywa mkoani Morogoro katika viwanda vya sukari na mashamba ya miwa umefanywa katika maeneo ambayo ni mapya kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoani Morogoro tuna viwanda ambavyo vipo *idle* na maeneo ambayo yako *idle* kwa muda mrefu sana. Sasa nataka kujiuliza kama haya maeneo yapo *idle* kwa muda mrefu na maeneo ambayo yako mjini miundombinu ipo, maji yapo, umeme upo, barabara zipo, ni kwa nini sasa haya maeneo yasipewe kipaumbele? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kama inawezekana *TISEZA* sasa atusaidie katika hili kwa sababu ameshatusaidia sehemu nyingi na hili najua haliwezi kumshinda. Pia kwa hivi viwanda na maeneo ambayo yako *idle* nadhani sasa ifike sehemu Serikali turudi tuangalie *commitment* ambazo tuliingia na hawa watu kabla hatujabinafsisha haya maeneo. Tukae na hao watu, kama haya maeneo wameshindwa kuyaendeleza, haya maeneo ya wazi na hivi viwanda ambavyo viko *idle* kwa muda mrefu ni nini sasa kifanyike, kama wameshindwa kuviendeleza basi tuwape watu ambao wana-*passion* na *commitment* ya kuendeleza hivi viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ninachokifahamu kitu chochote kinachofanya hata hivi viwanda mara nyingi watu wanavyotaka kufanya kitu hiki kitu lazima uwe na *passion* na *commitment,* lakini inaonekana *some point* watu ambao walivichukua haya maeneo hawakuwa na huo utayari na hicho ambacho ndio kimepelekea maeneo mengi ambayo yako *idle*, viwanda viko vingi ambavyo vipo *idle,* watu wamevitumia kama *collateral*, kuchukua mikopo na kupeleka hizi pesa sehemu zingine na hizo sehemu ambazo wamepeleka hizi pesa halikuwa lengo la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali lilikuwa viwanda hivi vifanye kazi, watu wapate ajira, uchumi ukue, lakini viwanda hivi na maeneo haya yamefanyiwa kama *collateral,* watu

wamechukua pesa wameenda kuwekeza sehemu nyingine ambayo tija kwa wananchi ni ndogo.

Sasa kama wameshindwa basi Serikali iingilie kati, tuvichukue tuwape watu ambao wanautayari. Wachangiaji waliotangulia wamesema kuna vijana wanashindwa sehemu za kuwekeza. Sehemu za mjini zote zimechukuliwa na watu na wamekaa hawazifanyii, inatokea kijana anatakiwa ukija Morogoro pale kijana anataka kuwekeza anatakiwa kwenda Malinyi. Kumbuka ukimpeleka Malinyi, ni maana yake sasa tunatakiwa miundombinu ya barabara, tunatakiwa miundombinu ya umeme na nini, wakati pale mjini miundombinu ipo tayari, kwa nini tusiwaweke mjini kupunguza gharama ambazo sio za lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nilikuwa nataka kuongezea kwa kusema, ni wakati sasa Serikali tuone ni jinsi gani tunaenda ku-*invest* teknolojia rahisi na nzuri kwa viwanda hivi ambavyo vimelala. Viwanda hivi ambavyo vimelala, hata kama ikitokea wakachukua wawekezaji wengine, nadhani sasa ni wakati wawekezaji hawa wakaja na mkakati wa kutuonesha ni teknolojia gani wanaenda kutumia. Kwa sababu shida ambayo ipo, viwanda hivi vinaweza vikachukuliwa lakini teknolojia ambayo itaenda kutumika haitakidhi mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafikia kwamba mwisho wa siku viwanda hivi vitafungwa tena na havitafanya kazi. Sasa tunavyokwenda kubinafsisha kwa watu wengine, watu hawa wanatakiwa waje na mpango ambao utatuonesha ni teknolojia gani wanaenda kuitumia, *industrial financing* gani wanaenda kuitumia, ubora na ubunifu gani wanaenda kuutumia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikielezea suala la ubunifu na ubora; leo hii tutafungua kiwanda cha kutengeneza *yeboyebo; yeboyebo* itakayotengenezwa hawa watu wakipeleka sokoni kwa kuuza shilingi 30,000 hatutapata wateja kwa sababu kuna *yeboyebo* Mchina anayoitengeneza yenye ubora na ni nzuri anayoiuza shilingi 2,000. Sasa mimi leo nikachukua kiwanda nikatengeneza *yeboyebo* nitakayoiuza shilingi 30,000 siwezi kupata mteja, kwa sababu kuna *yeboyebo* ya Kichina ya *pink*, ya

*blue*, ya manjano, vaa umependeza inayouzwa kwa shilingi 2,000. Kwa hiyo watu ambao tutawapa hivi viwanda watupe mkakati wa teknolojia gani watatumia, ubora na ubunifu gani na bei gani wataipeleka sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa ambao wana *commitment* na *passion* ya kwenda kufanya hizi kazi nadhani ni wakati sasa wa Serikali kuangalia ni vipi tunaenda kuwa-*finance*. Nchi ambazo zimeendelea India na China katika …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umeisha.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie.

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vitu ambavyo wamefanikiwa ni kuwa-*support* watu hawa kwenye suala la *industrial financing* ambalo tutawapa katika *payment terms* ambazo ni za muda mrefu kuanzia miaka 30 na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine nitayawasilisha mezani, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Nilimwita Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Saidi Johari, atafuatiwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya.

**MWANASHERIA MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Bunge lako Tukufu, lakini nimshukuru kwa dhati Mheshimiwa Edward Olelekaita, wakati anachangia alitoa ushauri kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu uhitaji wa kufanya marekebisho ya kifungu cha 11 cha Sheria ya Mamlaka ya Nchi katika Umiliki wa

Mali na Rasilimali Asilia, tunaita *The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty Act* Sura ya 449 kwa kuondoa sharti linaloelekeza mashauri yanayotokana na uwekezaji katika rasilimali asilia kushughulikiwa nchini pekee.

Nikushukuru sana kwa ushauri wako mzuri tumeupokea na *feedback* hii hatujaipata tu kutoka kwa Mheshimiwa Edward Olelekaita, bali imekuwa ni *feedback* ambayo tumekuwa tukiipata mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria, tulishaanza zoezi la kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali sio hii tu, lakini na zile zingine zote ambazo tunaziona tunazihitaji kuzishabihisha na Dira ya 2050. Kama wote mnavyokumbuka kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alimwelekeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha kwamba baada ya dira ile kuizindua na sasa tumeshaanza utekelezaji wake tunashabihisha sheria zote ziendane na Dira ya 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninaamini kabisa kwamba sheria hii Mheshimiwa Olelekaita ni miongoni mwa sheria ambazo tunahitaji kuhakikisha kwamba tunazishabihisha ili zinyumbulike vizuri na Dira ya 2050 ili zikawe daraja za kutufikisha kwenye malengo hayo ya 2050. Kwa hiyo, kazi hiyo imeshaanza, tafiti zinafanyika ikiwemo na sheria hii uliyoitaja. Kwa hiyo, nikutoe hofu Serikali inalifanyia kazi hili kwa umakini mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia alitaka ili kuweka nidhamu katika utekelezaji wa Dira ya 2050 alipendekeza kwamba Kanuni za Kudumu za Bunge zirekebishwe ili kuweka utaratibu wa upokeaji wa taarifa ya utekelezaji wa dira.

Kwanza niseme tu kwamba mamlaka ya kutunga au kurekebisha Kanuni za Kudumu za Bunge yako ndani ya Bunge na inaweza kufanya hivyo wakati wowote itakapohitaji kufanya hivyo, lakini nitoe tu angalizo kwamba bahati nzuri Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ile ya 63(3) inalipa Bunge hili mamlaka ya kumtaka Waziri au Serikali kuleta taarifa

yoyote au jambo lolote ambalo litahitaji kupata taarifa kama Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa sababu iko huku kwenye Katiba tusiishushe huku chini kwenye kwenye kanuni, tuache misingi ile ambayo imewekwa kwenye Katiba ili Bunge li-*exercise* mamlaka yake ya Bunge ndani ya Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Mheshimiwa Olelekaita, tunakushukuru na kama nilivyosema maoni yako tumeyapokea juu ya sheria ile na tutayafanyia marekebisho pamoja na sheria zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kuunga mkono hii hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Nimwite sasa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba kuchukua nafasi hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini kipekee nimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwenye Taifa letu, lakini kwa imani kubwa ambayo alinipatia mimi pamoja na Waziri wangu Profesa Kitila Mkumbo, kuwa sehemu ya ofisi yake kumsaidia majukumu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nimshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, lakini Waziri Mkuu wetu ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya na tumeshuhudia, mimi nimefanya ziara na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha. Kwa kweli nguvu aliyonayo Waziri Mkuu nilishangaa, kuna muda tulikuwa tunafika mpaka saa mbili usiku unakuta yeye anaendelea kufanya kazi. Nilikuwa na Profesa Shemdoe, Profesa wangu wa Chuo Kikuu cha *SUA* alikuwa anachoka, lakini Waziri Mkuu alikuwa hachoki. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nimpongeze sana Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo anaifanya lakini kama bosi wetu anatusimamia vizuri anatupa maelekezo vizuri, sisi tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nimshukuru vilevile Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika kwa miongozo yao mbalimbali wanatupatia ofisi yetu, mimi na Waziri wangu katika kutimiza haya majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii vilevile niipongeze kamati yetu, Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, ikiongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, lakini vile vile Makamu Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Edwin Swalle, kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya katika kuisimamia Wizara yetu, lakini katika kuishauri lakini vilevile kutoa miongozo mbalimbali ambayo kimsingi imetusaidia sisi katika kutekeleza majukumu haya ambayo tumekabidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii nimshukuru Waziri wangu, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, kaka yangu, kwanza kwa kunilea, lakini pili kwa kuni-*guide* na kunihakikisha kwamba nakuwa salama na ninafanya kazi zangu vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajisikia faraja kufanya kazi na Profesa Kitila Mkumbo, nafanya naye kazi kama kaka yangu, lakini kama ndugu yangu na kimsingi amenijenga sana, ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru Makatibu wetu Wakuu wawili; tunaye Dkt. Kida, ambaye kimsingi yeye ana-*double roles*, ni Katibu Mkuu upande wa Mipango, lakini vile vile anasimamia Tume yetu ya Mipango, lakini Dkt. Msemwa ambaye Katibu Mkuu ameteuliwa na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kusimamia suala la uwekezaji. Hawa watu wanatusaidia sana sisi kama wataalamu wetu na tunapowashauri kimsingi wamekuwa wepesi sana kupokea ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwashukuru na kuwapongeza wakuu wote wa taasisi zetu, akiwepo Msajili wa

Hazina, lakini *DG* wa *TISEZA* kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Umesikia wewe hapa leo, Waheshimiwa Wabunge wamewapongeza sana hawa wakuu wa taasisi kwa kazi kubwa na *transformation* kubwa ambayo wameifanya kuhakikisha kwamba hili lengo la Mheshimiwa Rais la kuhakikisha tunafikia trilioni moja ifikapo 2050 lakini tunakuwa na pato la mtu mmoja mmoja dola 7,000 ifikapo 2050 nadhani wanalifanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na mwisho, niishukuru Menejimenti ya Wizara yetu, kimsingi wanatupa ushirikiano mkubwa sana na wamefanya kazi kubwa sana: haya makofi haya yanayotokea hapa ni kwa sababu wao wamefanya kazi kubwa sana na wamekesha kuhakikisha kwamba mimi na Mheshimiwa Waziri tuna-*deliver* hiki kitu ambacho tume-*deliver*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamalizia nichukue nafasi hii kuwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Manyoni, nilikuwa sijapata nafasi ya kuchangia hapa tangu Mheshimiwa Rais, ameniteua kuwa Naibu Waziri katika ofisi yake. Kwa kweli niwashukuru sana kwa imani waliyonipatia, nimekuwa Mbunge kwa awamu ya kwanza na wameniongeza awamu ya pili. Ninawaahidi nitafanya kazi kwa juhudi zote kuhakikisha kwamba Jimbo letu la Manyoni linapata maendeleo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea michango mingi kutoka kwa Wabunge, nitayagusia maeneo machache kabisa na kimsingi mimi niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmechangia takribani Wabunge 20 wamechangia katika bajeti yetu hii na kuna maeneo matano nitachangia kwa kifupi kabisa, ninajua Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, atakuja kumalizia maeneo ambayo kimsingi sitayagusia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza, tumepata mchango kuhusu namna ya kupima hali na ukuaji wa uchumi wetu na ni eneo ambalo ni *very sensitive* lakini ni *very technical,* Mheshimiwa Profesa Muhongo, amelieleza kwa kina kabisa kwamba tusiangalie tu zile *monetary measures* za kupima ukuaji wa uchumi, tuangalie kwenye zile *measures* nyingine ambazo siyo

*monetary* zile *non-monetary*. Kwa mfano, mambo ya afya, mambo ya elimu na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mchangiaji mmoja aliongelea kuhusu *mushrooming* ya *informal sector* ambapo tunapo pima uchumi wakati fulani tuna-*ignore informal sector,* tuangalie ni jinsi gani tunaweza ku-*factor in* suala la *informal sector* hasa tunapopima suala la umaskini.

Kwa hiyo, ninaomba niwaahidi Waheshimiwa Wabunge hilo sisi tumelichukua na sisi pamoja na wataalam wetu tutaenda kulifanyia kazi ili tuje na mfumo rafiki ambao utahakikisha sasa tunatoa *measurements* ambazo kimsingi zitakuwa *very realistic* na zitatusaidia kujua hali yetu ya ukuaji wa uchumi ili tuweze kupanga mipango yetu ambayo itaenda kutusaidia kwa ajili ya kusogea na kufikia hiyo azma ya Dira 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nalo wamechangia Waheshimiwa Wabunge ni suala la ufuatiliaji wa hali ya umaskini. Ni kweli kwamba tuna afua nyingi sana za kupunguza umaskini ambazo zinafanyika, lakini kumekuwa na *concern* kwamba inaoneakana kama *pace* ya kupunguza umaskini siyo *significant,* kuna wasiwasi kwamba inawezekana hizi afua kuna tatizo aidha kwenye upangaji wa hizi afua au hizi afua hazina *convergence* ambayo inasababisha kwamba zinakuwa na mtawanyiko tunashindwa kufikia ila azma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamechangia hili hata kwenye Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala ninamkumbuka Mheshimiwa Hasunga amekuwa akipigia kelele sana suala hili. Ninaomba niwaahidi Waheshimiwa Wabunge tunakuja kuandaa kitu kinaitwa *poverty monitoring framework* ngazi ya Wizara ambayo kimsingi itakuja kutusaidia sisi sasa kuja kupima hali ya umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine mmechangia mkasema tusiangalie tu hali ya umaskini  ya kipato tuangalie hata zile *non-income measures* kwa kutumia ile *multidimensional poverty analysis.* Ninaomba niwaahidi tumelichukua na sisi tutaenda kushirikiana na taasisi za utafiti wakiwepo *ESRF,* vyuo vya utafiti

kuna *REPOA*, *UN Agency, World Bank* wamefanya sana kwenye maeneo haya ili tuje na taarifa sasa za ni jinsi gani hizi afua tulizonazo kimsingi zinasaidia katika kupunguza umaskini na itatusaidia kuweza kupanga upya taarifa zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, ni eneo la MKUMBI; Mheshimiwa Olelekaita ameeleza hapa alikuwa na hofu anasema mbona inaonekana ile *Blueprint I* kama haijafanya kazi yoyote ninaomba nikuambie Mheshimiwa Olelekaita na Waheshimiwa Wabunge tangu *Blueprint I* imeanzishwa kuna mafanikio makubwa sana yamefanyika, ingawa bado kuna changamoto zipo na tunapokea malalamiko mengi. Nitatolea mfano tu, kwa mfano, kuanzia mwaka 2019 hadi 2025 kulikuwa kuna marekebisho ya sheria 94 na ninajua Mheshimiwa Olelekaita, wewe ni Mwanasheria na ni msomaji mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo tuliweza kufuta kodi, tozo na faini 628 ambazo kimsingi zilikuwa vikwazo sana kwa biashara. Kwa hiyo, ukipitia hii unaona kabisa kwamba bado vilevile kulikuwa na mafaniko ya utekelezaji wa ile *Blueprint I,* lakini kuna marekebisho mbalimbali ya sheria yaliyofanyika kwa mfano Sheria ya *VAT,* lakini suala la kodi ya mapato, usimamizi wa kodi, Sheria ya Madini, Sheria ya *EPZA* hizo sheria zote zilifanyika na hiyo ilikuwa ni mojawapo ya ile *MKUMBI I.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme kwamba hata kama tunapokuja kwenye huu *MKUMBI II,* bado lazima tuseme zile *success stories* ambazo zilitokea kwenye *MKUMBI I,* na ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa kupitia *MKUMBI II,* chini ya *guidance* ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mambo makubwa yanaenda kufanyika kuhakikisha kwamba mazingira ya biashara na uwekezaji yanaenda kuwa mazuri kabisa ili tuwahakikishie ufanyaji biashara na uwekezaji Tanzania unakuwa ni mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, suala la mchango wa sekta binafsi. Katika Dira ya 2050 tumeipa sekta binafsi 70% ichangie kwenye pato la Taifa. kwa tafsiri nyingine sekta binafsi inatakiwa ichangie 70% ya ajira zote zitakazozalishwa, 30% ya ajira zitazalishwa na sekta ya umma lazima tujipange. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tumejipanga, kuna vitu vinne, vitano tunakuja kuvifanya; ya kwanza, tunakuja kutengeneza kitu kinaitwa *Private Sector Development Policy, Act* na *Strategy*. Hivi vitu tulikuwa hatuna, tunataka kuhakikisha kwamba sasa sekta binafsi ilete mageuzi kwenye uchumi, ili ilete maegeuzi ni lazima tutengeneze sera yake inayojitegemea, lazima tuitengenezee sheria inayojitegemea, lazima tuitengenezee mkakati ambayo zitatu-*guide* sisi kuhakikisha kwamba tunafikia hiyo, na hilo litaenda sanjari na ku-*formalize informal sector* ambayo kimsingi tunapoteza mapato mengi sana kwa sababu ya *black market* hawapo hawatambuliki na ni wengi. Kwa hiyo, kwa kupitia hilo nina uhakika tunaenda kuleta mabadiliko makubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, suala la vijana na uwekezaji; mimi niwapongeze sana Wabunge wanaowakilisha vijana kwa michango yao ambayo wamekuwa wakiitoa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tuna-*link* vijana na wawekezaji na sisi kama Serikali mwaka huu kwanza tuna programu maalum ya uwekezaji kwa vijana na mliona Mheshimiwa Waziri alizindua hiyo programu pale Dar es Salaam, lakini tumetenga maeneo maalum ya uwekezaji ambako tutakuwa na wawekezaji wakubwa, lakini mule mule ndani tunawaweka vijana kwa ajili ya kuwajengea uwezo, lakini kuhakikisha kwamba wanashirikiana na wawekezaji wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Wabunge wameshauri kwa nini tusitoe *tax credit* kwa makampuni ya wawekezaji tukiwa na mkataba kwamba tunapowapa *tax credit or any kind of incentive* ili nao waongeze jinsi gani wataweza kuongeza ajira kwa vijana. Hili wazo ni nzuri, ninaomba niseme tumelipokea, sisi kama Serikali tutaenda kulichakata, lengo letu tumsaidie Mheshimiwa Rais katika kupunguza tatizo la ajira, lakini tuhakikishe kwamba vijana wanaomaliza chuo kikuu ambao walisomeshwa na Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hawalandilandi mtaani wanufaike na uwekezaji unaotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya nirudie kushukuru kwanza kwa kutuendeshea vizuri sana kikao chetu na

baada ya kuyasema haya, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ninakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya.

Waheshimiwa Wabunge, ndani ya ukumbi wetu tuna wageni jioni hii; wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tuna wageni 102 wa Mheshimiwa Profesa Adolf Faustine Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na hawa ni Shirikisho la Wamiliki na Mameneja wa Shule na Vyuo Visivyo vya Kiserikali Tanzania *(TAMANGOSCO),* tuwaone. Karibuni sana, Bungeni. Tumefarijika kuwa nanyi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kundi la pili, ni wageni wawili wa Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge na hawa ni ndugu zake kutoka Mbulu, Mkoani Manyara. *(Makofi)*

Baada ya tangazo hilo, nimwite sasa mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii. Nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao makini sana Wabunge wote 20 ambao wamechangia hapa na tunashukuru kwa kutambua umuhimu wa Wizara yetu Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee tunashukuru sana kwa kutambua michango yetu sisi ambao tunafanya kazi kwenye Ofisi hii. Moja ya hitaji muhimu sana la binadamu ni kutambuliwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunawashukuru kwa jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mnapotushukuru hususani mimi lazima nikiri, niseme kama nilivyowahi kusema huko nyuma mmeweza kufahamu uwezo wetu kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupa fursa. Kwa hiyo, tunamshukuru kwa

fursa ambayo ametupa kumsaidia katika ofisi hii ambayo kwa kweli ndio na ninyi mmeweza kututambua. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimepata bahati ya kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara katika Serikali yake, sasa nipo Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji nimepata nafasi ya kuendesha zoezi kubwa la kuandika Dira, lakini nimepata nafasi ya kuandika Ilani ya Chama chetu Cha Mapinduzi. Kwa hiyo, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa fursa ambazo ameweza kunipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mchango wake hapa na ufafanuzi mzuri ambao ameutoa kuhusu masuala hayo ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo amefafanua baadhi ya hoja na niwashukuru sana Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa jinsi ambavyo wametoa maoni yao na kuunga mkono bajeti, lazima nikiri kwamba Waheshimiwa Wabunge sisi tuna Kamati ambayo ina Wajumbe makini sana na uongozi wake makini sana, wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, lakini Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Edwin Swalle, na Mheshimiwa Edwin Swalle nikushukuru kwa kuninukuu kwa kirefu, kwa sababu sisi ambao ni walimu tunafahamu umuhimu wa kunukuliwa, Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe ufafanuzi baadhi ya maeneo machache tu kwa sababu kwa kweli tunapokea hoja zote ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa na zote ni za muhimu zinastahili kupewa *attention* na sisi nikiri kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri na wenzangu Wizarani tutachukua hoja zote hizo na kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo ningependa kulitolea tu ufafanuzi wa haraka sana ni suala umuhimu wa kuwa na mipango na baadhi yenu mmesema Tanzania haina uhaba wa mipango na pengine tunapanga sana kuliko kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba tusichoke kupanga na tusichoke kufiri, fikra ni muhimu sana na ni kazi ngumu na wanaofahamu vita wanafahamu kwamba 50% ya vita huwa inashindwa mezani, watu wanapanga vita mezani unashinda hapo. Kwa hiyo, suala la kupanga ni muhimu na tusije tukaacha kupanga kwa sababu ni suala la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia kwamba nchi yetu ina historia ndefu sana ya mipango na Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo ameeleza hapa, lakini lazima tutambue tofauti. Nchi yetu ilipata mara ya kwanza mpango wa muda mrefu wa maendeleo mwaka 1964 mpaka mwaka 1980 na wanaofahamu historia ule mpango ulishindikana kutekelezwa kwa sababu ya hali ya hewa mbovu, ikatokea kuharibika kwa soko la mafuta, lakini muhimu sana ile vita ambayo tulipigana kati ya Tanzania na Uganda ilitukwamisha mpango huu haukutekelezwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukaandaa mpango wa pili 1981 mpaka mwaka 2000 na wenyewe ulipata changamoto kwa sababu *IMF* na *World Bank* wakaja na mipango yao, wakatulazimisha tutekeleze *structural adjustment programs* wakatuletea MKUKUTA huu na wenyewe ukalala na wanauchumi wanafahamu kwamba kipindi hiki cha 1964 mpaka 1980 ilikuwa ni kipindi ambacho ukuaji wa uchumi *basically* ulikuwa *flat,* ulikuwa umezimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kipindi hiki cha 1980 mpaka 2000 ndipo tukaanza mageuzi ya kiuchumi, tukaanza *liberalization* na uchumi wetu ukaanza kukuwa kidogo kidogo, lakini kipindi cha tatu ni 2000 hiyo mpaka 2015 baada ya kuandika dira mpya. Kwa hiyo, dira yetu ambayo imetekelezwa kwa mara ya kwanza ni Dira ya mwaka 2025 na yenyewe kwa kweli ilichelewa kwa sababu hatukuandaa *operational plan* ambayo inaitwa hiyo *LTPP,* tumekuja kuiandaa mwaka 2011, 2012 ndio tukaanza kuitekeleza ndiyo ambayo imetufikisha hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wake nini? Tunapozungumzia safari bado ndefu tunapoenda, tusisahau pia tumesafiri safari urefu kiasi gani, nchi hii mwaka 2000 *GDP* pato la

Taifa la nchi hii ilikuwa dola za Kimarekani bilioni 13. Leo miaka 20 baadaye kwa taarifa ya Benki ya Dunia ya juzi uchumi wetu sasa ni dola za Kimarekani bilioni 90.1. Pato la mmoja wakati ule, pato la mtu mmoja mmoja, *per capita* ilikuwa dola za Kimarekani 430, leo kwa taarifa ya juzi ya Benki ya Dunia pato la mtu mmoja Tanzania, dola za Kimarekani 1381.6. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ungeenda mwaka 2000 kuitafuta Afrika iko wapi kiuchumi ilikuwa lazima uanzie nchi 10 za mwisho, *we were among the top ten bottom economies* kule chini. Leo nchi hii miaka 20 baadaye Tanzania ni miongoni mwa uchumi kumi bora Afrika, tunaheshimika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunapozungumzia bado tuna safari ndefu lazima pia tuangalie tumetoka wapi, hiyo ni jambo la msingi. Hamna anayebisha kwamba bado tuna kazi kubwa ya kufanya, lakini muhimu pia tukakiri kwamba kazi kubwa imefanyika katika kujenga uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza vizuri juu MKUMBI ambao tumeutekeleza kuboresha mazingira ya biashara na siyo sahihi kusema kwamba mazingira ya biashara yameendelea kuwa *MKUMBI I,* haikufanya kazi imefanya kazi kubwa sana kama ambavyo ametoa takwimu Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini niwape *quotation* moja tu hapa Benki ya Dunia wanasema; "uchumi wa Tanzania umekuwa mfululizo katika hali ya afya kwa zaidi ya miaka 20," na kwa sababu gani? Wametoa sababu nyingi lakini mbili za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza, uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya usafiri na usafirishaji; ya pili, ambayo wameitolea ufafanuzi ni kuendelea kuboreka na kuimarika kwa mazingira ya biashara na uwekezaji, ndio sababu ambazo zimesababisha uchumi huu uwe hivi ulivyo na wametueleza Tanzania nafasi ya uchumi wake kukuwa vizuri zaidi ikifanya mambo mawili, ikiendelea kuimarisha mazingira ya biashara na ikiwekeza kwenye kunoa *human resource* yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana Mheshimiwa Rais alielekeza tuandae mkakati mpya wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili iendane na Dira mpya ya mwaka 2050. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kazi kubwa imefanyika, lakini kazi kubwa bado ipo ya kufanya na tumejipanga kuendelea kuifanya katika awamu inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ambalo ningetaka kutolea ufafanuzi, ni suala la mashirika ya umma. Ninaunga mkono maoni yenu yote kwa kweli na ndio maono ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais ameelekeza yafanyike mageuzi makubwa katika uendeshaji wa mashirika ya umma na ndio maana tumeeleza hapa kwamba tunakwenda kukamilisha ule Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma ambayo itaongoza mageuzi mengi humo ndani yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha wa michango yenu ni kwamba hili suala la kuunganisha na kufuta linaendelea, ni kazi kubwa kwa sababu linahitaji mabadiliko ya kisheria, zilipewa Wizara kadhaa, kila Wizara ipo katika hatua mbalimbali kwa sababu sheria, kila mashirika ya umma haya yameundwa kwa sheria yake. Kwa hiyo, sisi ya kwetu yaliundwa kwa sheria ile ya uwekezaji, bahati nzuri tumekamilisha ndio tumeunganisha *TIC* na *EPZ,* lakini ninafahamu kwamba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara anakamilisha uunganishaji wa mashirika ya *CAMARTEC, TEMDO* na mengine. Ninafahamu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Bunge hili litarajie kuona mabadiliko mengi ya sheria katika muktadha wa kuyaweka mashirika yetu vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ushindani tayari maelekezo yalishatoka, tunajua kwamba Wajumbe wa Bodi kwa baadhi ya mashirika hususani yanayofanya biashara na yale ambayo yanafanya urekebu tunakwenda kuhakikisha kwamba Wajumbe wa Bodi na wale ma-*CEO* wanapatikana kwa njia ya ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumeshaanza kama mnafuatilia juzi Bodi ya *TISEZA* ina nafasi za Wajumbe wa Bodi na

mimi ndio mteuzi, tumetangaza wazi kabisa kwenye magazeti watu waombe kuwa Wajumbe wa Bodi ya *TISEZA* na ninataka niseme hapa unajua hii nchi tumezoea mtu anakuletea, tumetangaza mtu anakuleta ka-*CV* na Mheshimiwa na mimi mtoto wangu mwangalie, tumetangaza wazi kwa njia ya ushindani kaombe. Na wala mimi sipo huko, Katibu Mkuu na utaratibu wake watafanya *set committee* wata-*interview* watu, wataleta majina matatu kwangu nitachagua moja. *(Makofi)*

Kwa hiyo, huo ndio utaratibu. Kwa hiyo, tumeshaanza utaratibu huu ni mchakato na ninaamini tunavyokwenda mbele tutaendelea kuboresha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tano, suala la kulinda viwanda vya ndani na Waheshimiwa Wabunge mmeongea kwa uchungu hapa juu ya kulinda viwanda vya ndani kupitia kodi zetu *(import duty)* na mmetoa mfano wa *calcium carbonate,* bado ninakumbuka hii *chemistry* yangu, kule kiwanda *somewhere* huko Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba msingi wa kutoza ama kusamehe kodi ya ushuru kwa maana ya *import duty* ni mmoja, pale ambapo tumejiridhisha kama Serikali kwamba humu ndani uzalishaji wa bidhaa husika unajitosheleza, huwa tunapiga kodi 25% wakati mwingine 35% na hata 100% kwa maana *import duty*. Kwa hiyo, hayo maoni ambayo mmeyaleta juu ya hicho kiwanda tutafanya tathmini kama tunazo bidhaa za kutosha hapa ndani hatuna sababu yoyote kuagiza kutoka nje na katika *Finance Bill* inayokuja Mheshimiwa Waziri wa Fedha ataiweka ili kuhakikisha kwamba tunalinda hiyo bidhaa inayozalishwa kwa sababu ndiyo msingi wa sera za kodi hususan ushuru wa forodha katika nchi yetu. Kwa hiyo tunapokea hilo na tutalizingatia katika *Finance Bill* inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie jambo moja la msingi sana; suala la ufuatiliaji na usimamizi wa utekelezaji wa mipango na vikwazo vyake nimevieleza kwa kirefu hapa, nimeeleza hapa misingi ya utekelezaji yetu moja ni mipango ya maendeleo ambayo tumeieleza hapa dira na kadhalika, lakini msingi mwingine mkubwa sana ni hotuba ya Mheshimiwa Rais ya

kufungua Bunge. Hii itatuongoza katika miaka hii mitano na Mheshimiwa Rais ameeleza vizuri katika hotuba yake juu ya misingi ya utekelezaji wa mipango yetu na anazungumzia suala la uwajibikaji na utawala wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimnukuu ukurasa wa 37 anaeleza; “Tumezungumzia masuala mengi, ila msingi wa mafanikio yote haya ni utawala wa sheria, uadilifu na uwajibikaji katika kila ngazi kuanzia juu mpaka chini. Kwa msingi huo na ili kuhakikisha wananchi wananufaika na rasilimali za nchi pamoja na kupata huduma wanazostahili tutaelekeza jitihada zetu kwenye mapambano dhidi ya rushwa, ufisadi, ubadhilifu, uzembe, ukosefu wa nidhamu na maadili. Ni lazima tuthibiti wachache wanaotaka kuturudisha nyuma kwa kuendekeza maslahi binafsi.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge suala la utawala wa sheria na uwajibikaji ni suala la msingi katika utekelezaji wa mipango yetu. Tunao mwongozo wa mkuu wa nchi, lakini pia sio mkuu wan chi tu Wabunge wengi wanasema hapa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, kazi yetu ni kusimamia haya ambayo tumeyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tusikwepe, tusioneane aibu kuwajibishana pale ambapo mtu anakwamisha utekelezaji wa mipango yetu, hili ni jambo la msingi, lakini msingi wa tatu, tulienda kwenye uchaguzi, tukashindanisha ilani na hatimaye wananchi wakachagua Ilani ya chama kimojawapo inaitwa ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nayo itatuongoza katika miaka mitano ijayo na safari hii Ilani ya CCM kwa mara ya kwanza imeweka sura mpya ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Ilani ipo hapa, inasema nini? Aya ya 108 ukurasa wa 71 tunakumbushana tu, CCM itahakikisha sambamba na Mheshimiwa Rais inapiga vita vitendo vyote vinavyoweza kukwamisha utekelezaji wa malengo yaliyowekwa ikiwemo rushwa, uzembe na umangi meza. CCM itahakikisha kuwa Serikali inaweka uongozi wenye dhamira thabiti, ndiyo sisi tumewekwa sasa, ndiyo sisi hapa Mawaziri na ninyi Wabunge tuna dhamira

katika ngazi zote, katika Serikali kuu na mamlaka ya Serikali ya mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini muhimu, mkazo utawekwa katika kupata matokeo ya haraka badala ya kutumia muda mwingi katika kushughulikia michakato. CCM haitavumilia uchelewashwaji wa utekelezaji wa programu ya miradi ya maendeleo iliyopagwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo pale ambapo tumepanga na tukachelewesha utekelezaji ni kukwamisha utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni nani hawa watekelezaji? Kwa sababu hapa Waheshimiwa mkisimama ni kama kwamba kuna mtu ambaye anahusika na wengine hawahusiki. Ilani inasema nini? Nani ni mtekelezaji na msimamizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kikatiba Bunge hili lina kazi tatu, kushauri, kuisimamia Serikali na kutunga sheria. Kwa hiyo tusikwepe wajibu wetu wa usimamizi, lakini ilani *is more specific,* inasema hivi ukurasa wa 77; "Katika ngazi ya Taifa, usimamizi wa utekelezaji wa Ilani ya CCM utafanywa na Wabunge pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi." Sasa Wabunge ni nani? Si ndiyo sisi hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tusinyooshe tu vidole kwa watu wengine, tunyoosheane. Mipango hii ikikwama wote tuliomo humu ndani tunahusika. Mipango ikifanikiwa wote tuliomo humu ndani tunahusika, kwa hiyo, tujipange tusimamiane, tuwajibishane. Hii ni ya kwetu, tuna mwongozo, tuna kila kitu ni jukumu letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala la wasiwasi wa lengo la trilioni moja dola *by 2050.* Miaka 25 ijayo hatukuwa na mbadala, mwaka 2050 kwa jinsi dunia inavyokwenda uchumi wa trilioni moja ni uchumi mdogo sana, hatukuwa na mbadala na kama kuna watu wanadhani tunataka tuwe chini ya trilioni moja *by then, then you are not serious. The minimum we can achieve by then* ni hiyo trilioni moja. China leo alikuwa anazungumzia

Profesa uchumi wake ni trilioni 20 dola na wana-*expect* kui-*double by then*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tujipange, tufunge mkanda, muhimu hapa tusitembee lazima tukimbie, lazima tukimbie. Hatuna mbadala wa trilioni moja, tunatakiwa tuwe na zaidi, lakini lazima tuende ile tunayosema *business unusual. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *otherwise* nichukue nafasi hii tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu, kwa upendo wenu, kwa mapenzi yen una kwa kututakia kila la heri na tuwaahidi sisi kwa niaba ya wenzangu Serikalini tumejipanga kuisimamia mipango hii ili ilete matokeo yanayotarajiwa na Mheshimiwa Rais, yanayotarajiwa na Chama Cha Mapinduzi, yanayotarajiwa na Wananchi wa Tanzania ambao wametuweka hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyekiti kwa kazi kubwa aliyofanya na Mwenyekiti wa asubuhi aliyeendesha mjadala huu, lakini nimshukuru Mheshimiwa Spika kwa jinsi ambavyo tumeendeshwa vizuri, lakini nirudie tena kumpongeza kwa jinsi ambavyo ameli-*modernize* Bunge letu, Bunge la kisasa hili, unacheki pale watu wangapi wapo, watu wangapi hawapo, kwa kweli kazi ambayo umeanza nayo ni kazi ya kuheshimika, wewe ni kijana kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Jumaa Aweso ambaye ameshikilia nafasi ya Waziri Mkuu leo, mambo yanaanzaga hivi hivi, Mungu akubariki uendelee namna hiyo. Kwa hivyo tunashukuru sana. *(Makofi)*

Nimshukuru Mwalimu wangu Profesa Palamagamba Kabudi - *Chief Whip* kwa jinsi ambavyo anatusimamia vizuri na nikuahidi tutaendelea kukupa ushirikiano ili Bunge hili na Serikali yetu iendelee kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo ninaomba kutoa hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa Kitila. Waheshimiwa hoja imetolewa, hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Kamati ya Matumizi.

Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 011 – Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji**

Kifungu1001 – *Administration & Human Resources Management*......................................Sh. 5,820,771,000
Kifungu 1002– *Finance and Account Unit*…………….Sh. 910,436,712
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Department*....Sh. 2,440,445,336
Kifungu 1004–*Legal Unit*…………….........................……Sh. 501,120,168
Kifungu 1005– *Government Communication Unit*...Sh. 1,097,866,172
Kifungu 1006– *Internal Audit Unit*..................................Sh. 547,547,908
Kifungu 1007–*Procurement Management Unit*..........Sh. 611,965,289
Kifungu 1008– *Information and Communication Technology Unit*.....................................Sh. 690,038,410
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*.......Sh. 1,490,687,214
Kifungu 2001 – *Public Sector Investment Division*....Sh. 1,928,300,544
Kifungu 2002 – *Private Sector Investment Division*...Sh. 7,570,369,230

Kifungu 2004 –*Business Environment Unit*….................Sh. 2,635,316,017

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*........................Sh. 8,290,326,660
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Division*.......Sh. 1,395,453,224
Kifungu 1003 – *Planning, Research & Development Division*...............................................Sh. 4,536,856,000
Kifungu 1004 – *Legal Service Division*........................Sh. 1,501,060,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*........Sh. 528,050,000
Kifungu 1006 – *Information and Communication Technology Division*..........................Sh. 3,546,836,800
Kifungu 1007 – Public *Investment Management Division*...............................................Sh. 1,044,892,2000
Kifungu 1008 – *Risk Management Unit*........................Sh. 926,169,000
Kifungu 1010 –*Monitoring and Evaluation Unit*........Sh. 1,024,440,000
Kifungu 2001 – *Public Investment Management Division*............Sh. 0
Kifungu 2002 – *Funds Management and Investment Division*...............................................Sh. 1,217,384,016
Kifungu 3001 – *Privatization and Monitoring*................................Sh. 0
Kifungu 4001– *Management Service Division*….......Sh. 7,101,487,000
Kifungu 4002– *Performance Management – Commercial Entities Division*.................................Sh. 24,605,212,040
Kifungu 4003 – *Performance Management – Non-Commercial Entities Division*… Sh. 3,952,923,040

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 066 – Tume ya Taifa ya Mipango**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*....................................Sh. 6,047,230,400
Kifungu1002 – *Finance and Accounts Unit*...............Sh. 1,301,040,000
Kifungu 1003 – *Planning & Budgeting Division*.........Sh. 2,263,458,095
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*...Sh.1,054,984,535

Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*................................Sh. 871,758,095
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*........Sh. 931,518,095
Kifungu1007 – *Legal Services Unit*................................Sh. 829,480,000
Kifungu1008 – *Information & Communication Technology Unit*....................................Sh. 967,618,571
Kifungu1009 – *Risk Management and Quality Assurance Unit*.......................................Sh. 765,280,000
Kifungu 1010 – *Monitoring and Evaluation Unit*..........Sh. 857,118,095
Kifungu 2001 – *National Planning Division*................Sh. 7,345,678,000
Kifungu 2002 – *Trade and Private Sector Engagement Division*........................Sh. 3,911,470,000
Kifungu 2003 – *National Key Results Areas Division*..Sh. 3,946,358,095
Kifungu 2004 – *Performance Monitoring & Evaluation Division*…………………………Sh. 5,525,888,495
Kifungu 2005 – *Innovation, Research and Development Division*.......................Sh. 2,703,202,524

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIRADI YA MAENDELEO**

**Fungu 011 – Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji**

Kifungu1001 – *Administration & Human Resources Management*.....................................Sh. 1,696,000,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Department*.......Sh. 150,000,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*..........Sh. 518,260,000
Kifungu 2001 – *Public Sector Investment Division*....Sh. 293,020,000
Kifungu 2002 – *Private Sector Investment Division*...Sh. 4,525,466,000
Kifungu 2004 – *Business Environment Unit*................Sh. 1,958,701,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Division*...........................Sh. 0

Kifungu 1003 – *Planning, Research & Development Division*....................................................Sh. 130,690,000
Kifungu 1006 – *Information & Communication Technology Division*.................................................Sh. 0
Kifungu 1008 – *Internal Audit Unit*…................................................ Sh. 0
Kifungu 1009 – *Risk Management Unit*.........................................Sh. 0
Kifungu 2001 – *Public Investment Management Division*............Sh. 0
Kifungu 2002 – *Funds Management & Investment Division*.........Sh. 0
Kifungu 3001 – *Privatization and Monitoring*.................................Sh. 0
Kifungu 4001 – *Management Service Division*..............................Sh. 0
Kifungu 4002 – *Performance Management Commercial Entities. Division*…...........Sh. 120,001,000
Kifungu 4003 – *Performance Management Non-Commercial Entities Division*.......................................Sh. 120,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 66 – Tume ya Taifa ya Mipango**

Kifungu 1003 – *Planning & Budgeting Division*.........Sh. 9,319,512,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge Linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 126(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2025 ninaomba Kutoa Taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2026/2027 na limekamilisha kazi zake. Ninakuomba kwamba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa vile taarifa imetolewa sasa nitawahoji ili tuweze kuhitimisha kwamba Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwenye Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2026/2027. *(Makofi)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ninashukuru sana. Kwa hiyo basi Bunge hili limepitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa kauli moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana kwa kazi kubwa, lakini nimpongeze vilevile Naibu wako ambaye tupo pamoja kwa kazi kubwa mliyoifanya, lakini niwapongeze vilevile Makatibu Wakuu wote wawili ambao ninadhani na wao wenyewe wamekuwa *engine* ya kutufikisha na watendaji mbalimbali katika Ofisi hii ya Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, ninadhani kwa michango iliyosikika hapa inakuwa hitimisho lako, umeonesha wazi kabisa kwamba yaliyopagwa yanawezekana na Watanzania wana matumaini

makubwa na mategemeo makubwa kwenye ofisi hii katika kuifikia ile safari ya Dira ya 2050. Kwa hiyo, ninadhani kama ulivyosema mwenyewe hautawaangusha Watanzania, sisi tukutakie kazi njema pamoja na timu yako yote na Bunge litaendelea kutoa ushirikiano katika kuhakikisha kwamba tunayafanya yote yaliyotajwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo ambalo limejitokeza kwa ukubwa hapa ni kwamba mipango tunaweza tukawa nayo, lakini tuisimamie, na bahati nzuri kauli yako ya *business unusual,* hiyo *theme* ikifanyika na ninadhani Ofisi ya Rais, Mipango inatakiwa iwe ndiyo mfano wa kuonesha maana halisi ya *business unusual* ni nini?

Kwa hiyo, sisi tuishie hapa kwa kuomba kuwatakia heri ili muweze kuyatekeleza hayo yote ambayo yameweza kufanyika.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaliahirisha Bunge mpaka kesho siku ya Ijumaa tarehe 17 Aprili, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1. 24 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 17 Aprili 2026 Saa Tatu Asubuhi)*